Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 26 Juni, 2010**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## DUA

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani kama ifuatavyo:-

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa Fedha 2010/2011.

**MHE. WILSON M. MASILINGI - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**:

1. Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

2. Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS (K.n.y. MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2010/2011 Wizara za Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama mtakavyoona *Order Paper* ya leo tunazo Wizara mbili, tutakachofanya ni kwamba kwanza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa atasoma hotuba yake, halafu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi atasoma hotuba yake na baadaye tunajadili kwa pamoja tukifika hapo watajibu kama kawaida, halafu tutapitisha fungu moja baada ya lingine.

Kwa hiyo, kwa sasa namwita Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kisha kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyenijalia kuwa na uzima na afya njema niliyonayo. Aidha, napenda tuungane pamoja sisi sote kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kukutana tena hapa Bungeni kwa shughuli hii muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena, ninayo heshima kubwa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa madhumuni ya kuwasilisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2010/2011.

Kabla sijafanya hivyo, naomba kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini kwa kuchambua na kushauri juu ya kuboresha mapendekezo ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2010/2011 ninayoyawasilisha leo hapa Bungeni. Wakati wote Kamati hii imekuwa mstari wa mbele katika kuishauri Serikali juu ya umuhimu wa kuimarisha utendaji wa vyombo vya ulinzi wa Nchi yetu. Wizara na Serikali kwa ujumla imezingatia ushauri wao huo. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ina dhamana ya kulinda mipaka ya Nchi dhidi ya adui ili kuhakikisha uhuru na hadhi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *(state sovereignty and territorial integrity*) vinadumishwa. Kutokana na umuhimu wa dhamana hii, kama ilivyo ada, naomba nitoe tathmini ya hali ya ulinzi na usalama wa mipaka katika mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina mipaka ya nchi kavu na nchi za Kenya na Uganda upande wa Kaskazini; Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) upande wa Magharibi na Zambia, Malawi na Msumbiji upande wa Kusini. Aidha, ina mipaka ya majini na Nchi za Comoro na Seychelles katika Bahari ya Hindi upande wa Mashariki. Hivyo, kimsingi usalama wa mipaka ya Tanzania hutegemea mwenendo wa hali ya usalama katika Nchi hizo, Nchi zinazopakana nazo na eneo hilo la Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini inaonyesha kuwa, katika mwaka 2009/2010 mipaka ya Tanzania kwa ujumla ilikuwa salama ukiacha matukio machache yaliyoathiri utulivu katika maeneo ya mpaka na nchi ya *DRC* upande wa Magharibi na katika eneo la Bahari ya Hindi upande wa Mashariki. Migogoro ya kisiasa na harakati za chini kwa chini za wapiganaji katika Nchi ya *DRC* imeendelea kusababisha kuwepo wahamiaji haramu katika maeneo ya mpaka na Nchi hiyo ambao wanahusishwa na uingizaji nchini wa silaha ndogo ndogo kinyume cha sheria na vitendo vya ujambazi wa kutumia silaha katika mikoa ya Magharibi ya nchi yetu. Aidha, tatizo sugu la uharamia katika Ghuba ya Aden ambalo linaendelea kusambaa kwa kasi hadi katika ukanda wetu wa Bahari ya Hindi linahatarisha usalama wa vyombo vya majini vinavyopita katika ukanda huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo matatizo hayo, Jeshi la Wananchi limejizatiti ipasavyo kudhibiti ulinzi na usalama wa mipaka yetu. Hali ya ulinzi na usalama kwa kila mpaka katika mwaka 2009/2010 ilikuwa ifuatavyo:-

Kwa ujumla hali katika mpaka huu haijatengemaa kutokana na vitendo vya uharamia katika mwambao wa Bahari ya Hindi hususan kwenye Ghuba ya Aden na Pwani ya Afrika Mashariki vinavyofanywa na maharamia wa Kisomali. Katika kipindi

cha mwaka huu hadi kufikia mwezi Mei, 2010, maharamia hao wameteka meli zipatazo tisa (9) na pia wamejaribu kuziteka meli saba (7) bila mafanikio. Kufuatia kuwepo kwa ulinzi wa melivita za majeshi ya nchi za Ulaya pamoja na za mataifa mengine makubwa kwenye Ghuba ya Aden, maharamia hao sasa wameelekeza mashambulizi yao upande wa Kusini mwa Bahari ya Hindi karibu kabisa na pwani ya Afrika Mashariki ambako hakuna ulinzi mkali wa melivita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na hali hiyo, Jeshi la Wananchi limeimarisha ulinzi kwa kufanya doria karibu na mwambao wa pwani ya Bahari ya Hindi pamoja na kusindikiza meli zinazoomba msaada huo. Aidha, ushirikiano kati ya majeshi ya nchi zaidi ya 20 za Umoja wa Ulaya yanayofanya operesheni ya kupambana na maharamia hao *(EU NAFOR ATLANTA)* na nchi za Afrika Kusini, Msumbiji, Tanzania, Seychelles na Kenya unachangia katika kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpaka huu, hali kwa ujumla ni shwari isipokuwa kuna matatizo ya kuharibiwa kwa alama za mipaka (*beacons*) na ujenzi holela katika maeneo ya Tarime na Maramba katika mpaka wa Kenya na Misenyi katika mpaka na Uganda. Hata hivyo, matatizo hayo yanaendelea kutafutiwa ufumbuzi kwa kushirikiana na Serikali za Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kwa upande wa mpaka na nchi za Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ni shwari. Hata hivyo, yalikuwepo matukio ya uhalifu wa kutumia silaha yanayofanywa na wahamiaji haramu wanaoshirikiana na raia wabaya wa Tanzania ambayo yamepungua katika kipindi hiki ukilinganisha na miaka iliyopita. Pamoja na kuwepo hali hiyo, Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola limeendelea kufuatilia kwa karibu hali ya usalama katika nchi hizo hususan katika kipindi cha kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu ili kuhakikisha amani na utulivu unakuwepo wakati wote wa kipindi cha uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama wa mpaka katika eneo hili ni shwari. Hakuna matukio yaliyojitokeza ya kuathiri usalama wa mipaka ingawa bado kuna tatizo la ujenzi holela katika mji wa Tunduma kwenye mpaka na nchi ya Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, zifuatazo ni Shabaha kuu za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

(i) Kujenga jeshi lenye taaluma, zana na vifaa vya kisasa kwa ajili ya majukumu yafuatayo ya kiulinzi.

(ii) Kulinda mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya uvamizi wa adui.

(iii) Kushiriki katika majukumu ya kulinda amani duniani.

(iv) Kusaidia mamlaka za kiraia katika kukabiliana na maafa ili kuokoa maisha na mali za wananchi.

(v) Kuandaa na kuongoza umma wa Watanzania katika jukumu la Ulinzi wa Taifa dhidi ya adui.

(vi) Kuimarisha Jeshi la Kujenga Taifa ili liwe na uwezo wa hali ya juu wa.

(vii) Kuwajenga vijana wa Kitanzania katika uzalendo, ukakamavu, usawa na umoja wa kitaifa na kuwaandaa katika uzalishaji mali na ufundi stadi.

(viii) Kuwa chimbuko la ajira kwa vyombo vya ulinzi na usalama hapa nchini.

(ix) Kuwa chombo cha uzalishaji mali nchini.

(x) Kuendeleza utafiti na kujenga uwezo katika teknolojia ya kijeshi.

(xi) Kudumisha amani na utulivu na nchi nyingine duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia shabaha hizo kwa mwaka 2009/2010 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilikuwa na Mpango ufuatao:-

(i) Kuimarisha mafunzo na mazoezi ya kijeshi na kuendeleza mafunzo ya mgambo.

(ii) Kuimarisha upatikanaji wa mahitaji na huduma muhimu kama vile vifaa na vipuri vyake, umeme, maji, simu, mafuta na vilainisho.

(iii) Kuimarisha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wa Kitanzania.

(iv) Kuimarisha utafiti na uendelezaji wa teknolojia katika mashirika ya Mzinga na Nyumbu.

(v) Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa stahili za wanajeshi, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na Watumishi wa umma.

(vi) Kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine duniani katika nyanja za kijeshi na ulinzi.

(vii) Kuboresha mazingira ya makazi kwa kukarabati, kumalizia viporo vya ujenzi na ujenzi mpya wa majengo na miundombinu katika makambi ya Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa.

(viii) Kutekeleza Kauli Mbiu ya “Kilimo Kwanza”

(ix) Kuimarisha shughuli za uzalishaji mali katika Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT).

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mpango huo ulikuwa ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafunzo ya Kijeshi na Mazoezi kwa Wanajeshi na Mgambo. Mwaka 2009/2010 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limetoa mafunzo kwa wanajeshi ndani na nje ya nchi ili kuboresha taaluma zao. Vyuo vya ndani ya nchi vya fani mbalimbali vilitoa mafunzo kwa wanajeshi kwa kiwango cha kuridhisha. Vyuo vya nchi za nje hususan nchi za China, Uingereza, Marekani, India na Afrika Kusini zimeshiriki kufundisha maafisa na askari katika fani mbalimbali.

katika mwaka wa fedha 2009/2010 mazoezi ya kijeshi yalifanyika kama ilivyopangwa; zoezi la Golfinho lilifanyika Afrika ya Kusini kuanzia tarehe 1 – 26 Septemba, 2009 kwa kushirikisha nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* ambazo ni Afrika Kusini, Angola, *DRC,* Madagascar, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Namibia, Seychelles, Swaziland, Tanzania, na Zambia. Zoezi *Natural Fire –* 10 lilifanyika tarehe 16 – 26 Oktoba, 2009 nchini Uganda na kushirikisha nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* ambazo ni Burundi, Kenya, Rwanda, Tanzania na Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya nchi yetu lilifanyika zoezi moja lililoitwa Mlima Kilimanjaro kuanzia tarehe 3 – 26 Septemba, 2009 katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga kwa kushirikisha majeshi ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mazoezi haya ya pamoja yana manufaa makubwa kwa Jeshi letu. Pamoja na kubadilishana uzoefu kiutendaji kivita mazoezi haya yanaimarisha ushirikiano katika ulinzi pale hitajio linapotokea hususan katika operesheni za ulinzi wa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mgambo ndiyo nguzo kuu ya Jeshi la akiba kwa Jeshi la Wananchi. Katika mwaka 2009/2010, mafunzo ya mgambo yameendelea kutolewa kwa kuendesha mafunzo ya awali na ya kujikumbusha (*refresher*) sambamba na mafunzo ya Uongozi Mdogo wa Mgambo. Katika mwaka 2009/2010 jumla ya wanamgambo 15,106 walihitimu mafunzo ya awali katika mikoa 21 ya Tanzania na wanamgambo 118 walifundishwa na kuhitimu kozi ya Uongozi Mdogo wa Mgambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa mahitaji na huduma muhimu ya vifaa, mafuta, vilainisho, maji na umeme kwa ajili ya uendeshaji wa majukumu ya kimsingi ndani ya Jeshi bado haijatengamaa kutokana na ufinyu wa bajeti. Mahitaji ya fedha kwa ajili ya vifaa, mafuta, vilainisho, maji na umeme ni makubwa na yanaongezeka licha ya Serikali kuboresha viwango vya bajeti kwa ajili ya mahitaji na huduma hizo.

Hata hivyo, kwa upande wa vifaa, Serikali imenunua vifaa vipya na Jeshi limevifanyia ukarabati na kuboresha uwezo wa vifaa vya zamani ili viweze kutumika katika mazingira ya sasa. Pamoja na hatua hizo, hatua nyingine zinazochukuliwa na Jeshi ni kuboresha mifumo ya hifadhi na matunzo (yaani maghala na karakana) ili kuviwezesha vifaa hivyo kutumika kwa muda mrefu zaidi na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua ufinyu wa bajeti, Wizara imeamua na imeanza kuchukua hatua za dhati kubana matumizi ya maji, mafuta, umeme na mahitaji muhimu makambini na wakati wa mafunzo. Hatua hizo ni pamoja na kukarabati mifumo iliyochakaa ya usambazaji wa huduma hizi katika makambi baada ya kubainika kuwa ni chanzo cha upotevu (*leakage*) wa maji na umeme unaolipiwa bila kutumika.

Vile vile Jeshi limeanza matumizi ya *LUKU* katika nyumba wanazoishi askari na kuweka viwango vya ukomo wa matumizi ya huduma za maji na umeme kulingana na stahili zao. Na kwa upande wa mafuta na vilainisho hatua zinazochukuliwa na Jeshi ni kutenganisha bajeti ya mafuta na vilainisho kwa ajili ya majukumu ya kimsingi kama vile operesheni za kiulinzi na mafunzo kwa upande mmoja na bajeti ya mafuta kwa ajili ya shughuli za kiutawala kwa upande mwingine. Hatua hizi zimeanza kwa vikosi vilivyopo katika Mkoa wa Dar es Salaam na Morogoro katika Shirika la Mzinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya maeneo muhimu katika azma ya kujenga jeshi dogo la kisasa ni kuimarisha uwezo wa utafiti wa teknolojia ya kijeshi kwa madhumuni ya kuliwezesha jeshi kuzalisha bidhaa kwa ajili ya matumizi ya vyombo vya ulinzi na usalama hapa nchini. Katika mwaka 2009/2010 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuweka mkazo katika kutekeleza jukumu hili kwa kuimarisha shughuli za utafiti na uzalishaji katika mashirika yake ya Mzinga na Nyumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 Shirika limeendelea na utekelezaji wa mradi wa kukarabati majengo na mitambo ili kuongeza uwezo katika shughuli za utafiti na uzalishaji. Majengo yamepanuliwa kukidhi maboresho ya Kiwanda ili kuongeza uwezo wa uzalishaji. Ujenzi wa majengo hayo umekamilika kwa awamu ya kwanza. Aidha, ukarabati wa miundombinu na uboreshaji wa mitambo umekamilika kwa asilimia 70. Hatua inayofuatia ni uzinduzi wa mitambo, kazi iliyopangwa kutekelezwa mwaka wa fedha 2010/2011. Vile vile, Shirika limeendelea na ukarabati wa vifaa vya kijeshi vilivyoharibika, kufanya utafiti wa kubuni teknolojia kwa ajili ya matumizi ya kiraia, ikiwemo mashine za kukereza mbao na kukoboa na kusaga nafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Shirika la Nyumbu limekamilisha kuandaa Mpango Mkakati wake wa muda mrefu ambao una lengo la kulifanya Shirika kuwa Kituo maalum cha kuendeleza teknolojia za magari na mitambo ndani na nje ya nchi. Pia Shirika limeendelea kuandaa mazingira mazuri ya uwekezaji katika teknolojia hizo, ambapo makampuni kadhaa kutoka nchi za India, China na Malaysia yameonyesha nia ya kushirikiana. Aidha, Shirika limeendelea kufanya utafiti na uzalishaji mdogo mdo go wa bidhaa na vipuri mbalimbali kwa ajili ya sekta za ulinzi na usalama, kilimo, viwanda na usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009/2010 Shirika limetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

(a) Mbegu bora za mazao mbalimbali tani 189 zilipatikana katika mavuno ya msimu uliopita na tayari zimeuzwa kwa Wakala wa Mbegu bora Tanzania *(ASA).*

(b) Shirika lilipata kandarasi za ujenzi wa majengo toka Wizara ya Ulinzi, NGOME, Kampuni binafsi na Idara mbalimbali za Serikali.

(c) Mfumo bora wa vitabu vya uhasibu tayari umeanzishwa, sasa shirika linatumia *"SUMAJKT Accounting Manual"* iliyoidhinishwa na Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi.

(d) Shirika limeweza kununua magari 30 aina ya "*Pick up*" ili kupunguza tatizo la usafiri katika utekelezaji wa miradi mipya mbalimbali.

(e) Shirika limeanzisha mradi wa unenepeshaji wa ng'ombe wa nyama na mbuzi kwa ajili kuuza huko Oljoro JKT Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira nadhifu na salama ya makazi makambini kwa wanajeshi na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa ni kati ya maeneo yanayopewa kipaumbele na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Katika mwaka 2009/2010 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutekeleza programu ya kukamilisha ujenzi na ukarabati wa majengo kwa ajili ya makazi pamoja na miundombinu makambini. Miradi ifuatayo imekamilika:- ujenzi wa bweni la maafisa Kapera – Kigamboni (Dar es Salaam), ujenzi wa mabweni ya askari - Masaki na Lugalo (Dar es Salaam) na Kizumbi (Shinyanga), ujenzi wa nyumba za kuishi - Makambako (Iringa) na ukarabati wa nyumba ya kuishi maafisa - Masaki (Dar es Salaam). Miradi inayoendelea kukamilishwa ni:- Ujenzi wa mabweni matatu - Kihagwa (Kigoma), ujenzi wa bweni la askari - Kigamboni (Dar es Salaam) na ukarabati wa mabweni sita ya askari - Pangawe (Morogoro).

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya makazi katika makambi bado ni makubwa na uwezo wa Serikali ni mdogo. Pamoja na jitihada zinazofanyika sasa kutekeleza jukumu hilo, Wizara inaendelea kufanya mazungumzo na taasisi za fedha ndani na nje ya nchi, zenye uwezo wa kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa lengo la kupunguza tatizo lililopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutoa kwa wakati stahili muhimu za mishahara, posho, malimbikizo ya mishahara kwa waliopandishwa na waliobadilishwa vyeo pamoja na huduma ya maziko kwa Wanajeshi, Watumishi wa Umma na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa. Hata hivyo, baadhi ya stahili zikiwemo mavazi, vifaa vya malazi na likizo zimetolewa kwa kiwango cha wastani kutokana na mahitaji kuwa makubwa kuliko uwezo wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 huduma za kinga na matibabu kwa wanajeshi na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutolewa kwa kutumia mtandao wa vituo vya tiba zaidi ya 70 ambavyo hutoa huduma za uchunguzi wa maradhi mbalimbali. Vituo hivyo ni pamoja na vilivyopo katika Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo - Dar es Salaam na Hospitali za Jeshi za Kanda za Mbeya, Mwanza, Pwani, Kigoma, Iringa, Tabora, Arusha, Morogoro, Zanzibar na JKT Mgulani - Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 vijana 4,297 wa Operesheni Uadilifu ambao kati yao wavulana ni 3,359 na wasichana ni 938 walimaliza mafunzo ya awali ya ukakamavu, uzalendo, usawa na umoja yaliendeshwa katika makambi sita (6) ya Mafinga - Iringa, Oljoro - Arusha, Mlale - Ruvuma, Ruvu - Pwani, Bulombora - Kigoma na Mgambo - Tanga. Baada ya kumaliza mafunzo hayo vijana hao kwa sasa wamesambazwa katika makambi yafuatayo:- Rwamkoma - Mara, Mgulani – Dar es salaam, Chita - Morogoro, Maramba - Tanga, Masange - Tabora, Chang'ombe - Dar es salaam, Kanembwa - Kigoma, Makutopora - Dodoma, Mbweni - Dar es salaam na Nachingwea - Mtwara kwa ajili ya mafunzo ya stadi za kazi na uzalishaji mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika mwaka 2009/2010 Jeshi la Kujenga Taifa lilichukua vijana 4,400 wa Operesheni KILIMO KWANZA kwa ajili ya mafunzo ya awali. Aidha, hatua zifuatazo zimechukuliwa ili kuboresha malezi na mafunzo ya vijana kwa kuwaandaa Wakufunzi ili kuimarisha kada ya ukufunzi kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuandaa mitaala mpiya inayoendana na hali ya wakati wa sasa katika malazi ya vijana, ikiwa ni pamoja na masomo ya uraia na uongozi.

(ii) Kupeleka wakufunzi kozi za ukufunzi zinazoendeshwa na Mamlaka ya Ufundi Stadi nchini *(VETA).*

(iii) Kuendesha Semina kwa wakufunzi zinazohusu kilimo, ufugaji na uhifadhi wa mazingira.

(iv) Kuendesha kozi za ujasiriamali kwa vijana.

(v) Kukarabati na kujenga mabweni 100 katika vituo tisa (9) vya kuendeshea mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana vya Bulombora, Rwamkoma, Masange, Kanembwa, Ruvu, Oljoro, Mgambo, Mafinga pamoja na Mlale ambapo kwa sasa vituo hivyo vina uwezo wa kuchukua vijana 17,978 kwa pamoja kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, Kilimo Kwanza. Katika mwaka 2009/2010 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imetoa mchango katika kufanikisha kauli Mbiu ya "Kilimo Kwanza". Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Taifa imelima jumla ya ekari 2,323.5 za mazao mbalimbali ya chakula na mbegu bora katika vikosi vya uzalishaji vya jeshi hilo. Aidha, wataalam wa kilimo na mifugo ngazi ya Shahada wamepangwa katika vikosi hivyo kama Mameneja wa mashamba hayo. Vile vile, wataalam 15 wa jeshi hilo wamepelekwa vyuoni kuongeza ujuzi katika maeneo ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuweka msukumo zaidi katika utekelezaji wa kauli mbiu ya Kilimo Kwanza. Katika jitihada za kuhakikisha zana za kilimo zinapatikana kwa urahisi kwa wakulima, *SUMA JKT* imepata mkopo wa riba nafuu kutoka nchi ya India, kwa ajili ya kununua na

kusambaza matrekta na 'power tiller'. Uunganishaji wa matrekta hayo utafanywa kwa kushirikiana na Shirika la Nyumbu.

Masuala Mtambuka Utawala Bora. Kupitia Programu ya uboreshaji wa Utumishi wa Umma Awamu ya II, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imezindua Mkataba wa Huduma kwa Mteja *(Client Service Charter)* mwezi Februari, 2010. Aidha, chini ya Programu hiyo Wizara imeandaa na kukamilisha Mpango wa Mafunzo kwa Watumishi wa Umma ambao utaanza kutumika mwaka 2010/2011. Pia, Wizara ipo kwenye mchakato wa kukamilisha na kuweka mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji wa Matokeo *(Monitoring and Evaluation System)* ambao utawezesha upimaji wa matokeo ya utekelezaji wa Mpango Mkakati.

Katika mwaka 2009/2010 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliandaa mikutano ya Baraza la Wafanyakazi sambamba na kuunda na kuzindua Baraza jipya la Wafanyakazi mwezi Februari, 2010 baada ya Baraza la awali kumaliza muda wake kwa mujibu wa Sheria. Aidha, Wizara imewawezesha wafanyakazi wake kushiriki kwenye sherehe za kitaifa yakiwemo Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka 2009 ambapo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilipata ushindi wa tatu wa Banda Bora *(Best Pavilion Award).* Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wananchi wote waliotembelea mabanda ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kutoa maoni yao ambayo yamezingatiwa kwa kuboresha maonyesho ya mwaka 2010 yaliyofanyika Mwanza hivi karibuni. Aidha, naendelea kuwaalika wananchi kujitokeza kwa wingi kutembelea mabanda yetu kila maonyesho haya yanapofanyika ili kuona bidhaa zinazotengenezwa na kupata maelezo kuhusu huduma zinazotolewa na taasisi za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, Mapambano Dhidi ya Janga la UKIMWI. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendeleza juhudi za kupambana na janga la UKIMWI kwa kuendelea kuwaelimisha Wanajeshi na Watumishi wa Umma namna ya kujikinga na maambukizi ya janga hili. Kamati mbalimbali za ushauri zilizoundwa vikosini zimekuwa zikitekeleza jukumu hilo ili kukabiliana na janga hili.

Waathirika hupata dawa za kurefusha maisha (ARVs) ambazo hutolewa bure kupitia vituo vya *"Care and Treatment Centres"* vilivyoko katika Hospitali Kuu ya Jeshi – Lugalo, Hospitali za Kanda za Jeshi Mbeya, Mwanza, Bububu - Zanzibar, Mazao Morogoro, *TMA* - Arusha, Mirambo – Tabora, Luhuwiko - Ruvuma na Nyumbu - Pwani. Vituo vyote hivyo hutoa huduma hizo pia kwa wanajamii wote wanaoishi maeneo ya karibu.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, Mapambano Dhidi ya Rushwa. Rushwa ni adui mkubwa wa haki. Kwa kutambua hilo, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendeleza mapambano dhidi ya rushwa kwa kuunda Kamati za Maadili sehemu za kazi ambazo hufuatilia uadilifu wa Wanajeshi na Watumishi katika maeneo yao ya kazi. Aidha, Kamati hizi huwakumbusha na kuwasisitiza wahusika juu ya kufanya kazi kwa uwazi, uadilifu na kuzingatia taratibu, kanuni na sheria zilizopo. Msisitizo maalum

umewekwa kwenye vitengo vya ununuzi wa vifaa na utoaji huduma ili kuzuia mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, Utunzaji wa Mazingira. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kupitia Kamati yake ya Mazingira imeendelea kuratibu utekelezaji wa sheria ya mazingira ya mwaka 2004 katika Wizara na Taasisi zake.

Kwa mwaka 2009/2010 Wizara imeendesha vikao vya Kamati ya Mazingira na kutoa mafunzo ya kujenga uelewa wa utunzaji wa mazingira kwa watumishi wa Umma na Wanajeshi pamoja na kuadhimisha kwa vitendo Siku ya Mazingira Duniani tarehe 5 Juni, 2010 katika Makao Makuu ya Wizara. Aidha, mafunzo ya muda mfupi kwa wanakamati na Wakufunzi wa vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa yametolewa sambamba na kuboresha mitaala ya mafunzo ya vijana hao kuhusu masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, Michezo. Kwa lengo la kusaidia kuimarisha afya, akili na ukakamavu kwa wanajeshi na watumishi wa umma, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuipa kipaumbele cha pekee michezo ya aina mbalimbali. Wizara imekuwa ikishiriki katika mashindano ya michezo mbalimbali inayoandaliwa na mashirikisho ya michezo hapa nchini kama vile SHIMIWI, Mei Mosi na Bonanza. Wizara imeendelea kuwezesha Wanajeshi, vijana wa JKT na Watumishi wa Umma kushiriki katika mashindano ya michezo kwani michezo hujenga umoja miongoni mwao.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, mafanikio ya utekelezaji wa malengo ya Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kwa kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010. Baada ya kueleza utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2009/2010 ningependa kueleza kwa kifupi mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kipindi cha 2005 – 2010. Kwa kipindi chote cha mwaka 2005 hadi 2010 mipango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Taifa imelenga na kutoa kipaumbele katika kutekeleza Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kuhusu ulinzi wa Nchi yetu. Kwa kuwa mwaka 2010/2011 ni wa mwisho wa utekelezaji wa Ilani hiyo, naomba kuchukua fursa hii kulieleza Bunge lako Tukufu mafanikio yaliyopatikana:-

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, Kuwa na Jeshi dogo la Ulinzi wa Nchi lenye taaluma, zana na vifaa vya kisasa. Pamoja na uwezo mdogo wa kifedha uliopo ikilinganishwa na mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya shughuli za kijeshi, Serikali imeendelea kutekeleza mkakati wa kuimarisha Jeshi la Wananchi kivifaa hatua kwa hatua. Katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010 Serikali imelipatia Jeshi la Wananchi vifaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na magari, helikopta na boti ziendazo kasi kwa ajili ya majukumu ya usafiri, usafirishaji, uokoaji na doria katika ukanda wetu wa Bahari ya Hindi na maeneo ya maziwa. Aidha, Serikali imelipatia Jeshi la Wananchi vifaa na mitambo kwa ajili ya utafiti na uendelezaji wa teknolojia, ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya viwanda na vituo vinavyofanya utafiti.

Pia, Serikali imepokea vifaa, zana na mitambo ya kijeshi kutoka Serikali za Nchi rafiki hususan Jamhuri ya Watu wa China na Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa Jeshi la letu. Hatua hizi kwa ujumla zimeendelea kuboresha uwezo wa Jeshi katika kutekeleza majukumu yake ya msingi ya ulinzi wa mipaka ya Nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, vifaa na zana zinazonunuliwa au kupokelewa kama msaada zinahitaji hifadhi salama na matunzo endelevu. Hivyo, jukumu lingine lililotekelezwa na Serikali katika kipindi hiki ni ukarabati wa maghala makubwa na madogo ya kuhifadhia zana, risasi, mabomu, milipuko na vifaa vingine. Serikali imeendelea kuimarisha mfumo wa matengenezo ya vifaa na zana jeshini kwa kufanya ukarabati na kuimarisha karakana kivifaa na kutoa mafunzo kwa watendaji.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, mkakati wa kuimarisha Jeshi la Wananchi kivifaa umetekelezwa sambamba na mkakati wa kuwapatia wanajeshi mafunzo ya kinadharia na vitendo ili kuwaendeleza katika fani zao. Mafunzo hayo yameendelea kutolewa katika shule na vyuo vya kijeshi hapa nchini na Nchi rafiki za Canada, India, Jamhuri ya Watu wa China, Marekani, Bangladesh, Indonesia, Misri, Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani, Ufaransa, Uingereza, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na *SADC*. Mafunzo hayo yamelenga kuwapatia wanajeshi wetu mbinu mpya za kimapigano na kuwajengea uwezo wa kutumia vifaa, zana na teknolojia ya kisasa kivita.

Aidha, mafunzo hayo yamelenga kuwajengea wanajeshi uwezo wa kushiriki katika majukumu ya Kitaifa na Kimataifa, hususan kukabiliana na majanga hapa nchini na kushiriki katika Ulinzi wa Amani kwenye nchi zenye migogoro. Ushiriki wa Jeshi letu katika majanga yaliyotokea hapa nchini ni kielelezo cha uwezo na utayari wa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, mkakati wa kuwapatia mafunzo wanajeshi umetekelezwa sawia na uboreshaji wa shule na vyuo vya kijeshi hapa nchini ili viendane na wakati kwa kuwa na hadhi ya kimataifa. Uboreshaji huo umehusisha ukarabati, umaliziaji wa viporo na ujenzi mpya wa majengo na miundombinu ya maji safi, maji taka na umeme. Shule na vyuo hivyo ni pamoja na *Tanzania Military Academy,* Shule ya Kijeshi ya Ulinzi wa Anga, Shule ya Mafunzo ya Infantria, Shule ya Mafunzo ya Huduma, Chuo cha Ukamanda na Unadhimu, *National Defence College* na *High Commander Defence College.*

Uboreshaji wa baadhi ya shule na vyuo hivi umefanywa kwa ushirikiano na Serikali za Nchi rafiki, hususan Chuo cha Ukamanda na Unadhimu kwa kushirikiana na Serikali ya Muungano wa Falme za Kiarabu na *National Defence College* kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, kulijengea Jeshi la Wananchi Mazingira Mazuri ya Kufanyia Kazi na Kuendelea Kutatua Matatizo ya Makazi na Maslahi ya Wanajeshi. Ili kujenga mazingira bora ya makazi, Serikali imejenga nyumba 366 kwa ajili ya askari katika makambi yaliyoko Arusha, Dar es Salaam, Iringa na Pemba. Aidha, Serikali imekarabati, kumalizia ujenzi au kujenga upya mabweni ya askari, mabwalo, ofisi,

madarasa, zahanati/vituo vya afya, na miundombinu ya maji safi, majitaka, umeme na mawasiliano katika makambi mbalimbali ya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, Serikali imeendeleza azma yake ya kuboresha maslahi ya wanajeshi. Katika kipindi hiki Stahili za wanajeshi hususan mishahara, posho ya chakula, likizo na sare zimeboreshwa na kutolewa kwa wakati katika viwango vya kuridhisha. Kwa mfano kiwango cha posho ya chakula kwa siku kwa mwanajeshi kimeongezwa kutoka shilingi 2,500/- mwaka 2004 hadi shilingi 5,000/- kuanzia mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, kuendeleza, Ufufuaji wa Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa. Serikali imeendeleza juhudi za kufufua na kuimarisha jukumu la kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya ukamamavu, uzalendo na umoja wa kitaifa pamoja na kuwaandaa katika uzalishaji mali na ufundi kupitia Jeshi la KujengaTaifa. Makambi 15 ya Jeshi la Kujenga Taifa ya Chita, Bulombora, Itende, Kanembwa, Mafinga, Makutopora, Maramba, Mgambo, Mgulani, Mlale, Masange, Nachingwea, Oljoro, Ruvu na Rwamkoma majengo yake na miundombinu imefanyiwa ukarabati mkubwa kwa kumalizia ujenzi au kujengwa upya. Hatua hiyo imewezesha makambi hayo kuwa na uwezo wa kuchukua vijana 17,978 kwa pamoja kwa wakati mmoja ikilinganishwa na uwezo wa vijana 2,000 mwaka 2001 wakati mpango wa ufufuaji wa shughuli za Jeshi la Kujenga Taifa ulipoanza baada ya kusitishwa mwaka 1994. Hadi hivi sasa jumla ya vijana 27,387 wamepata fursa ya kupitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa utaraibu wa kujitolea.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali kufufua mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wa kujitolea, Serikali bado ina lengo la kuwaita vijana kupata mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha JKT. Utekelezaji wa azma hiyo umekabiliwa na changamoto kubwa za ongezeko kubwa la idadi ya vijana wanaotakiwa kujiunga na mafunzo hayo kila mwaka ukilinganisha na uwezo mdogo wa makambi na miundombinu husika yanayohitajika kuwachukua vijana wote wa mujibu wa Sheria. Katika mwaka 2010/11 Serikali itakamilisha maandalizi na utaratibu wa kuanza kuwachukua vijana kwa mujibu wa Sheria na inatarajia kuanza rasmi kuwachukua vijana hao kwa mwaka 2011/12.

Zoezi hili litahusisha upanuzi wa majengo katika makambi ya mafunzo, ununuzi wa vifaa na kuandaa utaratibu wa kuwachukua vijana kwa kulingana uwezo wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, mpango na Bajeti ya mwaka 2010/2011. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika mwaka 2010/2011 imelenga kuimarisha utendaji na ufanisi wa Jeshi la Wananchi katika kulinda uhuru na hadhi ya nchi na kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, fedha zilizotengwa katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 ni kwa ajili ya utekelezaji wa mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Kuboresha uwezo wa Jeshi kiutendaji kwa kulipatia zana za kisasa na mafunzo.

(b)Kutekeleza miradi muhimu ya maendeleo ikiwemo ya maboresho ya kiwanda cha Shirika la Mzinga, uimarishaji wa miundombinu ya Shirika la Nyumbu, uboreshaji wa mtandao wa mawasiliano ya kipekee jeshini, upimaji wa maeneo ya jeshi na ulipaji fidia kwa maeneo yaliyochukuliwa kwa ajili ya matumizi ya jeshi na urejeshaji wa mkopo wa *NSSF* uliotumika katika ujenzi wa nyumba za kuishi wanajeshi.

(c )Ukarabati, ukamilishaji wa viporo na ujenzi wa majengo katika makambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ikiwa ni pamoja na 'National Defence College', Chuo cha Ukamanda na Unadhimu, kukamilisha ujenzi wa shule ya Kijeshi ya Ulinzi wa Anga (SKUA) – Tanga, mnara wa kuongozea ndege – Ngerengere, ujenzi wa mabweni 20 ya wanafunzi wa kijeshi, ukamilishaji wa nyumba za makazi ya askari huko Pemba na maeneo mengine. Kazi ambayo pia inajumuisha ukarabati wa miundombinu ya maji safi, majitaka na umeme katika maeneo hayo.

(d)Ujenzi wa mabweni ya askari na vijana, nyumba za maofisa, majengo ya ofisi za Makao Makuu ya JKT na ukamilishaji wa mfumo wa maji safi na maji taka kwenye makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa.

(e)Kutekeleza azma ya Serikali ya Kilimo Kwanza kwa kuongeza mashamba ya mbegu bora na uzalishaji wa zana za kilimo katika mashirika ya Nyumbu na Mzinga.

(f) Kulima ekari 2,389 za mazao mbalimbali na mbegu bora na kuunganisha na kuuza matrekta 1,700 ili kutekeleza Kauli Mbiu ya "KILIMO KWANZA"

(g) Kulipia mahitaji na huduma muhimu yakiwemo mafuta, vilainisho, umeme, maji na simu ambazo ni muhimu katika utekelezaji wa majukumu.

(h) Kulipa stahili za wanajeshi, Vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na watumishi wa Umma ikiwemo, mishahara, posho za kisheria, chakula kwa ajili ya wanajeshi, matibabu, maziko na likizo.

(i) Kuimarisha ushirikiano baina ya nchi yetu na nchi nyingine duniani katika nyanja za kijeshi na ulinzi kupitia ushirikiano kati ya nchi na nchi, ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

(j) Kuimarisha shughuli za uzalishaji mali za SUMAJKT ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuanzisha kilimo kikubwa cha mazao mbalimbali -Tanga, Arusha na Morogoro.

(ii)Kuanzisha viwanda vya kati 4 vya kusindika vyakula, nguo, samani, kokoto na matofali.

(iii) Kuingia katika Kandarasi mbalimbali za majengo, barabara na madaraja.

(iv)Kuwekeza katika miradi ya kuendesha Hotel – Mbweni, Kunduchi na Masaki (Dar es Salaam) na Makuyuni (Arusha)

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, shukrani. Kabla ya kumaliza Hotuba yangu naomba nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioniwezesha kuongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tangu niteuliwe kushika wadhifa huu mwaka 2008. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote waliochangia kufanikisha maandalizi ya mapendekezo ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2010/2011 ninayoiwasilisha leo hapa Bungeni. Naomba kutoa shukrani za kipekee kwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani aliyonayo juu yangu kwa kunikabidhi madaraka ya kuongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yenye dhamana nzito ya kulinda uhuru na hadhi ya Nchi yetu. Ni imani yangu kwamba katika kipindi hiki cha kuongoza Wizara hii nimeweza kufanikisha matarajio aliyokuwa nayo Mheshimiwa Rais juu yangu katika kutekeleza majukumu aliyonikabidhi.

Namshukuru sana. Vile vile, kwa niaba ya Makamanda, Maafisa, Wapiganaji na Watumishi wa Umma wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kumshukuru Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuendelea kulijali Jeshi la Wananchi kihuduma na kivifaa ili liweze kutimiza wajibu wake wa kulinda nchi yetu. Naomba nimshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.), na Mawaziri wote kwa msaada na ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu yangu wakati wote nikiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa mara nyingine tena napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Wilson Masilingi (Mb.) na Wajumbe wa Kamati hiyo kwa msaada na ushirikiano walioutoa kwangu wakati wote wa kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, mafanikio yangu ni matokeo ya ushirikiano mzuri niliopata kutoka kwa wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Naomba kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwao nikianzia na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi (Mb.), Katibu Mkuu, Bwana Andrew S. Nyumayo, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Davis A. Mwamunyange, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Luteni Jenerali Abdulrahaman A. Shimbo, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Samwel N. Kitundu, Makamanda, Maafisa, Wapiganaji na Watumishi wa Umma. Wote ninawashukuru kwa ushirikiano mkubwa walionipa na kwa

ushauri wao ulio makini na wenye uaminifu. Nawashukuru sana. Naomba pia kuwashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wao wanaotoa kwa Jeshi la Wananchi katika kulinda Nchi yetu. Kwa namna ya pekee, naomba kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwahani kwa ushirikiano wao walionipa katika kipindi chote cha miaka mitano tangu wanichague kuwawakilisha hapa Bungeni. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Kwa niaba ya Serikali naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali za Nchi mbalimbali kwa ushirikiano wao na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Napenda pia kumshukuru Mpigachapa Mkuu wa Serikali na Watumishi waliopo chini yake kwa kuichapa na kuikamilisha Hotuba hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi, Mawaziri wenzangu na Wabunge wote kwa ushirikiano walionipa ndani na nje ya Bunge wakati wote nikiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Aidha, nawatakia kila la kheri na fanaka kwenye uchaguzi mkuu ujao na ni matumaini yangu kuwa tutakutana tena hapa Bungeni katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, makadirio ya fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2010/2011. Ili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iweze kutekeleza malengo yake iliyojiwekea kwa mwaka 2010/2011, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha jumla ya Shilingi 621,493,667,515.00 ambazo kati yake Shilingi 461,273,688,000.00 zitatumika kwa ajili ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 160,219,979,515.00 ni Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, Shilingi 160,121,984,000.00 ni fedha za Ndani na Shilingi 97,995,515.00 ni fedha za Nje.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, fedha hizi zimegawanywa katika mafungu matatu kama ifuatavyo:-

**(a) Fungu 38 - Jeshi la Wananchi wa Tanzania**

(i) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida Shilingi 358,214,108,000.00

(ii) Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo Shilingi 18,454,334,000.00a.

**(b) Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa**

(i) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida Shilingi 88,469,947,000.00.

(ii) Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo Shilingi 12,649,883,000.00a.

**(c) Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

(i) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida Shilingi 14,589,633,000.00

(ii) Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo Shilingi 129,115,762,515.00 ambazo kati yake Shilingi 129,017,767,000.00 ni fedha za Ndani na Shilingi 97,995,515.00 ni fedha za Nje.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, naomba kutoa Hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2010/2011 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa mapema leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa muda naomba maelezo ya hotuba ya bajeti nitakayoitoa hapa, pamoja na hotuba nzima ya Bajeti iliyopo kwenye kitabu changu cha Bajeti zote ziingie kwenye kumbukumbu tasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, awali ya yote naomba kutumia fursa hii kuwapa pole Askari Polisi G.2008 PC Abbas na G.4882 PC Kelvin pamoja na Ndugu Erasto Magere na Saada Ngulilo watumishi wa NMB kwa kujeruhiswa na majambazi katika tukio la uporaji lililofanyika tarehe 23 Juni, 2010 kwenye Tawi la Benki la NMB Maswa. Napenda pia kuwapongeza Askari hao kwa moyo wa ujasiri kwa kupambana na majambazi saba wenye silaha kali nakufanikiwa kupunguza madhara ya tukio hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuungana na Wabunge wenzangu katika kutoa rambirambi zangu kwa familia na wananchi wa Jimbo la Ruangwa ambalo katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 limempoteza Mbunge mwenzetu Mheshimiwa marehemu Sigifrid Selemani Ng'itu. Namwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapa pole wananchi wa Wilaya ya Kilosa Mkoani Morogoro pamoja na maeneo mengine nchini kutokana na mafuriko yaliyosababisha uharibifu mkubwa wa mali na miundombinu na kusababisha familia kadhaa kuishi katika makazi ya muda baada ya nyumba zao kuharibiwa. Aidha, natoa pole kwa wananchi wa

Wilaya ya Same Mkoani Kilimanjaro kwa kukumbwa na maporomoko ya ardhi yaliyosababisha watu kupoteza maisha, mali zao na uharibifu wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maafa mengi yametokea zikiwemo ajali za barabarani, majini na migodini ambazo zimeendelea kupoteza maisha ya wananchi. Nachukua nafasi hii kuwapa pole ndugu na jamaa wa marehemu na waathirika wote wa maafa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe binafsi, Naibu Naibu Spika, Wenyeviti wetu ndani ya Bunge na wale wa Kamati za Bunge pamoja na wasaidizi wao chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kusimamia uendeshaji wa shughuli za Bunge. Nawapongeza pia Wabunge wenzangu wote kwa michango yao ndani na nje ya Bunge ambayo imelenga kulinufaisha Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba zao walizozitoa mapema katika mkutano huu wa 20 wa Bunge ambazo pamoja na mambo mengine zimetoa mwelekeo wa kazi za Serikali, bajeti na hali ya uchumi kwa jumla kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuonyesha imani kwangu kwa kunipatia nafasi ya kutumikia Taifa langu katika nafasi mbalimbali katika Serikali ya awamu ya nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, dira ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kutoa huduma bora katika kudumisha amani, utulivu na umoja nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhima ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kulinda usalama wa raia na mali zao, kuhifadhi na kuwarekebisha wafungwa, kudhibiti uingiaji na utokaji nchini wa raia na wageni, kutoa huduma za zimamoto na uokoaji na kuwahudumia wakimbizi waliopo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 na utekelezaji wake. Katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina majukumu 13. Ningependa kueleza majukumu hayo pamoja na utekelezaji wake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kwanza ni kuimarisha usalama migodini. Jeshi la Polisi limeendelea kutoa ulinzi migodini kwa kufanya operesheni, misako na doria mbalimbali. Hatua nyingine iliyochukuliwa ni kuwa na makubaliano maalum ya ulinzi na migodi husika. Katika mwaka 2009/2010, Jeshi la Polisi limeingia makubaliano ya ulinzi na mgodi wa Barrick Gold na migodi mingine ya Buhemba na Williamson Diamond kuendelea kulindwa na detach maalum ya askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la pili ni kuliimarisha Jeshi la Polisi kwa kuliongezea utaalam na zana ili upelelezi wa kesi ukamilike haraka hivyo kupunguza muda wa mahabusu kukaa magerezani. Kama hatua ya utekelezaji wa jukumu hilo maofisa na askari 502 walishiriki katika mafunzo ya taaluma ya upelelezi. Mafunzo hayo yalitolewa kwa lengo la kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika upelelezi. Askari wapya 310 wamepatiwa mafunzo ya msingi ya upelelezi.

Aidha, mfumo umeimarishwa kwa kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji wa mashtaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na mwongozo wa wapelelezi nchini umeandaliwa kwa lengo la kuboresha shughuli za upelelezi wa makosa ya jinai kwa taasisi zote zinazojihusisha na upelelezi. Vile vile Maabara ya Uchunguzi imeendelea kuongezewa rasilimali watu wenye taaluma na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la tatu ni kuendelea kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani. Kutokana na jitihada mbalimbali za Serikali za kukarabati na kupanua magereza yaliyopo na kujenga mabweni ya wafungwa katika vituo mbalimbali, na kwa kutumia utaratibu wa Parole, kifungo cha nje, programu ya huduma kwa jamii na msamaha wa Rais utolewao wakati wa kuadhimisha sherehe za kitaifa, uwezo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu umeongezeka kwa asilimia 22 kutoka nafasi 22,669 mwaka 2006 hadi kufikia 27,653 hivi sasa. Hata hivyo, bado msongamano upo, na hatua mbalimbali za kupunguza zaidi msongamano zinaendelea kuchukuliwa. Tarehe 1 Aprili, 2010 kulikuwa na wahalifu 38,148 katika magereza yote nchini. Kati ya hao 19,146 walikuwa ni wafungwa, na 19,002 ni mahabusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Aprili, 2010 wafungwa 251 waliachiliwa kwa utaratibu wa Parole. Hata hivyo, idadi ya wafungwa wanaoachiliwa kwa utaratibu huu imeendelea kuwa ndogo kutokana na Sheria ya Bodi za Parole ya mwaka 1994 kutoruhusu wafungwa waliofanya makosa makubwa kuachiliwa chini ya utaratibu huu. Hii inatokana na makosa yao kuwa na hisia kali na kutokubalika kwao katika jamii. Ili sheria hii iweze kutumika kikamilifu, sera ya kifungo inatakiwa ipitiwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya wafungwa 7,236 walifaidika na msamaha wa Rais ambapo wafungwa 4,135 walifaidika na msamaha uliotolewa tarehe 9 Desemba, 2009 wakati wa sherehe za kuadhimisha miaka 48 ya Uhuru na wengine 3,101 waliachiliwa tarehe 26 Aprili, 2010 wakati wa kuadhimisha sherehe za miaka 46 ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Aprili, 2010 jumla ya wafungwa 778 walikuwa wanatumikia kifungo cha nje kwa kutumia kanuni za kifungo cha nje za mwaka 1968. Vile vile wafungwa 412 waliachiliwa na Mahakama ili kutumikia kifungo cha nje chini ya Sheria ya Huduma kwa Jamii. Hivi sasa programu ya

huduma kwa jamii inatumika katika Mikoa 12 ya Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Dodoma, Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Iringa, Mara, Kagera na Shinyanga. Tangu programu hii ilipoanza kutumika mwaka 2005 jumla ya wafungwa 1,591 wamefaidika nayo hadi kufikia mwezi Aprili, 2010. Kati yao wanaume ni 1,146 na wanawake 445. Wafungwa hawa wamekuwa wakifanya kazi kwenye taasisi mbalimbali za umma bila ya malipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la nne ni kushughulikia kwa ufanisi malalamiko ya wananchi ya kero ya rushwa ndani ya Jeshi la Polisi. Jumla ya malalamiko 31 ya wananchi ya kero ya rushwa yameshughulikiwa. Askari 19 wamefukuzwa kazi, watatu kesi zao zinaendelea katika Mahakama za jinai na wengine tisa uchunguzi unaendelea. Aidha, Jeshi la Polisi limeanzisha utaratibu wa kuwazawadia askari wote watakaokataa kupokea rushwa katika utendaji wao wa kazi. Vile vile Idara maalum inayoshughulikia malalamiko ya wananchi dhidi ya vyombo vya Wizara likiwemo Jeshi la Polisi imefanikiwa kuanza mchakato wa kutunga sheria ili kuipa nguvu ya kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la tano ni kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuviongezea uwezo kitaaluma na zana za kisasa. Wizara imeweza kutoa mafunzo katika taaluma za upelelezi, intelijensia, usimamizi wa kumbukumbu za uhalifu, uchunguzi wa makosa yahusuyo fedha haramu, uendeshaji wa magereza, shughuli za zimamoto na uokoaji na uhamiaji. Mafunzo hayo yametolewa kwa askari Polisi 8,948, Magereza 2,052, Zimamoto na Uokoaji 267 na Uhamiaji 364.

Kwa upande wa zana, Wizara imeweza kutumia bajeti yake ya mwaka 2009/2010 na kulipia magari 91, kati ya hayo magari 79 ni kwa ajili ya Polisi na 12 Magereza. Aidha, magari 260 yatanunuliwa kwa udhamini wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la sita ni kuwahamasisha wananchi kushiriki katika ulinzi wa maeneo yao na kuhakikisha usalama wao na mali zao. Katika kutekeleza jukumu hili, Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Wakuu wa Polisi wa Wilaya na vituo wameendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu dhana ya Polisi Jamii katika maeneo yao.

Kitengo cha Polisi Jamii Makao Makuu ya Jeshi la Polisi kimesambaza machapisho mbalimbali kama vile vitabu vya Mpango wa Ulinzi Jirani, Safiri Salama Tanzania na Falsafa ya Polisi Jamii/Ulinzi Shirikishi, kwa lengo la kuhamasisha wananchi kushiriki katika ulinzi. Vikundi 2,632 vya ulinzi shirikishi vimeanzishwa tangu mwaka 2005. Elimu ya kuhamasisha wananchi inaendelea kutolewa kupitia vipindi vya redio na runinga. Nashukuru kwa ushirikiano na moyo unaotolewa na wananchi katika kuanzisha vikundi vya kujilinda katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la saba la Wizara katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ni kuvijengea mazingira mazuri vyombo vya ulinzi na usalama, na kutatua matatizo ya makazi na maslahi ya watumishi wake.

Katika mwaka 2009/2010 Wizara imekamilisha ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Dar es Salaam na Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Dodoma, Tabora, Morogoro, Kilimanjaro na Mbeya. Kupitia udhamini wa Serikali, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* umekamilisha awamu ya kwanza ya mradi wa ujenzi wa nyumba za askari Polisi Dar es Salaam Kambi ya Polisi Barabara ya Kilwa na katika kambi za Ziwani na Limbani Zanzibar, ambapo jumla ya familia za askari 240 zimepata makazi. Hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na kukamilisha kanuni za fidia kwa askari watakaoumia wakiwa kazini, mapendekezo ya viwango vipya vya mishahara ya askari na kuandaa orodha ya bidhaa zitakazotumika katika maduka yenye msamaha wa kodi *(duty free shops)* kwa ajili ya kutolewa katika Tangazo la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la nane ni kuongeza uwezo wa Taifa wa kupambana na ujambazi na kuzagaa kwa silaha ndogondogo. Katika kukabiliana na uhalifu ukiwemo ujambazi, Jeshi la Polisi limeendelea kuimarisha Kitengo cha Intelijensia kwa kukipatia mafunzo na vitendea kazi na kukipanua hadi ngazi ya Mkoa na Wilaya. Jumla ya askari 72 wamepatiwa mafunzo. Kikosi Kazi cha Taifa kilichoundwa mwaka 2006 kukabiliana na hali ya kutisha ya ujambazi iliyokuwepo wakati huo, kimeendelea kukabiliana na uhalifu kwa kuendesha upelelezi wa matukio makubwa ya uhalifu na kufuatilia mwenendo wa uhalifu nchini na kuchukua hatua. Ninaishukuru Serikali kwa hatua inazochukua kukiwezesha Kikosi Kazi hiki katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Jeshi la Polisi limeendelea kuhakiki umiliki wa silaha ndogondogo ambapo katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Aprili, 2010 jumla ya silaha 150 zimehakikiwa na silaha 2,500 kumbukumbu zake zimeingizwa kwenye mfumo wa kutunza kumbukumbu *(database)* wa silaha ambao ulianzishwa mwaka 2005. Hadi sasa jumla ya silaha 80,150 zimehakikiwa na 62,650 kumbukumbu zake zimeingizwa kwenye mfumo huo. Jeshi la Polisi liliendesha misako na operesheni za kusaka silaha, na silaha 375 zilikamatwa kwa kumilikiwa kinyume cha sheria. Zoezi la uhakiki wa silaha ni la kudumu. Aidha, katika kuadhimisha Siku ya Amani Afrika, iliyofanyika tarehe 25/5/2010 jumla ya silaha haramu 2,565 ziliteketezwa kwa moto Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la tisa ni kuandaa Sera ya Uhamiaji yenye kubainisha masuala ya uraia na ukaazi katika mazingira ya kuelekea ushirikiano katika *SADC* na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mchakato wa kuandaa sera hii ulikwishaanza mwaka 2007 na rasimu yake kujadiliwa na wadau mbalimbali. Wadau walishauri kuwa ni vyema majadiliano yanayoendelea katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu uhuru wa watu wa kuingia na kutoka katika nchi wanachama wa Jumuiya na majadiliano ya UNIVISA katika Jumuiya ya *SADC* yazingatiwe katika sera hiyo. Majadiliano hayo bado yanaendelea. Hivyo, sera hii itakamilishwa baada ya majadiliano hayo kuhitimishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kumi ni kuanzisha mfumo wa Taifa wa utambuzi na usajili wa watu na kutoa vitambulisho vya Taifa. Ili vitambulisho vya Taifa viweze kutolewa, panahitajika kujenga mfumo wa Taifa wa utambuzi na usajili wa watu. Kimsingi kadi ni matokeo tu ya mfumo mzima wa utambuzi na usajili wa watu. Hivi sasa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa inaendelea na jitihada za kujenga uelewa wa pamoja kuhusiana na dhana ya mfumo huu. Elimu kwa umma imeanza kutolewa kwa

Waheshimiwa Wabunge, Majaji, Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa, na Waandishi na Wahariri wa vyombo vya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2009/2010 nililiarifu Bunge lako Tukufu kwamba tungeanza na miradi ya majaribio kwa matarajio kwamba Mkandarasi angekuwa amepatikana katika mwaka 2009/2010.

Hata hivyo, matarajio ni kumpata Mkandarasi mwezi Desemba, 2010 kwani tayari Serikali imeingia mkataba na Mshauri Mwelekezi mwezi Januari, 2010 na mwezi Aprili, 2010 ameanza kazi ya kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa kujenga mfumo wa Taifa wa utambuzi na usajili wa watu. Matarajio ni kuanza awamu ya kwanza ya kutoa vitambulisho ifikapo mwezi Agosti, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imeanza mchakato wa kujaza nafasi 38 za watendaji katika kada mbalimbali kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma na kulingana na muundo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, malengo ya mwaka 2010/2011 ni kufungua Ofisi za utambuzi na usajili katika Wilaya 20, kujenga jengo la *Identification Management Centre* Jijini Dar es Salaam, kuweka mfumo wa mawasiliano ya elektroniki kati ya Ofisi Kuu na Ofisi za Wilaya tano za majaribio, kujenga Kituo cha Taifa cha kuhifadhi taarifa *National Data Centre,* kuendeleza mchakato wa marekebisho ya Sheria Na. 11 ya Utambuzi na Usajili wa Watu ya mwaka 1986, kuajiri watumishi wapya 159 na kununua magari 20.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kumi na moja ni kuongeza kasi ya kuwarejesha wakimbizi kwao. Jumla ya wakimbizi 285,507 walikuwepo nchini mwezi Julai, 2009. Katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Aprili, 2010 jumla ya wakimbizi 162,156 walipatiwa uraia wa Tanzania na wengine 16,080 walirejea kwao kwa hiari. Kati yao, wakimbizi 14,943 wamerejea nchini Burundi, na 1,137 Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC).* Hata hivyo, kasi ya urejeaji sio ya kuridhisha kutokana na machafuko yanayoendelea maeneo ya Mashariki mwa DRC wanakotokea wakimbizi wa DRC walioko nchini.

Mheshimiwa Spika, tangu zoezi la kuwarejesha wakimbizi katika nchi zao za asili lilipozinduliwa mwaka 2002 kwa wakimbizi wa Burundi na mwaka 2005 kwa wakimbizi wa DRC, hadi kufikia mwezi Aprili, 2010 jumla ya wakimbizi 568,322 wamerejea kwao. Wakimbizi 501,682 walirejea nchini Burundi ambapo 417,164 walirejea kwa msaada wa Shirika la UNHCR na wengine 84,518 kwa kujitegemea wenyewe. Aidha, wakimbizi 66,640 walirejea nchini DRC.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kumi na mbili ni kuendeleza kampeni ya upandaji miti. Katika mwaka 2009/2010 Jeshi la Magereza liliendelea kuboresha mazingira kwa kupanda miti katika maeneo yake kote nchini. Jumla ya miti 450,000 ilipandwa kwenye eneo la hekta 400 katika Magereza ya Ushora, Malya, Songwe, Kasulu, Isupilo, Mgagao, Bariadi, Wami Kuu, Idete, Songea, Mollo, Mvuti, Msalato na Karanga. Lengo la mwaka

2010/2011 ni kupanda miti 450,000 katika eneo la hekta 400 katika Magereza ya Isupilo, Mgagao, Njombe, Malya, Ushora, Songea, Bariadi na Mollo. Jeshi la Magereza pia linasimamia mradi wa kupanda miti katika hekta 1,214 unaofadhiliwa na *NORAD* kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mradi huu unatekelezwa katika Magereza ya Isupilo, Msalato na Idete ambapo mpaka sasa jumla ya hekta 603 zimepandwa miti 670,950. Upo pia mradi wa upandaji miti unaofadhiliwa na UNDP ukiwa na misitu yenye ukubwa wa hekta 353 katika Magereza ya Bariadi na Malya Mkoani Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, tarehe 1 Aprili siku ya upandaji miti kitaifa, jumla ya miti 150,000 ilipandwa katika baadhi ya maeneo yaliyokuwa yamepata mvua. Aidha, katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika tarehe 5 Juni 2010 Wilayani Bahi – Dodoma, Jeshi la Magereza liliweza kupata zawadi ya ushindi wa kwanza kutokana na upandaji wa miti, uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji uliofanyika kwenye eneo la Gereza Karanga – Moshi.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kumi na tatu na la mwisho la Wizara katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 ni kuendeleza vita dhidi ya dawa za kulevya ili kuwakinga watoto wasiathirike na dawa hizo.

Tatizo la dawa za kulevya limeendelea kuwa changamoto siyo kwa nchi yetu tu, bali kwa nchi nyingi duniani. Utandawazi, kukua kwa sayansi na teknolojia, kuongezeka kwa maingiliano ya watu duniani na upana wa mipaka ya nchi yetu vyote vimechangia hali hii. Kati ya Julai, 2009 hadi Aprili, 2010 Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola lilikamata watuhumiwa 740 na kilo 122 na gramu 760 za dawa za kulevya za viwandani. Kilo 188,994 za bhangi na kilo 798 za mirungi vile vile zilikamatwa, na watuhumiwa 8,429 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani. Jumla ya ekari 190 za mashamba ya bhangi ziliharibiwa katika Mkoa wa Tanga na ule wa Kipolisi wa Tarime/Rorya.

Mheshimiwa Spika, Kikosi Kazi cha Taifa kinachodhibiti biashara haramu ya dawa za kulevya kwa kushirikiana na *Interpol* kiliwakamata watuhumiwa sita na kilogramu 95 za dawa za kulevya za viwandani aina ya heroin inayokadiriwa kuwa na thamani ya zaidi ya shilingi 25 bilioni. Kiasi hicho ni kati ya kilo 122 zilizokamatwa katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Aprili, 2010. Hili ni tukio kubwa na lilitokea tarehe 8 Machi, 2010 katika Kijiji cha Kabuku Wilayani Handeni Mkoani Tanga. Kiasi hiki ni kikubwa kukamatwa nchini na kingeleta madhara makubwa kwa nguvu kazi ya Taifa kama kingefanikiwa kuingia katika soko. Washtakiwa wote wamefikishwa katika Mahakama Kuu Jijini Tanga.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Usalama Nchini na Changamoto zilizopo: Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ulinzi na usalama. Aidha, ushauri uliotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama umesaidia sana katika kuimarisha utendaji wa shughuli za Wizara. Mheshimiwa Spika, tathmini ya hali ya usalama nchini inatokana na takwimu za taarifa za vyombo vya dola. Kwa ujumla hali ya amani na utulivu nchini imeendelea kuwa ya kuridhisha licha ya kuwepo kwa baadhi ya

makosa kama vile mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi ambayo yalionekana kuleta hisia kali kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuvishukuru vyombo vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yaani Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji kwa ushirikiano wao na vyombo vingine vya dola kwa kutoa mchango mkubwa katika kudumisha amani na utulivu nchini katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010 pamoja na changamoto zinazowakabili zikiwemo bajeti isiyokidhi mahitaji, kuongezeka kwa mbinu za uhalifu, upungufu wa askari, uhaba wa vitendea kazi, uhaba na uduni wa makazi na ofisi, msongamano magerezani, majanga mbalimbali na uhamiaji haramu.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo zinaonyesha makosa ya jinai makubwa na madogo 567,288 yaliripotiwa katika Vituo vya Polisi nchini katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2009 ikilinganishwa na makosa 506,030 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2008. Idadi ya makosa imeongezeka kwa makosa 61,258 sawa na asilimia 12.1. Jeshi la Polisi limeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na uhalifu zikiwemo kuendesha mafunzo ya utayari kwa maofisa na askari, kuongeza nguvu ya rasilimali watu katika Mikoa yenye upungufu wa askari mfano Kagera, Mara, Kigoma, Rukwa na Tabora, kufanya doria za kutambua maficho ya wahalifu na kuwashirikisha wadau mbalimbali katika kukabiliana na uhalifu kupitia Polisi Jamii/Ulinzi Shirikishi, kubadili mwenendo wa utendaji kazi wa Makamanda na askari, kuimarisha mahusiano baina ya taasisi na vyombo vingine vya dola kwa kubadilishana taarifa za kiintelijensia na kufanya doria za pamoja kati ya Jeshi la Polisi, TRA, EWURA, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi lina upungufu mkubwa wa nguvu kazi kwani idadi inayokubalika kimataifa ni askari mmoja kwa watu 450 (1:450), nchi jirani ya Kenya ina uwiano wa askari mmoja kwa watu 821 (1:821), Tanzania ni askari mmoja kwa watu 1,300 (1:1,300). Hali hii inafanya maeneo mengine kutofikiwa na huduma ya Polisi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makosa ya usalama barabarani, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2009 makosa makubwa na madogo ya usalama barabarani yaliyoripotiwa Polisi ni 359,305 ikilinganishwa na makosa 229,451 yaliyoripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2008. Idadi ya makosa imeongezeka kwa makosa 129,854 sawa na asilimia 56.6.

Mheshimiwa Spika, Kikosi cha Polisi cha Usalama Barabarani kwa kushirikiana na wadau wengine kimeendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo operesheni za kukamata magari mabovu na kuyaondoa barabarani, kubaini mtandao wa kundi linalotoa leseni za udereva za bandia, kutoa elimu ya usalama barabarani kwenye mashule, ukaguzi wa leseni za udereva, magari na shule za udereva. Aidha, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu imeandaa mwongozo wa madereva wanafunzi na kuusambaza kwenye vyuo vya udereva.

Pamoja na hatua mbalimbali zinazochukuliwa, bado tatizo la ajali za barabarani ni kubwa na linahitaji nguvu za pamoja za wadau wote wa masuala ya usalama barabarani.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania lipo katika mchakato wa kubadilisha mfumo wa utoaji leseni za udereva ambapo mpango ni kuanza kutoa leseni za elektroniki awamu ya kwanza katika vituo tisa vya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mbeya, Dodoma, Mwanza, Ilala, Temeke na Kinondoni mwezi Septemba, 2010. Leseni hizi zitaongezeka kutoka aina nane za sasa hadi kufikia 14 na zitakuwa na fursa ya kuweka kumbukumbu sahihi za dereva mara anapokiuka Sheria za Usalama Barabarani. Aidha, hazitakuwa rahisi kugushiwa.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za kukabiliana na ajali za barabarani, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanza kuhakiki umiliki wa leseni ya udereva daraja la *C* kwa lengo la kubaki na wamiliki wale tu wenye sababu za msingi za kumiliki aina hiyo ya leseni. Leseni ya udereva daraja la *C* inaruhusu uendeshaji wa magari aina zote na pikipiki yakiwemo Mabasi ya Abiria. Wamiliki watakaoonekana hawana sababu za msingi za kuendelea kumiliki aina hiyo ya leseni watapatiwa leseni ya udereva daraja la *B au D*.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2009/2010 na Malengo ya Mwaka 2010/201:

Katika mwaka 2009/2010, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilipangiwa kukusanya maduhuli ya Serikali ya jumla ya shilingi 42 bilioni. Hadi tarehe 30 Aprili, 2010 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 30.9 bilioni sawa na asilimia 74 ya lengo la mwaka. Lengo la mwaka 2010/2011 ni kukusanya jumla ya shilingi 50 bilioni.

Mheshimiwa Spika, Matumizi: Katika mwaka 2009/2010 Wizara iliidhinishiwa shilingi 395 bilioni kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili 2010, shilingi 280 bilioni zilikuwa zimetolewa na HAZINA na shilingi 245 bilioni zimetumika sawa na asilimia 88 ya fedha zote zilizotolewa. Katika mwaka 2010/2011, Wizara imetengewa shilingi 446 bilioni kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.Katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Wizara imeweza kutumia fursa mbalimbali zilizojitokeza na kuweza kupata misaada ambapo imefanikiwa kupata msaada wa Serikali ya Marekani ya ujenzi wa Chuo cha Polisi Wanamaji kinachotarajiwa kujengwa Jijini Mwanza ambapo maandalizi ya awali yamekamilika na watatoa boti za doria 12 ambazo zitatolewa kwa awamu na msaada wa magari 107, pikipiki 104 na kompyuta 170 kutoka kwa wadau mbalimbali. Kati ya magari hayo, 79 ni kwa ajili ya udhibiti wa mipaka. Upatikanaji wa vitendea kazi hivi utasaidia jitihada za Serikali za kuvipatia vitendea kazi vya kisasa vyombo vya ulinzi na usalama. Wizara imeendelea kuzingatia suala la jinsia na anuai za jamii katika maeneo mbalimbali ya kazi ili kuona idadi ya watumishi wanawake katika utumishi wa Wizara inaongezeka kila wakati kulingana na majukumu na kazi zilizopo. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Wizara ilitoa mafunzo kwa askari/watumishi 11,173 ambapo

wanawake ni 1,723 sawa na asilimia 15.4. Pia Wizara iliwapandisha vyeo jumla ya askari/watumishi 3,551 ambapo wanawake ni 673 sawa na asilimia 18.9. Suala la jinsia ni mtambuka, hivyo litaendelea kuzingatiwa katika mipango ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Changamoto: Changamoto kubwa zilizojitokeza katika utekelezaji wa bajeti ya 2009/2010 ni fedha kuchelewa kutolewa na HAZINA na hivyo kuathiri utekelezaji wa kazi zilizopangwa kutekelezwa, tatizo la ajali za barabarani, kuongezeka kwa makosa yanayohusisha matumizi ya *TEKNOHAMA* na ushirikiano mdogo kutoka kwa wananchi kuhusiana na suala la wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Polisi: Katika mwaka 2009/2010 Jeshi la Polisi limeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi yanayolenga kuhakikisha nchi inakuwa na usalama, amani na utulivu. Jeshi la Polisi limefanikiwa kwa kiasi cha kuridhisha katika kuwalinda wananchi na mali zao, kusimamia utii wa sheria za nchi, kuzuia makosa, kupeleleza makosa ya jinai yaliyoripotiwa katika Vituo vya Polisi, kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani watuhumiwa wa makosa ya jinai na makosa ya usalama barabarani.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Polisi Jamii/ Ulinzi Shirikishi umeendelea kuwa chachu ya mafanikio ya Jeshi la Polisi katika kuzuia na kudhibiti vitendo vya uhalifu. Ufahamu sahihi wa wananchi kuhusu mkakati huu umesababisha ongezeko la idadi ya makosa yanayoripotiwa katika Vituo vya Polisi, ukamataji wa watuhumiwa wa makosa hayo na kasi ya upatikanaji wa ushahidi unaohitajika Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, sanjari na ushirikiano uliopo kati ya Jeshi la Polisi na wananchi, operesheni za kawaida zinazolenga kuzuia na kudhibiti uhalifu zimeendelea kufanywa na vikosi mbalimbali vinavyounda Jeshi la Polisi kwa mfumo wa *Joint Operations Intelligence and Investigation.*

Mfumo huu unahusisha utendaji wa pamoja wa askari Polisi wa kawaida, Kikosi cha FFU, Kikosi cha Usalama Barabarani na wa Idara ya Upelelezi umeongeza kasi ya kutanzua uhalifu kwenye maeneo ya matukio na katika mfumo wa utoaji haki nchini.

Mheshimiwa Spika, yapo baadhi ya maeneo ambayo kutokana na sababu mbalimbali za kijamii, kisiasa, kiutamaduni au kiuchumi yalikithiri kwa vitendo vya uhalifu vilivyosababisha uvunjifu wa amani na hofu kubwa miongoni mwa wananchi.

Hali ya namna hiyo ilipojitokeza, Jeshi la Polisi lililazimika kuongeza nguvu na kuendesha operesheni maalum kwenye maeneo husika. Katika mwaka 2009/2010 operesheni maalum ziliendeshwa katika Wilaya za Tarime, Rorya na Musoma Mkoani Mara kwa lengo la kudhibiti ongezeko la unyang'anyi wa kutumia silaha na wizi wa mifugo na iliyofanyika katika mbuga ya wanyama ya Selous ili kudhibiti ongezeko la ujangili katika hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limeendelea kuimarisha doria na operesheni katika maeneo ya Mikoa ya Kagera, Singida, Kigoma na Shinyanga pamoja na maeneo ya misitu ya Bukombe alikovamiwa Mheshimiwa Emanuel Luhaula Mbunge wa Bukombe. Nachukua nafasi hii kumpa pole sana Mheshimiwa Luhaula na kumwombea kwa Mwenyezi Mungu amrejeshee afya njema. Napenda pia kujulisha kuwa upelelezi wa tukio hilo unaendelea na tayari watuhumiwa saba wamekamatwa na kufikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, napenda kupitia Bunge hili Tukufu kukemea tabia inayojirudia ya wananchi kutoheshimu utawala wa sheria kutokana na imani za kishirikina na kutoheshimu haki za binadamu kwa wananchi kujichukulia sheria mikononi kwa kuvamia Vituo vya Polisi kwa lengo la kuwatoa watuhumiwa na kuwaadhibu. Tukio lililotokea hivi karibuni katika Kituo cha Polisi cha Hedaru Mkoani Kilimanjaro sio la kiungwana. Watuhumiwa wote waliohusika na tukio hili watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limeendelea kushirikiana na vyombo vingine vya dola pamoja na wadau mbalimbali ikiwemo majeshi mengine ya Shirikisho la Polisi la Kimataifa - *Interpol,* Shirikisho la Polisi la nchi za Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika – *EAPCCO* na Shirikisho la Polisi la nchi za Kusini mwa Afrika - *SARPCCO* kupitia ubadilishanaji taarifa za uhalifu na wahalifu, mafunzo, operesheni mbalimbali za pamoja na mikutano ya Wakuu wa Majeshi na Wakuu wa Upelelezi wa nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, operesheni ya pamoja ilifanyika iliyohusisha Tanzania, Mauritius, Zambia, Malawi, *DRC* na Ofisi za INTERPOL Kanda ya Kusini mwa Afrika zilizoko Harare – Zimbabwe. Makosa yaliyopewa kipaumbele katika operesheni hii ni wizi wa magari, biashara ya dawa za kulevya, silaha haramu na wahamiaji haramu. Hapa nchini operesheni hii ilifanyika katika Mikoa ya Arusha, Mbeya, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Mara, Dar es Salaam, Zanzibar na Mkoa wa Kipolisi wa Tarime/Rorya. Katika operesheni hiyo yalikamatwa magari 54, silaha haramu tatu wahamiaji haramu 25 na dawa za kulevya heroin kete 28, bhangi kilo 801 na mirungi kilo 608. Jumla ya watuhumiwa 107 walikamatwa kuhusiana na makosa hayo na hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yao.

Mheshimiwa Spika, Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu: Naomba kupitia Bunge lako Tukufu niarifu kuwa maandalizi ya ulinzi katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2010 yanaendelea vizuri. Magari 260 yanatarajiwa kupokelewa mwezi Agosti, 2010. Mafunzo ya utayari kwa askari yamekamilika. Wito wangu kwa wananchi wote waliotimiza masharti ya kupiga kura wajitokeze kwa wingi kuwapigia kura viongozi wanaowapenda bila woga kwani hali ya amani na utulivu itaendelea kudumishwa katika kipindi chote cha zoezi la uchaguzi. Wizara kupitia Jeshi la Polisi imeandaa na kusambaza kitabu kijulikanacho *Haki na Wajibu wa Mpiga Kura*. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla wakitumie kitabu hicho kujielimisha na kuwaelimisha wengine pia.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Nyumba za Makazi: Awamu ya kwanza ya ujenzi wa maghorofa umekamilika ambapo katika Kambi ya Polisi Barabara ya Kilwa Dar es Salaam familia 216 zimepata makazi, Kambi ya Polisi Ziwani – Unguja familia 12 na Kambi ya Limbani – Pemba familia 12. Aidha, ujenzi wa nyumba sita umekamilika Wilayani Bahi, nne Kikosi cha *FFU* Finya – Kaskazini Pemba na 10 Kambi ya Katubuka Kigoma. Katika mwaka 2010/2011 ujenzi utaendelea wa awamu ya pili wa maghorofa 30 Kambi ya Polisi Barabara ya Kilwa, maghorofa sita Kambi ya Mabatini - Mwanza, sita Musoma- Mara na matatu Byekera – Bukoba, nyumba 12 Ludewa Iringa, nane Kiwanja cha Ndege Arusha, mbili Unguja Ukuu - Unguja na mbili Finya - Kaskazini Pemba.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Ofisi na Vituo vya Polisi: Ujenzi wa Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Tabora, Kilimanjaro, Dodoma, Morogoro na Mbeya na vituo vya Makambako, Chato, Bukombe, Meatu, Bahi na Mpanda umekamilika. Katika mwaka 2010/2011 ujenzi utaendelea wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai Jijini Dar es Salaam, majengo ya Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Kusini Pemba, Mara na Manyara na Vituo vya Polisi vya Ludewa, Newala, Namtumbo, Bagamoyo, Njombe na Vituo vya Wilaya ya Kipolisi ya Mbagala na vya daraja *"C"* vya Horohoro – Tanga, Mtambaswala – Mtwara, Ukara - Ukerewe na Nshamba – Kagera.

Mheshimiwa Spika, Ukarabati wa Ofisi, Vituo na Kambi: Ukarabati umefanyika katika Ofisi na Vituo vya Polisi vya Tabora, Nkasi, Polisi Kati, Kijitonyama na Magomeni Dar es Salaam. Katika mwaka 2010/2011 ukarabati utafanyika katika Ofisi za Polisi Mtwara, Kigoma na Makao Makuu ya Polisi Dar es Salaam na Zanzibar, Vituo vya Polisi Manyovu, Ziwani – Unguja na Kengeja – Kusini Pemba.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo: Ujenzi wa Chuo cha Upelelezi Dodoma umeanza na utaendelea katika mwaka 2010/2011. Ukarabati uliendelea katika vyuo vya Kidatu na Moshi. Mwaka 2010/2011 ukarabati utaendelea katika vyuo vya Kidatu, Moshi na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo na Ajira: Katika mwaka 2009/2010 Jeshi la Polisi limetoa mafunzo mbalimbali kwa askari 8,948 na kuajiri askari wapya 5,145. Katika mwaka 2010/2011 Jeshi la Polisi linatarajia kutoa mafunzo kwa askari 5,715 wakiwemo askari 150 katika fani ya upelelezi wa makosa ya kimtandao ( cyber crime) na kuajiri askari wapya 2,500.

Mheshimiwa Spika, Mapambano Dhidi ya VVU/UKIMWI: Wadau mbalimbali mfano *Marie Stopes (T) Ltd, Pharm Access* na Kikundi cha Akinamama ndani ya Jeshi la Polisi cha *Home Based Care* wameshirikishwa katika kuelimisha na kuwahudumia askari waathirika. Aidha, kiwango cha maambukizi kimeshuka kutoka asilimia 4.7 mwaka 2007 hadi asilimia 4 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Magereza: Jukumu la msingi la Jeshi la Magereza ni kuwahifadhi wafungwa wa aina zote katika magereza pamoja na mahabusu

wanaosubiri kesi zao Mahakamani. Urekebishaji wa tabia za wafungwa hufanywa kupitia programu za mafunzo kwa njia ya vitendo na nadharia, ili wamalizapo vifungo vyao wawe raia wema katika jamii. Programu hizo huendeshwa kupitia miradi ya ujenzi, viwanda vidogovidogo, kilimo, mifugo na mazingira.

Mafunzo ya nadharia huendeshwa katika Chuo cha Ufundi cha Magereza Ruanda - Mbeya, Gereza la Wami Vijana - Morogoro na utoaji ushauri nasaha kwa kutumia walimu wa dini na Maafisa Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, Usafirishaji wa Mahabusu Kwenda Mahakamani na Kurudi Magerezani: Ili kuboresha usafirishaji wa mahabusu kwenda Mahakamani na kurudi Magerezani, katika mwaka 2009/2010 yamenunuliwa magari 12 yaani Mabasi makubwa mawili, magari madogo matano na *Pick – Ups* tano. Baada ya upatikanaji wa magari hayo huduma ya kusafirisha mahabusu kwenda Mahakamani na kurudi Magerezani itatolewa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Jukumu litaendelezwa kwa awamu kwenye Mikoa mingine kadri bajeti itakavyoruhusu. Katika mwaka 2010/2011 lengo ni kununua magari manane kwa ajili ya kuhudumia Wilaya za Kibaha, Bagamoyo na Rufiji Mkoani Pwani, Mkoa wa Arusha hususan katika Gereza Kuu la Arusha kwa mahabusu katika Wilaya za Longido na Monduli na Mkoani Mwanza katika Gereza Butimba na Wilaya ya Magu.

Mheshimiwa Spika, Programu za Urekebishaji wa Wafungwa: Utekelezaji wa mpango wa kuendesha shughuli za wafungwa kwa kutumia mtandao wa kompyuta (*Offenders Management Information System*) upo katika hatua za mwisho kwa Mkoa wa Dar es Salaam ambapo uunganishaji wa kompyuta *(connectivity),* usimikaji wa *Operating system* na *Oracle Database* kwa ajili ya ubebaji wa Software ya OMIS umekamilika. Uendeshaji wa mafunzo kwa askari watakaohusika na uingizaji wa taarifa za kumbukumbu za wafungwa katika mtandao tayari umeshakamilika na kazi ya uingizaji wa taarifa hizo utaanza hivi punde katika eneo la majaribio. Matarajio ni kuanza kueneza mpango huu kwenye vituo vya Magereza tisa ambavyo ni Uyui, Butimba, Ruanda, Isanga, Lilungu, Lindi, Maweni, Arusha na Karanga. Utekelezaji wa mradi huu utaendelezwa katika Mikoa yote nchini kwa awamu kadri fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, Ajira: Katika mwaka 2009/2010 askari wapya 1,075 wameajiriwa baada ya kuhitimu mafunzo ya awali ya uaskari katika Chuo cha Magereza Kiwira Mkoani Mbeya. Mwaka 2010/2011 Jeshi la Magereza litaendesha kozi ya mafunzo ya awali kwa askari wapya 962 ambayo yataanza tarehe 1 Julai, 2010 na watumishi raia 43 katika kada mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Uimarishaji wa Magereza Makongwe Yenye Ulinzi Mkali: Ukarabati na uboreshaji wa majengo na miundombinu ya magereza yenye ulinzi mkali umefanyika na unaendelea katika Magereza ya Uyui – Tabora, Butimba – Mwanza, Maweni – Tanga, Karanga – Kilimanjaro na Gereza Maalum Isanga – Dodoma. Katika

mwaka 2010/2011 ukarabati wa majengo na miundombinu utaendelea katika Magereza ya Ukonga , Uyui, Maweni na Lilungu.

Mheshimiwa Spika, Upanuzi, Ukarabati na Ujenzi wa Mabweni ya Wafungwa: Kazi ya upanuzi na ukarabati wa mabweni ya wafungwa uliendelea katika Magereza ya Geita, Mugumu, Loliondo, Meatu na Kwamngumi. Ujenzi wa mabweni ya wafungwa uliendelea katika Magereza ya Rombo, Hanang, Mbinga na Kambi ya Chikuyu. Katika mwaka 2010/2011 lengo ni kuendelea kukamilisha baadhi ya miradi viporo vya ujenzi wa mabweni ya wafungwa katika Magereza ya Rombo, Isupilo, Masasi, Mpwapwa, Geita na Kahama na kuanza ujenzi wa Gereza la Wilaya ya Karatu.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Magereza wa Mikoa: Kwa muda mrefu sasa Jeshi la Magereza limekuwa na tatizo la ukosefu wa ofisi stahiki za Wakuu wa Magereza wa Mikoa katika Mikoa yote nchini isipokuwa Mikoa ya Kagera, Arusha, Iringa, Tabora, Pwani, Mtwara, Mara na Dodoma. Mikoa mingine iliyobaki ofisi zake ama ni nyumba za kuishi askari ambazo zipo ndani ya kambi au majengo ambayo hayajajengwa kwa madhumuni ya kuwa ofisi. Katika mwaka 2009/2010 Jeshi la Magereza limeanza ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Magereza wa Mikoa ya Singida na Dar es Salaam. Katika mwaka 2010/2011, Jeshi la Magereza litaendelea na ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wakuu wa Magereza wa Mikoa ya Dar es Salaam na Singida.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi, Ukamilishaji na Ukarabati wa Nyumba za Askari: Kazi ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa nyumba za kuishi askari ziliendelea katika Magereza ya Tanga, Igunga, Nzega, Makete, Mahabusu Iringa, Rombo na Kikosi Maalum Ukonga. Ukarabati wa nyumba za askari uliendelea katika Magereza ya Biharamulo, Ukonga na Chuo cha Maafisa Ukonga. Katika mwaka 2010/2011 Jeshi la Magereza litaendelea na ujenzi wa nyumba za askari katika Magereza ya Karatu, Singida, Ludewa, Kihonda, Pangani, Chuo Kiwira na Magereza Mkoa wa Kagera. Ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba utafanyika katika Magereza ya Mbinga, Mollo, Mahabusu Iringa, Kiomboi, Nachingwea, Mbarali, Ilagala, Pawaga na Isupilo. Ukarabati wa nyumba utaendelea katika Magereza ya Butimba, Ngwala, Lushoto, Mkono wa Mara na Wami Kuu. Aidha, Jeshi la Magereza linaendelea kuwasiliana na Mifuko ya NSSF, PSPF na LAPF ili kupata fedha za mkopo kwa ajili ya kujenga nyumba zaidi za askari.

Mheshimiwa Spika, Uimarishaji wa Mifumo ya Maji Safi na Maji Taka: Magereza mengi yaliyopo mijini yanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa maji ya uhakika na uchakavu wa miundombinu ya maji safi na maji taka na ni magereza ambayo yanaelemewa na msongamano mkubwa wa wafungwa na mahabusu. Katika mwaka 2009/2010 ukarabati wa miundombinu ya maji taka ulifanyika katika Magereza ya Meatu, Kingurungundwa, Butundwe, Kiabakari na Chuo Ukonga. Katika mwaka 2010/2011 lengo ni kuimarisha mifumo ya maji safi na maji taka katika Magereza ya King’ang’a, Msalato, Kihonda, Kambi Mlolo, Isupilo, Tunduru, Kikosi Maalum Ukonga, Ngwala, Handeni, Kibondo, Kondoa na Kitete.

Mheshimiwa Spika, Fidia na Upimaji wa Maeneo ya Magereza: Katika mwaka 2009/2010 fidia ya shilingi 24 milioni kwa ajili ya mazao na majengo imelipwa kwa ajili

ya eneo linalotarajiwa kujengwa Gereza la Wilaya ya Chato. Upimaji wa maeneo umefanyika katika Magereza ya Kibiti, Matongo, Kondoa, Rwamrumba na Mwanga. Katika mwaka 2010/2011 Jeshi la Magereza linakusudia kupima maeneo ya Magereza ya Kalilankulukulu, Chuo Kiwira na kukamilisha upimaji wa Gereza Ubena.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Magereza: Katika kutekeleza Kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, katika mwaka 2009/2010 Shirika la Magereza limeendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Gereza la kilimo la Kitengule na uchimbaji wa bwawa la umwagiliaji katika Gereza Mang'ola. Aidha, Shirika limeendelea kuimarisha viwanda vidogovidogo kwa kuvipatia zana na vitendea kazi zikiwemo mashine za viatu, useremala na ushonaji. Katika mwaka 2009/2010 Shirika la Magereza lilipewa kazi ya kutengeneza samani za Ofisi za Makao Makuu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa hapa nchini.

Ninatoa wito kwa Wizara na taasisi nyingine kuiga mfano huu wa kupenda kutumia samani zinazotengenezwa hapa nchini kwani zitakuwa na ubora wa hali ya juu na imara. Matarajio ya Shirika kwa mwaka 2010/2011 ni kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula katika Magereza ya Idete, Mbigiri, Isupilo na Ludewa na kuendelea kukarabati viwanda vyake. Katika Mwaka wa Fedha 2010/2011 Wizara itaangalia upya mfumo wa uendeshaji wa Shirika la Magereza ili kuliwezesha kuongozwa na raia wenye utaalam stahiki na siyo lazima askari Magereza.

Mheshimiwa Spika, Uzalishaji wa Mbegu Bora za Kilimo: Katika mwaka 2009/2010 Jeshi la Magereza lilizalisha mbegu bora za kilimo kwa kushirikiana na Wakala wa Mbegu za Kilimo *(Agricultural Seeds Agency)* katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Manyara, Lindi, Iringa, Mbeya, Kilimanjaro na Morogoro ambapo hekta 1,014 zililimwa na kupandwa mbegu bora za mazao ya mahindi na mpunga, mikunde, mbegu za ufuta na mboga za majani. Matarajio ni kuvuna tani 1,297 za mbegu bora. Katika mwaka 2010/2011 Jeshi la Magereza linatarajia kuhudumia hekta 4,984 za mazao mbalimbali kwa mategemeo ya kupata mavuno tani 8,312. Ununuzi wa Magari na Zana za Kilimo: Katika mwaka 2009/2010, Jeshi la Magereza limenunua matrekta manane na zana nyingine za kilimo kwa lengo la kuboresha mashamba ya kilimo. Malengo ya mwaka 2010/2011 ni kununua magari 11 ya aina mbalimbali kwa ajili ya shughuli za utawala, matrekta 10 na zana nyingine za kilimo. Matrekta pamoja na zana hizo ni kwa ajili ya Magereza ya Songwe, Idete, Mollo, Kitai, Ushora, Wami Kuu, Kiabakari, Pawaga, Ludewa na Mbigiri.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Nishati Mbadala Magerezani: Juhudi za kupata nishati mbadala ya kuni zinaendelea kwa kukamilisha mradi wa majaribio wa matumizi ya gesi itokanayo na tungamotaka (*biogas*) katika Gereza la Ukonga ambapo kwa sasa tayari majaribio ya kupikia *biogas* yanaendelea kwa mafanikio makubwa. Kuanza kutumika kwa mradi huu kutapunguza kwa kiwango kikubwa matumizi ya kuni na hivyo kuwa rafiki mkubwa wa mazingira. Katika Gereza la Keko upo mradi wa majaribio wa matumizi ya gesi asilia *(Natural gas)* ambao nao pia upo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji wake. Matumizi ya makaa ya mawe yanaendelea katika Magereza ya Mkoa wa Mbeya na matarajio ni kueneza matumizi ya nishati hii katika Mikoa jirani ya

Iringa na Rukwa kwa awamu. Matarajio ya muda mrefu ni kueneza matumizi ya nishati hizi katika magereza mengine kadri uwezo utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, Juhudi za Kupambana na Janga la UKIMWI: Katika suala la kupambana na maambukizi mapya ya UKIMWI, Jeshi la Magereza limejizatiti kwa kutoa elimu ya kujikinga kupitia waelimishaji rika kwa askari, familia zao na wafungwa. Katika mwaka 2009/2010 hali ya maambukizi mapya katika Jeshi la Magereza ilipungua kutoka asilimia 5.7 hadi kufikia asilimia 4.4 kwa askari, familia zao kutoka asilimia 5 hadi asilimia 4.1 na asilimia 12 hadi asilimia 8.4 kwa wafungwa. Ufuatiliaji wa waathirika majumbani pamoja na utoaji wa virutubisho umefanyika. Katika mwaka 2010/2011 lengo ni kuweka mkazo zaidi katika kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Huduma kwa Jamii: Programu ya Huduma kwa Jamii ilianza kutumika rasmi mwaka 2005. Hii ni mojawapo ya adhabu mbadala ya kifungo gerezani na hadi sasa inatekelezwa katika Mikoa 12 ya Tanzania Bara. Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Dodoma, Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Iringa, Kagera, Mara na Shinyanga.

Lengo la programu hii ni kutekelezwa katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Aprili, 2010 jumla ya wafungwa 412 wamefaidika na programu hii ambapo wanaume ni 313 na wanawake 99. Wafungwa hao hutumikia vifungo vyao nje ya magereza kwa kufanya kazi bila malipo kwenye taasisi za umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, muundo wa Idara ya Huduma kwa Jamii umeimarishwa kwa kuajiri Maafisa Majaribio (*Probation Officers*) 100 ambao watasimamia utekelezaji wa sheria zinazohusu adhabu mbadala za Huduma kwa Jamii, Huduma za Majaribio, Sheria ya Bodi za Parole na utaratibu wa kifungo cha nje. Watumishi hao wamepatiwa mafunzo maalum.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Zimamoto na Uokoaji: Katika mwaka 2009/2010 nchi imeendelea kukabiliwa na matukio ya ajali za moto kwenye majengo mbalimbali na kwenye vyombo vya usafiri. Vikosi vya uokoaji kwa kushirikiana na wananchi vilikabiliana na matukio hayo ingawa sio kwa ufanisi mkubwa sana kufikia matarajio ya wananchi. Nawashukuru wananchi waliotoa msaada katika kukabiliana na matukio hayo.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Tahadhari na Kinga ya Moto: Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea na zoezi la ukaguzi wa tahadhari na kinga dhidi ya moto katika maeneo mbalimbali na kwenye vyombo vya usafiri. Pamoja na kufanya zoezi la ukaguzi pia elimu ya kinga na tahadhari dhidi ya moto na majanga mengine nayo ilitolewa. Katika kipindi cha Julai 2009 hadi Aprili 2010 jumla ya maeneo 2,945 yalifanyiwa ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limekuwa na mahusiano ya kindugu na baadhi ya nchi duniani kama ifuatavyo: Jiji la Dar es Salaam lina mahusiano na Ujerumani, Mwanza na Finland, Tanga na Marekani, Morogoro na Finland, Sweden na Shinyanga na Marekani. Mahusiano hayo yamewezesha kuvipatia vikosi vya

Zimamoto na Uokoaji katika miji hiyo vitendea kazi yakiwemo magari. Ninashukuru kuwepo kwa mahusiano hayo na ninaomba yawe endelevu.

Ninatoa wito kwa Halmashauri husika kuthamini msaada uliotolewa kwa kuyatunza magari hayo na ni matumaini yangu kwamba msaada huo utakuwa ni chachu ya kuongeza ufanisi katika utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sheria ya Zimamoto na Uokoaji Na. 14 ya mwaka 2007 pamoja na muundo mpya wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji chini ya komandi moja na kuanzisha Ofisi za Mikoa unaendelea.

Ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Zimamoto na Uokoaji umeanza katika mwaka 2009/2010 na utaendelea katika mwaka 2010/2011 na ukarabati wa ofisi utafanyika katika Mikoa minne ya Kilimanjaro, Morogoro, Iringa na Rukwa.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo na Ajira: Katika mwaka 2009/2010 mafunzo ya uaskari yametolewa katika Chuo cha Magereza Kiwira Mbeya. Mafunzo ya uongozi yametolewa kwa askari 60 na ya awali kwa askari 200 ambapo askari 187 wamehitimu mafunzo hayo. Watumishi raia 22 wameajiriwa. Katika mwaka 2010/2011 askari wapya 107 wataajiriwa na kupatiwa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Uhamiaji: Katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Aprili, 2010, jumla ya wageni 664,037 waliingia nchini, ikilinganishwa na wageni 680,168 walioingia nchini katika kipindi kama hiki mwaka jana.

Wageni 638,376 walitoka nchini ikilinganishwa na wageni 652,720 waliotoka nchini katika kipindi kama hiki mwaka uliopita. Idadi ya wageni walioingia imepungua kwa watu 16,131 sawa na asilimia 2.4. Kushuka kwa idadi hii kunaweza kuelezwa pamoja na mambo mengine ni kutokana na kudorora kwa uchumi wa dunia ambao kwa sasa unaelekea kuimarika.

Mheshimiwa Spika, Wageni Waliopatiwa Hati za Ukaazi: Katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Aprili, 2010 wageni 10,890 walipewa hati za ukaazi nchini ikilinganishwa na wageni 10,682 waliopewa hati hizo katika kipindi kama hiki mwaka jana. Idadi ya hati zilizotolewa imeongezeka kwa hati 208 sawa na asilimia 2. Hali hii ni matokeo ya kuanza kuimarika kwa hali ya uchumi duniani baada ya kudorora kwa muda.

Mheshimiwa Spika, Wageni Waliopatiwa Uraia wa Tanzania: Katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Aprili, 2010, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imetoa uraia wa Tanzania kwa wageni 199 waliotimiza masharti na kuyakataa maombi mengine 14.

Wageni waliopata uraia ni wa kutoka mataifa ya India, Somalia, Rwanda, Kenya, Uingereza, Uganda, Burundi, Lebanon, Yemen, Pakistan, Switzerland, Iran, Sudan, Jordan, Zimbabwe, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Marekani, China, Misri na wasio na utaifa *(Stateless)*.

Mheshimiwa Spika, Watanzania Waliopatiwa Uraia wa Mataifa Mengine: Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Watanzania 52 walipata uraia wa mataifa mengine ya Kenya, Ujerumani, Norway, Denmark, Zambia, Uingereza, Australia, Namibia, Sweden na Singapore na hivyo kupoteza haki ya kuwa raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Na. 6 ya mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, Wakimbizi wa Kwenye Makazi Waliopatiwa Uraia: Jumla ya wakimbizi 162,156 kutoka katika makazi ya zamani ya Mishamo, Katumba na Ulyankulu yaliyopo katika Mikoa ya Rukwa na Tabora wamepatiwa uraia wa Tanzania ambapo wanatarajiwa kuhamishiwa katika Mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Pasipoti Zilizotolewa: Katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Aprili, 2010 Idara ya Uhamiaji ilitoa jumla ya pasipoti 39,241. Kati ya hizo 37,664 ni za kawaida, 1,269 za Afrika Mashariki, 209 za kibalozi na 99 za kiutumishi, ikilinganishwa na jumla ya pasipoti 39,522, ambapo pasipoti 37,754 za kawaida, 1,452 za Afrika Mashariki, 260 za kibalozi na 56 za kiutumishi zilizotolewa katika kipindi kama hiki mwaka jana. Vijana wa Kitanzania Waliorudishwa Nchini

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Aprili, 2010, vijana 353 walirudishwa nchini toka nchi mbalimbali baada ya kubainika kwamba wapo kwenye nchi hizo kinyume cha sheria ikilinganishwa na vijana 372 waliorudishwa katika kipindi kama hiki mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika,Misako na Doria: Katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Aprili, 2010 Idara iliendesha doria na misako yenye lengo la kudhibiti wageni haramu nchini ambapo jumla ya wageni 2,272 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria ikilinganishwa na wageni 3,109 waliokamatwa katika kipindi kama hiki mwaka jana. Miongoni mwa idadi ya wahamiaji haramu waliokamatwa, 1,915 walitokea nchi za Pembe ya Afrika ambapo 1,838 wamekwisharejeshwa kwao na 77 wapo katika magereza mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika,Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Ofisi: Katika mwaka 2009/2010, ukarabati wa nyumba nane umekamilika katika Kituo cha mpakani cha Rusumo Mkoani Kagera. Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Dar es Salaam umekamilika. Upanuzi wa Afisi Kuu Zanzibar upo katika hatua za mwisho na ujenzi wa nyumba za makazi katika Kituo cha Mkenda Nakawale mpakani mwa Tanzania na Msumbiji Mkoani Ruvuma umeanza. Aidha, Mkandarasi wa ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Shinyanga amepatikana. Katika mwaka 2010/2011 Idara itaendeleza miradi viporo na kuanza ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Ruvuma na Morogoro. Idara pia itafanya ukarabati wa majengo ya ofisi na nyumba katika vituo vya Kyela, Tunduma, Horohoro, Manyovu, Mabamba na Sumbawanga.

Mheshimiwa Naibu Spika,Ajira na Mafunzo: Katika mwaka 2009/2010, askari wapya 156 wameajiriwa, na askari/watumishi 41 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2010/2011, askari 130 wataajiriwa na mafunzo yatatolewa kwa watumishi 50.

Mheshimiwa Naibu Spika,Ununuzi: Katika mwaka 2009/2010, Idara imenunua pikipiki 20 na mwaka 2010/2011 zitanunuliwa pikipiki 15.

Mheshimiwa Naibu Spika,Mapambano Dhidi ya VVU/UKIMWI: Katika suala la kupambana na maambukizi mapya ya UKIMWI pamoja na kuwahudumia watumishi wanaoishi na VVU/UKIMWI, Idara imeendelea kuwahudumia watumishi hao na kutoa elimu kwa watumishi na familia zao katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Singida na Zanzibar. Pia liliendeshwa zoezi la kupima afya ambapo watumishi 455 pamoja na familia zao walipima VVU katika Mikoa hiyo. Vipeperushi vimesambazwa katika vituo vya kuingilia nchini kwa lengo la kutoa elimu kwa wageni wanaoingia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya Wakimbizi: Tarehe 30 Aprili, 2010 walikuwepo wakimbizi 108,472 nchini. Warundi 47,269, Wakongo 59,425, Wasomali 1,460 na 318 ni wakimbizi wa mataifa mbalimbali. Katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Aprili, 2010 jumla ya wakimbizi 16,080 walirejea kwao ambapo Warundi ni 14,943 na Wakongo 1,137. Aidha, kambi moja ya Lugufu II iliyopo katika Wilaya ya Kigoma Vijijini Mkoani Kigoma ilifungwa. Tangu zoezi la kuwarejesha wakimbizi kwao lianze mwaka 2002, jumla ya wakimbizi 568,322 tayari wamerejea kwao ambapo Warundi ni 501,682 na Wakongo ni 66,640 na jumla ya makambi 12 yamefungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika,Huduma ya Kushughulikia Malalamiko: Ili kuratibu ushughulikiaji wa malalamiko ya wananchi dhidi ya vyombo vya kijeshi ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ambavyo ni Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji pia malalamiko ya askari na watumishi wa Wizara, ipo Idara maalum kwa ajili ya kushughulikia malalamiko hayo ili kuboresha na kuleta ufanisi wenye tija ndani ya vyombo vinavyolalamikiwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi. *(Makofi)*

Katika mwaka 2009/2010, Idara ilipokea na kushughulikia jumla ya malalamiko 125 mengi yakihusu Jeshi la Polisi kuhusiana na vitendo vyao dhidi ya raia hususan ubambikizaji wa kesi na ucheleweshaji wa makusudi wa upelelezi wa makosa ya jinai. Aidha, yapo malalamiko ya askari wa vyeo vya chini ya kutotendewa haki katika mashauri ya nidhamu na matokeo yake kufukuzwa kazi kutokana na uonevu na chuki miongoni mwao.

Mheshimiwa Naibu Spika,Idara imekuwa ikifanya kazi zake bila taratibu zilizoainishwa kisheria na hivyo maamuzi yake kutopewa umuhimu unaostahili. Ili kuipa Idara nguvu ya kisheria, katika mwaka 2009/2010 Mshauri Mwelekezi ameanza mchakato ambao utapelekea kutungwa kwa sheria itakayosimamia utendaji kazi wa Idara hii. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha wa 2010/2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika,Usajili wa Vyama vya Kijamii na Huduma ya Sheria: Katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 jumla ya vyama 294 viliandikishwa na hii inafanya jumla ya vyama vilivyoandikishwa hadi sasa kuwa 6,016. Pia Idara iliendelea

kutatua migogoro ya vyama mbalimbali vikiwemo 10 vya kidini na vingine sita vya kiraia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha utendaji kazi katika Idara ya Huduma ya Sheria ambayo pia inasimamia usajili wa vyama vya kijamii, katika mwaka 2009/2010 imeanza mchakato wa kuwa na mfumo wa kutunza kumbukumbu za usajili wa vyama. Kazi hii inafanywa kwa ushirikiano na Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika,katika mwaka 2010/2011, Idara itaendelea kutafuta suluhu ya migogoro ya vyama kadri itakavyojitokeza, kuhakiki utendaji na uhai wa vyama hivyo na kutoa elimu kwa vyama hivyo juu ya umuhimu na wajibu wao wa kutoa taarifa mbalimbali za vyama vyao na kulipa ada ya kila mwaka kwa mujibu wa Sheria ya Vyama Sura ya 337 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika,Shukurani: Natoa shukurani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi Mbunge wa Muleba Kusini kwa kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2010/2011 pamoja na ushauri wao katika masuala mbalimbali yahusuyo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika,naomba kutoa shukurani za pekee kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Balozi Khamis Suedi Kagasheki, Mbunge wa Bukoba Mjini, Katibu Mkuu Ndugu Mbarak Abdulwakil, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Elizabeth Nyambibo, Wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Inspekta Jenerali wa Polisi Ndugu Saidi Mwema, Kamishna Mkuu wa Magereza Ndugu Augustino Nanyaro, Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji Ndugu Matwani Kapamba, Kaimu Kamishna Mkuu wa Uhamiaji Ndugu Cunbert Sambalyegula na wakuu wote wa Idara na Vitengo, Makamanda wote, askari pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambao kwa ushirikiano wao hotuba hii imeweza kuandaliwa na kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika,naomba kutoa shukurani kwa nchi wahisani za Marekani, China, Misri na Israel na kwa taasisi za kimataifa za *INTERPOL, UNHCR, UNDP, WFP, IOM, UNICEF, NORAD, CIDA, DFID, Hanns Seidel Foundation, Pharm Acces* na Benki ya Dunia kwa misaada yao ambayo imeongeza uwezo wa kiutendaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika,mwisho ingawa sio mwisho kwa umuhimu ninawashukuru sana wana CCM wa jimbo la Nyamagana kwa kuniamini na kunisimamisha kama mgombea ubunge kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi miaka mitano iliyopita.

Aidha, kwa dhati kabisa ninawashukuru wananchi wote wa Nyamagana kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao hapa bungeni kwa kipindi cha miaka mitano. Ninawashukuru wote kwa ushirikiano walionipatia katika juhudi za kuleta maendeleo. Na

kupitia kwako naomba kuwafahamisha kwamba niko tayari kuendelea kuwatumikia. *(Makofi)*

Kipekee kabisa ninaishukuru familia yangu hasa mke wangu Stella, watoto wangu Chela, Amani na Lau Jr kwa upendo, faraja na uvumilivu wao kwa muda wote nilipokuwa natekeleza majukumu yangu ya kitaifa kama Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Hali kadhalika, ninawashukuru wazazi wangu Dkt. Fortunatus na Laura Masha kwa kunilea, kunipatia elimu na kunifundisha umuhimu wa kuishi na watu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika,Maombi Ya Fedha Kwa Mwaka 2010/2011:Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipitishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2010/2011 ya shilingi bilioni mia nne arobaini na sita, milioni mia tatu arobaini na saba laki nne themanini na moja elfu ( 446,347,481,000) kama ifuatavyo:-

**Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

| | |
|---|---|
| Matumizi Mengineyo shilingi | 2,219,384,000 |
| Mishahara shilingi | 1,298,506,000 |
| Maendeleo shilingi | 899,217,000 |
| **Jumla shilingi** | **4,417,107,000** |

**Fungu 28 - Jeshi la Polisi**

| | |
|---|---|
| Matumizi Mengineyo shilingi | 137,136,488,000 |
| Mishahara shilingi | 111,214,457,000 |
| Maendeleo shilingi | 18,967,837,000 |
| **Jumla shilingi** | **267,318,782,000** |

**Fungu 29 - Jeshi la Magereza**

| | |
|---|---|
| Matumizi Mengineyo shilingi | 49,498,754,000 |
| Mishahara shilingi | 44,727,185,000 |
| Maendeleo shilingi | 11,613,583,000 |
| **Jumla shilingi** | **105,839,522,000** |

**Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

| | |
|---|---|
| Matumizi Mengineyo shilingi | 3,468,750,000 |
| Mishahara shilingi | 1,610,162,000 |
| Maendeleo shilingi | 3,601,361,000 |
| **Jumla shilingi** | **8,680,273,000** |

**Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji**

| | |
|---|---|
| Matumizi Mengineyo shilingi | 17,172,092,000 |
| Mishahara shilingi | 16,111,038,000 |
| Maendeleo shilingi | 26,808,667,000 |
| **Jumla shilingi** | **60,091,797,000** |

Mheshimiwa Naibu Spika,nakushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika,naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja hii pia imeungwa Mkono kwa hiyo, nitamuita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama.Kuhusu utelezaji wa Majukumu ya Wizara na majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Masilingi. *(Makofi)*

**MHE. WILSON M. MASILINGI- MWENYEKITI KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 01 Juni 2010, Kamati ilikutana kupokea na kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa Fedha 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa Fedha 2010/2011 iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein A. Mwinyi (MB). Taarifa hiyo ilihusu Fungu 38 – Ngome, Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa na Fungu 57- Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea na uwasilishaji naomba uniruhusu nitoe salamu za rambimrambi kufuatia ajali ya mitumbwi miwili katika Ziwa Victoria ambayo ilisababisha kwa ujumla wapiga kura wetu zaidi ya 20 kufariki. Naungana na Mkuu wa Wilaya na Jeshi la Polisi waliokuwa karibu na wafiwa na zoezi la uokoaji ili wale waliofiwa na wapendwa wao waweze kupewa nguvu na mwenyezi Mungu, nawapa pole sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kwenye Kamati, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati imeridhishwa na

kazi nzuri ya Serikali ya Awamu ya Nne, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, katika kusimamia ipasavyo masuala ya Ulinzi na Usalama wa Nchi kwa kipindi chote tangu kuingia madarakani. Kamati inatoa shukurani na pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kwa kuliimarisha Jeshi letu. Aidha, tunawapongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, MB, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, MB, kwa kazi nzuri katika kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Majeshi yetu yameendelea kufanya vizuri katika ulinzi wa mipaka yetu na Operesheni nje ya nchi. Kamati inampongeza Jenerali Davis A. Mwamunyange , Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama kwa mafanikio hayo. Aidha, tunawapongeza Luteni Jenerali Abdulrahmani A. Shimbo, Mnadhimu Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Meja Jenerali Samwel N. Kitundu, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa na wapiganaji wote kwa umakini katika kazi na utendaji. Aidha, Kamati imeridhishwa na usimamizi wa mafunzo ya ukakamavu na uzalendo kwa vijana wetu katika majeshi ya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa majukumu ya Wizara:Kamati ilielezwa jinsi Wizara ilivyotekeleza majukumu yake na malengo ya Bajeti kwa mwaka 2009/2010 pamoja na mwelekeo wa matumizi ya fedha hadi Juni 2010.

Aidha, tulielezwa mafanikio ya utekelezaji wa malengo ya mpango wa Mwaka 2009/2010 na changamoto zilizoikabili Wizara kwa kipindi cha 2009/2010. Naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa utekelezaji wa majukumu ya Wizara umefikia hatua kubwa kwa kuzingatia maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio Ya Mapato Na Matumizi Kwa Mwaka Wa Fedha 2010/2011: Kamati ilielezwa kuwa katika kufanikisha azma ya Serikali na malengo yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaomba kuidhinishiwa Makadirio yake ya Mapato kwa Mafungu matatu kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | **Fungu 38 - Ngome** | **Sh.** | **2,650, 000.00** |
| (ii) | **Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa** | **Sh.** | **30,003,000.00** |
| (iii) | **Fungu 57 - Wizara** | **Sh.** | **25,002,000.00** |
| | **JUMLA** | **Sh.** | **57,655,000.00** |

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa upande wa Matumizi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imekadiriwa kutumia jumla ya Sh 621, 493,667,515.00/- Kati ya fedha hizo, Sh 461,273,688,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh 160,219,979,515.00 /- kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni Na Ushauri Wa Kamati:Kamati ilijadili kwa kina Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na mpango wa Wizara hii kwa mwaka wa Fedha 2010/2011. Baada ya kupitia kifungu kwa kifungu katika mafungu yote matatu, napenda kuliarifu Bunge hili kwamba Kamati inaunga mkono maombi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 na kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iandae programu itakayotoa nafasi ya kutumia ujuzi wa Majenerali na Maafisa wa ngazi za juu wastaafu.

(ii)Kamati imeridhishwa na kazi nzuri ya Jeshi la Wananchi kwa Ukarabati wa Reli ya Kati ambao umedhihirisha uwezo mkubwa uliopo jeshini na hivyo tunawapongeza sana. Tunashauri kuwa Serikali iandae Sera ya kujenga uwezo wa vikosi vya uhandisi vya Majeshi yetu kifedha na kiteknolojia ili kuviwezesha kutekeleza kandarasi za Ujenzi daraja la kwanza.

(iii)Pamoja na ufinyu wa bajeti, Uamuzi wa kupokea vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria, utekelezwe haraka kwa maslahi ya usalama na ustawi wa taifa letu.

(iv)Utaratibu wa ajira mpya katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania uendelee kila mwaka pasipo kuathiriwa na uamuzi wa kupunguza ajira Serikalini.

(v)Serikali iendeleze kasi yake ya kuimarisha majeshi yetu ili yaendelee kuwa katika utayari wa kuilinda nchi yetu.

(vi)Zoezi la ukaguzi na uhakiki wa madai mbalimbali ya askari unaofanywa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali liharakishwe ili madeni hayo yalipwe mapema na hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho: Kabla ya kuhitimisha nachukua fursa hii kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge la tisa kwa kasi na viwango na kuliwezesha kuwa chombo halisi cha wananchi.

Aidha, nakupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Anne Makinda, Mbunge, kwa umahiri na uhodari wako kila mara. Vile vile, pongezi tunazitoa kwa Wenyeviti wa Bunge chini ya uongozi wenu, kwa kusimamia ipasavyo taratibu za uendeshaji wa shughuli za Bunge kwa kipindi chote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuwashukuru tena Mheshimiwa Dkt. Hussein A. Mwinyi, MB, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Mheshimiwa Dkt. Emmanuel J. Nchimbi, MB, Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, na Wataalam wote wa Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa tangu kuundwa kwa Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Musa A. Zungu, Mb, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana nami katika kuiongoza vyema Kamati. Kwa namna ya pekee, nawashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa ushirikiano wao, busara, uzalendo na umakini mkubwa waliokuwa nao katika kuchambua Taarifa na Makadirio ya Wizara hii. Uzoefu wao wa muda mrefu katika nyanja mbalimbali za sekta ya ulinzi, usalama na utawala bora umesaidia kwa kiasi kikubwa kufanikisha majukumu ya Kamati kwa kipindi chote, nawashukuru sana. Kwa kuuthamini mchango wa Wajumbe wa Kamati, naomba niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, - Mwenyekiti, Musa A. Zungu,MB - Makamu Mwenyekiti wakati wajumbe ni Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Mohammed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Col. Mst. Saeh A. Farrah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah na Mheshimiwa William J. Kusilla.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wengin e ni Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mheshimiwa Dkt. John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Col Mst. Feteeh S. Mgeni, Mheshimiwa Ali A. Mohamed, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa Brg.Jen. Mst. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Muhammad I. Sanya, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Magalle J. Shibuda,

Mheshimiwa Naibu Spika,naomba kuhitimisha kwa kuwashukuru watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Nawashukuru sana Makatibu walioihudumia vyema Kamati hii wakati Kamati ilipokuwa ikifuatilia utekelezaji wa majukumu ya Serikali na hata wakati wa kuchambua Taarifa za Wizara hii, Makatibu hao ni Ndugu Theonest Ruhilabake na Ndugu Stella Mlambo.

Mheshimiwa Naibu Spika kabla ya kumalizia na mimi nachukua nafasi hii kwa dhati kabisa kuwashukuru sana Wapiga kura wangu wa Jimbo la Muleba Kusini kwa

Imani ambayo wamekuwa nayo muda wote na kunivumilia ninapokuwa nje ya Jimbo nikilitumikia Jimbo na Wananchi kwa ujumla.

Napenda kukanusha kwa dhati kabisa kuhusu taarifa zinazoendeshwa baada ya kuingia katika kipindi hiki cha mchakato cha uchaguzi zikiongozwa na Gazeti la ajabu la TAIFA TANZANIA la tarehe 25 Juni hadi Julai 2010, jana wamenitukana sana kwa mfululizo wiki tatu hivi. *( Vicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukanusha haya yote kwa kunishuhudia uongo sijaenda TAKUKURU kumshtaki mpinzani wangu yoyote, sijaenda hata kwenye Chama Cha Mapinduzi kumlalamikia mpinzani wangu yoyote, sijaenda polisi. Wote ninawakaribisha misaada walete, sitalalamika TAKUKURU kipigo kiko palepale. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, gazeti la TAIFA TANZANIA toleo Na 124 Juni – 1 Julai 2010 limeanza mkakati baada ya kushindwa Kisiasa kunichonganisha na familia. Wapinzani wangu wote mimi ni Wazazi wangu wale Mheshimiwa Tibaigana ni Mjomba wa Baba yangu, Mheshimiwa Professor Annah Tibaijuka ni Mama mdogo wa Mama yangu siwezi kuwapeleka TAKUKURU na sijatukana mtu kama mnavyonifahamu mimi ni mtu mstaarabu sana siwezi kuhangaika ila kipigo kiko palepale.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mke wangu Mary Stella, na watoto wangu Nelson na Yustina kwa kunivumilia nilipokuwa ninahangaika kuwatetea wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini ambao wameonyesha bado wana imani na mimi.

Nilikuwa huko wiki jana kwa sherehe tu sijafanya mkutano wa hadhara wamesema nirudi haraka sana kukabidhiwa dhamana napenda kukushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kuwasilisha Taarifa hii. Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha na asante sana kwa kunisikliza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati. Mimi nawaambia wananchi kwamba hizi ndizo lugha za wakati huu, saa zingine *quoram* haitoshi, watu wamesikia maneno kule wamechepuka, basi ndiyo mchezo wenyewe wa wakati. (*Kicheko*)

Naomba nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima na kwa niaba ya Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kuhusiana na Makadirio na Mapato ya Wizara kwa Mwaka wa 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, aliyenijalia uzima na afya njema, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kifungu cha 99(3) na (7), Toleo la Mwaka 2007, kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na JKT kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inakupongeza sana wewe na Mheshimiwa Spika, kwa kazi nzuri mnayoifanya kuliongoza Bunge hili kwa viwango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii pia kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Mtambile, hasa Wanachama wa Chama cha Wananchi *(CUF),* kwa kunipa ridhaa yao tena kwenye kura za maoni hivi karibuni ili niendelee kuwa mgombea wa nafasi ya Ubunge kwa kipindi kingine cha 2010. Nasema ahsanteni sana kwa imani zenu kwangu na ninaahidi kuwa, nitaendelea kutekeleza majukumu yangu ndani ya Chama, ndani ya Jimbo na ndani ya Bunge hili Tukufu kwa ushirikiano wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa sikuwatendea haki hata kidogo kama sikuwashukuru Viongozi wa Upinzani Bungeni; Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Naibu Kiongozi wa Upinzani, Dr. Willibrod Slaa, pamoja na Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani, kwa ushirikiano walionipa katika kufanya kazi zangu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kisiasa, kisayansi, kijamii na kadhalika, Sera na Sheria yetu ya Ulinzi imepitwa na wakati kwani ni ya zamani na haikidhi haja ya matakwa ya Jeshi la Karne ya 21 ya dunia inayoshuhudia maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri mwenye dhamana aliliambia Bunge lako Tukufu la Bajeti 2008/2009 kuwa, ataunda Kamati ya kushughulikia milipuko wa mabomu ya Mbagala; ninasema kuwa Kamati iliundwa na ilipewa muda wa mwisho wa mwezi wa tisa iwe imewasilisha Ripoti yake Wizarani na kupeleka kwa Kamati ya Ulinzi ili tuifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inauliza ni miaka miwili sasa tangu ahadi hiyo itolewe na Mheshimiwa Waziri; je, mchakato huo umefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya Pensheni ya Majeshi ya Ulinzi **"***The Defence Force Service Pensions and Gratuities Regulations"* inawanyima haki zao wanajeshi, wakati wanajeshi hao wallitakiwa na Serikali kuendelea kuitumika nchi zaidi ya miaka 36 lakini mafao yao ni ya miezi 36 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua ni wanajeshi wangapi wameathirika na Kanuni hii tangu pale ilipoanzishwa? Je, Serikali itakuwa tayari kutoa haki zinazostahili kwa wanajeshi baada ya marekebisho ya Kanuni hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika kipindi chote cha uhai wa Bunge hili Tukufu tumekuwa tukihoji umiliki wa Mgodi wa MEREMETA na Serikali imeshindwa

kutoa majibu sahihi kwa wananchi. Wakati huo huo tunakumbuka kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitamka kuwa masuala ya MEREMETA yako juu ya uwezo wake na yanahusiana na ulinzi na usalama wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani haikuridhika kabisa na majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusiana na suala zima la MEREMETA. Sisi tunawajibika kwa Wananchi na hivyo ni jukumu letu kuwaeleza Wananchi hasa wale waliofukuzwa katika maeneo ya machimbo ya dhahabu huko Musoma kwa kisingizio cha eneo la Jeshi; nini mustakbali wa MEREMETA na Kampuni tanzu yake ya *TANGOLD*?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu anaelewa ni watu gani ambao ni vinara wa ufisadi katika Mradi huo uliokuwa na nia njema kwa Jeshi letu la Wananchi. Kama tendo limefanywa na mtu mmoja mmoja ni kwa nini sura hiyo ya ufisadi inapewa Jeshi zima kama Taasisi? Tunawaomba Watanzania wasiondoe imani yao kwa Jeshi letu, bali waihukumu Serikali kwa kuwalinda watu wachache ambao wameharibu sifa nzuri ya Jeshi letu kwa manufaa yao binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamandi ya *Navy* – Kigamboni; katika kipindi cha hivi karibuni kumeibuka vitendo vya utekaji wa meli vinavyofanywa na Maharamia kuanzia Ghuba ya Aden na Bahari ya Hindi ya Afrika ya Mashariki kwa ujumla wake. Maharamia hawa wana athari kubwa za kisiasa, kiuchumi na kijamii, kwa nchi ambazo meli hizo zinatarajiwa kupeleka bidhaa.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwapatia Kambi ya *Navy* meli tatu kubwa za uhakika, zenye uwezo wa kuvuka Bahari Kuu ili kuweza kukabiliana na maharamia hao. Aidha, inaitaka Serikali kuipatia Kamandi ya *Navy* mafuta ya kutosha ili kuzifanya meli zetu ziweze kutembea na kufanya kazi iliyokusudiwa ili kuepuka kuchakaa iwapo zitakaa bandarini bila ya kufanya zoezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, JWTZ kumiliki maeneo; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaendelea na utaratibu wa upimaji wa maeneo ya JWTZ na JKT, sambamba na kuyapatia maeneo hayo hatimiliki na hatimaye kutolewa fidia kwa yale maeneo ambayo JWTZ na JKT waliyachukua kwa Wananchi kwa manufaa ya kijeshi. Kambi ya Upinzani inataka kujua maeneo yaliyopimwa na je, fidia imetolewa kwa Wananchi husika?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba ufafanuzi wa maeneo yafuatayo kwani mengi ya maeneo hayo yamezungukwa na makazi ya watu: Oldonyo Sambu JWTZ - Arusha; Kunduchi Transit Camp - Dar es Salaam; Bulombora JKT - Kigoma; Makutupora JKT - Dodoma; Kiabakari (253 KJ) - Mara; Biharamulo (23 KJ) - Kagera; Buhemba JKT - Mara; Maramba JKT - Tanga; Tunduru - TPDF; Mlale JKT - Ruvuma; Rwankoma JKT - Mara; Chita JKT - Morogoro; Umoja Camp JWTZ - Mtwara; Kasanga TPDF Det - Rukwa; Mgambo JKT - Tanga; na Ronsoti (TPDF) - Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia inataka kuelewa ni maeneo gani ya Wananchi yaliyochukuliwa na Jeshi la Ulinzi wa Taifa na ambayo hadi leo hayajapimwa na ni mangapi yana migogoro na Wananchi na ni hatua zipi Serikali itazichukua? Tunaamini kwa njia hii wahusika na maeneo hayo wanaweza kufanya utaratibu wa kuandaa makazi yao mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri, wakati wa kuhitimisha atoe ufafanuzi wa kina kwa suala hili, kwani Jeshi letu linajulikana Duniani kuwa ni Jeshi la Wananchi na mambo haya madogo yasipopatiwa ufumbuzi mapema, yanaweza kuchafua sura yake njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi wetu wanafanya kazi kwa maadili ya hali ya juu na inaonekana wanavumilia kwa kiasi kikubwa madeni wanayoidai Serikali. Ni vyema basi, Serikali ikaandaa mazingira ya kulipa madeni ya Askari JWTZ, JKT na Wazabuni ili kupunguza manung'uniko ya Askari kupata haki zao nyingi wanazostahiki na kwa wakati.

Kambi ya Upinzani inaitaka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuharakisha ukaguzi ili madeni yanayodaiwa yaweze kulipwa mapema toka Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inajifunza nini kwa kuendelea kulimbikiza madeni mbalimbali ya Askari wa JWTZ pamoja na madeni ya Wazabuni ambao hawalipwi inavyostahili hali inayotishia kupatikana kwa huduma za uhakika kwa Wanajeshi wetu? Je, Serikali haioni ni busara kuelewa kuwa katika Ulinzi ni vyema bajeti yao ikawa ya uhakika na ya kutosheleza?

Mheshimiwa Naibu Spika, JWTZ na JKT kuelekea Uchaguzi Mkuu 2010; Kambi ya Upinzani inarudia kutoa tahadhari kuwa Sera, Sheria na Kanuni za Ulinzi wa Taifa ziangaliwe upya ili tuweze kuboresha mazingira ya Kijeshi zaidi na ili kufuata Mfumo wa Siasa za Vyama Vingi. Katika hili Jeshi la ulinzi linatakiwa kuwa *non-partisan.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya Jeshi letu bado yanaonekana kujiimarisha kwa kufuata zaidi mipango, sera na mwelekeo wa chama kilichopo madarakani. Hili ni kosa kubwa, hivyo hali hii inazidi kutupa mashaka kama kweli Jeshi letu halitotumiwa na Chama cha Mapinduzi kutimiza mkakati wake wa kuhakikisha inashinda hata kama kura za Wananchi kwa chama hicho zitakuwa hazitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi hili ni la Watanzania wote bila ya kujali itikadi zao za kisiasa; hivyo, Kambi ya Upinzani inaamini Jeshi halitakiwi kufuata sera za chama chochote bali linatakiwa kufuata sheria za nchi na mipango yake au sera zake kama Jeshi la nchi bila ya kuegemea upande wowote wa chama cha siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya 147(3), imeeleza wazi kuwa, nanukuu; "Ni marufuku kwa Mwanajeshi yeyote kujiunga na chama chochote cha siasa, isipokuwa tu atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika ibara ya (5) ya Katiba hii." Ibara ya 147(4) inatafsiri "Mwanajeshi"

kuwa ni askari aliyeajiriwa kwa masharti ya muda au ya kudumu katika Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza au Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kambi ya Upinzani ina matumaini kuwa, upungufu uliotokea miaka iliyopita wa baadhi ya Wanajeshi kushabikia na kutumika kuhakikisha kuwa Chama Tawala kinashinda na hivyo kusahau wajibu wao, hayatajirudia tena katika Uchaguzi wa Oktoba 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani haitasita kumtaja hadharani askari wa aina yoyote ambaye atabainika anakwenda kinyume na maadili ya kazi yake kama ilivyoonekana katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 147(3).

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelewa kuwa kila jambo linaloendelea hapa nchini na pahala pengine Duniani ni lazima lihusiane na siasa; hivyo ni vigumu kabisa kwa binadamu yeyote ambaye ana uelewa wa kutosha kwa njia moja ama nyingine kutokuwa na itikadi ya kisiasa. Kambi ya Upinzani inachosema na kuwataka askari wetu, wajitahidi kudhibiti hisia zao binafsi za itikadi za siasa zinazoweza kupelekea kutumiwa na wale walio kwenye madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inakumbusha tena na tena kuwa, Jeshi la Wananchi ni Jeshi la Watanzania wote bila ya kubagua, hivyo linatakiwa kuwa ndiyo kioo katika utendaji wake kwa nyanja zote. Jambo hilo litawavutia vijana mahiri wenye uwezo mkubwa kitaaluma kuingia katika Jeshi kwa maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, sasa nitamwita Msemaji wa Kamati iliyohusika na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi atoe maoni ya Kamati.

**MHE. JANETH M. MASSABURI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2009/2010 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nachukua nafasi hii kumshukuru sana mume wangu Dokta Didas Massaburi; watoto wangu Steven, Juliana, Jacqueline, Angelina na Albetina. Mama yangu Felister, Baba yangu Mtikile na familia yangu yote kwa ujumla, kwa kunivumilia wakati wote na kunishauri vyema ninapokuwa kwenye majukumu ya kuwatumikia Wananchi hususan Wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam na Taifa zima kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii, kuwashukuru sana Wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam, kwa kuniamini na kunipa ushirikiano wa kutosha wakati wote ninapowawakilisha. Ninaamini wao pia ni mashahidi kwamba, sijawaangusha na wala sitawaangusha kamwe. Kubwa zaidi, tuendelee kuaminiana na kushirikiana bila kuyumbishwa bali tujipange vyema na kuendelea kuniamini ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakishukuru sana Chama cha Mapinduzi, hususan Uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam, kwa kuniongoza vyema na kunishauri mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninatoa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99 (7) na Kanuni ya 114(11), naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili Taarifa hii na kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ilikutana tarehe 2 Juni, 2010 ili kupokea na kuijadili Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa hiyo, Mheshimiwa Lawrence Masha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, alieleza pamoja na mambo mengine, kazi zilizofanyika kwa fedha zilizotengwa kwa kipindi cha 2009/2010. Maelezo hayo yalihusu Fungu 14 - Zimamoto na Uokoaji, Fungu 28 - Jeshi la Polisi, Fungu 29 - Magereza, Fungu 57 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Fungu 93 - Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kueleza Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Mheshimiwa Waziri alitueleza kuhusu utekelezaji wa malengo ya Bajeti kwa kipindi cha 2009/2010 ambapo alifafanua mambo mbalimbali yaliyotekelezwa na mafanikio yaliyopatikana. Aidha, tulielezwa kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati kila mara tulipokutana na Wizara hii. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, utekelezaji wa mipango ya Wizara umefanikiwa kwa kuzingatia maoni na ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kueleza Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Waziri aliieleza Kamati malengo

ya Wizara kwa Mwaka 2010/2011. Ufafanuzi kuhusu malengo hayo ulitolewa kwa mafungu yote na Wajumbe kupata nafasi ya kujadili kwa kina hatimaye kuridhika nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza vyema majukumu yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 446,347,481,000 kwa mafungu yote. Kati ya fedha hizo, shilingi 174,013,978,524 ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na Shilingi 155,914,301,776 zimetengwa kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijadili kwa kina taarifa ya utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2010/2011 na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2010/2011. Baada ya kupitia na kuchambua mafungu yote matano, Kamati inaunga mkono hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kuliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha maombi hayo kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati, naomba kuipongeza Serikali kwa mafanikio makubwa katika kuimarisha usalama wa raia na mali zao na kujenga imani ya wananchi kwa vyombo vya usalama vilivyo chini ya Wizara hii. Pamoja na pongezi hizo, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Jeshi la Polisi liimarishe usalama wa raia na mali zao, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali inapotangaza eneo jipya la utawala, suala la kujenga Vituo vya Polisi na Nyumba za Askari katika maeneo hayo lipewe umuhimu mkubwa;

(ii) Ili kuimarisha utekelezaji wa dhana ya ulinzi shirikishi, vituo vidogo vya Polisi vilivyojengwa zamani viimarishwe. Aidha, Mpango Mahususi wa Ujenzi wa Vituo vya Polisi Ngazi ya Kata kwa kuhusisha wananchi uandaliwe kama ilivyokuwa kwa Mpango wa Elimu ya Sekondari;

(iii) Kamati imeridhishwa na kazi nzuri ya ujenzi wa nyumba za Askari Polisi na kutoa pongezi. Tunashauri kuwa, umakini uongezwe katika usimamizi wa ujenzi huo. Aidha, ni vyema kutumia vikosi vya uhandisi vya majeshi yetu katika kuharakisha na kuimarisha utekelezaji wa miradi hiyo;

(iv) Kamati inalaani vikali utaratibu wa Wananchi kuvamia Vituo vya Polisi na kuua wahalifu. Tunashauri kuwa, ufumbuzi wa msingi wa tatizo hili upatikane haraka;

(v) Kikosi cha *Police Marine* kiimarishwe zaidi ili kukabiliana na changamoto mbalimbali za ulinzi na uhalifu katika bahari na maziwa yetu; na

(vi) Serikali iliwezeshe zaidi Jeshi la Polisi kifedha na kiufundi ili liendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia utendaji wa Jeshi la Magereza na malengo yake ya bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iongeze kasi ya kurekebisha Sheria zinazosababisha msongamano magerezani;

(ii) Jeshi la Magereza liwezeshwe kwa kupewa zana na bajeti ya kutosha ili liweze kuzalisha chakula cha kutosha;

(iii) Sheria ya *Parole* iangaliwe upya ili kukabiliana ipasavyo na tatizo la msongamano magerezani; na

(iv) Serikali iongeze kasi ya kutatua tatizo la nyumba kwa ajili ya Askari Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na majanga ya moto kwa ufanisi zaidi, Serikali ikiwezeshe Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji kwa kukipatia vitendea kazi muhimu na vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Uhamiaji, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iboreshe Vituo vya Uhamiaji mipakani kwa kuweka miundombinu ya utendaji wa vituo hivyo katika hali iliyo bora zaidi;

(ii) Tatizo la wahamiaji haramu litatuliwe kwa kutumia ujirani mwema baina yetu na nchi jirani; na

(iii) Zoezi la utambuzi wa raia kwa ajili ya kuandaa vitambulisho vya uraia likamilishwe haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kuwasambaza Wakimbizi waliopewa uraia kwa mpigo lisimamiwe kwa uangalifu na kushirikisha Kamati za Ulinzi na Usalama katika Mikoa na Wilaya husika. Aidha, taarifa kuhusu zoezi hilo zifikishwe kwenye Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kila mara.

(i) Baada ya kukamilisha uhakiki wa madeni ya Serikali, utekelezaji wa zoezi la kulipa madeni ya askari ufanyike haraka;

(ii) Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu yaende sambamba na kuimarisha ulinzi, amani na usalama kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo wananchi na mgambo; na

(iii) Ili kupunguza msongamano wa mashauri yanayofikishwa Polisi, Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha Mabaraza ya Kata ya Usuluhishi kuhusu makosa ya jinai ambayo yatatumika kutatua baadhi ya migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jinsi anavyoliongoza Bunge hili kwa kasi na viwango na kuliwezesha kuwa chombo halisi cha Wananchi. Tunampongeza pia Mheshimiwa Anne Makinda, Naibu Spika, kwa umahiri na uhodari wake kila mara alipomsaidia Mheshimiwa Spika. Aidha, pongezi za dhati tunazitoa kwa Wenyeviti wa Bunge chini ya Uongozi wa Spika, kwa kusimamia ipasavyo taratibu za uendeshaji wa Shughuli za Bunge kwa kipindi chote walipokusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana Mheshimiwa Lawrence K. Masha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, pamoja na Ndugu Mubaraka Abdulwakil, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii, kwa ushirikiano mzuri na maandalizi ya taarifa zenye maelezo ya kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Inspekta Jenerali Said A. Mwema, Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, kwa kuliongoza vyema Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, shukrani nazitoa kwa Kamishna Augustino Nanyoro, Mkuu wa Magereza Nchini, Kamishna Msaidizi Mohamed Kapamba, Mkuu wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji na Askari na Watumishi wote katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa utekelezaji mzuri wa majukumu ya Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa, naomba niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii, kwa busara zao na michango yao ya kina katika uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii na kukamilisha taarifa hii kwa wakati ili iwasilishwe mbele ya Bunge lako Tukufu. Ninaomba kuwatambua Wajumbe hao kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Wilson M. Masilingi - Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Col. Mst. Saleh. A. Farrah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Kahalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Dkt. John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Col. Mst. Feteh S. Mgeni, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Dkt. Ibrahim S. Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mhangama, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Muhammad I. Sanya, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Magalle John Shibuda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuhitimisha kwa kuwashukuru Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, akiwemo Katibu wa Kamati hii, Ndugu Stella Mlambo, kwa kuratibu vyema na kufanikisha shughuli za Kamati kama zilivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI NA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *Bismillahi Rahman Rahim*. Ni wajibu wetu kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kuwepo hapa tukiwa hai na wenye afya na kujadili mambo muhimu yanayogusa maslahi ya Umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, Kanuni ya 99(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Chama changu cha Wananchi (*CUF*), Wanachama na Wapiga kura wangu wa Jimbo la Mji Mkongwe, Zanzibar, kwa imani kubwa na ninawashukuru sana kwa kunipitisha tena kuwa Mgombea wa Kiti cha Ubunge katika Jimbo hilo. Ninatoa ahadi kuwa, nitaendelea kuwatumikia kwa uwezo wangu wote ndani na nje ya Bunge ili kuhakikisha kuwa malengo yetu yanatimia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kuushukuru Uongozi wa Kambi ya Upinzani chini ya Mheshimiwa Hamad Rashid, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Slaa, kwa mchango wao mkubwa katika kuniwezesha kuwa Mwakilishi bora wa Wananchi hapa Bungeni. Pia ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa ushirikiano wao mzuri wanaonipa katika kutimiza wajibu wangu kama Waziri Kivuli wa Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza Viongozi wawili wa Zanzibar, yaani Mheshimiwa Dr. Aman Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi *(CUF)*. Hawa ni Viongozi mahiri na wa kupigiwa mfano na wawe ni kigezo kwa Bara la Afrika, ambalo mara nyingi tumeshuhudia jinsi nchi mbalimbali zinavyokumbwa na mifarakano ya kisiasa ambayo hupelekea machafuko na hata mapigano yanayopoteza maisha ya raia na mali zao. Heshima za nchi hizo hushuka, hurudisha nyuma maendeleo na kuchukua muda mrefu kuweza kufuta makovu ambayo yangeweza kuepukika iwapo wangetumia meza ya duara na kalamu kwa mazungumzo yanayoweza kuleta faraja na kuepusha shari kama walivyofanya Rais Karume na Maalim Seif. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya Jeshi la Polisi na hali ya Usalama hapa nchini; kwa mujibu wa takwimu zilizopo zinaonesha kuwa, kuna ongezeko la makosa ya

jinai 69,134 yaliyoripotiwa katika Vituo vya Polisi kwa mwaka 2009, ukilinganisha na makosa ya jinai ya 68,023 ya mwaka 2008, hivyo kuna ongezeko la makosa ya jiani 1,111. Ajali za barabarani nazo zimeongezeka hadi kufikia 22,019 katika mwaka 2009, ukilinganisha na ajali 17,768 za 2008. Hii ni hatari kwa nchi changa kama zetu, kwa vile zinapotokea ajali, mali hupotea na watu ambao ndiyo nguvu kazi hupoteza maisha au kubaki na ulemavu wa maisha. Vile vile gharama za matibabu huwa ni kubwa na hivyo kudumaza maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya biashara ya madawa ya kulevya bado ni kitendawili, ingawa jeshi la polisi linajitahidi na pale wanapopata taarifa hufanya kazi za ziada, lakini bado vigogo wa biashara hii wapo na biashara inashamiri. Kigezo cha kushamiri kwa biashara hii ni kuongezeka kwa watumiaji wa madawa haya au kwa jina lingine huitwa "Wateja". Tunaomba jitihada zaidi ziwepo kwani vijana hawa ndiyo tegemea na nguvu kazi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ujenzi wa demokrasia ya kweli na kwa dhamira nzuri, nchi yetu inalazimika kufanya mabadiliko mazito katika taasisi zake nyingi ili kuondoa dhana ya chama kushika hatamu. Moja kati ya mabadiliko hayo yanavihusu vyombo vyote vya ulinzi kwa ujumla wake, lakini kwa hapa leo nitagusia tena Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitairudia tena kauli yangu niliyoitoa katika hotuba yangu ya mwaka 2007/2008 kwamba, Taasisi ya Umoja wa Mataifa inayoitwa *United Nations International Police Task Force inasema, naomba kunukuu: "In democratic society, the police serve to protect rather than to impede freedoms, the very purpose of police is to provide a safe orderly environment in which these freedoms can be exercised."*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kujiuliza je, Jeshi letu la Polisi linaendana na nukuu hiyo? Kulingana na hali halisi iliyopo katika jamii ya Kitanzania inayoanza kuzoea mfumo wa siasa za vyama vingi kwa minajili ya kuleta mfumo mpya ndani ya Jeshi la Polisi; basi ni vyema Sheria Namba Tano ya Mwaka 1992 ikatumika ipasavyo. Sheria hii ndiyo iliyofungua milango ya Siasa ya Vyama Vingi hapa Tanzania. Sheria hii imetamka wazi kutohusisha taasisi za umma na vyombo vya ulinzi katika harakati za kisiasa, lakini inasemekana kwamba, bado wapo baadhi ya Askari Polisi, bila ya kificho wala woga ila kwa utashi wao tu, hawajaonesha kubadilika kitabia katika mfumo wa Siasa za Vyama Vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wote lazima waelewe kwamba, hiki ni kipindi muhimu sana kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu. Hapa ni pahala pa kujipima ni kiasi gani nchi yetu imepea kidemokrasia. Uchaguzi Mkuu unaotukabili wa mwezi wa Oktoba uwe ni kioo kwa nchi yetu, Afrika na Dunia nzima. Tuwe wastaarabu na tuachane na fitina zisizo za msingi, kwani sote tunachotafuta ni uongozi na siyo ufalme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawaomba pia wagombea wote na wa vyama vyote, watumie nafasi ya kujinadi kupitia ilani za vyama vyao na siyo vyenginevyo ili

tusikaribishe fitina na lugha chafu zinazoweza kuleta mfarakano na machafuko yanayoweza kuzaa vurugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wabaki kuwa walinzi wakati wote wa zoezi la kampeni hadi kufikia siku ya uchaguzi. Ni mategemeo yetu kuwa, IGP Mwema ni msomi mzuri, mchapakazi mahiri na anaweza kusimamia Jeshi lake ili wasitokee baadhi ya Askari kuwa na utashi wa kisiasa au kutumiwa na baadhi ya Viongozi walio na upofu wa demokrasia kutaka kushabikia kundi fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi za dhati zimwendee IGP Mwema, kwa busara zake za kutunga kijitabu kidogo kinachoitwa "Haki na Wajibu wa Mpiga Kura" ambacho kinaelekeza ni namna gani mchakato mzima wa uchaguzi unavyotakiwa uwe kuanzia kampeni, upigaji wa kura hadi kutangazwa kwa mshindi. Ni vyema kumpongeza kwani kitabu hiki kitawasaidia siyo tu wapiga kura wa nchi hii, bali hata polisi kujua wajibu wao wakati wote wa zoezi hilo. Hii inaonesha ukomavu wa IGP Mwema kujiandalia yeye mwenyewe mazingira mema kwa Jeshi lake katika wakati huu wa kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu na ni tofauti na IGP ambaye badala ya kujenga mazingira kama haya yeye alifanya tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli uliowazi kuwa, juhudi kubwa zinazofanywa na IGP kuweza kulifanya Jeshi letu la Polisi kuwa la kisasa na linalokwenda kisanyansi, zinakwama kutokana na Serikali kutokutoa kipaumbele kwa Jeshi hili. Ukiangalia bajeti ya maendeleo iliyotengwa katika mwaka huu ya shilingi 18,967,837,000 ni pungufu kwa shilingi 921,163,000 ukilinganisha na bajeti ya mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inauliza hivi ni kweli tuko makini na kulifanya Jeshi letu la Polisi kuwa la kisasa katika nyanja zote au ni maneno ya kuwapa moyo Askari wetu ambao miaka yote wanafanya kazi zao katika mazingira magumu waendelee kuteseka?

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Polisi kupata uhamisho ni haki yao kwa mujibu wa Sheria za Jeshi hilo. Cha kushangaza na kusikitisha ni pale ambapo Askari hupewa uhamisho bila ya kuzingatia haki zao za msingi. Suala hili ni gumu na ni dhahiri kwamba, tunakuwa hatuwatendei haki Askari Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo askari ambao wamepata uhamisho toka Zanzibar na kuja upande wa pili wa Muungano. Leo ni zaidi ya mwaka, lakini wengi wao bado kabisa hawajafikiriwa kulipwa fedha zao na kila wanapodai wanapewa ahadi hewa ambazo huwafanya kuvunjika moyo katika utendaji wa kazi zao za kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi utamtumaje Askari Polisi kwenda kusimamia au kuvunja maandamano ambayo wafanyakazi huwa wanadai haki zao zinazofanana na madai ya askari?

Je; ni kweli polisi watafanya kazi zao iwapo na wao wenyewe wana madai kama ya wenzao? Tunaomba walipwe tena haraka na iwapo fedha za uhamisho hazipo basi

warejeshwe makwao na Wizara hii ihakikishe kuanzia sasa uhamisho uambatane na hundi zao, la sio hivyo zoezi hilo lisitishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, madai ya wazabuni limekuwa ni tatizo sugu ambalo Wizara hii imelifumbia macho. Tunaomba wazabuni hawa walipwe kwani na wao wanadaiwa na mabenki mbalimbali ya nje na ndani ya nchi, ambayo huwa yanawapandishia riba. Vile vile kuchelewesha kuwalipa huzorotesha kutoa tena huduma kwa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonyesha kuwa, kiasi cha shilingi 245,376,758 kilipokelewa lakini hakikuingizwa katika Akaunti ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Hii maana yake ni kwamba, kuna uwezekano mkubwa fedha hizo ziliishia mifukoni mwa wajanja ndani ya Jeshi hilo. Hivyo basi, tunaitaka Serikali kulitolea kauli suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama wa nchi hii unakuwepo pale tu Askari Polisi wanapokuwa nao salama, kwa maana kuwa wanachokipata kinakidhi mahitaji ya familia zao. Katika Bajeti ya Usalama wa Raia mwaka 2006, Waziri alitangaza humu Bungeni kuwa, Askari Polisi watapewa shilingi 200,000 kwa mwaka ikiwa ni fedha za matibabu. Mwaka 2007 tukaelezwa kuwa fedha hizo ni kidogo kweli na hivyo wanafanyiwa utaratibu wa kuingizwa katika mfumo wa Bima ya Afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ni kuwa, fedha hizo shilingi 200,000 hazikulipwa kwani ilitakiwa ziwekwe katika mishahara yao ya kila mwezi. Utaratibu wa Bima ya Afya ni kuwa Mwanachama anakatwa kwenye mshahara wake wa kila mwezi.

Hii inaonesha kuwa, Askari Polisi wamepigwa changa la macho na Serikali haisemi ukweli! Je, usalama wa nchi yetu upo? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa majibu sahihi kwa Watanzania kuhusiana na ahadi zake zisizotekelezeka kwa Askari Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Wizara na Idara nyingi za Serikali kuna bajeti ya kuwahudumia watumishi wao wanapopatwa na majanga mbalimbali kama vile kufiwa na mengineyo. Jambo hili ni jema mno na linasaidia kupandisha ari ya mtumishi na uaminifu kwa mwajiri wake. Utaratibu huu haupo katika Jeshi la Polisi kwani askari analazimishwa kuchangia shs.5000/- kila mwezi kwa kadhia hiyo. Amri inatoka ngazi ya juu bila kukubaliana na askari wote. Kumbuka Jeshi la Polisi hakuna chama cha wafanyakazi, hivyo askari hawana mtetezi katika suala zima la maslahi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuchangia mfuko kama huo ni hiari ya mtu mahali popote pale katika sehemu za kazi, hivyo kukatwa kwenye mshahara bila idhini ya askari ni kinyume kabisa na ni uonevu mkubwa kwa askari hao ambao mishahara yao kabla hata ya makato haitoshi kabisa. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alitolee kauli suala hili ambalo tunaamini kuwa ni kinyume cha misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza uimara wa viongozi wa juu katika Jeshi la Polisi umeanzishwa mfuko wa *URA SACCOS* ambao kila askari anatakiwa kutoa kiingilio cha shs. 50, 000 na makato ya shs. 5000/- kila mwezi. Askari atakayeshindwa kuwa mwanachama maana yake ni kwamba hatodhaminiwa wakati atakapohitaji kupata mkopo kutoka kwenye mabenki ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani katika bajeti yake ya mwaka 2007 iliitaka Jeshi la Polisi kufuata *Police General Order* zake zinazomtaka askari kila baada ya miaka mitatu kwenda mafunzo na akirudi apandishwe cheo. Kwa masikikitiko makubwa Jeshi hili linashindwa kusimamia kanuni zake. Hivyo, tunaomba mafunzo yawe yanatolewa kwa muda muafaka ili askari wawe wanapanda vyeo kwa mujibu wa sheria za Jeshi la Polisi. Tunamtaka *IGP* aliangalie vizuri suala la maslahi ya askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wetu kwa kweli wanaishi katika mazingira ambayo si salama kwao na afya zao, hivyo ile kauli ya kusema kuwa usalama wa nchi ni shwari si kweli. Kama askari hawako salama usalama wa nchi utatoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, askari kutokana na ugumu wa makaazi inawabidi wajenge nyumba zao za matope ndani ya eneo la nyumba za polisi kwa gharama zao wenyewe. Mfano mzuri Waziri akajionee mwenyewe hapa Dodoma, pale *police line* jinsi nyumba za matope zilivyojengwa ambazo ni za askari wanaolinda usalama na mali za wananchi na viongozi wa nchi. Kambi ya Upinzani inauliza Serikali inayaona madhila haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri ya mwaka 2006/2007, alisema kuwa Serikali inaanza maandalizi ya ujenzi wa chuo cha *CID* hapa Dodoma. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe tathmini ya maendeleo ya ujenzi wa chuo hicho, kwani imekuwa ni kawaida Serikali kuomba fedha hapa Bungeni lakini utekelezaji wake unakuwa haupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukio lililotokea huko Moshi katika Hospitali ya *KCMC* kwa vijana kuvamia na kupiga watu kama ilivyoripotiwa na baadhi ya magazeti ni la kusikitisha na ni la kihuni lakini kwa kuwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kilimanjaro bwana Lucas Ngoboko amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kufafanua kuwa uchunguzi wa awali umeonyesha tukio hilo lilichochewa zaidi na ushabiki wa kisiasa. Hivyo, tunaomba uchunguzi huo ufanyike kwa kina ili wale watakaobainika kufanya vurugu hizo waweze kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hatukuwa waangalifu na kuzuia matukio ya aina hii mapema basi tunaweza kuitumbukiza nchi hii katika dimbwi la chuki na kuweza kuzaa vurugu, hasa ukizingatia kuwa vijana hawa walivamia eneo muhimu la hospitali ya *KCMC* ambapo hapatakiwi kuingizwa fujo za aina yeyote zinazoweza kupelekea wagonjwa kukosa utulivu na kupata tiba na hata kuwafanya madaktari kutofanya kazi zao inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo askari polisi ambao inasemekana wamefanya mambo ya unyanyasaji yanayokwenda kinyume na sheria ya Jeshi la Polisi huko Tarime ni kitendo cha kusikitisha. Hivyo, tunaomba uchunguzi wa kina ufanywe na kama ushahidi wa tukio hilo utathibitishwa basi askari hao wachukuliwe hatua kali za kinidhamu ili iwe fundisho kwa wengine na kuliweka Jeshi la Polisi kuwa safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya uhamiaji ni muhimili mkubwa wa kuangalia mzunguko mzima wa wageni wanaoingia na kutoka katika nchi hii, uimara au ulegevu wa idara hii unaweza kusababisha mafanikio au madhara makubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufanikiwa au kutofanikiwa kwa chaguzi katika nchi nyingi kwa kiasi kikubwa huchangiwa na takwimu za wageni wanaopewa au kutopewa idhini ya kupiga kura katika nchi mbalimbali. Hapa inasemekana kwamba wageni kadhaa wamekwisha jiandikisha katika daftari la kudumu la kupiga kura kwa pande zote za Muungano, hili linaweza kupelekea kuvuruga matokeo ya kura zitakazopigwa, hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulitolea kauli suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonyesha kuwa makusanyo ya shs.3, 083,580,051/- kutoka ofisi ya Zanzibar hayakuwasilishwa makao makuu. Aidha, makusanyo ya *USD* 75,580 sawa na shs. 92,963,400/- toka Arusha hayakuonyeshwa katika taarifa za benki, maana yake ni kwamba fedha hizo bado ziko ofisini kwa mtunza fedha hadi sasa? Sambamba na hilo ni kwamba makusanyo ya mwezi wa mei toka huko huko Arusha ya shs.42, 505,000/- hayakupelekwa benki wala kuingizwa vitabuni. Huu ni ukiukwaji wa kanuni za kiuhasibu au ni wizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuimarisha kitengo cha ukaguzi wa ndani ili kiweze kukagua mara kwa mara na sio kusubiri Mkaguzi Mkuu wa Serikali ndiye agundue kasoro hizo wakati zingeweza kugundulika mapema na hatua zikachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya magereza yetu bado ni mbaya ukilinganisha na idadi ya wafungwa wanaoishi humo. Kwani magereza hayo yamezidiwa maradufu na uwezo uliyonayo. Tuelewe mfungwa mbali ya kuwa ni mfungwa lakini bado anabaki kuwa raia ambaye anahitaji huduma bora za Serikali ikiwemo chakula na namna anavyoishi katika magereza. Tunaitaka Serikali kupitia Wizara hii kutenga fedha za kutosha na kutafuta maeneo mengine ili wajengewe magereza mapya na kuwafanya wafungwa waweze kuishi kwa mujibu wa sheria za Kimataifa na sio kuwekwa ndani kama vile sio binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupitia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, inaonyesha kuwa idara hii ilinunua gari la kutoa huduma ya zima moto lenye thamani ya shs.705, 197,958/- lakini hadi sasa gari hilo halijapokelewa. Kambi ya Upinzani inashindwa kuamini kama kweli fedha hizo zililipwa kwa ajili ya gari hilo au ni maandishi tu wakati fedha zilikwenda sehemu nyingine ya kifisadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuna malipo yaliyofanywa ili kununua saruji tani 130 yenye thamani ya shs.22, 040,000/- lakini hadi taarifa hii inawasilishwa saruji haikupokelewa. Kambi ya Upinzani inashindwa kuelewa inachukua muda gani kuleta saruji ambayo inapatikana hapa hapa nchini? Ni bora tukapata maelezo ya ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, gari aina ya *bus* ya *IVECO* lenye namba ya usajili STJ 9578 lilipelekwa *INCAR (T) Limited* kwa matengenezo yaliyogharimu Tshs 5,877,641/- toka mwaka 2007 na hadi leo *bus* hilo halijarejeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo inasemekana kulikuwa na udanganyifu wa deni la shs. 378,846,239/- wakati deni halisi lilikuwa ni shs.224, 768,115/- na hivyo kusababisha tofauti ya shs.154, 078,124/=

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni njia nyingine ya wizi ambao unasababisha Jeshi la Polisi kutokuwa katika nafasi ya kuweza kujibadilisha kwa askari wake na vitendea kazi. Inawezekana wizi huu wa kuongeza madeni ni mtandao ambao umekuwepo siku nyingi katika taasisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hii ni hotuba yangu ya mwisho katika muongo huu wa 2005-2010 kama Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii, ni wajibu wangu nimpongeze Spika, wewe Naibu wake pamoja na Wenyeviti wako wote watatu kwa mashirikiano mazuri, busara na umahiri mkubwa kwa kuliendesha Bunge letu hili. Ili pia nisiwe mwizi wa fadhila nimshukuru Katibu wa Bunge pamoja na wasaidizi wake wote wanaotusaidia katika shughuli zetu za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza wafanyakazi wote wa ofisi yako kwa huduma zao mbalimbali walizokuwa wanatupatia. Lakini mbali na hilo niwashukuru kwa dhati kabisa wakazi wote wa jiji la Dodoma, kwani sehemu kubwa ya mahitaji yetu mbalimbali huwategemea wao. Tunamuomba Mungu kwa kila mwenye dhamira nzuri kwa nchi hii, *Inshallah* atarudi katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, kwa mara nyingine nawashukuru sana sana wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Mji Mkongwe. Nawaahidi kuwa nitaendelea kuwaheshimu, kuwaenzi na kufanya kazi nao bila ya ubaguzi na pale nitapokosea nawaomba wanikosoe na nitakuwa tayari kuchukua ushauri wao ili niwe kiongozi bora kwao na Taifa letu.

Hongereni watu wa Jimbo langu la Mji Mkongwe na nawashukuru kwa kunipa kura za kutosha katika kura za maoni. Kwa hilo hamjakosea na mtapata matunda yake. *Viva* Mji Mkongwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha na kuitaka hotuba yangu hii yote ichukuliwe kama ilivyo katika *Hansard*. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana wamesikia watu wa Mji Mkongwe. Waheshimiwa Wabunge utaartibu wetu wa jumamosi kidogo una kuwa una tatizo lake, kwa hiyo, naona niwatambulishe kwanza wageni halafu nitoe na matangazo ya kazi kwa baadhi ya

Kamati. Waheshimiwa Wabunge waliopo hapa Bungeni asubuhi hii ni wageni wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Watendaji Wakuu wa Wizara ni kama ifuatavyo:-

Kuna Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ndugu Baraka Abdulwakil, kuna Naibu Katibu Mkuu ambaye ni Ndugu Elizabeth Nyambibo, ahsante sana. Tunaye *Inspector General* wa Polisi Ndugu Saidi Mwema, Bunge zima linakupongeza kwa kitabu hicho ulichogawia nchi, nashukuru sana. Tuna Kamishna Mkuu wa Magereza, ndugu Agustino Nanyaro, tuna Mtendaji Mkuu wa vitambulisho vya Taifa ambaye na sisi wote tunamfahamu Ndugu Dickson Maimu nafikiri hayupo, yupo upande mwingine. Basi tunashukuru na tunaomba hiyo kazi iweze kufanyika vizuri kwa sababu ni muhimu sana.

Pia tuna Kamishna wa Polisi *Operation,* huyu ni Ndugu Paulo Chagonja, tuna Kamishna wa Polisi Zanzibar huyu ni Ndugu Mussa Ali Mussa, ahsante karibu sana, tuna Kamishna wa Magereza, Utawala na Fedha Ndugu Elias Nkuku, ahsante sana. Tuna Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar Ndugu Mwichumu Salum, ahsante sana. Tuna Kamishna *General* wa Jeshi la zimamoto na uokoaji, Ndugu Matwani Kapamba, ahsante sana, karibu. Tuna Kamishna Uhamiaji, Utawala na Fedha, Ndugu Peniel Mgonja ahsante sana.

Tuna Kamishna wa Polisi, Utawala na rasilimali watu, Ndugu Lodwing Mtweve, ahsante karibu sana, huyu ni jirani yangu kule kwetu Njombe na tuna Kamishna wa Mipaka na Operesheni Ndugu Philo Nombo, ahsante sana. Halafu wageni wengine wa Wizara hii ni Manaibu Kamishna, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo mbalimbali wa Wizara ya Mambo ya Ndani, popote walipo kila mahali wasimame tuwaone, ahsanteni sana tunawakaribisha wote ambao wapo hapa.

Halafu tuna wageni wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Katibu Mkuu, Ndugu Andrew Nyumayo, ahsante sana. Tuna Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Wananchi Tanzania, Ndugu Luteni General Abdulrahman Shimbo. Tunaambiwa Ndugu Mamnyange, yeye amesafiri lakini amewakilishwa vizuri. Tuna Mkuu wa JKT *Major General* Samuel Kitundu, ahsante sana. tuna Kamishna wa Sera na Mipango, Ndugu A.H.B. Gayonga, ahsante sana. Halafu tuna Mabrigedia *General* wote, Makamishena wasaidizi wote, Makanali wote, Wapiganaji wote na Wajumbe kama 52 wa Baraza la Wafanyakazi. Kwanza nianze na wale wanajeshi wenyewe naomba wote walioko wasimame na Wabunge wawaone, ahsante sana karibuni sana.

Halafu tuna wapiganaji wote na wajumbe 52 wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, hao nao wasimame walipo, ahsanteni sana na wengine wote ambao hatukuwataja hapa lakini wanakaribishwa kwa sababu Bunge hili ni kwa watu wote.

Kwa namna ya pekee ninao wageni wa Mheshimiwa Dr. John E. Nchimbi, Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hawa ni mke wake na watoto wake, naomba wasimame, ahsanteni sana ana watoto wawili na mke wake. Watoto mmoja ni John na mwingine ni Joan.

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Waziri Prof. Juma Kapuya, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ya *ZETSSF* ambao wamekuja kukagua miradi ya *NSSF* Dodoma ikiwemo Jengo la Bunge, hawa ni Ndugu Rashid Kibao, Ndugu Tarib Mbwana, Ndugu Sarah na yupo Ndugu Juma H. Mussa na yupo Ndugu Abdulwakil Hafidh yeye ni Mkurugenzi wa *ZETSSF*, karibuni sana na ni vizuri kujifunza kutokana na vyombo vinavyofanana katika kufanya kazi zao na kama mtakavyoona *NSSF* na wenzao wamejenga Chuo Kikuu kule cha *UDOM*.

Halafu tuna viongozi wanne wa asasi ya *The East African* Nguvu kazi na Juakali *Partners*, karibuni sana wamekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge. Tumesikia habari zenu, nguvu kazi ni huku kwetu na jua kali ni kule Kenya, nadhani na ninyi mtabadilisha hivyo.

Halafu tuna watumishi tisa wa Idara ya Huduma kwa Jamii iliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, wamekuja kwa ajili ya kusikiliza hotuba ya Wizara yao. Nao sijui wako wapi inawezekana ukumbi wamejaa kwa hiyo wako *basement*. Pia wageni wengine wote walioko hapa tunawakaribisha, hawa tumewatambulisha kwa sababu majina yao yamekuja lakini wote wanakaribishwa.

Baada ya matangazo ya wageni sasa tuna matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaang' anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na mkutano katika ukumbi wa namba 231, saa saba mchana, nashukuru umefanya saa saba mchana maanake idadi yetu wakienda kwenye Kamati itakuwa haitoshi kabisa.

Halafu Mwenyekiti wa Chama cha Kibunge kinachojishughulisha na masuala ya idadi ya watu na maendeleo ambae ni Mheshimiwa Paul Kimiti, anaomba niwatangazie wajumbe wa Chama cha Kibunge kinachoshughulikia masuala ya idadi ya watu na maendeleo wakishirikiana na Chama cha Wabunge kinachoshughulikia masuala ya UKIMWI, *TAPAC* kwamba kesho siku ya jumapili tarehe 27 Juni, 2010 saa tano asubuhi kutakuwa na kikao cha vyama hivyo kitakachofanyika Dodoma *Hotel*. Wanachama wote wanaombwa wasikose kuhudhuria maana hiki ndio kikao chao cha mwisho kwa Bunge hili, kwa hiyo, wanachama wa *TAPAC* na wanachama wa *TPAPD* wanatakiwa wahudhurie kesho saa tano Dodoma *Hotel*.

Baada ya kusema hayo tunaendelea na shughuli zinazofuata. Waheshimiwa Wabunge tunao wachangiaji wengi sana lakini tutaishia asubuhi hii tu basi. Kwa hiyo, wale ambao hawajachangia hata mara moja ndio watakaopewa nafasi, halafu waliochangia mara mbili bahati mbaya kwa suala hilo. Kwa hiyo, tunamuita kwanza Dr. Wilbroad Slaa atafuatiwa na Mheshimiwa Idd Azan, atafuatiwa na Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Khasim Issa atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Juma Seleweji, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Mwera, atafuatiwa na Mheshimiwa James Lembeli, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Juma Haji na Mheshimiwa Meryce Emmanuel atafuatiwa na James Musalika. Hao wanatosha asubuhi hii.

**MHE.DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niwapongeze Mawaziri wote na wataalam wao wote bila kuingia kwenye kutaja majina mmoja mmoja kwa ajili ya muda. Niwapongeze vile vile wakuu wa vyombo vyetu vyote vya jeshi, nao pia kwa ajili ya muda nisitaje mmoja mmoja. Nimpongeze vile vile Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani ambao naungana na hoja zake zote, wote wawili naungana na hoja zao zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze na mambo labda ya Jimbo la Karatu kwa sababu ambayo ilinifanya kwanza nisimame, Waziri amenituliza kidogo ilikuwa leo nimwambie kwamba ile heka 50 tulizompa kwa ajili ya ujenzi wa magereza Karatu tunaliondoa, lakini naona ameliweka kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana. Ametaja juu ya Kituo cha Polisi nimepitia kitabu chake chote sikukiona kiko wapi, lakini asubuhi alikuwa ananihakikishia kwamba kipo sasa, Waziri labda baadaye atapenda kunithibitishia iko wapi kwa sababu kwenye maandishi haipo, sasa isiwe ameniambia halafu ikawa imeishia hapo, ikiwa ni pamoja na gari, pamoja na nyumba za askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo mawili yanayohusu Jimbo la Karatu, labda niseme la jumla pia kwa Mheshimiwa Waziri wa Jeshi letu la Ulinzi, jambo *specific*, jambo maalum kwa ajili ya jeshi letu, kikosi cha 39 *KJ* Arusha sihitaji kulizungumzia nimeshampa kwa maandishi nadhani inahitaji tu achukue hatua, pamoja na mambo mengine yaliyoko mle ndani kwa sababu ya muda sitaki kuyazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme vile vile kwamba ningependa sasa nizungumze mambo yafuatayo:-

La kwanza, ni kuhusu utendaji kazi wa jeshi letu kwa ujumla jeshi letu linafanya kazi nzuri, hata mimi ni muumini sana wa Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi na naamini majeshi yetu yote yakikosekana kwa sekunde moja Watanzania tutakatana mapanga. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuwa na majeshi yetu yote. Lakini niseme kwamba kuna wachache ndani ya jeshi ambao wanachafua sura nzuri ya jeshi letu na sasa haya ninayoyasema naomba Waziri anisikilize na atupe majibu ya kina. Kitendo kilichotokea Moshi kiko ndani ya hotuba ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama ni kweli nilichosoma kwenye magazeti kwamba hawa ni vijana walitoka kwenye Kambi ya Chama Cha Mapinduzi kilichokuwa kule Kibosho wakaandamana chini ya usimamizi wa Polisi wakapiga watu njiani na walipokimbilia eneo la *KCMC* ndani ya jengo la Hospitali wakafuatana ndani wakawapiga mbele ya Polisi. Mheshimiwa Waziri tunahitaji maelezo ya kina kwa sababu kwanza tunahitaji sasa ufafanuzi, jeshi hili au watu hawa wanaotoka Kambi inayofanya kazi ya ukakamavu ni watu gani na ukakamavu huu ni nini? *(Makofi)*

Serikali imetangaza mara nyingi kwamba jeshi ni moja na ile iliyoko katika Katiba, hakuna majeshi mengine na watu hawaruhusiwi na Sheria tuliyopitisha juzi

imekataza. Lakini hawa wanakwenda kwenye Kambi wanafundisha, Wanakwenda kupiga watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliunganishe hilo na matukio yaliyopita kwa sababu Waziri amesema ametunga kitabu. Naomba nimhakikishie kwamba kutunga kitabu peke yake haitoshi kama hamtasimamia haki nyie wenyewe. Kule Tarime tulipata matatizo, lakini yalianzia Kiteto ambapo tulitambua vijana ambao walikwenda kupiga vijana wetu. Wamewapiga ndani ya Kituo cha Polisi Kijungu, tukawatambua ni akina nani, ni vijana wa CCM waliotoka Dar es Salaam. Tukatoa taarifa wamepiga vijana wetu ndani ya Kituo cha Polisi na baadaye vijana wangu wengine wakiwemo Wabunge waliokuwa kwenye eneo hilo walipopewa taarifa wakaenda nao wakakamatwa na wao wakapigwa ndani ya Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji maelezo, haitoshi kutuambia umeandika kitabu. Tunataka namna gani jeshi lako litajitenganisha na siasa, jeshi lako litaacha ubaguzi, jeshi lako litalinda sheria ya nchi hii. Wale waliofanya kazi hiyo mpaka leo wapi, yule *OCD* mwenyewe yuko. Mimi mwenyewe nimekwenda kufuatwa kwenye Kituo cha Polisi, Kituo Kikuu cha Mjini na sikumbuki jina tena, Kiteto pale. Nimekuta wale waliopigwa wanatoka damu, wameumia sana, ndiyo wamewekwa ndani badala ya wale waliowapiga. Hiki ni kitendo kisichokubalika kwa kigezo chochote na hakuna kesi inayoendelea mpaka leo. Haya hatuwezi mkatuambia tu kwamba mmeandika kitabu. *(Makofi)*

La pili, ni kitendo kilichotokea Busanda. Vijana wangu saa sita usiku wamevamiwa kwenye *Guest* waliyolala, wamekwenda kupigwa, wamepelekwa kwa Diwani. Mbunge wa Chama Tawala alikuwepo kwenye eneo hilo. Wamekatwa mapanga, askari afande Anakleti anayajua yote haya. Mpaka leo hakuna kinachoendelea. Hawa watu wanaopiga ni wale wale ambao tuliwatambua Kiteto, tumewatambua Tarime, wametufuata mpaka kule kwingine. Lakini haya hayachukuliwi hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba, tunakwenda kwenye uchaguzi, kwa niaba ya vyama vyote iwe CCM, iwe CHADEMA, iwe vyama vingine vyote, naomba Sheria isimamiwe na majeshi yetu kazi yao ya kwanza iwe ni kusimamia Sheria, si kulinda chama chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, niseme kwa ufupi sana, jeshi letu linachafuliwa na watu wachache na niseme kwamba Mheshimiwa Waziri ukiona kwamba wananchi wanachukua Sheria mikononi ni kwa sababu Sheria zako zimeshindikana, hazitunzwi, hazilindwi, hazifuatwi. Sheria ikivunjika, Sheria ikishindikana wananchi watachukua hatua mikononi. Siwaungi mkono wale wananchi wanaochukua hatua mikononi kwa sababu wataumiza na wasiohusika. Lakini ni kwa sababu sisi kama vyombo vya dola hatutafuti misingi ya matatizo haya. Sababu iliyotokea juzi Hedaru umeitaja, lakini sababu yake nini. Kitendo kilichotokea cha kuwalambisha akina mama sehemu za siri kule Tarime, hayo yote ni matukio ambayo hayatakiwi kuwepo katika nchi ambayo kweli inafuata mfumo wa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Karatu Mheshimiwa Waziri nimemwambia, na Mheshimiwa Waziri kweli amenipa kauli nzuri kila wakati kwamba Jeshi la Polisi limefika mahali, sasa linamlinda tajiri mmoja na nimempa majina ya watu ambao wamelalamika. Tunaomba kujua hatua gani zinachukuliwa. Mtu ameuawa kwenye Ofisi, amepigwa kwenye Ofisi, Mtendaji wa Kijiji anasema jamani acheni kumpiga, wananchi wameandika *affidavit* wameleta polisi kwenu kwamba tumeona huyu mtu amepigwa mpaka amekufa njiani, lakini polisi haichukui hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kulindana hatuhitaji na kwa hili la Kande ningeomba Tume Huru iundwe kwa sababu wananchi wameleta *affidavit* polisi haiwezi kujichunguza yenyewe kwa sababu hata ngazi ya Mkoa unaelekea umewalinda na wale waliokuwa wamehusika na tuhuma hizo. Wamefanya kikao na wafanyabiashara, wamechangisha hela, wamekwenda mpaka Arusha na yule bwana anarudi anasema nimewaweka wote sawa. Sasa kama na *IGP* naye anawekwa sawa, sijui! Lakini suala linafika. Haya yanachafua sura ya jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema mimi ni muumini wa Jeshi la Polisi, muumini wa majeshi yetu ya wananchi, wakikosekana kwa sekunde moja nchi haitakuwa salama, hatutakuwepo wote. Lakini hawa wachache wanaochafua naomba hatua ichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda niombe tu, niseme kwamba kuna suala la msingi kwa sababu Wizara yako inasimamia *NGO* kuna tatizo kwenye *NGO* nyingi hasa zile zinazosimamia wanaoitwa yatima, wanaoitwa sijui watoto wenye mazingira magumu. Wamesajiliwa chini ya Wizara yenu. Naomba muwe mnafanya ukaguzi. Kuna matatizo ya msingi. Juzi nimekwenda *Immigration,* Waziri nilimletea tatizo kwamba wanahujumiana wenyewe kwa wenyewe. Lakini wanaathiri na watoto pia. Naomba tafadhali sana hao watoto ambao hawana mtu mwingine wa kuwapa upendo na hao wanajitolea kwa nia ya kutoa upendo lakini baadaye wanageuka kuwa wanyanyasaji. Naomba Wizara ambayo ina jukumu la kulea hizi *NGO* zichukue hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja lakini ni kwa sababu najua Waziri atatupa majibu mazuri.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi. Lakini pia namshukuru sana Waziri wa Mambo ya Ndani na Waziri wa Ulinzi kwa hotuba zao nzuri. Nichukue nafasi hii pia kuwashukuru sana wapiga kura wa Jimbo langu la Kinondoni kwa kuendelea kuniunga mkono na kufanya kazi zangu ziende vizuri. Naomba waendelee kuwa na moyo huo na waendelee kuniunga mkono zaidi. Nawashukuru sana viongozi wangu wa Chama Cha Mapinduzi kwa kunisaidia kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, viongozi wangu wote ngazi zote za Matawi hadi Wilaya pamoja na Mwenyekiti wangu wa Wilaya Mzee Aron Mwaikambo kwa kunishauri na kunisaidia kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mchango wangu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, naomba nirudie, niliwahi kuchangia mwaka 2006. Nilizungumzia mambo

mbalimbali lakini nilizungumzia sana suala la ujambazi. Ni kweli Serikali imechukua hatua kubwa sana kuweza kupambana na suala hili la ujambazi. Katikati hapa ilikuwa hali mzuri sana, lakini hivi sasa mambo yameanza kujirudia. Ujambazi umeongezeka na watu wanafanyiwa vitendo vibaya kila kukicha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara kwenye suala hili siyo la kufanyia mchezo. Tujipange vizuri kuweza kupambana na tatizo hili la ujambazi kwa sababu linaathiri sana wananchi wetu. Upo ujambazi mkubwa mkubwa lakini ule ujambazi mdogo mdogo wa vibaka ambao wameenea mtaani. Kila kukicha utasikia watu wamekatwa mapanga watu wanapigwa nondo, watu wanachomwa bisi bisi, watu wanaibiwa kila kukicha. Kibaya zaidi ni kwamba hata sisi tunaoibiwa tumekuwa kama tumezoea sasa, ukiporwa simu, ukiporwa begi hata ukienda Polisi hakuna msaada wowote. Kwa hiyo tunaomba jeshi la polisi lizidi kujiimarisha kwenye suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yapo matatizo ambayo tunayalea ya vijana hawa wa mtaani. Tunaita watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Kundi hili kwa kweli linahusika na mambo mengi sana ya uhalifu. Dar es Salaam wahusika wapo na bahati mbaya sana hata hapa Dodoma juzi nimewaona. Ukipita karibu na Makao Makuu ya Chama pale utawakuta. Kazi yao ni kuvuta bangi, kuvuta gundi na kucheza kamali na haya yote ni makosa. Lakini wanaachiwa hawafanywi chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baya zaidi hawa wanatumika, wale majambazi wanapotaka kufanya uhalifu wao wanawatumia vijana hawa kuvusha silaha, utawakuta wamebeba viroba utasema ni vyuma chakavu kumbe ndani wameweka silaha. Lakini pia wanatumika kwenye uhalifu mwingine, wenyewe wanaitwa mijusi. Likivunjwa dirisha au tundu dogo wanapitishwa wanakwenda kufungua uhalifu unafanyika. Kwa hiyo, naomba sana Jeshi la Polisi lijiimarishe kuweza kupambana na hali hii kwa sababu hali si nzuri mtaani. Hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote yanatokea kutokana na uhaba wa askari. Lazima tukubali kwamba Tanzania tumekuwa tukiongezeka mara kwa mara, tuko wengi sana. Tumeshafikia sasa karibu milioni 40. Lakini ongezeko la askari bado ni dogo mno. Sasa askari wachache hawa kuweza kupambana na ujambazi ambao unaenea kila kukicha inakuwa ni tatizo. Niliwahi kuomba, tunavyo vikosi vingi vya ulinzi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunaona tabu gani kuomba Idara nyingine za ulinzi kusaidiana na Polisi kuweza kukabiliana na hali hii ya ujambazi. Silaha zinazotumika kwenye ujambazi ni mbaya, sijui mnataka kifanyike kitu gani ili mjue kwamba hali ni mbaya. Watu wameshaiba kwa kutumia mabomu, watu wanaiba kwa kutumia *SMG*, watu wanaiba kwa kutumia *AK* 47, silaha za kivita. Sasa kukabiliana nao hawa ni lazima tuongeze wingi wa askari wetu kuweza kukabiliana na hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka miaka ya 80 wakati wa marehemu Mzee Mwalimu Julius Kambarage Nyerere tulikuwa tunaona wanajeshi, Jeshi la Kujenga Taifa

linakuja kusaidiana na askari Polisi kupambana na uhalifu. Ukipita na vifurushi unaweza ukasachiwa, ukaulizwa umebeba nini. Ile ingesaidia na sijui kwa nini mnakataa kuirudisha hiyo. Lakini kutokana na uhaba wa askari Polisi kwa kweli wananchi wataendelea kuteseka. Niombe tena kama nilivyoomba mwaka wa 2006, tuangalie uwezekano wa kutumia majeshi yetu mengine kuweza kukabiliana na hali mbaya ya ujambazi ambayo imekithiri hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema silaha zinazotumika ni kubwa, ulinzi shirikishi ni sawa unatusaidia, sungusungu wapo wengi tu, tunajitahidi. Lakini sungusungu na rungu utakabiliana na mtu ambaye ana *SMG*. Kwa hiyo niombe sana kama tunaweza kutuma askari wetu hao kwenda kulinda amani kwenye nchi nyingine Darfur, Lebanon na nchi kadhaa, tunashindwaje kuwatumia askari wetu kutusaidia kulinda ama kupambana na hawa wahalifu ambao wanazidi kila kukicha. *(Makofi)*

Uhalifu umekuwa ni mkubwa majumbani, uhalifu umekuwa mkubwa hata barabarani. Juzi mwenzetu mmoja hapa amekatwa na panga, kavamiwa na majambazi wamemkatakata, wamechukua na silaha yake. Hivi kifanyike kitu gani ili mjue kwamba hali ni mbaya. Kwa hiyo, niseme tu wananchi tunaathirika sana kutokana na hali ya ujambazi ambayo imezidi kukua siku hadi siku. Kadri tunavyowaacha itaendelea kukua. Tukubaliane tuna bahati nzuri leo mko Wizara mbili hapa, Mkuu wa Majeshi yupo, Mkuu wa Polisi yupo kaeni mshauriane mnafanyaje. Wananchi wa Tanzania wanataka kuishi kwa amani. Wananchi wa Tanzania tunataka kuishi kwa usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa hali inavyokwenda hivi sasa inatukatisha tamaa sana. Wananchi tunaporwa sana. Huko Uswahilini tunakokaa kila kukicha watu wanavamiwa na mapanga. Watu wanavamiwa na mabisibisi, watu wanaibiwa. Lakini bahati nzuri mpaka limeshafika mpaka kwenu, yuko Naibu Waziri mmoja alishavamiwa mpaka nyumbani kwake. Hivi mnataka muambiwe kitu gani mjue kwamba hali imeanza kuwa mbaya? Nawaomba sana tujitihadi kuimarisha ulinzi wetu ili usalama kwa wananchi wetu na mali zao uweze kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba Wilaya ya Kinondoni imepewa hadhi ya Mkoa wa kipolisi. Lakini majengo yaliyopo ni yale yale, huduma ambazo zinatolewa pale Magomeni kwenye Kituo cha Magomeni ni sawa sawa na huduma ambazo zinatolewa na Kituo cha Polisi cha Mkoa kwa baadhi ya Mikoa kutokana na uwingi wa watu kwenye eneo lile. Kwa hiyo kukiacha kituo kile kuwa vile vile hatutendi haki. Kama tumepandisha hadhi kuwa Mkoa basi tupanue na majengo tuongeze na askari. Lakini baya zaidi ni askari wale wanapolala.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimwomba Mheshimiwa Waziri wakati nachangia bajeti ya 2007, twende akaangalie wanapolala, lakini mpaka leo hajawahi kwenda kuwaangalia wanaishi vipi. Lakini wanalala kwenye ma-*box* kwenye banda la *full suit,* ukuta bati na juu bati. Ndani wameweka *partition* ya ma-*box* ndimo wanamolala na wana familia. Hivi wataendelea kukaa mle mpaka lini. Kwa nini tusione umuhimu wa kuwajengea nyumba na kuwaweka mahali pazuri pa kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wa Magomeni wanateseka kwa ajili ya makazi, lakini hata na Polisi Mabatini pale na kwenyewe ni hivyo hivyo. Tunayo maeneo makubwa ambayo mnaweza mkajenga majengo kwa ajili ya kuwaweka askari wetu. Lakini mmeng’ang’ania kila kukicha majengo yakijengwa ni Kurasini, majengo yakijengwa ni Kurasini. Jamani na sisi wa Magomeni na sisi wa Kinondoni pia tunazo nafasi. Njooni mjenge ili askari wetu waweze kukaa kwenye maeneo yale. Kumwacha askari wa Magomeni anakwenda kulala Kitunda au Segerea, likitokea tatizo huku kumpata ni tabu. Naomba niombe sana kwenye suala la ujenzi. Tuhakikishe kwamba vituo hivi vya Magomeni na Polisi Kijitonyama Mabatini vinapewa kipaumbele ili waweze kupata majengo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni vitendea kazi. Dar es Salaam imekuwa kubwa, watu wengi lakini magari hakuna, magari ni machache mno. Matukio ya uhalifu ni mengi, unampigia simu askari atokee, atakuja baada ya masaa matatu au manne au atakwmbia usafiri hakuna. Kwa hiyo, hili nalo linatukatisha tamaa sana. Kwa hiyo pamoja na mambo mengine yote lakini tutoe kipaumbele kwa Mkoa wa Dar es Salaam na hususan katika Wilaya ya Kinondoni kwa sababu wakazi ni wengi, vitendea kazi hakuna. Magari hakuna lakini hata vituo vingine vyote hivyo pia hakuna. Sasa kazi itafanyika vipi. Kwa hiyo naomba tujaribu kuwapa kipaumbele askari wetu ili waweze kufanya kazi vizuri kwa kuwapatia vifaa na zana za kisasa kuweza kukabiliana na uhalifu ambao unazidi kukua kila kukicha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, usalama wa barabarani. Ajali zimekuwa zikiongezeka mara kwa mara. Lakini magari yanayotembea usiku utakutana na malori ambayo hata taa hayana. Nyuma hayana taa na mnayaruhusu yanapita yanatembea. Kwa hiyo haya yanasababisha ajali. Magari yanaharibika yanaachwa katikati ya barabara. Imetungwa sheria hapa juu ya magari yanayoharibika na kuachwa katikati ya barabara kuweka majani. Lakini hadi leo hilo linaendelea kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa Rehema ambaye ametuwezesha wote tukae kwenye Ukumbi huu kwa muda wa miaka yote tuliyokaa hapa. Nina imani kwamba tukijaliwa na kama tulivyowatendea haki wapiga kura wetu basi nao watatundea haki turudi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Bububu bila kujali vyama vyao kwa ushirikiano wao walionipa katika kusogeza maendeleo katika Jimbo letu. Bububu ya mwaka 2005 siyo Bububu ya mwaka huu. Maendeleo yamepatikana, ni mazuri na mwenye macho haambiwi tazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali zote mbili, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kusukuma maendeleo katika Jimbo langu la

Bububu. Nahisi kwamba ni kama nimepata upendeleo kwa sababu miradi mikubwa mingi imeshafanyika mle. Sasa hivi kunajengwa Taasisi ya Mwalimu Nyerere na pia tumepata hospitali nzuri ya kisasa katika Kambi ya Jeshi la Bububu. Ni hospitali ya pekee ambayo nafikiri ni hospitali mbili tu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini tumepata vifaa vingi vya mawasiliano katika Kituo cha Polisi cha Bububu na sasa hivi panajengwa bweni la Askari Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niwashukuru Mawaziri wote wawili na Manaibu wao, Makatibu Wakuu na Watendaji wote na Makamanda kazi nzuri wanazozifanya ili kuhakikisha ulinzi wetu katika nchi yetu unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukurani hizo nataka kuzungumza machache tu kuhusu matatizo ambayo yanayojitokeza katika Jimbo langu kwa Wizara hizi mbili. Niseme tu kwamba Jimbo langu limebahatika kuwa na kambi mbili za jeshi. Kambi ya Jeshi ya Wananchi Bububu na Kambi ya Jeshi Mwanyanya. Kambi ya Jeshi Mwanyanya ni kambi ambayo ina historia kwa historia kwa askari ambao ni wa siku nyingi wanafahamu nini kambi hii ilikuwa inafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ile ilikuwa inatoa makomando katika nchi hii ya Tanzania na baadaye imehamishiwa katika maeneo mengine ambayo si vema kuyataja kwa usalama wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Jeshi la Wananchi. Waheshimiwa wengi wamezungumza kuhusiana na makazi ya askari wetu. Niseme tu kwamba kilio nilikianza tangu mwaka 2006 kwamba kambi zangu hasa Mwanyanya pale askari hawana mahali pa kukaa na majengo waliyopo nafikiri hata ukarabati haufanyiki. Naomba sana, najua ufinyu wa bajeti ni mkubwa lakini angalau ukiangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri hajagusa kabisa Kambi hata moja kwa Zanzibar, amegusia kambi tu za Tanzania Bara. Ni vema na kule basi akaziangalia na kambi zetu za Zanzibar. Matatizo ya makazi yapo, lakini hata ukarabati wa majengo. Jengo la siku nyingi ukarabati haufanyiki tunasubiri mpaka jengo lianguke.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la kisima katika Kambi ya Mwanyanya. Kipindi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi sasa hivi, Mheshimiwa Omar Yussuf, aliniahidi kwamba Kambi ya Mwanyanya pangechimbwa kisima cha maji na bahati nzuri *water table* kwa upande wa Zanzibar ipo juu sana, hata ukienda mita 10 tu, tayari umeshayapata maji. Sasa naomba niikumbushie tena Serikali kwamba, kichimbwe kisima pale ili askari wetu wasiwe wanagombana na wananchi, kwenda mitaani kuchota maji na heshima haitakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la uzio. Kambi ya Mwanyanya imezungukwa na raia wengi sana, kwa hiyo unapopita pale unamuona kabisa askari yule anafanya nini. Kwa hiyo, naomba zoezi hili lianze, japo kitengwe kiasi fulani, iwe

inajengwa japo mita 200, 100, angalau tuwahifadhi askari wetu. Suala la usafiri, bado ni matatizo na lenyewe naiomba Serikali iliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, *JKT;* vijana wetu wengi wamekuwa wanajiunga na *JKT,* wakiwemo na wa Zanzibar, lakini wanapomaliza wengi wanarudi hawana kazi. Sasa wasiwasi wangu ni kwamba tusiwe tuna-*accumulate* vijana ambao baadaye wanaweza wakabadilika, kwa sababu vijana wa sasa wanataka kuajiriwa, sasa suala la kuanzisha masomo ya ufundi ni jambo zuri sana. Ufundi wenyewe kwa kweli, ulingane na mahitaji halisi kwa maeneo wanayokwenda na isiwe ya jumla, kwa mfano, ukimpeleka mtu kwa mambo ya kilimo, kuna vijana wanakaa mijini, wakimaliza wakija mjini watalima wapi? Sasa tuangalie hasa masuala ya kiufundi zaidi ili wanapomaliza wapate kujiajiri wenyewe badala ya kukaa kwenye makundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia suala la elimu, wanaojiunga na kambi wana elimu tofauti, wengine darasa la 11 na la 12 *failure,* lakini wakati wa ajira wasiwatenge sana, wawachukue kwa sababu nina imani kabisa *JKT* lina shule za Sekondari ambazo ziliainishwa kwa ajili ya kuwaelimisha askari wake. Basi liwachukue na wenyewe wakaelimishwe ili baadaye nao waendelee kuwa wafanyakazi badala ya kuwarejesha nyumbani na baadaye wanakuwa ni mzigo kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie Mambo ya Ndani. Kama nilivyosema naishukuru Serikali kwa kuweza kutoa msaada mzuri sana kwa kutoa vifaa vya mawasiliano kwenye kambi ya Bububu pale, lakini bado kuna hili tatizo la usafiri. Wilaya ya Magharibi ina gari moja tu la *OCD* ambalo ndilo linalozunguka Wilaya nzima, lakini ukiangalia *population* ni kubwa sana na mafuta yanayotiwa ni kidogo. Kwa hiyo, ningeliomba Jeshi la Polisi, pamoja na kwamba kuna hilo tatizo la upatikanaji wa pesa, lakini kwa hotuba ya Waziri amesema kwamba kuna Wafadhili ambao watatoa vifaa vya usafiri ikiwemo pikipiki. Basi angalau na vituo vyetu navyo vipewe pikipiki na mafuta ya kutosha wawe wanafuatilia. Suala la *stationary* nalo ni tatizo, ukimkuta askari anataka kuandika basi anahangaika. na lenyewe liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni ukamilishaji wa ujenzi wa bweni la askari pale Bububu, limeshafikia hatua nzuri na naiomba Serikali ilikamilishe kwa sababu lisije likakaa siku nyingi na baadaye ikawa tena ni gofu. Lakini nimpongeze sana Waziri na Naibu wake, kwa kukamilisha ile ahadi yake ya kutia umeme kwenye ile nyumba ya askari wanayokaa familia mbili. Sasa hivi, nafikiri wanafurahia matunda ambayo kwa kweli ndio lengo la hawa askari wetu nao wafurahie.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni suala la ukarabati wa majengo. Tunajua fedha hamna, lakini Zanzibar kwa kweli tukichukua Wilaya ya Magharibi, kuna vituo kama vitano hivi ambavyo ni vya zamani, lakini ukarabati bado.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara zote hizi mbili, Wizara ya Ulinzi pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani. Vilevile nawashukuru Mawaziri wote pamoja na watendaji wao wote kwa kazi nzuri wanayofanya ya kusimamia Wizara hizi. Vilevile nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Mpendae, kwa kuniamini kuwatekelezea Ilani ya Chama cha Mapinduzi na *Inshallah*, tutarudi tena kwenye ukumbi huu, kwa sababu ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, imewajibika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwanza namshukuru sana ndugu Said Mwema, kwa umahiri wake na nampongeza sana kwa kuweza kutuwekea Kamishna mpya Zanzibar, Ndugu Mussa Ali. Sitasema tena kwamba uje Zanzibar kuangalia uovu uliokuweko, sasa hivi mambo yamekuwa mazuri na yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni Wizara hizi, leo wamekaa pamoja, ni kwa nini mpaka leo Wanajeshi na Polisi, hamuwaweki katika steji moja ya *ration allowance* ya 150,000/= na wote kazi zao ni ulinzi wa Taifa hili? Naomba sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, iwaangalie askari wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu kuna samaki anaitwa joza, lakini akitembea hutembea na visamaki vidogovidogo, sisi huviita vipavaa. Joza mpaka anapocheuka ndio vipavaa vile; ndio Chama cha Mapinduzi Joza, vipavaa hivi vyama vidogo vidogo. Msishughulike wapiganaji, Chama cha Mapinduzi na Serikali yake inawajali na wala haitawadharau kwa sababu, Serikali hii ni sikivu na haina matatizo. Hongera sana Serikali ya Awamu ya Nne, inayoongozwa na Mheshimiwa Dr. Jakaya Kikwete, pamoja na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda. Nakushukuru sana vilevile kwa kulijali Jimbo langu, Mungu akubariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Maaskari wana matatizo makubwa. Nikizungumza nazungumza kuhusu Askari Polisi na Askari Jeshi. Askari wana matatizo ya maslahi, ni lazima tuwajali. Najua kwamba mnawajali lakini mnatuambia sungura ni mdogo, tumuongeze, tuweke mbuzi badala ya sungura, ili askari wapate haki, wafanye kazi vizuri. Kukoroma kwetu sababu ni maaskari, usiku tunalala vyema kwa sababu ya hawa askari, msifanye masihara na mtu anayekaa na *SMG* na wanatulia, wana uchungu wa nchi yao. Hakuna Kilimo Kwanza kama sio usalama wa maaskari, ni lazima tuwajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwaone kwamba hawa ndio silaha yetu ya amani na utulivu wa nchi hii; leo ni kwa nini askari anapelekwa kozi, anaambiwa ni mpaka arudi ndio alipwe haki yake, kule atafikaje? Huku anaacha familia, tunafanya nini? Askari anapopelekwa kozi ni wajibu apewe haki yake aondokenayo mfukoni. Kwa sababu,

akifika kozi *ration allowance* hataipata, yuko kozi. Leo tunasema askari atakuwa abaki na deni, askari amdai nani? Askari mdogo atalalamika wapi? Askari mdogo hana pa kulalamika, hili ni lazima tuliangalie vyema. Tatizo la madeni liondoke kwa maaskari wote na haki zao wapewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nitazungumza kuhusu habari ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Hali ya makazi ya askari pamoja na familia zao ni mbaya. Kwa nini, nikazungumza kuwa hali zao ni mbaya? Nilipokuwa nafanya kazi ya Jeshi, makambini askari ana godoro lake na kitanda; hebu tukaeni tutanzue tatizo hili la askari kupata vifaa. Anakuwa na hamu ya kulala kambini askari kwa sababu anapo mahali pazuri pakulala.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungukwa na Makao Makuu ya Nyuki Brigedi, leo namjua Mr. Shimbo, ni msikivu lakini ana majukumu mengi. Lile jukumu langu la ile mota ya maji ya kisima, naomba mnipelekee ili askari waache kwenda sehemu nyingine kuchota maji; kweli mota tu, inawashinda Jeshi la Wananchi wa Tanzania? Mheshimiwa Waziri, aliniahidi kwamba atanipa na nikamletea aina ya mota inayotakiwa, mpaka leo hajaniletea, ndugu yangu huyu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kuchota mambo kwake na yeye ananisaidia! Nataka nikifika Jimboni, niambiwe mota imefika; wala haifiki milioni 15, ni kwa nini hajanipelekea? Achukuea mahali pengine, ninawapiga kura akinamama pale, Wanajesjhi wanaume hawanipigii, lakini kura za maoni wapo akinamama wananipigia, au hutaki nirudi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Abdulrahman Shimbo, unipelekee mashine ili Wanajeshi wajisikie, makazi ya maaskari na familia zao ni mabaya na hasa Nyuki Brigedi. Leo Dr. ananitajia sehemu za Bara tu, kule Unguja sisi tumekosa nini? Mimi hapa wajibu wangu ni kuwatetea wanajeshi, ndio kilio chao na mimi ni mpiganaji mwenzao; ni kwa nini mpaka leo ananiambia sijui hali ya uchumi, hali ya uchumi, nyumba zinavuja, ukifika Mwanajeshi analala na mtoto wake chumba hicho hicho, pazia lake ni chandarua, hali hii haifai, Wanajeshi tuwatunze.

Jamani na mimi nimepitia kule kwa hivyo nayajua. Nawaombeni sana tuwajali Wanajeshi wetu ndipo tutakapopata nafasi ya kupumua. Tunaringa amani na utulivu ni hawa, tuwatunzeni. Wapeni pesa, ni kitu gani Serikali mnashindwa? Nchi gani inayojadili bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Mambo ya Ndani? Peleka tu, unajadili nini? Wapelekee pesa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, wapelekeeni pesa Jeshi, wapelekeeni pesa Polisi ili Mwema afanye kazi. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheikh Saidi Mwema namwambia spidi yake lakini anavutwa shati nyuma na watendaji wake, apitishe fagio Makao Makuu, kama anashindwa atutume sie tuseme ili yeye afuatwe kutokana na spidi yake anayokwenda. Leo hapa kila mmoja anamsifu Mwema, lakini Maofisa wake pia wanavujisha siri halafu

anakwenda kwenye vyombo vya habari anatoa maelezo. Hawa wako palepale Makao Makuu, ni Maofisa wake ndio wanaovujisha siri; lakini Sheikh Mwema, mswalie Mtume, mswalie Mtume, mpaka lini? Sisi tunaondoka lakini tutarudi tena tuhakikishe kwamba vyombo vya ulinzi vinakwenda kulingana na *standard* ya Bunge inavyokwenda. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja hizi mbili. Kabla sijachangia hoja hizi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe pamoja na mimi, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Kabla sijaendelea, ninawaeleza wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe, nikonao pamoja na vilevile natangaza nia ya kuitetea nafasi yangu hii ya Ubunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitaanza na takwimu iliyotolewa ya askari mmoja kuwa na watu 1000. Kwa kweli, tuko nyuma sana na takwimu hii inahuzunisha sana na hasa kutokana na ulimwengu wetu unavyokwenda. Ulimwengu wa sasa sio ulimwengu wa zamani, tunasikia kwamba majambazi wana silaha za kisasa; kwa hivyo ni dhahiri kwamba wakati askari mmoja analinda watu 1000 na kitu, Serikali ni lazima ilitazame hili na askari wetu kuwapa vifaa vya kutendea kazi ambavyo vinaendana na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema mwenzangu kwamba alikuwa ni Mwanajeshi na nilikuwa Polisi. Enzi zangu, nafsi yangu nilikuwa na pikipiki tatu, pikipiki ya doria, pikipiki ya *escort* kwenye *traffic* na pikipiki moja tulikuwa tunaiita *Kenge BSA,* hiyo ukifika kwanza unafundishiwa hiyo, kiki irudi ikupige miguuni ndio upate kujua pikipiki. Leo nasikitika usalama wa barabarani pale Zanzibar tena mjini, wanatumia baiskeli! Wakati kuna matatizo chungu nzima au *vespa* ya binafsi! Tunaendana na wakati namna hii kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile ninasikitika kwamba hakuna 99 hata moja inayotumika, na ilikuwa *shift* ya kuanzia saa 01.00 mpaka saa 08.00 kuwe na 99, saa 08.00 mpaka saa 04.00 usiku kuwe na 99, saa 04.00 usiku mpaka saa 01.00 kuwe na 99; linatokea tukio watu wa mwanzo kabisa kufika ni Askari Polisi wa 99, anafika pale anatamba, watu wanastaajabu! Hivi hii simu niliyopiga kwamba kuna tukio, tukio hili linakwenda moja kwa moja mpaka kwenye gari hili au ni vipi? Kumbe linafika *Radio Control, Radio Control* anauliza 99 soma 3 uko wapi? Sasa hivi niko Maruhubi, kimbilia

upesi Mwembe Makumbi kuna moja mbili tatu, kalikabili. Hivyo ndivyo Jeshi la Polisi linavyotakiwa liwe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakaa hapa tutajadili kwamba askari kakawia, ukienda hayupo, kumbe hata gari la kutendea kazi hana; atafanya kazi vipi mtu huyu. Ili kuwaweka askari wetu pazuri ni lazima tuende na wakati. Askari wa *traffic* wawe na vitendea kazi kama pikipiki, askari wa *patrol* wawe na 99, linatokea tatizo, walikabili haraka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukarabati wa majengo. Sasa hivi ningeomba tu tuendelee na utaratibu wa kukarabati majengo yetu, hasa vituo vya Polisi. Kama Kituo cha Polisi kilichopo kwangu pale Mwanakwerekwe, ukipita kwa nje ni kizuri sana, lakini ukiingia ndani kimeoza. Kituo hicho hakina *ceiling* juu, kituo hicho mafeni hayafanyi kazi, kituo hicho naweza kuthubutu kusema hata simu hawana. Pale ni katikati ya mji, lakini linatokea tukio, hata gari la kutendea kazi hawana. Mpaka wapate gari la *OCD* halafu ndio wafanye kazi, wakati gani mambo kama hayo? Sasa tutakuwa tunawalaumu Polisi wetu, lakini lawama ziko kwa Serikali Kuu. Kwa hivyo yale ambayo ni ya lazima ni lazima tuyafuatilie, halafu yaliyokuwa sio ya lazima, tuyaweke upande. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Askari wetu wa Jeshi la Polisi pamoja na Jeshi la Ulinzi, wakistaafu. Kuna malalamiko makubwa sana na halafu tunayaingilia sisi Wabunge; lakini nashukuru tukifika Makao Makuu, huwa tunapokelewa vizuri tu. Askari wetu wa Jeshi la Polisi wakistaafu pamoja na la Ulinzi kiinua Mgongo chao huwa kinachelewa sana takribani na *pensioner* huwa inakawia sana. Lakini kama ndugu alivyosema hapa kwamba sasa hivi kuna Mkuu wa Polisi mpya kule Zanzibar labda mambo yanaweza kukaa vizuri kwa sababu watu hawa wakiwa wanadai sana na kama wanatutumia sisi viongozi wao, basi wale wanaoshughulika na mambo ya fedha kule Makao Makuu Zanzibar, utasikia kamaliweziwe na huyo huyo Mbunge wako. Nashaka hili litakuwa haliko tena askari wetu watatendewa haki kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nazungumzia kuhusu haki, nadhani Mkuu wa Polisi Kamishna akishastaafu huwa anapata haki zake lakini nasikitika tu Mkuu wa polisi aliyekuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi Zanzibar mpaka leo anatumia gari yake na nasikia ana haki ya kupata gari kutoka Jeshi la Polisi au Serikali ya Jamhuri ya Muungano mpaka sasa hajapata kama hivyo ndivyo ilivyo basi ndugu *Inspector Generally* umpatie haki yake huyu kama wale wengine walivyopata haki na yeye ajisikie kwamba kafanya kazi nzuri kwenye Jeshi la Polisi hana matatizo, hana makosa naye afaidike na matunda hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, natumai hoja hii au mpango huu leo itakuwa mara ya pili nautoa, ningeomba tu majeshi yetu haya ya ulinzi, Jeshi la Polisi na Jeshi la Ulinzi basi wapatiwe vifaa vya kujengea. Kwa sababu askari wengi wakishastaafu jeshini wanakuwa na hali duni kabisa kabisa, wanakuwa hawana pa kulala, wanakodi nyumba, sasa utakuta askari badala ya kujidai kwamba nilikuwa askari anakuwa mtu wa chini kabisa kabisa. Moja kwa moja anakuwa hana pa kulala, kwa hiyo ningeomba na hili lishughulikiwe, viongozi wetu wawakopeshe vifaa ili wajenge, wakati wakistaafu wawe na amani na utulivu katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza kuhusu Polisi Jamii, Ulinzi shirikishi, ningeomba tu kutokana na...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Bahati mbaya sana.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami pia nichangie kwenye hoja hii lakini kwanza nianze kwa kusikitika Wizara ambazo ni muhimu, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Ulinzi inapewa siku moja ya kujadiliwa. Hiyo ni kwamba Serikali hamuoni umuhimu wa Wizara hizi.

**NAIBU SPIKA**: Muda wako utakwisha kwa kusema hivyo. *(Kicheko)*

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuwashukuru sana wananchi wangu wapiga kura wangu wa Tarime, kwa kazi nzuri na kwa ushirikiano mzuri ambao wamenipa. Nakumbuka kazi kubwa waliyoifanya mwaka 2005 kunichagua kuingia ndani ya Bunge hili na niwahakikishie kwamba kuna baadhi ya watu wamekuwa wakipita pale Jimboni wakisema kwamba Mwera mwaka huu hagombei, sasa nataka nitangazie Taifa kwamba mwaka huu nitagombea na nitatetea nafasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kushukuru sana Jeshi la Polisi hasa katika Wilaya ya Tarime ambapo kumekuwa na ujambazi na wizi wa mifugo, Polisi wamefanya kazi kubwa sana na sasa hivi amani ipo na hiyo ndiyo kazi ambayo kwa kweli naweza nikalishukuru Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze upande wa Jeshi la Polisi kuhusu mishahara. Kwa kweli Jeshi la Polisi mishahara yao ni midogo, ni lazima mishahara yao iweze kuimarishwa iwe mikubwa sana. Ukiangalia upande wa Polisi, Jeshi la Polisi ni sehemu inahusika sana kwenye upande wa wananchi. Ukifika kwenye rushwa imeshaenea sana upande wa Polisi, huenda ni kwa sababu ya mishahara ambayo ni midogo kwa Jeshi la Polisi. Naomba Jeshi la Polisi liongezewe mishahara pamoja na Jeshi la Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa posho, wakati wa uhamisho hasa wakati wa uchaguzi, upande wa Jeshi la Polisi, wanajeshi wengi walikuja pale wakawa wanalipwa shilingi 1000 kwa siku mpaka sasa hivi ninavyosikia ni kwamba bado wanadai. Naomba

kwamba Waziri ahakikishe kwamba Polisi wanaokwenda kufanya kazi wakati wa madoria, wakati wa shughuli nyingi waweze kulipwa kama wanavyoamshwa usiku kwenda kwenye kazi za ziada waweze kulipwa. Unapomwambia mfanyakazi aende kwenye kazi ya ziada huwa analipwa fedha za kutosha, lakini sasa unapomwangalia Polisi je, ni amri unamwamrisha lakini kwanini asilipwe haki yake, ni lazima tuhakikishe kwamba posho wanajeshi, polisi kama wamefanya kazi masaa ya ziada walipwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa mishahara yao ambayo nimeanza kuiongelea, kuna wafanyakazi wamekuwa wakihusishwa kwamba wafanye migomo, je, wanajeshi, polisi wakiamua kufanya mgomo kwamba mishahara yao midogo, nini kitatokea katika nchi hii? Hatatutaki kuhamasisha Wanajeshi, Polisi wagome na wakigoma ina maana nchi itakuwa imepinduliwa. Tunaomba mishahara yao ihakikishwe kwamba inaongezwa. Kwenye utendaji wa kazi unapoona Wanajeshi, Polisi unakuta wakati mwingine Polisi wana-*retire* wakiwa na umri mdogo sana, unakuta wana miaka 35, wengine 40 wakiwa na nguvu basi utaratibu ufanywe ili waendelee kufanya kazi na katika miaka yao waendelee kupewa mafunzo mbalimbali waweze kujua haki za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la bajeti iliyopita, Waziri alitangaza kwamba tutakuwa na ujenzi wa vituo vya Nyamwaga, Kegonga, Borega, lakini sijaona kitu kinachofanyika pale na wakasema kwamba tungeongeza nyumba za polisi na sasa mmeshaweka Kanda Maalum ya Kipolisi, lakini pale askari hawana sehemu za kulala, wanalala maporini, wananyeshewa mvua, kwa hiyo tunahitaji kwamba zile bajeti ambazo Serikali imeshapanga zitekelezwe na niambiwe baada ya majumuisho kwamba, je, maendeleo ya ujenzi wa nyumba hizi umefikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la rushwa na *traffic* wa barabara, kwa kweli hao maaskari njia sioni Tarime tu, Taifa zima askari *traffic* unakuta ni kuchukua rushwa kwa wananchi yaani utafikiri kwamba hamna Serikali na Serikali ipo na hao ndiyo Polisi wenyewe wanachukua rushwa ni sehemu ambayo inatakiwa iangaliwe sana hasa *traffic* wa njiani. Tuhakikishe kwamba hao maaskari wanaangaliwa ambao wamekuwa wakichukua rushwa katika maeneo mbalimbali. Nenda katika vituo vya polisi kwenye *out post, post* za kawaida, maaskari ambao wako kwenye ngazi za juu hawana matatizo, lakini maaskari hawa wadogo ukiingia katika Kituo cha Polisi wao ni kufoka, hawana ustaarabu, sasa huwa nashindwa. Kwanza nimshukuru sana *RCO* wa Tarime, ni kiongozi kwa kweli ambaye ni kiongozi mzuri amesimamia pale amani unamuona kwamba ni kiongozi mzuri. Niombe kwamba *AGP* Mwema umuangalie kiongozi huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa hali ambayo ilitokea Tarime, katika kijiji cha Keboye, si lazima nirudie, ni kweli mambo yalikuwa ni ya aibu na nimekuwa nikisikia baadhi ya viongozi wa Mkoa, viongozi wa Wilaya wanatishia kwamba Mwera akitoka Bungeni tutamshughulikia, tarehe 16 natoka Bungeni nione

mtakavyonishughulikia, nawakilisha wazo la wananchi wangu sio wazo langu, mimi ni mwakilishi wa wananchi, sasa kwa kuwa mnavyokuwa mnanitishia pamoja na Mbunge ambaye yuko madarakani mkifikiri kwamba nitaogopa, mimi nitayasema na sitaki niyasema hayo leo maana ni maneno ya aibu, kila mtu ataziba masikio. *(Makofi)*

Lakini kwa vile niliongea na Waziri Mkuu, mtoto wa Mkulima, mtendaji mzuri ambaye nakubaliana naye tunataka tupate majibu ni nini kinachofanyika pale hatutaki kuonea askari lakini sitaki wananchi wangu wafanyiwe matendo ya aibu, matendo ambayo hata kimsingi tukiamua kwamba tuyabadilishe wafanyiwe maaskari nao watashangaa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mnafahamu kwamba wale wananchi mnaokaa nao pale ni dada zenu, ni mama zenu, ni babu zenu, kwa hiyo lazima muwatendee haki, hiyo mishahara ambayo tunawalipa, ni kwa ajili ya wananchi wetu. Kwa hiyo, naomba kwamba Jeshi la Polisi hasa maaskari wachache ambao wanachafua Jeshi la Polisi mhakikishe kwamba wanafanyiwa kazi. Katika kuwaajiri hawa maaskari, lazima tuangalie taratibu nzuri za kuajiri, tunaweza tukaajiri vijana ambao sio wazuri katika Jeshi letu la Polisi, tunaweza kuajiri hata majambazi ndani ya Jeshi la Polisi, ni lazima tuwe na mchakato mzuri wakati wa kuajiri ambao wamepitia JKT tuwachuje, tuhakikishe tunawapata askari ambao ni wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa Jeshi la Wananchi, Jeshi la Wananchi limefanya kazi kubwa la kulinda mipaka yetu, hawahusishi na mambo ya rushwa, wao ni kulinda nchi yetu, niombe sana Waziri nilishaleta malalamiko kwako kuhusu suala la Ronsoti ambalo wananchi pale wamelalamika na wanajeshi wamevamia ile sehemu tuone kwamba tumepata ufumbuzi na wanajeshi waweze kurudia sehemu yao ya Nyandoto ambayo ni sehemu yao waliyokuwa wamepangiwa waweze kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo yale wanaishi kwa amani, hatuna ugomvi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, wanafanya kazi kubwa ya kulinda mipaka, hatutaki tuingie mgogoro na Jeshi la Wananchi na kama kuna maeneo waweze kupewa maeneo ambayo hayana migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa hatusikii, hebu hamia mahali pengine pa kusemea, shuka mstari wa pili.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti. Nitachangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya

Mambo ya Ndani, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kahama napenda nianze kutoa mchango wangu kwanza kwa kusema naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kulishukuru Jeshi la Polisi, Wilaya ya Kahama kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya kuhakikisha kwamba ulinzi, amani, mali za wananchi katika Wilaya hii ni shwari. Licha ya uhaba wa vitendea kazi, hususan magari, Wilaya ya Kahama ina eneo la kilomita za mraba zaidi ya 8000 lakini ina gari moja, ambalo linapaswa kufanya kazi katika eneo kubwa kama hili na pikipiki chache. Lakini pamoja na uhaba wa vitendea kazi, idadi ya askari katika Wilaya ya Kahama ni ndogo na nimewapongeza kwa sababu ujambazi katika Wilaya ya Kahama limekuwa ni jambo la kawaida lakini katika siku za karibuni wamejitahidi kwa kweli kuhakikisha kwamba hali inakuwa shwari na wiki iliyopita tu waliweza kukamata majambazi ambayo yalikuwa yakiendesha mtandao wa uhalifu katika Mji wa Kahama na maeneo ya vijiji ambako wananchi wengi wameuawa wameweza kuwakamata majambazi na silaha ambayo imekuwa ikitumika wameikamata.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikichangia bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani mwaka 2008, nilizungumzia tatizo la kihistoria la Wizara hii kupewa pesa kidogo kila mwaka na ni tatizo la kihistoria kwa sababu kuanzia miaka ya 60, 70 mpaka 80 kipaumbele kwa Serikali inapotenga bajeti kwa taasisi hizi au Wizara zinazohusika na masuala ya Ulinzi na Usalama au Wizara ya Mambo ya Ndani daima imepewa fungu dogo. Sasa nakubaliana na historia kwamba miaka ile maadui wa nchi hii walikuwa nje ya mipaka ya nchi yetu, lakini leo hii hali imebadilika, maadui wa nchi hii tunao ndani ya nchi, majambazi yametapakaa kila kona ya Tanzania kiasi kwamba wananchi wanaishi kwa hofu kubwa wanashindwa wakati mwingine kushiriki katika utekelezaji wa mipango yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Serikali ijaribu kuliangalia suala hili badala ya kuitengea pesa kidogo Wizara hii ielekeze nguvu zake kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani, tuchukue mwaka mmoja kama walivyofanya kwa Wizara ya Kilimo, peleka pesa nyingi Wizara ya Mambo ya Ndani waweze kujikwamua na matatizo ya usafiri kwa askari, kwa sababu sioni kana kwamba hali ya ujambazi ikiendelea kama masuala ya kilimo kwanza yatawezekana. Ni nani atakubali kwenda shambani kulima wakati ana wasiwasi na familia yake nyumbani na hata kama atazalisha mahindi kwa wingi au pamba kwa wingi akivuna anajua wazi kwamba atashambuliwa na majambazi. Katika hili nafikiri Serikali ifike wakati ilione suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Tume ambazo zimekuwa zikiundwa kila panapotokea matatizo au mauaji yanayofanywa na Polisi, wakati wakipambana na majambazi. Hili nina wasiwasi nalo kwa sababu Tume nyingi zimeundwa kwa mashinikizo ya kisiasa, sasa sijawahi kuona nchi yoyote duniani, ambapo Polisi wanapokuwa wameua jambazi mtu ambaye anazaniwa kama jambazi imeundwa Tume na jambo hili sasa hivi limeanza kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo mengi ambapo askari wamepelekewa taarifa kwamba tumevamiwa kuna majambazi hapa nyumbani, Polisi hawafiki muda

unaofaa, kwa sababu wanaogopa, askari wakiambiwa kwamba kuna majambazi wanaondoka na silaha zao tayari tayari hawana muda wa kufika pale na kuanza kuulizia nani jambazi nani sio jambazi. Wanachelewa kufika kwa sababu wanajua wakifika wakitekeleza wajibu wao kesho yake wanaundiwa Tume, na ukiangalia Tume hizi zinaundwa kwa mashinikizo. Sijawahi kusikia kwamba mtu aliyeuwawa ni mtoto wa mkulima au wa mtaani Tume imeundwa. Wengi wanaoundiwa Tume ni watoto aidha wa viongozi au wafanyabiashara wenye pesa ambao wanashinikiza viongozi kuunda Tume hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana taratibu za kisheria ndani ya majeshi yenyewe zifuatwe, mbona huko miaka ya mwanzo miaka ya 60, 70, 80 hatukuwa tunashuhudia Tume, kila siku Tume inaundwa lakini matokeo yake hatuyapati, sijawahi kuona Tume ambayo imeundwa na imeleta tija, kesi zinakwisha hivi hivi, watu wanadanganywa danganywa. Naomba turudi kwenye utaratibu na Askari Polisi hawa wawe na imani ya kazi wanayoifanya. *(Makofi)*

Sijasikia Serikali inaunda Tume kwa askari ambaye ameuwa na kundi la wananchi majambazi, sasa ni kwa nini Tume ziundwe askari anapotekeleza wajibu wake tu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usalama katika maeneo ya hifadhi hasa mapori ya akiba na hapa nataka kuzungumzia maeneo kama Bukombe ambapo ujambazi umekuwa ukifanyika mara kwa mara na hakuna anayeonekana kulichukulia tatizo hilo kwamba ni tatizo la kusikitisha. Lakini yapo maeneo mengine kama kule Loliondo, eneo la Loliondo ni kama eneo ambalo halina mwenyewe, majambazi ya Kisomali yanajificha kule, wananchi wananyanyaswa na kadhalika. Lakini tatizo hapa ni kwamba Askari hawatoshi na kama wapo basi hawana vifaa.

Mimi naomba Serikali iliangalie suala hili, inatia aibu na kusikitisha. Maeneo kwa mfano ya Loliondo, kuna viwanja vya ndege mpakani kabisa mwa nchi hii, mimi nimetembelea maeneo hayo, sidhani hata kama kuna Afisa Uhamiaji anayeangalia nani ameingia pale ili mradi tu nchi inakwenda kadri wananchi au majambazi katika maeneo hayo wanavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni *Traffic*. Hivi kwa nini *Traffic* waliopo kwenye *main roads* kazi yao ni kusimamisha malori na mabasi tu? Hivi haya magari mengine madogo madogo hayana matatizo? Hiyo inaashiria rushwa ya wazi wazi na Madereva wanajua kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam kuna vitu vingapi, hamsini, ameweka shilingi elfu hamsini pembeni, akisimamishwa tu tayari anatoa hela anandelea. Hivi hawajui hayo magari madogo ndiyo yanayobeba silaha na majambazi, kwa nini hawayasimamishi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwa siku ya leo umeishia hapo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ali Juma Haji atafuatiwa na Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hizi mbili zilizo mbele yetu za Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mambo ya Ndani. Mimi niwapongeze Mawaziri wote, Manaibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hizi mbili kwa kazi zao nzuri wanazozifanya. Lakini mchango wangu wa kwanza kutokana na muda unavyokwenda, nianzie kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake Waziri wa Ulinzi, katika ukurasa wa 29, ametueleza kama hivi ifuatavyo, naomba kunukuu:-

*“Katika kipindi hiki, stahili za Wanajeshi hususani mishahara, posho, chakula, likizo na sare zimeboreshwa na kutolewa kwa wakati katika viwango vya kuridhisha”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafarijika sana kusikia maneno kama haya, kwamba Askari wetu wanaboreshewa mishahara, posho, sare na mengineyo. Lakini napata wasiwasi katika baadhi ya mambo kwanza nije katika posho. Nampongeza kwa hatua moja Mheshimiwa Waziri ya kuwalipa Wanajeshi wetu posho ya nyumba kwa wale ambao hawajapata makazi katika kambi. Lakini posho hii ina ulipaji wa staili yake sijui kama ndiyo stahili alizozisema Mheshimiwa Waziri. Posho hii inalipwa kwa MaAskari wengine ambao wameoana pale basi posho hii inasemekana analipwa kwa Askari mmoja tena wa kiume, ikiwa wameoana wote MaAskari basi wa kike halipwi kwa sababu wanaishi pamoja.

Hii mimi naona kama si staili nzuri kama ndiyo staili yenyewe kwa sababu katika sehemu zote kwenye Wizara hata hapa kwenye Bunge lako watu wameoana, lakini wanapolipwa posho zote wanalipwa kila mtu na ya kwake. Lakini ajabu kwa Askari hawa. Kama kweli hii inatendeka mimi ninamuomba Mheshimiwa Waziri hii haistaili na iondolewe mara moja na wote walipwe posho zao kwa mujibu wa ajira zao na tukianza kufanya hivi kwamba analipwa mwanaume kwa kweli huo ni ubaguzi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba alifuatilie hili kama analijua aliondoe na kama halijui alifuatilie kama lipo alirekebishe mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu tumepata taarifa sisi wanaume pamoja na mimi nimo lakini simo katika haya nitakayoyasema, wanaume wengine wakishapokea hizi posho basi siku ile ndiyo wanapokwenda baa na kukalia kiti kirefu, anazimaliza pesa zote kule, akija nyumbani mke akisema kodi ya nyumba hatujalipa basi ugomvi unaanza na posho kapewa yeye. Sasa mwanamke pale inabidi achukue ule ule mshahara wake ambao yeye hakupewa stahili ya nyumba alipe kodi kwa sababu yeye anaishi na watoto pale na kero itampata yeye lakini mume wake kakalia kiti kirefu. Mheshimiwa Waziri, naomba hili alifuatilie sana na ikiwa lipo lisawazishwe mara moja kwani hii siyo haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye jambo lingine la sare. Hapa pameboreshwa sare kwa viwango vinavyoridhisha, lakini ajabu tunapishana na

Wanajeshi huko njiani, juu wamevaa shati na suruali safi lakini chini ana raba, aah! Sasa hizi *uniform* zinagawiwa vipi kwa viwango vinavyoridhisha? Sasa kama ni kweli Mheshimiwa Waziri umegawa sare hizi kwa wakati mzuri na kwa viwango vinavyoridhisha na kama kuna MaAskari bila ya dharura ya msingi wanapotosha huu uvaaji wa sare basi wachukuliwe hatua kali sana za kisheria kwa sababu hawa wanaliweka Jeshi katika muundo ambao siyo wakati hapa mnasema mmeshatoa sare.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna malalamiko kwamba kuna Wanajeshi hawapati sare mpaka wakati wa sherehe fulani. Sasa Mheshimiwa Waziri, si Wanajeshi wote wanashiriki katika sherehe. Kwa hiyo, namuomba ahakikishe sare hizi zinagawiwa kwa Wanajeshi wote maana pengine taarifa inatolewa kwamba sare hizi zimetolewa kwa wanaostahili kumbe ni viongozi wa juu tu, wale maofisa. Mimi sijawahi kumuona Afisa ana shati ambalo limepaukapauka, wao kila wakati wanang'ara lakini hawa wa chini ndiyo wanaovaa nguo ambazo zimeshapauka, kwa kweli hazistahili. Naomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie vizuri sana suala hili.

Lingine katika Jeshi la Ulinzi, kuna mambo ya pensheni, kuna Maofisa wa zamani kwa mfano kuanzia Luteni na kuendelea juu, pensheni zao wanazidiwa na Ma-*NCO* ambao wanastaafu kwa kipindi hiki cha karibuni, wale Maafisa wa zamani basi wanashindwa na Ma-*NCO* ambao wamestaafu kwa miaka ya karibuni.

Sasa hapa hatujui kunatokea nini mpaka kunakuwa na tofauti hii. Wakati wa maboresho ya pensheni hizi hawa huwa hawazingatiwi sana, viinua mgongo vyao havipandi, wako palepale na hawa wanaostaafu karibuni wao wanaendelea kupeta na ukiangalia walipostaafu hawa wana vyeo vikubwa ukilinganisha na Luteni au Meja na mtu kama Koplo ama Sajenti, lakini kipensheni Luteni wa zamani anapitwa na *NCO* yaani Sajenti au Koplo anayeachia ngazi sasa hivi. Naomba haya tuyafuatilie kwa umakini na hawa watu wanaostahili na wao wanapatiwa posho vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwa Wizara ya Mambo ya Ndani. Hapa mimi nina mchango mdogo tu kwa Waziri, katika Jimbo langu la Chaani, kuna kituo kidogo cha Polisi. Kituo kile tumekijenga wananchi kwa nguvu zetu mpaka kikamalizika, tukaweka umeme kwa nguvu zetu na mimi mwenyewe ninayezungumza nikiwa mshiriki mkubwa lakini hadi sasa hivi kituo hiki hata choo hakina, tumeshindwa kujenga choo na mchango wetu umefikia hapo? Mheshimiwa Waziri hatuoni aibu kwamba wale Askari wanakwenda kuomba vyoo nyumba za jirani? Kwa hiyo, naomba na hili, mega pesa mahali, nadhani choo hakitachukua fedha nyingi, naomba mtujengee choo pale katika kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu sitaki nigongewe kengele ya pili, nitakuwa mwizi wa shukurani kwa sababu na mimi hiki ndiyo kikao cha mwisho kwa muda wetu wa Ubunge, niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Chaani, kwa moyo wao mkunjufu walionionyesha muda wote na ushirikiano wao na nadhani tumekwenda vizuri, nimewatendea mema mengi. Mimi nategemea nitakaporudi tena na wao watanionyesha moyo wao katika uchaguzi unaokuja. Pia niishukuru familia yangu yaani mke wangu na

watoto wangu, kwa uvumilifu wao mkubwa wakati ninapofanya kazi zangu Jimboni na hata nikiwa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru pia na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja hizi muhimu zilizopo mbele yetu asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu kupongeza Wizara hizi mbili ambazo kwa kweli zimefanya kazi nzuri pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa kutuonyesha mwelekeo wa bajeti yetu ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii, kupongeza Jeshi la Polisi Wilayani Maswa, kwa kazi nzuri na kubwa waliyoifanya yenye ujasiri na ushujaa mkubwa iliyotokea pale Maswa NMB, Jumatano wiki hii. Lakini nimpongeze zaidi vijana wetu MaAskari wawili, PC Abbas na PC Kelvin, kwa kazi nzuri waliyoifanya, wametoka *depot* muda si mrefu, ni vijana ambo wamekuwa kazini hata hawajafikisha miezi sita lakini wameonyesha mapambano makubwa sana. Kwa hiyo, nina kila sababu ya kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kwenda moja kwa moja kwenye mchango wangu niliokuwa nimeuandaa. Ninapenda kujua kitu kimoja ambacho kinaitwa Mfuko wa Huduma za Jamii ambacho kimeanzishwa ndani ya Wizara hii. Mfuko huu unamtaka kila Askari Polisi kukatwa mshahara wake shilingi 5,000/= na mfuko huu lengo ni kwamba atakapokuwa amepata msiba atapata huduma kutoka katika mfuko huu, akifariki hata yeye mwenyewe atapata huduma kutoka katika mfuko huu na hata kama kutakuwa na wastaafu wana matatizo watapata huduma katika mfuko huu lakini kingine ni kwamba akifariki hata mstaafu atapata huduma kutoka katika mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waziri anajibu nadhani kuna haja ya kutuweka sawa juu ya jambo hili kama kuna haja ya kumkata Askari Polisi kwenye mshahara wake kiwango cha shilingi 5,000/= je, Serikali imejitoa katika huduma ya kuhudumia matatizo yote ya misiba itakayotokea kwa MaAskari hawa? Kwa sababu kitu ninachojua ni kwamba jukumu la kumhudumia Askari Polisi au mtumishi wa aina yeyote ni jukumu la Serikali na Wizara husika. Sasa napata taabu kuona kwamba mshahara wa huyu Askari ukizingatia mshahara wenyewe ni mdogo, inafikia mahali wanakuwa na uchangiaji katika huduma ambayo ni muhimu sana Serikali ichangie yenyewe. Ninataka kujua je, Serikali bado inawajibika katika hili? Je, kama inawajibika katika hili kuna haja gani ya kumkata Polisi mshahara wake?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nadhani wakati tunajibiwa, kuna haja ya kujua jambo hili ambalo ni muhimu sana ili kama mstaafu atahudumiwa katika mfuko huu, sina hakika kama anaweza akaipata huduma hii kwa sababu akishastaafu naona wengi sana hata malipo yao yanakuwa ni ya matatizo sana, sasa kama atakuwa ameshastaafu na yeye

anapewa matumaini kwamba ukistaafu utahudumiwa katika mfuko huu, mimi nadhani imani yangu inakuwa ndogo sana kwamba anaweza akapata huduma katika mfuko huu.

Lakini kingine waangalie basi wanapokuwa wanaendelea kukata mshahara wa huyu Askari anabaki na kiasi gani katika mshahara wake? Nadhani iko haja kama kuna kitu cha namna hii kifanyiwe kazi upya, mjaribu kuangalia ni jinsi gani mnawasaidia ili huduma ile ile ya toka mwanzo ibaki palepale na mshahara wa Askari huyu angalau ubaki pale pale ili uweze kumsaidia katika maisha yake ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo ambalo mimi limenitatanisha na linanipa shida sana. Pale Wilayani kwangu Maswa, MaAskari Polisi walikuwa wanatumia umeme kama kawaida yaani kama zamani walivyokuwa wanatumia, nikiwa na maana kwamba walikuwa hawajafungiwa Luku lakini baada ya muda si mrefu wakawa wametolewa yale matumizi ya kawaida ya umeme wakafungiwa Luku, sasa tatizo linakuja wapi?

Tatizo ni kwamba Maaskari zaidi ya 15 au 20 wanakuwa na matumizi ya ile ile Luku moja, sasa hii inaleta tatizo kubwa sana na kila mtu katika familia yake ana matumizi tofauti tofauti, sasa wanapounganishwa pamoja kwamba watumie Luku moja sidhani kama ni sahihi. Mwingine anataka azime umeme muda huu na mwingine anataka awashe muda huu, mwingine labda ana *heater* na mwingine ana friji, mwingine labda ana jiko la umeme na mwingine hana. Sasa hii inawapa taabu sana kwa sababu kimsingi hata wakati wa kulipia Luku inabidi wachange kwa pamoja, sasa hawawezi kukubaliana kwa sababu kuna mwingine hana matumizi makubwa ya umeme. Hili ni jambo ambalo nimelisema kwa muda mrefu sana nashukuru pia kwa sababu Wizara hii imekuwa ikinipa ushirikiano kwa kweli na wamekuwa wakinijibu majibu ambayo kidogo yanaleta matumaini japo hayaendi katika kukamilisha majibu yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilikuwa nadhani iko haja sasa hawa watumishi kila mmoja afungiwe Luku yake, lakini inasemekana kwamba inahitajika shilingi milioni 17 ili waweze kufungiwa Luku kila mtu peke yake. Sasa mimi najiuliza kama hii pesa ilikuwa haijapatikana ni kwa sababu gani walifunga matumizi ya mwanzo ambayo walikuwa nayo MaAskari hawa? Wangesubiri wakapata hii pesa ndiyo wakawaondolea kisha wakawafungia Luku kila mtu peke yake. Sasa nadhani hili suala ni la kuwadhalilisha MaAskari Polisi na kingine ni kuwagombanisha wao kwa wao kutokana na matumizi ya Luku hii. Ninaomba Wizara hii ijaribu kuangalia suala hili ambalo ni muhimu sana ili waweze kuangalia ni jinsi gani wanawasaidia MaAskari hawa ili kila mtu awe na uhuru wa kutumia umeme kwa Luku yake mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kuzungumzia pia madeni ya MaAskari Polisi, Askari Polisi akipata uhamisho anaondoka anakwenda alikopangiwa baadaye kudai pesa zake za uhamisho. Kuna posho za Askari Polisi wanaofanya *over time* anatakiwa alipwe pesa yake lakini anakwenda kufanya kazi baadaye anakuja kudai. Kuna Mapolisi wanaolinda nyumba za Viongozi Wastaafu, tena hili ni tatizo sugu na la muda mrefu na kwa sababu ni Kiongozi Mstaafu na huyu yuko kazini amekula kiapo hawezi kukataa, kwa hiyo, anachofanya ni anakwenda kufanya kazi lakini huku anabaki anadai. Kwa kweli watu wana madeni ya muda mrefu sana. Ninaomba Askari anapopata uhamisho

basi uhamisho uambatane na pesa yake ya uhamisho kama wanavyofanya katika Wizara nyingine. Ninadhani hili ni jambo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine hawa MaAskari Polisi wanaolinda nyumba za Wastaafu, nadhani na wenyewe walipwe. Hakika kuna watu wanadai madeni ya zaidi ya miaka mitatu au minne. Jaribuni kuwatazama, kazi wanayoifanya ni ngumu, nzito na kingine ni kwamba inatuletea manufaa mazuri katika nchi yetu. Nadhani tujaribu kuangalia ili tuweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha mwisho ninachotaka kusema ni kwamba tujaribu kuangalia lile Fungu lakini tujaribu kuangalia ni jinsi gani tunasaidia awamu kwa awamu majengo ya hawa MaAskari Polisi mahali wanapoishi. Msongamano sehemu wanazoishi umekuwa ni mgumu sana, maisha wanayoishi yamekuwa ni ya matatizo sana, wamekuwa wakichangia, wengine wanaweka *ceiling board* na wengine wanaweka mabati. Sasa mimi ninadhani pamoja na kwamba kweli inakuwa ni ngumu na ikiwezekana mahali penye miradi labda kuna sehemu nyingine wanaweza wakafanya wao wenyewe na kujaribu kutafuta majengo, ninadhani Serikali ijaribu kuichangia ili waweze kuishi kama watu wengine kwa sababu ni vigumu sana kwenda kuishi sehemu za uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ijaribu kuangalia hawa Askari wanaishi namna gani katika familia zao. Wana watoto, inakuwa ni taabu sana hata kama usiku ukiingia watu wanataka kuzungumza mazungumzo yao labda kupanga maisha yao yanakwendaje inakuwa ni taabu inabidi wazungumze kwa nidhamu na nidhamu iwe ni ya hali ya juu ili watoto wasije wakashtuka. Kwa hiyo, nafikiri iko haja ya kuangalia maisha wanayoishi na wao ni binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa nitamwita Mheshimiwa James Musalika na Mheshimiwa Mohamed Said Sinani atamalizia.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii, kukushukuru sana kupata nafasi ya kuongea, japo muda hautoshi lakini nianze kabisa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipeleke salamu nyingi sana kwa niaba ya wananchi wa Geita kwa kupewa Mkoa wa Geita, ni mchakato mrefu sana, tumeanza siku nyingi toka mwaka 2002 na tumeshirikiana Wabunge watatu wakati huo tunaita 'Utatu Mtakatifu' akiwemo Marehemu Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba ambaye tunamwombea Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, haikuwa safari fupi, nakumbuka tulifanya mkutano wa mapendekezo Mikoa mitatu, zile Kamati za ushauri *RCC* za Shinyanga, Mwanza na Kagera tulikutana Mwanza. Wakuu wa Mikoa walikuwepo na Wabunge waliokuwepo ni wale wa Geita, sisi watatu yaani Mimi, Mheshimiwa Ernest G. Mabina na Mheshimiwa

Marehemu Kabuzi Faustine Rwilomba na leo tumefikia hapa, tunaishukuru Serikali kwa kusikiliza hoja sahihi na haki ya watu zaidi ya milioni moja, Geita peke yake kupewa Mkoa pamoja na Mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Serikali ichukue mkondo wake, hekima na busara zake katika kuweka Makao Makuu ya Mkoa. Geita ina historia yake, Geita ni chimbuko kwenye vuguvugu la kupigania uhuru wa Tanganyika, watu wa Geita hawakukukubali Serikali ya mseto, Serikali ya Waingereza iliwapiga mabomu, wako wazee ambao ni Marehemu ambao ni Mzee Udodi, Kisenang'hwi, Mwihendi na wengine wengi walipigwa mabomu na historia ipo kutoka Geita, wanatafuta uhuru, wakishirikiana na Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere.

Geita imezaa Wilaya za Sengerema na Wilaya ya Nyang'hwale, Geita ni katikati ya Wilaya zote hizo za Nyang'hwale, Bukombe, Mbogwe na Chato. Geita sasa hivi ina miundombinu inayostahili kuwa Mkoa kwa maana ya barabara ya lami, umeme wa gridi na Mkongo wa mawasiliano yaani *Optical Fibre* ambao unaunganisha Geita na dunia yote. Kwa hiyo, mtu yeyote mwenye akili ya kawaida sitaki kusema mwenye akili timamu lakini mtu yeyote mwenye akili ya kawaida na mwenye mapenzi mema atasema Makao Makuu ya Mkoa wa Geita yawe Geita Mjini na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dr. Jakaya M. Kikwete, Rais wetu na Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi kwamba matatizo aliyoyaona ameyashughulikia. Alikuja Jimboni Nyang'hwale katika kijiji cha Kalumwa Msalala na Wazee pale walimvika Uchifu. Pale kulikuwa na Chifu Chassama, sasa wakamvika Uchifu kwa maana ya kumvika nguo, wakampa heshima na nembo yake ya Uchifu Ndeji. Sasa kumbe Mheshimiwa Dr. Kikwete alikuwa anajua matatizo yao na leo ametupa Wilaya ya Nyang'hwale, nashukuru sana.

Mimi tangu mwaka 2002 nimekuwa nikiomba Wilaya hii na nimeshirikiana na Chama cha Mapunduzi, Wilaya na Mkoa, leo tumepewa Wilaya na siyo Jimbo na Halmashauri, kwa kweli tunaishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dr. Kikwete na tunamuomba sasa aje awasalimie wazee waliompa Uchifu pale Kalumwa Msalala. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kutangaza nia kwamba nagombea tena Jimbo la Nyang'hwale. Wapo wanaopitapita sasa hivi lakini mimi sina tatizo nao ila tatizo ni kwamba kuna wengine wanasema wametumwa na Rais Kikwete. Mwingine amesema kwamba akipewa yeye Ubunge atakuwa Waziri wa Miundombinu nafasi ya Mheshimiwa Dr. Shukuru J. Kawambwa, ndiyo anavyosema lakini Mheshimiwa Kikwete ameshasema hapa hajamtuma mtu kwa hiyo waje tu kwa amani na mimi nawakaribisha ili wananchi watupime kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya kusema hayo, nizungumzie Jeshi la Polisi, nashukuru sana limepata mafanikio mengi sana, wimbi la ujambazi kwa kweli limepungua kuanzia mwaka 2005 hata kwa takwimu ambazo zinatolewa kwa kweli

ujambazi umepungua sana lakini yapo maeneo ambayo Jeshi lazima lijikite. Sina tatizo sana na ngazi za juu za Jeshi na hata ngazi za Mikoa na kidogo Wilaya, lakini kule chini bado MaAskari nadhani hawana elimu ya kutosha. Kuna Polisi Jamii, naomba hapa *IGP* Said Mwema anisikilize vizuri, kule chini kuna hawa wakuu wa vituo wanaitwa *OCDs* kwenye Kata, sidhani kama wanakwenda sawasawa kabisa na maadili na mtazamo wa Jeshi, hawajui Polisi Jamii. Kule kuna Sungusungu au wananchi wenye mapenzi mema wanaosaidia sana Polisi lakini inapotokea wanasaidia hivyo Polisi wanawageuzia kibao wanawaweka ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumza hivi yametokea kwenye Jimbo langu, ndiyo maana nasema *IGP* asikilize, katika kijiji cha Ifugandi, Kata ya Busolwa, Wilaya ya Nyang'hwale, kuna ujambazi ulitokea katika Wilaya ya Sengerema, lakini katika ujambazi ule wale majambazi waliua hata Askari Polisi. Katika kufuatilia baadaye iligundulika jambazi mmoja anatoka kwenye Jimbo langu anaitwa Bahati Lusona, alikuwa na bunduki. Askari wa Wilaya zote mbili walikuja kutafuta hiyo bunduki hawakuipata lakini wananchi kijijini wakaisaka katika siku mbili au tatu hiyo bunduki wakaipata na huyo jambazi akakimbia lakini baadaye alikamatwa. Alipokamatwa alichukuliwa na Polisi baadaye wakamuachia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina tatizo na *OCD* wa sasa hivi ni mgeni Geita, sina tatizo na *RPC* wa sasa hivi, ni mgeni Geita, hili tukio limetokea wakati hawapo, waliokuwepo wamemuachia, alipokuja akatangaza kwamba atafanya ujambazi atawavamia, mmojawapo ni Felician Katambe na Mzee Katemi kwamba ndiyo katika orodha ya wale watakaouawa, atawafanyia *line* wauawe. Usiku wa jana mimi sikulala, walikuja MaAskari wamekamata Wazee karibu watano na kijiji kizima, nusu ya kijiji sasa hivi hawako kwenye majumba yao wamekimbia msako wa Polisi. Huyu Bahati ambaye ni jambazi aliyeachiwa amekwenda kusema Polisi kwamba amenyang'anywa mali yake kwa hiyo Polisi wamekuja kukamata wale watu wote kijiji kizima na mpaka mimi Mbunge na Diwani anayeitwa Lucas Maziza hatukulala. Lakini nashukuru yule *OCD* amenielewa, amewaachia wale watu, lakini bado wale watu hawana amani kijiji kizima, nusu ya kijiji hawapo kwenye nyumba zao wanamkimbia huyu jambazi, anatangaza ufalme kwamba atawashughulikia, Jeshi la Polisi wamemuachia wakati Bunduki walikamata kwake na ushahidi upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huyu mhalifu leo amekuwa mfalme, hawa wananchi pamoja na Mbunge wao hatuna amani. *IGP* Mwema si upo? Leo kuna Tume ya Wazee watano wakiwakilishwa na Mzee Katambi wamekwenda kukuona Dar es Salaam, hawakujua kama leo utakuja hapa kwenye bajeti, sasa wameambiwa hawatakuona, kwa hiyo, wamemuona Kamanda Kova, nadhani na yeye atakuwa hapa, kuna ujumbe huo unangozwa na Felician Kambi, kuhusu tatizo la kijiji hicho. Nataka kusema kwamba hii dhana nzima ya Ulinzi Shirikishi haipo kule chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kura za maoni zimepigwa za majambazi na wauaji wa Albino, hatujajua matokeo yake. Kuna waganga ambao wanafanya kazi kihalali wamefungiwa, mtu anatoka Bugando au Muhimbili hawezi kutibika lakini walikuwa wanasaidia, sasa uchambuzi mzuri, yakinifu ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika,   naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED S. SINANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja hii iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wenzetu katika kuwapongeza Waziri,  Naibu Waziri na wataalamu wake wote, kwa hotuba nzuri ya bajeti na pia kwa kazi nzuri wanayoifanya katika ulinzi wa mali na maisha ya wananchi wetu. Kwa kweli, tunaitambua na ninaamini hata Mwenyezi Mungu pia anawaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwapongeza viongozi wetu hawa, naomba nichukue nafasi hii, nimpongeze pia *RPC* wa Mtwara na Jeshi la Kuzima Moto la Bandari ya Mtwara, kwa kufika haraka katika eneo la tukio sokoni Mtwara. Kama si jitihada zao, soko zima lingekuwa limeungua. Kwa hiyo, nalipongeza Jeshi la Zimamoto la Bandari na *Regional Police Commander* wa Mtwara na vijana wake, kwa kufika katika eneo la tukio haraka na pia kuleta ulinzi na kwa bahati nzuri ni kiasi kidogo tu cha uharibifu  umetokea. Tunampa pole sana yule mwathirika lakini moto ulizimwa na ajali kubwa ikawa imekingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuomba Wizara kuweka ulinzi katika Bahari ya Hindi hususani katika maeneo ya Mtwara. Sasa hivi Mtwara kuna uwekezaji mkubwa wa uchimbaji wa gesi unaofanywa na *ARTUMAS* na sasa hivi *OPHIR* nao wataanza kuchimba gesi katika Bahari yetu ya Hindi, utekaji nyara wa meli nao unaongezeka. Kwa hiyo, ninaomba Wizara ilitazame suala hili nasi tupate boti ya kulinda katika maeneo ya Bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumetokea ajali ambapo wananchi walipoteza maisha yao ikawa kuna taabu kubwa kwenda kuokoa maisha ya wananchi wale na pia kutafuta miili yao. Bahati nzuri kukawa na boti za *Marine Parks* ndizo zilizosaidia katika uokoaji. Lakini Jeshi la Wanamaji Mtwara hawana vitendea kazi, kwa hiyo, tunaomba Wizara ilitazame hili kwa macho mawili ili kupatikane vitendea kazi hususani boti za Jeshi la Wanamaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije katika eneo la usalama barabarani. Usalama barabarani sasa hivi limekuwa ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu, wananchi wengi wanapoteza maisha na sasa wakati umefika kutafuta mbinu mbalimbali za kuweza kuokoa maisha ya wananchi hawa. Sasa hivi tukipita katika barabara zetu kwa mfano ukitoka Dar es Salaam mpaka Dodoma utakuta miji mingi inajengwa kandokando ya barabara na ajali zinatokea kwa sababu watu wamesongamana katika barabara matokeo yake kujengwa matuta ili Madereva wapunguze mwendo. Lakini ikiwa miji itajengwa hovyo kwa mfano Chalinze, Morogoro hadi Dodoma, hebu tufikirie itakuwaje na kote kumejengwa matuta itakuwa kama tunapita katika shamba la viazi maana kutakuwa matuta matupu.

Mimi ninashauri Wizara hii ikishirikiana na Wizara nyingine hii miji ipimwe nje ya barabara kuu walau mita 500, mtu akitaka kwenda Chalinze basi aingie mita 500 afanye shughuli zake halafu atoke upande mwingine, nadhani nchi nyingi ndivyo wanavyofanya na sisi tungefanya hivyo. Kuweka matuta kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma au mpaka Mwanza hili litakuwa tatizo kwa sababu kila siku miji kandokando ya barabara inazidi na inaendelea kujengwa. Kwa nini basi kusiwe na utaratibu wa kujenga walau mita 500 kutoka barabarani? Hii itapunguza msongamano wa watu, magari yatakwenda kwa raha na ajali zitapungua na vilevile itasaidia miundombinu mingine kama barabara inataka kupanuliwa, nina uhakika barabara hii iliyopo sasa itahitajika barabara nyingine ijengwe, itajengwa wapi? Tutalipa fidia kuanzia Dar es Salaam mpaka Mwanza? Kwa hiyo, naomba hili liangaliwe, Wizara hii na Wizara nyingine wakae walione hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, magari ya Polisi hususan katika Jiji la Dar es Salaam yanatembea yakiwa na tairi vipara, *stop light* nyuma haziwaki, wakati mwingine yanapita usiku taa inawaka moja, gari la Polisi linakwenda katika utaratibu huo? Mimi naona hii ni aibu sana kwa Jeshi la Polisi kuwa na magari mabovu barabarani na wakati huo huo tukiwa na Askari ambao wanaangalia magari mabovu yakikamatwa na yakipigwa faini, sasa hawa Polisi ambao wanatembeza magari mabovu barabarani watakamatwa na nani na watapigwa faini na nani? Naomba Wizara ilirekebishe suala hili ili gari ziwe na *indicator, stop light*, yakitembea usiku yawe na taa mbili kamili badala ya kuwa na taa moja ambayo inaweza ikasababisha ajali, pia gari ziwe na tairi ambazo zinakubalika lakini kuwa na tairi mbovu hii ni aibu kwa Jeshi letu. Naomba Wizara inayohusika irekebishe suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchangia pia kuhusiana na Daraja la Umoja ambalo hivi sasa limekamilika. Sijui Wizara imechukua hatua gani ya kuweka Vituo vya Uhamiaji, Polisi na majengo mengine na huduma nyingine zinazohusiana na Wizara hii maana daraja limekwisha, tunahitaji kulitumia daraja hili sasa magari yameshaanza kupita, kwa hiyo, tunaomba Wizara iliangalie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Magereza. Magereza wana eneo kubwa wanalolihodhi katika Manispaa ya Mtwara lipatalo hekari 2000. Eneo hili liko katikati ya Manispaa ya Mtwara Mikindani, haliendelezwi. Tunaomba basi hili eneo liendelezwe kama hawana kazi nalo, lirudishwe katika Manispaa lifanyiwe kazi kuliko kukaa tu watu wanaogopa lile ni eneo la Jeshi na Jeshi linatisha hawawezi kuingia pale. Utakuta kuna eneo ambalo halina kazi hekari karibu 2000 katikati ya Manispaa, naona hili si jambo zuri.

Tunaomba basi Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho atuambie eneo hili limewekwa kwa ajili gani? Linataka kufanyiwa mambo gani? Kuna utekelezaji gani wa maendeleo unaotaka kufanywa pale? Kama halina kazi basi tulirejeshe katika Manispaa ili lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi yangu yalikuwa ndiyo hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iangalie upya suala la Wanajeshi kukaa kikosi kimoja kwa miaka mingi. Nashauri wale waliofikisha miaka kumi katika kikosi kimoja wahamishiwe katika vikosi vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Brigedia ya Nyuki, Kambi za Dunga wapatiwe usafiri. Aidha, nashauri Kambi ya Dunga, ifanyiwe matengenezo. Ni aibu Kambi iko barabarani hairidhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hospitali ya Bububu wapatiwe madawa ya kutosha pamoja na fedha za kuwahudumia wagonjwa na wale waliolazwa wapatiwe huduma ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri Wizara ikae pamoja na wananchi wa Cheju na Unguja Ukuu, kuhusu matatizo ya maeneo Jeshi kuweka mabango, ahsante.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii, kumpongeza sana Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Jeshi kujenga Taifa, Makamanda wote na Wapiganaji, kwa kazi nzuri ya kuigwa kwa nidhamu na utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nashauri JKT – SUMA ipewe fedha za kutosha na ipandishwe daraja ili iweze kupata kazi za ujenzi wa barabara na majengo ya Serikali na Tasasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Jeshi liongezewe uwezo wa kifedha kwa kununua boti za doria katika Bahari na Maziwa ili kuimarisha ulinzi wa majini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Makamanda Wastaafu, Serikali iwatumie katika masuala mbalimbali ya kiutawala kwa kuwapatia nafasi za u-*DC* na u-*RC* ili watoe mchango wao katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa 100%.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba kushukuru kwa kupata nafasi hii ili nami nichangie Wizara hii japo kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa pongezi za dhati kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Wasaidizi wake, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa na Wasaidizi wake, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha nchi

yetu inaendelea kuwa ya amani, ndani na kwenye mipaka yetu ya nchi. Pia kuwa na mahusiano mazuri na nchi za nje. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, nina maombi machache tu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, hapo awali kulikuwa na utaratibu wa vijana wakimaliza Elimu ya Juu kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa ndipo wapate nafasi ya kuajiriwa na hata baadhi ya Watumishi walitakiwa kujiunga na Jeshi hilo, hali hiyo iliwajengea Watanzania uzalendo zaidi na kuwa wakakamavu na waaminifu katika nafasi zao za kazi. Lakini tangu utaratibu huo umesimamishwa, hali imekuwa shagalabagala Maofisini, nidhamu imekuwa ndogo. Sasa je, kuna utaratibu gani wa kurejesha kama ilivyokuwa awali kuliko ilivyo sasa ambapo wanaokwenda JKT ni kwa vijana ambao wamejitolea tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, je, ni kwa nini Mkoa wa Singida hauna Kambi yoyote ya kikosi cha Jeshi, iwe la Wananchi au la Kujenga Taifa tangu uhuru?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, je, ni kwa nini Askari wote hawapewi posho ya nauli ili waweze kujilipia kwenye usafiri wa daladala wa kwenye shughuli mbalimbali? Kwani wakati mwingine hudhalilika sana kwenye upande wa usafiri maana wenye magari yao huwapita wawaonapo kituoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kwa kuwa amani iliyopo nchini mwetu inaweza kutoa nafasi ya Askari wa Jeshi la Wananchi na Kujenga Taifa kushiriki shughuli zingine, je, Wizara inaonaje kutoa msaada wa Walimu katika Shule zetu za Kata za Serikali japo kwa mkataba maalumu na kwenye Vituo vya afya (Zahanati za Vijijini) ili kuipa Serikali msaada wakati ikiwa kwenye mchakato wa kuzalisha Walimu na Wauguzi wa kutosha? Nasema hivyo kwa kuwa naamini kuna wataalam wengi Jeshini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wote walioanda bajeti hii na kuweza kuleta kwa majadiliano. Jeshi letu limeendelea kulinda mipaka ya nchi yetu na kutuwezesha kuwa na amani. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Jeshi letu bado linakumbwa na matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imejegwa katika misingi ya ujamaa na kujitegemea, hii ikiwa ni pamoja na uzalendo. Kimsingi uzalendo huu ulijengwa zaidi kwa vijana kuingia katika Kambi za Kujenga Taifa. Programu hii iliondolewa miaka ya tisini. Hali hii imefanya vijana wetu kutokuwa na uzalendo hali inayopelekea vijana kutokuwa na maadili ya Kitaifa ambayo yalifundishwa katika kambi zetu. Sijui sababu za kuondolewa kwa programu hiyo lakini cha msingi ni lini basi vijana wetu watapita katika kambi hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi letu kwa jinsi wanavyoingia katika operesheni mbalimbali kama ile ya Comoro, ujenzi wa Reli ya Kati na nyinginezo nyingi. Pamoja na kazi kubwa za operesheni zinazofanywa na Jeshi letu bado halina vifaa vya kutosha na vya kisasa mfano boti za kasi za kuweza kukimbiza boti/meli za maharamia/majambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu migogoro ya ardhi, kumekuwa na malalamiko makubwa ya wananchi kwamba Majeshi yetu yamekuwa yakijipanua na kuvamia maeneo halali ya wananchi na wakati mwingine wakiwapiga wananchi. Kwa kuwa tunaamini kuwa Jeshi letu linasimamia ulinzi na usalama na kwa kuwa wananchi wana imani nalo, inakuwa jambo lisilokubalika kwa Wanajeshi kuvamia na kuwapiga wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kumekuwa na tabia ya baadhi ya Wanajeshi kuwapiga wananchi (kujichukulia sheria mkononi) mfano tukio la Wanajeshi kumpiga hadi kufariki Bwana Fundikira eti kwa kile walichodai kuendesha gari vibaya. Lakini tumeshuhudia baadhi ya Madereva wakipata kipigo pale wanapofanya makosa ama ya kuchomekea na kadhalika, kazi yao ingekuwa kuwaripoti Polisi na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Uchaguzi Mkuu, kama Kambi ya Upinzani ilivyosema katika hotuba yao, naomba sana Wanajeshi wasijihusishe katika siasa ila wasimamie kwa haki uchaguzi huu kwani wanapokuwa na upande, ni hatari kwa kuwa hawajui nani atashinda. Hivyo, watende haki, wapige kura lakini wasishabikie Chama fulani kwani nchi yetu hii ni yetu sote.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nichukue nafasi hii, kukupongeza wewe mwenyewe, Waziri wa Ulinzi na Kujenga Taifa, pamoja na Naibu wake, kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa niaba ya Makumbusho ya Taifa ya Majimaji kwa msaada mliotoa na ushiriki wenu wa dhati kwa chakula na gwaridi siku ya Tamasha la Kwanza la Majimaji lililofanyika tarehe 27/2/2010 (kilele) katika mji wa kihistoria na kishujaa Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na shukrani hizo, pia nampogeza kwa dhati Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa kukubali kuingia katika uchaguzi wa Serikali yake na hivyo kuwezesha uhuru wa demokrasia na amani nchini mwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imekuwa na ongezeko kubwa la idadi ya watu, wengi ni watoto na vijana. Hali ya kupandikizwa kwa uzalendo ni ndogo kwa kutumia vikosi vyetu vya Jeshi la Ulinzi na JKT. Matokeo yake hali ya maasi na ujambazi inazidi kuongezeka, pamoja na juhudi kubwa inayofanywa na Serikali yetu. Maneno yamekuwa mengi na hivi siasa za vyama vingi na kuongezeka kwa mapokeo toka nchi nyingine, uzalendo umekuwa mdogo mno katika mioyo yetu na pengine ni uzalendo wa *business as usual*. Lengo langu ni kukinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, turejee nyuma wakati wa Vita vya Kagera, watu walijitolea kwa hali na mali, walichanga chakula mpaka wanyama idadi mnayo. Je, hali ile ingetokea leo (Mungu aepushe), mwitikio ungekuwa ule ule? Watu wanahitaji kulelewa na kupandikizwa uzalendo kila wakati ili ujengwe toka ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *CD* ile ya Vita vya Kagera, nashauri iwekewe utaratibu maalum wa kipindi kwenye vyombo vya habari ili kuamsha ari ya Watanzania kama ambavyo Warusi wanafanya kuhusiana na Vita vya Dunia na walipojenga ukuta wa Berlin. Tunaomba pia tupate baadhi ya kumbukumbu za zamani na historia za Jeshi letu katika Makumbusho ya Majimaji yenye uasili wa vita na kulinda demokrasia na uzalendo wa Waafrika dhidi ya Wazungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba pia ushirikianao katika kuboresha Makumbusho ya Taifa ya Majimaji katika masuala ya kihistoria ya Jeshi kwa mambo yale ambayo yanaweza kuhifadhiwa na makumbusho yetu. Tunawaomba pia mtenge tena fursa ya kushiriki katika makumbusho ya wiki, inayofikia kilele tarehe 27/2/2011 na mara hii kwa kuwa tumetoa taarifa mapema ni vema na Askari watakaoshiriki, waandaliwe mapema, tunategemea sherehe nzuri zaidi.

Katika wiki hiyo, tutatoa fursa ya siku moja kwenu ili mtusaidie kutoa semina kwa vijana wa Mjini Songea na Wilaya nyingine kuweza kuhamasishwa kizalendo kwa njia ya simulizi *(motivation).* Naamini mtarudi Bungeni na hivyo haya yatetekelezeka. Nami pia naamini hivyo, kuwa nitarudi Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nauga mkono hoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza mtoa hoja pia naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wanaowasaidia kazi, ni waaminifu, waadilifu na wachapa kazi. Hata hivyo, yako machache napenda niyawasilishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara irejee ombi langu la kujenga Hospitali ya Jeshi, Kituo cha Kambi ya Kabaya 21KJ. Hivi sasa pana Zahanati ndogo inayotoa huduma kwa Askari na raia kwa ufinyu sana. Naomba, ahadi hii niliyopewa na Mkuu wa Jeshi mwaka jana, sasa itekelezwe. Wananchi wanaridhika sana na huduma hii na mimi ni mdau wao pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nililishauri Jeshi pia lianzishe Makumbusho ya Taifa pale 21KJ kwa ajili ya yale makaburi. Watanzania wenye umri mdogo hawajui historia yake. Ni vizuri vijana na Watanzania wote kuzingatia uzalendo wa kujitoa kweli kweli kwa ajili ya wenzao pasipo kujifikiria. Uzalendo huo na moyo huo ndio matokeo ya vifo vya wale Askari. Walipoteza maisha katika ujana, lakini wakifia Taifa letu. Nashauri, hili likichelewa, basi kuwe na siku chache katika wiki au miezi fulani ili patolewe

maelezo na wananchi hasa wanafunzi wa Sekondari, Vyuo na Shule za Msingi kwenda kujua historia ya makaburi yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kuomba ni kuharakisha kumaliza mgogoro wa mipaka kati ya Kambi ya Kaboya 21KJ na wanakijiji Bugasho, Kitongoji cha Nyamigaju. Hili imekuwa kero ya muda mrefu. Hivi panaelekea kununiana kitu ambacho ni hatari, hakileti afya kwa majirani kununiana. Hivi juzi akina mama wamezuiwa wasipande mazao yao ya muda mfupi katika mbuga ambayo walikuwa tayari wamelima na wamekuwa wakilima kila mwaka. Pafanyike utaratibu mzuri wa kuleta amani ya kudumu hasa baada ya uchaguzi huu ili tusikose amani katika kipindi hiki cha uchaguzi. Nashauri wananchi wapewe nafasi ya kushiriki mazungumzo hayo ili ijulikane wana maoni gani. Lengo letu ni amani iwepo kwa pande zote na mimi mwenyewe nipate faraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na hivyo kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Kujenga Taifa pamoja na Watendaji na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni kero kwa wananchi wa Kizumbi, Shinyanga ambako kuna tatizo kubwa la:-

(a) Upanuzi wa eneo la Kambi ya Kizumbi kufanywa mara kwa mara bila kushirikisha wananchi wa maeneo jirani. Hali hii imepelekea baadhi ya nyumba za familia nane (8) kuonekana kuwa ndani ya eneo la Kambi kwa mujibu wa mipaka mipya inayojaribu kuwekwa na Jeshi, kazi inayoelekea kufanywa "Kinyemela";

(b) "Kumezwa" eneo la kilimo cha umwagiliaji la Mwamashele la hekta 400 linalotambuliwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji; na

(c) Wafugaji wa Mwamashele (Kizumbi) kunyanyaswa na baadhi ya Askari wanaokamata mifugo na kuiswaga kuiingiza ndani ya eneo la Jeshi ili kuwatoza hela isivyo halali kwa kiwango cha Shs.10,000/= kwa ng'ombe mmoja kwa siku. Huu umefanywa mradi wa kujipatia fedha kwa Askari hao wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeyasema haya baada ya kufanya utafiti na kuridhika kuwepo kwake. Ni lazima tuyatafutie ufumbuzi. Napendekeza Mkuu wa Kambi ya Kizumbi aitwe kwenye Mkutano wa Wananchi wa Mwanashele ili asikilize haya kutoka kwa wananchi wenyewe. Mkutano huu uitishwe na Mkuu wa Wilaya na mimi mwenyewe Mbunge nitakuwepo. Lengo ni kumaliza kero hizi sasa. Mkutano huu ufanyike ndani ya wiki mbili kuanzia sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi tunalithamini sana lakini kasoro hii inalichafua. Serikali pia inachafuliwa mbele ya Umma wa Wananchi wa Kizumbi. Chama changu CCM pia kitapata taswira nzuri mbele ya wananchi hawa? Lidumu Jeshi letu na Wananchi wetu wadumu, wote hawa ni kitu kimoja.

**MHE. JOHN. P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi la Ulinzi na Usalama, kwa uaminifu na uadilifu kwa Amiri Jeshi Mkuu na kwa wananchi wa Tanzania. Ni Jeshi lenye nidhamu na uzalendo tokea lianzishwe mwaka 1964. Nalipongeza kwa kazi nzuri huko Darfur na pia operesheni maalum iliyofanya huko Comoro. Hakuna Jeshi kama letu Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu hapa ni uanzishwaji wa makambi ya JKT Mikoani/Wilayani. Tokea mwanzo wa kipindi cha 2005 – 2010, nimekuwa nikiisii Wizara hii ione umuhimu wa kuanzisha kambi ya JKT eneo la Mgandu – Itigi (Itigi – Mbeya *dusty highway*) ili pamoja na shughuli za kiuchumi, Jeshi hilo liweze kusaidia kwa njia moja au nyingine kuyafukuza majambazi na majangili kwenye maeneo hayo yenye utajiri mkubwa lakini yakageuzwa kama “shamba la bibi”.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitenga maeneo matatu yenye ardhi ya kutosha na hata *“structure”* za kuanzia ujenzi wa majengo kama vile Kirumo, ilikuwa shule ya kati; Kitaraka, ilikuwa *holding ground* ya *Tanganyika Packers* na Sanjaranda, kijiji chenye umeme. Jibu la Naibu Waziri tarehe 9/6/2010 wakati anajibu swali langu la nyongeza alisema:-

*“Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri kwamba Wizara yeu imeshafanya utafiti wa kutosha katika maeneo aliyoyataja na tunaendelea na mchakato tayari kuanzisha kambi katika eneo hilo”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jana tarehe 25/6/2010 wakati anajibu swali na. 114 la Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Naibu Waziri alisema hivi:-

*“Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya Wilaya 127, ni Wilaya 16 tu ndizo zenye makambi ya JKT, hii inatokana na ufinyu wa bajeti hali itakaporuhusu Wilaya ya Singida itapewa kipaumbele”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nauliza hivi kama ni Wilaya 16 tu kati ya 127 kweli inawezekana kuanzisha kambi mbili Mkoani Singida moja Manyoni na nyingine Singida? Ningependa kujua kipaumbele ni Wilaya ipi? Wakati Manyoni, maombi yake yalipitishwa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama (W), Kamati ya Ulinzi na Usalama (M), RCC na yakawasilishwa rasmi Makao Makuu na Makamanda wakaja wakafanya utafiti na mchakato wa kuanzisha Kambi Sanyaranda unatarajiwa kuanza. Eneo hili ni kilomita 12 tu mpaka Singida Vijijini ambako Mheshimiwa Missanga anaomba kambi. Napenda kupata maelezo ya kina juu ya suala hii, kama siyo kutugombanisha ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pia kwamba Wizara iwe inayafanyia utafiti maswali yote yanayoulizwa na majibu yake kabla ya kufika Bungeni na kutoa majibu

yanayochanganya maana wananchi wanasikiliza sana vipindi vya Bunge. Wizara inapaswa kuwa na usimamizi unaoleweka na si kutoa majibu yanayoweza kuleta mkanganyiko kwa sababu ndio Wizara nyeti.

**MHE. BALOZI DR. GERTURDE I. MONGELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Kambi ya JKT, Wilaya ya Ukerewe yenye Mchepuo wa Uvuvi.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwanza hotuba ya ulinzi. Nashukuru kwa kupata fursa hii ili niweze kuchangia katika hotuba hii. Awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na watumishi wote katika Wizara hii, kwa mafanikio yote yaliyopatikana katika kipindi hiki. Mara ya kwanza Mheshimiwa Waziri alipoteuliwa, nilikuwa na mashaka kama angelimudu Wizara hii. Ninampongeza sana kwa jinsi alivyofanikiwa. Mheshimiwa Waziri ni mtu rahimu, mtaratibu, mpole, asiyeonekana kama ni mpenzi wa mambo ya kashikashi. Leo nakiri kafanya vizuri sana, ninampongeza sana kwa hekima aliyokuwa akiitumia, napongeza sana kwa hotuba aliyoitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii, kulipongeza Jeshi la Wananchi na JKT kwa mafanikio mbalimbali waliyoyapata katika kipindi hiki cha miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maombi kadhaa, vikosi vya ujenzi viimarishwe na kadri itakavyowezekana vipewe fursa za ujenzi wa majengo na miundombinu ya umma kwa kushirikiana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, JKT, kulikuwa na dhamira nzuri na muhimu sana ya kila Wilaya kuwa na kikosi/kambi ya JKT, je, dhamira hiyo nzuri ya Serikali imefikia hatua zipi za utekelezaji? Je, Kambi ya Kikosi cha JKT katika Wilaya ya Kwimba itaanzishwa lini? Naomba kufahamishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachozidi kuomba ni mafunzo ya vijana wa JKT wakiwa makambini yaendane na mahitaji ya kijamii ili mara wamalizapo mafunzo yao wasizubaezubae bila kitu cha kufanya kwa muda mrefu. Ni vyema wamalizapo mafunzo wakapewa vitendea kazi vya kuanzia maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi Waziri mwenye dhamana na Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya kuandaa bajeti ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi la Wananchi kwa kazi nzuri ya kurejesha Reli ya Kati eneo la Kilosa baada ya kuharibiwa na mafuriko. Jeshi letu linastahili pongezi kwa kazi nzuri na ya kizalendo waliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nyongeza ya bajeti hasa katika eneo la chakula na vitendea kazi muhimu ili kujenga heshima ya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi liendelee kuajiri vijana wenye taaluma mbalimbali ili kuwa na hazina ya Taifa, pindi tatizo linapojitokeza, basi hazina hiyo itumike kama ilivyojitokeza katika uharibifu wa reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa Makambi uendelee ili kuleta ufanisi ikiwa ni pamoja na nyumba za wapiganaji kuondokana na tabia ya Askari kukaa nje ya Kambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria inayoainisha wananchi kukaa eneo la mbali na Kambi za Jeshi *(Buffer Zone),* sheria hii ifanye kazi Aidha, kikosi kazi cha Jeshi kiendelee kubaini maeneo ambayo wananchi wamevamia maeneo jirani na Kambi, wanaondolewa mara moja na mamlaka zinazohusika na ugawaji wa viwanja jirani na Makambi, zionywe kuachana na tabia hiyo kwani isije ikaleta madhara kama ilivyokuwa eneo la Mbagala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la kujenga Taifa (JKT) Suma JKT ijengewe uwezo hasa kwenye masuala ya fedha kwenye eneo la Ujenzi ili Jeshi hili lishiriki katika kuomba zabuni mbalimbali za ndani kama vile ujenzi wa majengo, barabara na kadhalika, suala ambalo litaongeza maduhuli ya Wizara na hivyo kujengea uwezo Jeshi ambalo litaondoa utegemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ainisho la namna ya kusajili vijana sehemu mbalimbali za nchi kujiunga na JKT ufike maeneo yote hasa vijijini ili tuwe na vijana ambao wanaandaliwa katika maadili ya kizalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufafanuzi juu ya kurejeshwa kwa JKT kwa mujibu wa sheria (kwa wale wahitimu wa Sekondari kidato cha sita) utekelezaji wake utaanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuunga mkono hoja ya bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa kwa asilimia mia moja. Baada ya kuunga mkono bajeti hiyo ninapenda kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma na Wilaya zake umekuwa na matukio ya ujambazi ambayo yamekuwa sugu katika Mkoa mzima. Ninaiomba Wizara iweke utaratibu wa kuimarisha vikosi vilivyoko mpakani na wanaoungana na vitendo vya ujambazi kwa majambazi hawa sugu wanaokuja kuwaua wananchi wetu kwa kutumia silaha kubwa.

Katika uchunguzi uliofanywa kwa kila tukio linalotokea, silaha kubwa hutumika na wanaohusika na ujumbazi wametambulika kuwa wengi wao wanakuwa ni wanajeshi wa nchi jirani za Burundi na Rwanda. Ninashauri JWTZ wawe mstari wa mbele katika hilo kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kupambana na tukio hilo linalopoteza maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara ijipange pia katika kulipa madeni mapema kwa Askari wanapostaafu pamoja na wazabuni wanaolisha vikosi. Mara nyingi kumekuwa kukitokea ucheleweshaji kutokana na bajeti ndogo ya fungu linalohusika. Wizara ipewe bajeti ya kutosha na hasa kwa kuliwezesha Jeshi (Ngome) kuwa bajeti ya kutosha kama wanavyoomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazabuni wanaopewa jukumu la kulisha vikosi wafanyiwe uchunguzi wa kutosha kabla ya kupewa tenda hizo kwa sababu miongoni mwa wazabuni hao wamegundulika kutokuwa na sifa zisizofaa kuhusu dunia, chombo hicho cha nchi muhimu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa -Mheshimiwa Hussein Mwinyi, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi - Mheshimiwa Lawrence Masha, Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi, Makatibu Wakuu wa Wizara zote mbili pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hizi vizuri. Ni matumaini yangu kuwa watazitumia bajeti hizi kama walivyoainisha kwa kufuata vipaumbele vya kila Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya JKT ya kujitolea, ninaipongeza Serikali kwa mpango wake mzuri wa kuwapeleka vijana wengi kujiunga na mafunzo ya kujitolea ya Jeshi la Kujenga Taifa. Kitendo hicho kinasaidia kuwapa elimu vijana pia kuondoa wimbi kubwa la vijana pale wanapomaliza Elimu ya Msingi au Elimu ya Sekondari kwani sio wote hupata nafasi za kuendelea na masomo ya juu au kujiunga na vyuo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa linalojitokeza hapa ni pale vijana wamalizapo mafunzo, Serikali huchukua vijana wachache tu kujiunga na Jeshi la Ulinzi na kundi kubwa hurudi vijijini. Hii Serikali haioni kuwa vijana hawa kurudi vijijini wakati tayari wamehitimu mafunzo ya kijeshi hasa namna ya kutumia silaha kuwa wameongeza wimbi la majambazi mijini na vijijini? Ninaomba majibu ya Serikali wakati Waziri akihitimisha, kwa nini vijana wote wasichukuliwe kwenye nafasi mbalimbali za Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna tatizo la mishahara ya askari wa Jeshi la Polisi kuwa bado midogo kulingana na kazi zao ukizingatia hawana muda wa kufanya shughuli nyingine za kuzalisha mali ili kuweza kumudu ukali wa maisha pamoja na posho zao ndogo pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna kila sababu Serikali kuangalia upya mishahara ya askari pamoja na posho zao ili kuwapa moyo na ari ya kazi, pia kuondokana na tabia ya kuomba rushwa au kujihusisha na ujambazi. Nitashukuru endapo Serikali itasema lolote katika ombi langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za Askari Polisi na Jeshi la Ulinzi pia, ni ukweli usiyopingika kuwa askari wa Wizara zote mbili, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mambo ya Ndani wengi wao hawana nyumba, wanakaa uraiani au kwenye nyumba ambazo ni ndogo sana, mfano kuwa na chumba kimoja na sebule au kimoja bila sebule wakati askari hawa wanawake zao watoto wa jinsia tofauti.

Ninaomba sana Serikali ifanye juhudi ya kujenga, kwani kuishi kwenye nyumba ndogo watoto wao hawatapata maadili mazuri na kukaa uraiani, pia tunawahatarishia maisha yao na kushindwa kutenda haki kwani wakati mwingine wahalifu wanakuwa ndio wenye nyumba anakoishi askari au kuwa jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali sehemu kubwa ya bajeti ijenge nyumba za askari, mawaziri watoe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukiri kuwa Serikali hupeleka askari kwenye mafunzo ya kuongeza cheo chake kila mara ingawa bado kuna udhaifu wa wengine kusahaulika hasa wale waliojiendeleza kielimu ili apate cheo chenye kuendana na elimu aliyonayo kwa wakati huo. Vilevile utaratibu wa kuongezewa mshahara kwa wale waliojiendeleza kielimu hauko wazi. Wengi wao wamesoma, lakini bado wana vyeo hivyo hivyo hata mishahara haijabadilika. Ninasubiri pia maelezo ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuiarifu Serikali kuwa kumekuwa na mauaji ya mara kwa mara kwa wafanyabiashara wa mjini Singida. Hii inatokea tu pale mfanyabiashara anapoonekana kufanikiwa sana kifedha. Kumbukumbu zangu kama sijakosea, wafanyabiashara wakubwa wanne hadi sasa wameuwawa kinyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali kufuatilia jambo hili ili wafanyabiashara wasikimbie kufanya biashara Singida mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja hii nikiwa na imani kuwa hoja zangu zitajibiwa na kufanyiwa kazi.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumejitokeza malalamiko kadhaa kwamba Jeshi la Ulinzi linavamia maeneo ya raia na kusababisha migongano baina ya raia na Majeshi ya Ulinzi. Hali hii wakati mwingine hupelekea uvunjifu wa amani katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kushangaza kwamba kwa muda mrefu Serikali imekuwa inalea mizozo ya aina hii isiyo ya lazima. Hapana budi ni lazima hatua madhubuti zichukuliwe kuondoa mizozo ya aina hii ili jamii ifahamu maeneo ambayo inamiliki. Aidha, maeneo yote halali ya Kambi za Jeshi yapimwe na kuwekewa mipaka

na hati za kumiliki ardhi hizo zitolewe kwa wahusika. Migogoro ambayo imejitokeza miaka ya hivi karibuni ni pamoja na ule wa mpaka JWTZ, kambi ya *Tanganyika Packers* na wananchi wa Kata ya Mlangalini, Mushono na Luhulumo, pamoja na mengine mingi iliyotapakaa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu la wananchi wa Tanzania lina historia iliyotukuka, limefanya kazi nzuri katika ukombozi wa nchi za kusini mwa Bara la Afrika. Linashiriki katika kulinda amani katika nchi ambazo zina mapigano na mengi mengine ambayo yameliletea sifa Jeshi letu pamoja na nchi kwa ujumla sote tunajivunia utendaji wa jeshi letu.

Mheshimiwa  Naibu Spika, nguvu ya Jeshi lolote lile duniani ni kuwepo kwa nidhamu ndani ya Jeshi hilo. Bila ya nidhamu hakuna Jeshi lolote linaloweza kuleta mafanikio. Nidhamu inajenga mshikamano wa kifikra na utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nidhamu ninayoizungumzia hapa ni nidhamu ya kujituma na msingi wa jambo hili ni kuwa Jeshi letu liwe na uzalendo, kwa sasa tunajivunia  jambo hili kwa sababu limelifanya Jeshi letu kuwa imara sana. Nidhamu ya uwoga katika Jeshi isipewe nafasi hata kidogo kwa sababu itadhoofisha utendaji uliotukuka wa Jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niipongeze Serikali kwa kurudisha JKT kwani umuhimu wake unajulikana katika kuweka nidhamu na ukakamavu wa vijana wetu na vilevile kuimarisha shughuli za uzalishaji katika nyanja za kilimo, ufugaji, viwanda vidogo vidogo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuitanabahisha Serikali wakati inafanya taratibu za kuwapata vijana kujiunga na Jeshi hilo uadilifu liwe ni jambo linalozingatiwa, tujiepushe na upendeleo wa aina yoyote ile iwe ya kisiasa, chuki binafsi, rushwa na aina yoyote ya uchafu wa aina hiyo.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu kwamba wanajeshi wetu wana jukumu pamoja na mambo mengine kulinda mipaka ya nchi yetu. Bahati nzuri mipaka yetu haiongezeki, imebaki pale pale lakini kwa bahati mbaya kutokana na matokeo mbalimbali yamepelekea kuongezeka kwa majukumu ya wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu haya yamepanuka na kuchukua sura mpya. Kumekuwa na ongezeko la uharamia wa utekaji meli katika bahari ya Hindi, uvuvi haramu unaoendeshwa na meli za kigeni katika bahari kuu. Aidha, kutokana na maafa ya mara kwa mara yanayosababishwa na mafuriko yanayopelekea pia wanajeshi wetu kufanya kazi ya uokozi lakini ujenzi wa miundombinu ambayo imeharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na majukumu haya na mengine mengi ambayo sikuyataja hapa, Serikali inalazimika kujipanga upya kukabiliana na majukumu

haya yanayolikabili Jeshi letu. Ni lazima Jeshi letu lipewe nguvu kulingana na uzito wa majukumu yalivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mambo ambayo yanapaswa kuangaliwa ni pamoja na mafao ya walinzi wetu, viwango vyao vya mishahara, posho, chakula pamoja na viwango vya pensheni baada ya kustaafu. Tusingependa kusikia kwamba walinzi wetu baada ya kustaafu kulitumikia Jeshi letu wakawa wao sasa wanaendesha shughuli za ujambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, walinzi wetu wakiangaliwa vizuri na kupata mafao mazuri baada ya kustaafu watakuwa wanaishi maisha yaliyo bora na kamwe hawatashawishika kujiingiza katika ujambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele kikubwa katika nchi yetu sasa ni Kilimo Kwanza. Nadharia ya Kilimo Kwanza ni pana sana na watendaji *(actors)* ni wengi mno kulingana na kila mtu na nafasi aliyonayo. Jeshi letu la JKT lina nafasi kubwa sana ya kushiriki Kilimo Kwanza. Pamoja na shughuli za kijeshi wanazofanya vijana hawa, lakini ni lazima wapewe mafunzo ya ziada ya uzalishaji wa mazao ya kilimo, mafunzo ya ufundi na kazi nyingine za awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba Jeshi letu la kujenga Taifa liwe mhimili mkuu wa kuwafanya vijana washiriki kikamilifu katika kukuza shughuli za kilimo, ufugaji, ufundi wa aina zote, pamoja na mambo mengine ambayo yanapelekea kuongeza kipato na ujuzi kwa matumizi ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapana budi JKT wapatiwe ardhi ya kilimo ya kutosha na zana za kisasa pamoja na wataalam wa kuwaelekeza ili waweze kuisaidia nchi hii kuzalisha mazao ya chakula na biashara, uzalishaji wa mazao ya mifugo na kadhalika. Aidha, wapatiwe fedha za kutosha ili waweze kujikimu kwa yale mambo ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wa JKT pia wanaweza kutumika sambamba na vikosi vingine vya ulinzi kuimarisha usalama wa nchi raia na mali zao. Kwa kufanya hivyo, Taifa litakuwa linafaidika na nguvu ya vijana tulionao katika ujenzi wa Taifa.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI**: Mheshimwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Viongozi wote wa Jeshi la Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ushirikiano miongoni mwao na hotuba nzuri sana ya bajeti 2010/2011.

Mheshimwa Naibu Spika, napenda pia kutoa ushauri na maombi machache kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuimarisha ulinzi katika mipaka yetu na Rwanda, Burundi na DRC Kongo, baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na mauaji ya *Kimbari* nchini Rwanda,

uongozi wa sasa Rwanda unaongoza kwa msingi wa kukataa ukabila wa makabila makuu yaliyoko Rwanda Watusi na Wahutu na kauli ya sasa wote ni Wanyarwanda.

Kwa msingi huo wale ambao bado wanakwenda kinyume na msingi huo hawana nafasi ya kuishi Rwanda, kundi hilo ndio linalokimbilia na kujificha katika nchi yetu na kuongoza uhalifu, fujo, ujambazi na chuki kati ya nchi yetu na majirani. Kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa liongeze upenyezo wa waovu hao.

Pili, umiliki wa shamba la Songa *Sisal* Muheza *Estate* kwa ajili ya Jeshi la Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, sehemu ya shamba hili la Mkonge lilikuwa haliendelezwi hivyo wananchi waliingia na kujenga na kulima mazao ya kudumu zaidi ya miaka 15 -20 iliyopita. Jeshi la Ulinzi Tanzania lilipewa eneo la shamba hilo na sasa linakusudia kuweka rasmi kambi. Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imefuata utaratibu wa kuomba kufutwa hati ya umiliki wa awali ya shamba hilo ili kisheria iweze kutolewa hata kwa mmiliki Meya.

Mheshimwa Naibu Spika, hatua ya kwanza ya kufutwa hati hiyo itatoa nafasi ya majadiliano na mgao mpya wa eneo hilo kati ya Jeshi la Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na wananchi walioishi ndani na eneo hilo kwa muda mrefu na kujenga na kupanda mazao ya kudumu hasa katika mzunguko wa vijiji jirani vya Songa, Batini, Kwakibuyu, Mkulumilo na Kilongo. Naomba Serikali na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa litafakari jambo moja kubwa lifuatalo:-

Mheshimwa Naibu Spika, Wilaya ya Muheza imezungukwa zaidi ya mashamba 16 ya Mkonge kuanzia mpaka wa Korogwe na Muheza Kata ya Songa hadi mpaka wa Muheza na Tanga - Pongwe. Ukitoka Hale kuelekea Tanga barabara nzima kushoto na kulia ni mfano halisi wa mashamba hayo. Songa *sisal estate* kwafungo *sisal estate* hale *sisal estate*, Bwembwera *sisal estate,* Muheza *sisal estate* kitisa *sisal estate* kubwi *sisal estate,* Kibaranga *sisal estate*, Kilipwa *sisal estate*, Azimio *Dairy farm*, Kibaranga *sisal estate* na hewa *sisal estate*.

Mheshimwa Naibu Spika, narudia kuiomba Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa litafakari hali hiyo ya ardhi ya Wilaya ya Muheza asilimia 60 kuwa mashamba ya mkonge na wananchi kukosa ardhi ili wawe tayari kugawana ,aidha ya shaba la Songa *sisal estate* na wananchi wa Kata ya Songa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimwa Naibu Spika, napenda kabla ya yote kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi na wapiganaji wote kwa kazi nzuri na yenye ufanisi wa hali ya juu sana kwa nchi yetu, licha ya matatizo mbalimbali tunayo kabiliana nayo katika kuwapa wapiganaji wetu mahitaji yao muhimu.

Mheshimwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo kadhaa ambayo ningependa nipate maelezo maana yamebaki kuwa ni kero:-

- Ndege za kivita za kichina zinazoegeshwa katika viwanja mbalimbali. Je, haziwezi kukarabatiwa au zichukuliwe na watengenezaji ili wajipatie hata chache za kufanyia mazoezi mafundi wetu na marubani ili utaalamu wao usipotee bure kwa kutopata mazoezi.
- Kituo cha Nyumbu kimekuwa kikitolewa maelezo kila mwaka kuwa kitapewa msukumo zaidi, mbona naona kuwa hatujatekeleza azma ile ile aliyoiacha Baba wa Taifa Mwalimu J.K. Nyerere zaidi ya miaka 30 iliyopita kwa nini tusiiingie katika mikataba wa kushirikiana na Mataifa makubwa kama Ireland ili utengenezaji wa magari na kadhalika uanzishwe sera na sheria ya *(P.P.P)* ikipitishwa tu tuanze. Ujenzi wa nyumba pia uwe sehemu ya mpango *Public Private Partnership*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Jeshi letu limepewa jukumu la kuwafundisha vijana wetu JKT, nashauri kuwa Serikali itumie nafasi hii kuimarisha mafunzo ya vijana hawa ili waweze kujitegemea katika fani za ufundi uashi, useremala, ufugaji kilimo ili wawe wajasirimali wema wa nchi hii. Tuwapatie mitaji zana na teknolojia ili waweze kuajiri na siyo kutegemea wote wapate ajira ya majeshi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naliomba tena Jeshi letu likamilishe kuwa usahihi, madai ya wanajeshi wote na hata wastaafu ili tuone namna ya kupunguza malalamiko hayo ya siku nyingi. Nalipongeza Jeshi letu kwa kazi nzuri ya kulinda amani ya nchi hii, lakini nazidi kuuomba uongozi wa jeshi letu kupitia kwa Generali Mwamnyange aendelee kuwa na vikao na wanajeshi waliostaafu ili kusikia kilio chao maana kisheria hawa bado ni wanajeshi (*reserve*) hasa Maafisa ili kuwaweka karibu na maendeleo ya hali ya ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Mheshimwa Naibu Spika, masuala ya *pension* zao hao wastaafu zisimamiwe vizuri maana tumeshuhudia wanavyopata matatizo hapa Hazina.

Mheshimwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA**: Mheshimwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Kwanza, kama nilivyomweleza Mheshimiwa Waziri kwa mdomo, kuna taarifa ya malalamiko kutoka kwa vijana wetu, Askari waliojiunga 09 June, 2003. Vijana hao walimaliza mkataba wao wa miaka sita wa kutokukaa na familia zao au kukaa uraiani 09/06/2009. Pamoja na mkataba huo kwisha, vijana hao wameendelea kulazimishwa kukaa kama Makapera, jambo ambalo linawanyima haki zao za msingi za kibinadamu. Hali hii ipo 39KJ Arusha na uchunguzi unaonyesha vijana wa *intake* ya 16 kwenye makambi mengine wameruhusiwa kuishi nje ya kambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hisia kuwa hili linatokana na Luteni Kanali Lissu na lina maslahi ya kitenda. Vijana askari wanapodai haki zao wanafungwa kijeshi na hivi sasa wako vijana 21 ndani kwa siku 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii si nzuri inavunja haki za binadamu, inakatisha tamaa vijana na inaashiria mazingira ya rushwa. Naomba hali hii idhibitiwe haraka na au mazingira haya yachunguzwe kikamilifu kulinda taswira nzuri ya Jeshi letu.

Mheshimwa Naibu Spika, nimekwisha kuzungumza na Mheshimiwa Waziri kuhusu migogoro inayozuka hivi sasa kati ya Jeshi letu ambalo tangu limeundwa linaitwa Jeshi la Wananchi. Sura hii sasa inaelekea kupotea kwenye makambi mbalimbali kwa kuwa na mgogoro wa ardhi kati ya Jeshi la Wananchi.

Naamini kuna nia njema pande zote, mathalan kesi ya Tarime ambapo baada ya mafuriko jeshi lilikaribishwa katika eneo la kijiji, kwa kuwa hapakuwa na ushirikishwaji wa pande zote na kwa kutosimamia zoezi hilo leo uhusiano ni mbaya sana kati ya Jeshi na wananchi. Nashauri kama hatua ya haraka na dharura iundwe Kamati inayoshirikisha pande zote kwa kila eneo kuchunguza migogoro hii yote hasa Tarime kwa lengo la kupata ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimwa Naibu Spika, Jeshi letu linahudumiwa kwa kuwa na maduka yenye lengo la kupunguza makali ya maisha kwa askari wetu. Serikali kwa lengo hilo imeondoa kodi na ushuru mbalimbali ili kufanya bidhaa kwenye maduka hayo kuwa ya chini, kuna malalamiko kwa muda sasa kuwa mengi ya maduka hayo bei inafanana na mitaani jambo linaloashiria kuna mchezo unachezwa.

Mheshimwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri achukue hatua ya kufanya uchunguzi wa kina kuona kinachojiri si vema kuwe na malalamiko hayo kwa vijana wetu ambao tumewakabidhi si tu ulinzi wa mipaka ya nchi yetu lakini amani na utulivu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakupongeza kwa hotuba yako nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yako. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo :-

- Serikali ihakikishe kwamba wanajeshi wote wanajengewa nyumba za kuishi kwenye makambi yao badala ya wanajeshi hao kuendelea kupanga mitaani.

- Serikali ihakikishe kwamba maslahi ya wanajeshi yanaboreshwa.

- Kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa nalipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kazi nzuri waliyofanya katika Wilaya ya Mpwapwa kwa kujenga daraja la Gulwe na Godegode na pia namshukuru sana Mkuu wa Majeshi kwa kutembelea eneo hilo.

- Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha usafiri katika makambi ya Ihumwa, Msalato na Makutupora kwa kuwapatia magari ya kutosha ili waweze kutekeleza majukumu yao bila matatizo yoyote? Je, Serikali ina mpango gani wa kuyafanyia ukarabati majengo ya makambi hayo?

- Kupandishwa vyeo ni haki ya mtumishi. Je, katika mwaka 2009/2010 ni wanajeshi wangapi wamepandishwa vyeo na pia ni sababu gani za msingi zinazofanya wanajeshi wengi kuchelewa kupandishwa vyeo?

- Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua makambi ya JKT yaliyofungwa ikiwemo Kambi ya Mpwapwa.

Mheshimwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimwa Naibu Spika, jukumu kubwa la Jeshi letu ni kuhakikisha kunakuwa na usalama katika mipaka ya nchi yetu. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa tano, inasema mipaka ya Burundi, Kongo (DRC) ni shwari. watu wa Kigoma Mjini hatuoni kama hili ni la kweli, kwa upande wa mpaka wa Kongo si shwari maana Wavuvi wetu wanavamia kila baada ya kipindi kifupi hata wiki tatu zilizopita Wavuvi wa Kibirizi na Katonga katika Manispaa ya Kigoma Vijijini walivamiwa na kunyang'anywa mali zao, mashine 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua hali itaendelea mpaka lini? Tunaomba maelezo katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nawapongeza kwa kazi nzuri.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza juhudi za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kazi ya ulinzi na usalama wa nchi. Kazi hii iendelee vema sababu mipaka ya nchi yetu ni mipana mno. Mipaka yetu iko wazi kiasi adui anaweza kupenya popote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira magumu ya Askari na posho zao zilipwe kwa wakati ili wanajeshi waweze kufanya kazi kwa uaminifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Detach* ya Kasanga inafanya kazi nzuri ya Ulinzi na wawezeshwe zaidi ili waendelee kufanya kazi yao vizuri. Ombi langu la miaka yote

watafutiwe mahali safi, salama na palipo na hadhi kuliko kuishi katika Ngome Kongwe ya Wajerumani ili eneo hili liachwe kwa Bandari ya Kasanga na Utalii.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatamka nini kuhusu umuhimu wa kurejesha mafunzo ya JKT kwa Vijana wanaotoka Vyuoni kwa mujibu wa Sheria? Ni lini Jeshi litarejesha mafunzo haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini magari yanayotokana na utafiti uliofanywa na Shirika la Nyumba yataanza kutengenezwa kwa wingi (*Commercial Production/Manufacturing*)?

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Daraja la Jeshi Mlalakuwa (Kawe). Hali ya usalama katika daraja sio nzuri kabisa limekuwa ni kichaka cha kujifichia majambazi ambao wanapora watu pale. Hii haionyeshi picha nzuri kwa Jeshi la Kujenga Taifa ukizingatia na Kambi yao ipo pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, tunaliomba Jeshi la Kujenga Taifa wakate kile kichaka pale na pawekwe taa zitakazowaka usiku na pawe na ulinzi wakati wote wa usiku ili kulinda usalama wa wananchi wanaopita katika barabara hiyo ya *Old* Bagamoyo.

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wake wote, pia naunga mkono asilimia mia hotuba ya bajeti hii, ni hotuba yenye kueleweka na kufahamika.

Mheshimiwa Spika, nalipongeza Jeshi letu la Ulinzi kwa kazi kubwa inayofanya ya kusaidia mambo ya maafa yanayotokea nchini kama vile mafuriko na kadhalika. Kazi zao za ufundi na Uhandisi ni mchango mkubwa wa Taifa na wanapunguza gharama Serikalini, hivyo kikosi hiki cha mambo ya Ufundi na Uhandisi kiboreshwe na kupewa kipaumbele zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Jeshi la Kujenga Taifa nalo linafurahisha mipango na huduma zilizowekewa, vile vile nasisitiza Jeshi hili lizidi kupewa taaluma na ujuzi ili lizidi kuleta ukombozi zaidi kwenye kilimo kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye mambo ya ufugaji bora na uvuvi wa kisasa, pia ikiwezekana wawe mfano kwa Taifa wakianzia kwenye Kambi zao pamoja na wananchi walio karibu nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naitakia kila la kheri Wizara.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika nchi zilizo za Kiafrika Tanzania ni nchi ambayo ina usalama na utulivu zaidi. Pamoja na hayo napenda niipongeze Serikali yetu na Jeshi letu la Tanzania kwa mipango thabiti wanayoiboresha katika maeneo yetu ya mipaka ya nchi zetu kwani muda huu kuna wimbi kubwa sana la wavamizi haramu wanaovamia mipakani na kuingia katika nchi yetu hasa hao Wasomali kutokana na uvamizi huo kunatia mashaka sana kwani usipoziba ufa utajenga ukuta, nina imani nchi inahitaji ulinzi na amani iendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matatizo, napenda kuelezea kwamba, Serikali imepunguza sana pesa kwa upande wa Jeshi letu la kujenga Taifa kwani lazima tufahamu makazi yao sio mazuri kama Tabora ni makambi ya muda mrefu na ni muhimu sana kwa nchi yetu hii, lakini makazi wanayoishi hayaridhishi kabisa kwani mlinzi anatakiwa kula vizuri, kulala vizuri na kumtimizia mahitaji yake vizuri, hatokuwa na roho ya kurubuniwa hata kidogo, ni wajibu wa Serikali kutambua mambo muhimu kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia katika kitabu cha matumizi naona kwamba pamoja na kuona kitabu cha shughuli za maendeleo katika Majeshi yetu yamepunguziwa matumizi ya maendeleo kwa maana ya mafuta na mengineyo. Kwani ni ishara ya kuzorotesha shughuli hizo pengine kigezo ni uchaguzi kwani uchaguzi ulishafahamika miaka mitano kabla, kwa nini kusiwe na mfuko wa uchaguzi ambao hautoathiri bajeti za Wizara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi wana familia zao na kama familia zao zinahitaji maendeleo na katika hayo maendeleo. Je, kuna utaratibu gani wa kusaidia kwa mikopo wake wa Wanajeshi hao hasa wale niliowapa mafunzo ya ujasiriamali huko Tabora, wanajua kutengeneza sabuni, batiki, maziwa ya soya, mafuta ya kujipaka ili wanawake hao waweze kuendelea na kujenga Taifa vizuri. Je, katika Jeshi kuna fungu la huduma za maendeleo kwa Wanajeshi na wake zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA SALEH NGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, Naibu Waziri na Watendaji wake kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ili kuhakikisha nchi inabakia na utulivu ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipongeze Serikali zote mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuimarisha Muungano na kuhakikisha mipaka yote ya nchi nzima iko salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni sikivu, ni Jeshi pekee lenye nidhamu ya hali ya juu na la kupigiwa mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari hawa wanapokuwa kazini wanafanya kazi kwa bidii bila malalamiko mpaka wanapofikia kustaafu, wanastaafu wakiwa bado wana nguvu na kusababisha kufanya mambo ya ajabu ajabu. Hivyo, naomba Serikali kwa wale

wastaafu hizi posho wanazolipwa kila baada ya miezi sita walipwe kila mwezi, kwani miezi sita ni mingi. Mwisho wake wanaishia kuwa waganga wa kienyeji, walinzi wa milangoni na wengine kuwa wahalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuendelee kuwaenzi Askari wote wastaafu kwani ni hazina kubwa ya ulinzi ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**NAIBU S PIKA:** Washimiwa Wabunge, nafurahi kusema kwamba wale wote ambao walioomba na walikuwa hawajachangia kabla ya hapo wamepata nafasi, sasa wale wengine ambao wameomba na wamechangia zaidi ya mara moja bahati mbaya nafasi hiyo haitapatikana. Kwa hiyo, tukirudi saa kumi na moja tutaanza na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Naibu Waziri atapata nafasi ya kujibu hoja na Waziri wake halafu atajibu Waziri wa Mambo ya Ndani halafu tunaingia kwenye Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, kwa sasa hivi, nafikiri hakuna mabadiliko, Kamati ya Uongozi ya Bunge kwa maana ya Wenyeviti wa Kamati mbalimbali wanatakiwa kwenda kwenye kikao kule kwenye *Board Room* ya Spika.

Baada ya hapo, nasitisha shughuli hizi mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.56 Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wale wote ambao walioomba kuongea ambao hawajachangia kabisa waliweza kupata nafasi na orodha tuliifunga mchana. Utaratibu wa sasa tutamwita Naibu Waziri, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa atajibu kwa dakika 20 na Waziri atafuatia kwa dakika 20. Halafu pia tutamwita Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Waziri wake halafu tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi tutapitisha Wizara moja baada ya nyingine. Kwa hiyo tunaanza na Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kuunga mkono hoja kama ilivyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii, kwanza kwa namna ya pekee, nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa fursa aliyonipa ya kuendelea kumsaidia katika utekelezaji wa shughuli za Serikali Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia kwa dhati Waziri wangu, Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi, kwa malezi yake, ushirikiano wake na mafunzo ambayo amekuwa akinipa kwa muda wote ambao nimefanya kazi chini yake. Nitumie

fursa hii, kumshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Ndugu Andrew Nyumayo, kwa ushirikiano mkubwa ambao amekuwa akitupatia.

Kwa namna ya pekee, nimshukuru Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Davis Mwamunyange na Mnadhimu Mkuu, Luteni Jeneral Abdulrahaman Shimbo, kwa namna ambavyo hawajachoka kutufundisha mambo mbalimbali yanayohusu uendeshaji wa shughuli hizi za ulinzi na usalama wa nchi yetu. Namshukuru vile vile Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Samwel Kitundu, Makamanda Maafisa, Wapiganaji na Watumishi wa Umma wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii vile vile kumshukuru Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa ushirikiano mkubwa ambao wametupatia katika kipindi chote tulichotumikia Wizara hii. Vile vile namshukuru sana Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati Mambo ya Nje, Ulinzi, Usalama pamoja na Kamati yake kwa ushirikiano mkubwa ambao ametupatia katika kipindi chote ambacho tumefanya kazi chini ya Kamati hiyo. Kwa namna ya pekee, niwashukuru sana waajiri wangu, wananchi wa Jimbo la Songea Mjini, kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakinipa katika kipindi chote nilichowatumikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii vile vile kumshukuru sana msaidizi wangu, Meja Lugino Mgumba, Katibu Muhtasi wangu, Mama Talawa, Dereva wangu, Alfred Mbena na Mhudumu wetu, Monica Mkanuoga, kwa ushirikiano mkubwa ambao wamenipatia katika kipindi tulichofanya kazi nao. Nitumie fursa hii vile vile kumshukuru mke wangu Jane, watoto wetu, ndugu na rafiki zangu kwa kunivumilia sana katika kipindi hiki kigumu cha kutumikia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo, sasa naomba nianze moja kwa moja kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Naomba nianze na kujibu hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Paul Kimiti kuhusu uwepo wa Ndege Vita katika maeneo mbalimbali kwenye viwanja vya ndege.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Paul Kimiti kwamba katika viwanja mbalimbali vya ndege katika nchi yetu hatuna Ndege Vita. Ndege ambazo zinaonekana katika maeneo hayo ni ndege za usafiri za kawaida za Jeshi. Ndege Vita zote ziko katika vituo vinavyotakiwa kuwepo. Lakini tunatambua ndege hizi za usafiri zina matatizo, zimefanyiwa utaratibu wa kuchunguzwa na Bodi ambayo inaundwa kwa mujibu wa sheria na baada ya uchunguzi huo sasa uamuzi utafanywa kuhusu zile zinazotengenezeka ziweze kutengenezwa na zile ambazo haziwezi kutengenezwa ziweze kuuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye hoja ya Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally ambayo alitaka kujua kama fungu la huduma za maendeleo ya Wanajeshi na wake zao lipo. Nitumie fursa hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally kwa yeye binafsi kushiriki kikamilifu katika kutoa mafunzo kwa wake za Askari katika Mkoa wa Tabora. Tunapenda watu wengine waendelee kuwa na moyo kama huo wa kwake. Kwa sasa Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa, ni kuwahamasisha Askari na familia zao katika kujiunga na Vyama vya Kuweka na Kukopa ili wajenge

utaratibu wa kujiwekea akiba lakini vile vile waweze kupata mikopo kupitia katika *SACCOS*. Tunatoa wito kwa Askari na familia zao kuchangamkia wito huu ambao ndio changamoto ya sasa kwa Taifa letu katika kujenga mustakabali wa maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu hoja ya Mheshimiwa Massaburi ambaye kwa nia njema kabisa alitaka kuona JKT katika eneo la ujenzi wa barabara ikipandishwa daraja kutoka Daraja la Nne mpaka Daraja la Kwanza. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Janet Massaburi kwamba hoja yake ni ya msingi na ilikwishaanza kufanyiwa kazi, tulikuwa tunakamilisha kupata sifa za msingi kwa ajili ya chombo au Kampuni kupandishwa daraja, sifa za msingi ni pamoja na kuwa na wataalamu pamoja na vifaa vya kutosha ili kuweza kupata sifa hiyo. Sasa hivi tuna wataalamu wa kutosha na tumepata vifaa vingi vya kutosha na hivyo SUMA JKT iko katika mchakato wa kuomba kupandishwa kufikia daraja la pili kwa kufuata utaratibu wa kisheria ambao ndio unafuatwa na Kampuni zote katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijibu hoja ya Mheshimiwa George Malima Lubeleje, kuhusu utaratibu unaotumika katika kupandisha vyeo Askari wetu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwanza niseme katika mwaka uliopita mwaka 2009/2010 jumla ya Maafisa 698 na Askari 7,216 wamepandishwa vyeo na kufanya jumla ya Maafisa na Askari 7,914. Sababu zinazofanya wengine wachelewe kupata vyeo ni pamoja na kutohudhuria kozi za uongozi na za kitaaluma ambazo ni muhimu kwa mujibu wa taratibu za Kijeshi, lakini wengine kutofanya mitihani inayowapasa ili waweze kupanda vyeo lakini na wengine kushindwa ama kutofaulu katika mitihani hiyo ya kujiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile muundo wa Jeshi letu una utaratibu wa vyeo vinavyotakiwa katika kila kada. Kwa hiyo, Jeshi halipandishi vyeo kama havihitajiki kwa wakati huo. Kwa hiyo, ikama inaamua pia wangapi wapandishwe vyeo na wangapi wasipandishwe vyeo. Vile vile Jeshi linazingatia tabia njema na maisha ya Askari wake katika maisha ya Kambi ili kujua ana sifa za kuongoza wenzake. Kwa utaratibu wetu wa kawaida, Askari anapopanda cheo maana yake amepata sifa ya kuongoza Askari wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa George Lubeleje vile vile alitaka kujua kuhusu haja ya kuboresha usafiri katika Makambi ya Ihumwa, Msalato na Makutupora. Nafurahi kumfahamisha Mheshimiwa Lubeleje kwamba kilio chake hiki pia kimezingatiwa na Kambi ya Ihumwa itapewa mabasi mawili, Makutupora watapata basi moja na vile vile utaratibu wa mafuta ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za kila siku umeimarishwa hivyo watapewa mafuta zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijibu hoja ya Mheshimwa Dr. Willibrod Slaa aliyetaka kujua kwa nini maduka ya *Duty Free* yana bei sawa sawa na maduka mengine ya kawaida wakati yalitegemewa kuwa na bei nafuu zaidi. Katika ziara zetu, Mkuu wa Majeshi, Mnadhimu Mkuu, Waziri, pamoja na Naibu Waziri, tulipata kilio hicho cha Wanajeshi na tulikichukulia hatua. Wizara imeunda Kamati Maalum ya Uchunguzi

inayohusisha Maafisa wa *TRA*, Maafisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania pamoja na wamiliki wa maduka hayo ili kujua chanzo cha tatizo na kuhakikisha kwamba lengo lililokusudiwa la kuhakikisha Askari wetu wanapata bidhaa kwa bei nafuu linafikiwa. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Dr. Slaa kwamba jambo hili litafanyiwa kazi kwa kasi inayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Slaa vile vile alitaka kujua kwa nini baadhi ya Askari ambao wanafikia muda ambao wanastahili kupewa ruhusa ya kuoa au kuolewa hawapati ruhusa baada ya muda wa kisheria wa miaka sita kutimia. Umri wa kawaida ambao Askari anatakiwa kukaa katika Kambi kabla ya kuruhusiwa kuoa au kuolewa ni miaka sita na wale ambao wamepitia katika Kambi za JKT muda waliokaa JKT unahesabiwa pamoja na hiyo kwamba kama mtu amekaa JKT kwa mfano miaka mitatu maana yake ni kwamba miaka atakayotakiwa kukaa kule Jeshi la Wananchi ni mitatu ambayo inafanya jumla inakuwa miaka sita. Isipokuwa inawezekana kukawa na malalamiko mawili, matatu ambayo hayawezi kuwa sababu za kisheria huenda ikawa ni sababu za kizembe. Ndiyo maana nataka leo nimhakikishie Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa kwamba changamoto yake kwamba Kikosi cha 39KJ kina watu ambao hawapewi haki hiyo zitafanyiwa kazi, zitachunguzwa na hatua stahili zitachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijibu hoja ya Mheshimiwa Issa Kassim Issa kuhusu Askari kukaa kikosi kimoja kwa miaka mingi. Labda niseme tu kwamba utaratibu wa Jeshi hauna utaratibu wa Askari akae eneo moja kwa kipindi gani. Anapokuwa anaapa kutumikia Jeshi letu anasema ataitumikia nchi yetu saa yoyote, wakati wowote na mahali popote.

Kwa hiyo, ni mahitaji ya ikama ambayo yanaamua nani awe wapi na kwa wakati gani. Lakini vile vile mahitaji ya kitaaluma nayo pia yanaamua nani awe wapi na kwa wakati gani. Kwa mfano, huwezi kumchukua Rubani wa Ndege ukampeleka kwenye kikosi cha Songea ambako hakuna ndege yoyote wala hakuna utaratibu wa kurusha ndege. Kwa hiyo, mambo hayo yanaamua. Lakini vile vile inategemea uwepo wa bajeti ya kushughulikia uhamisho wa namna hiyo. Wale Askari ambao wanazo hoja za kimsingi za kufanya wapate uhamisho ziko taratibu ambazo Askari wote wanazifahamu vizuri ambazo watafuata na kupata uhamisho wa namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Issa Kassim Issa vile vile alitaka kujua kuhusu haja ya hospitali ya Bububu kuongezewa fedha na madawa, lakini vile vile kupata chakula cha kuhudumia raia. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Issa Kassim Issa kwamba changamoto yake tumeisikia, tutahakikisha kwamba kwa kila inavyowezekana tutaongeza idadi ya dawa na fedha zinazotumika katika hospitali hiyo. Lakini kwa chakula cha raia, wapiga kura watambue kwamba umejitahidi lakini imeshindikana, bado hatujawa nayo katika bajeti yetu. Kwa hiyo, jitihada zako zisichoke na sisi hatutachoka kukusikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijibu hoja ya Mheshimiwa John Paul Lwanji kuhusu kipaumbele cha Kambi ya JKT katika Mkoa wa Singida. Katika Mkoa wa Singida tumefanya upembuzi yakinifu katika maeneo mawili Iramba na Manyoni ili

kuona eneo ambalo linatufaa zaidi katika kuweka Kambi ya JKT. Mpaka hapa ninapoongea sasa hivi kipaumbele kiko Manyoni. Kwa hiyo, tunaomba na Manyoni yenyewe itoe ushirikiano wakati tutakapokuwa tukishughulikia mambo ya msingi ambayo yanahitaji ushirikishwaji wa eneo linalohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zulekha Yunus alitaka kuona JKT ikishiriki kikamilifu kuleta ukombozi wa kilimo. Kwanza nakubaliana naye mia kwa mia kwamba JKT ina dhamana kubwa ya kusaidia kuleta mapinduzi ya uchumi na kilimo katika nchi yetu. Tumeanza kuchukua katika hatua kubwa kuhakikisha kwamba JKT inashiriki kikamilifu katika jambo hili ikiwemo kuongeza zana na kuongeza wataalamu. Lakini vile vile JKT imeingia katika utaratibu wa kuagiza matrekta mapya 1,760 kwa mkopo nafuu hii pia yote kwa moja ya ushiriki katika mchakato huu wa kujaribu kuufuta umaskini katika nchi yetu. Tunawahakikishia Wabunge kwamba tutawapa ushirikiano wa kutosha JKT kuona kwamba wanafikia lengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Felix Kijiko, wote waliongelea ujambazi katika Ziwa Tanganyika na katika maeneo ya Kigoma na Rukwa. Katika maeneo ya Kigoma na Rukwa unategemea sana utulivu ulioko katika nchi jirani za Burundi, Rwanda na DRC. Serikali kwa upande wake itaendelea kufanya kila jitihada kuhakikisha kwamba tunashiriki katika kuwezesha nchi hizi jirani zote zinaendelea kuwa na utulivu wa kutosha ili na sisi tupate utulivu. Ndiyo maana nchi yetu imekuwa kinara katika mazungumzo ya amani katika nchi zote hizi tukijua kwamba utulivu wao ni utulivu wetu na matatizo yao ni matatizo yetu. Lakini vile vile nimhakikishie Mheshimiwa Peter Serukamba kwamba tatizo la Ujiji na Kibirizi, tumelichukua kwa uzito unaostahili na tutashauriana nao kuona namna bora ya kuwasaidia kupata utulivu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Killimbah aliongelea hoja ya SUMA JKT kuongezewa uwezo. Kama nilivyosema awali hoja hii nzuri, tunatambua umuhimu wa JKT, Mheshimiwa Waziri amekuwa akifanya jitihada kubwa kuhakikisha kwamba SUMA JKT inapata uwezo zaidi wa kifedha na wa kiutalaam. Niwahakikishieni kwamba jitihada za Wizara zitaendelea katika kuliona hilo na kulitambua na kulifanyia kazi inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hoja ya mama yangu Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella na Mheshimiwa Bujiku Sakila ambao kwa pamoja wote walitaka Kambi za JKT kuwepo katika maeneo yao kwa maana ya Ukerewe na Kwimba. Ni nia ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuona kwamba maeneo yote ya nchi yetu, Wilaya zote za nchi yetu zinakuwa na Makambi ya JKT. Lakini kama wote ambavyo mnafahamu vizuri, uwezo wa nchi yetu kwa sasa ni mdogo, hatuna uwezo wa kuwa na Kambi katika maeneo yote ya nchi yetu. Kwa hiyo, tutaendelea kuongeza Kambi kadri uwezo utakavyoruhusu na pia tukikumbuka maeneo ambayo yamekuwa kilio zaidi kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ephraim Madeje, yeye aliongelea habari ya Nyumbu kupewa uwezo wa kuzalisha kibiashara ili utafiti wake uweze kuwa na faida

kwa Watanzania na waweze kuona matunda ya utafiti huo na uzalishaji wake. Tunao mpango wa miaka 15 wa kuimarisha SUMA JKT, mpango ambao ni pamoja na kuwa na miradi ya ubia kati ya SUMA na Taasisi zingine za Kimataifa ambazo zina uwezo zaidi ya utafiti, teknolojia na wa fedha ili ziweze kushirikiana na SUMA JKT katika kuhakikisha kwamba inaibuka na kuwa na uzalishaji wa faida lakini vile vile utafiti wake kuwa na tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, aliongelea tatizo la ujambazi katika daraja la Mlalakuwa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Owenya kwamba kwa bahati wakati hoja yake ikifika tulikuwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tumemwambia na amelipokea kwa uzito unaostahili na ameandika kwenye *diary* yake nzito ambayo huwa haandiki ovyo ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijibu hoja ya Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya kuhusu haja ya kuimarisha uzalendo kwa Watanzania kwa kuwa na *CD* za vita vya Uganda lakini vile vile kuwa na kumbukumbu za vita vyetu mbalimbali ambavyo vilichangia katika uhuru wa nchi yetu. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Eng. Stella ambaye tunatambua kwamba ni Mjumbe wa Bodi ya MajiMaji kule Mkoa wa Ruvuma kwamba hoja yake ni ya msingi na itafanyiwa kazi kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nijibu hoja ya Mheshimiwa Blasio Msafiri kuhusu Kambi ya Kaboya kujengewa hospitali. Naomba nikiri kama ni kweli Serikali ilitoa ahadi ya kujenga hospitali katika eneo lile lakini kutokana na ufinyu wa bajeti hatujaweza kulifanya. Lakini nimhakikishie sasa tunakamilisha ujenzi wa hospitali ya Mirambo kule Tabora na mara itakapokamilika na kama bajeti itaturuhusu tunakoelekea ni kwenye eneo lake, avute subira akitambua kwamba ombi lake lilishakubaliwa na sasa linafanyiwa kazi. Katika mfumo wa Serikali yetu tatizo ni ombi kukubaliwa, likishakubaliwa basi unachotakiwa ni kuvuta subira. Mheshimiwa Ruth Msafiri tutakupa ushirikiano wa kutosha kufanikisha azma yako ya jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nirudie tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mkubwa ambao mmetupa. Lakini vile vile nirudie kuwashukuru wananchi wa Songea, kwa heshima waliyonipa ya kuwatumikia kwa miaka mitano iliyopita. Nawashukuru vile vile Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Songea Mjini ambao ndio walinipa nafasi ya kunipigia kura niwe mgombea wa Chama cha Mapinduzi na hivi sasa wanaendelea na mkutano wao, nawatakia kheri katika mkutano wao na kuwahakikisha kwamba niko pamoja nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa nitamwita mtoa hoja wa hoja ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuja kuhitimisha hoja yangu. Lakini

kama ilivyo kawaida nianze kwa kuwatambua wachangiaji waliochangia katika hoja yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao wachangiaji waliochangia kwa maandishi na wale waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni. Naomba nianze kuwatambua wale waliozungumza. Kwanza Mheshimiwa Wilson Masilingi, kwa niaba ya Kamati, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Mohamed Said Sinani na Mheshimiwa Haji Juma Sereweji. *(Makofi)*

Aidha wapo waliochangia wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nao ni Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Philemon Sarungi na Mheshimiwa Mwinchoum Msomi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi wako 25 ambao ni Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mheshimiwa Epharaim Madeje, Mheshimwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Eng. Stela Manyanya, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongela na Mheshimiwa Khadija Ngozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niingie katika kujibu baadhi ya hoja zilizotelewa na Waheshimiwa Wabunge lakini nitawaomba sana kwa wale ambao muda wangu utakuwa umekwisha kabla sijawafikia, waniruhusu niwajibu kwa maandishi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, muda tunaanza kuhesabu sasa, muda wa kutambua wachangiaji tumekuachia.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nianze na hoja ya Kambi ya Upinzani. Kwanza, kulikuwa na hoja ya kuimarisha uwezo wa Kamandi ya Wanamaji, kukabiliana na vitendo vya uharamia baharini. Utekelezaji wa suala hili umepangwa katika awamu mbili, kwanza kuna hatua za muda mfupi ambazo ni kuimarisha doria baharini na katika fukwe za Pwani kwa kushirikiana na Kamandi nyingine kama vile *Land Forces* na *Air Force*. Pili, kusindikiza meli zinazohitaji kupatiwa huduma hii. Lakini kuna hatua za muda mrefu nazo ni ununuzi wa meli vita ili kukidhi hitaji la kufanya doria hadi katika eneo letu la *EEZ* ili kuzuia uharamia, uharifu wa kimataifa na uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa juu ya Sheria ya Ulinzi wa Taifa kwamba imepitwa na wakati. Tunakubaliana na hoja hii na ndiyo maana nilisema siku za

nyuma kwamba kwa kuwa sheria hii ni ya muda mrefu lazima ifanyiwe kazi ili hatimaye tulete mabadiliko hapa Bungeni. Hatua tuliyofikia kwa sasa ni kwamba ile Kamati tuliyoiunda ya kuipitia Sheria ile ili itoe mapendekezo ilimaliza kazi yake na ikakabidhi ripoti yake Makao Makuu ya Wizara ya Ulinzi baada ya kupitishwa na Kamati yetu Maalum inayoitwa *Defence Force Committee,* suala hili limepelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupata maoni yake ya kisheria kabla haijapelekwa kwenye *Cabinet Secretariat* kwa madhumuni ya kupitishwa na Baraza la Mawaziri na baada ya hapo Muswada wa Sheria utatengenezwa ili hatimaye ufike kwenye Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kanuni ya Pensheni inayowanyima haki Wanajeshi kwa kutowalipa pensheni kwa kipindi kilichozidi miaka 36 na nusu, ni kweli kwamba kuna Kanuni katika Kanuni za Majeshi zinazosema kwamba Pensheni hatalipwa mtu ambaye amevuka miaka 36 na nusu ya utumishi. Suala hili limefanyiwa kazi na mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni hii yamepelekwa kwa Waziri wa Fedha ili aridhie. Baada ya hapo yatapelekwa kwa Mheshimiwa Rais ili atoe kibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge jambo lolote linalohusu mabadiliko ya Kanuni katika Wizara yoyote ambalo hatimaye linaathiri bajeti, ni lazima kibali cha Hazina kipatikane. Baada ya sisi Wizara ya Ulinzi kupitia hili na kupeleka Hazina, ni matumaini yetu kwamba suala hili sasa litapata kibali cha Hazina ili hoja hii ifutwe na tunapata matumaini kwa sababu Mheshimiwa Rais alishaidhinisha kuongezwa kwa muda wa kustaafu kwa Wanajeshi. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Rais ameongeza muda wa kustaafu haiwezekani suala lile la miaka 36 na nusu likabaki palepale.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililotolewa na Kambi ya Upinzani wanasema ni vema Serikali ikaandaa mazingira ya kulipa madeni ya Askari na wazabuni. Jibu ni kwamba Serikali imekwishatoa maelekezo kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kukusanya takwimu na nyaraka zote za madeni li madeni yote yaweze kuhakikiwa na kulipwa. Mpaka sasa madeni yote yamekwishakusanywa na kuwasilishwa Hazina. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ameanza mchakato wa kuhakiki madeni hayo. Ni matumaini yetu kwamba suala hili litamalizika katika muda ambao si mrefu ili hatimaye Wanajeshi wapate haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna suala lingine la Meli Vita kupewa mafuta. Kambi ya Upinzani ilitaka meli vita zitengewe mafuta ya kutosha ili kuweza kufanya doria zinazotakiwa. Jibu ni kwamba Jeshi limeanzisha utaratibu wa kutoa *sub-votes* kwa Kamandi zake ikiwemo Kamandi ya Wanamaji. Katika *Sub-vote* hiyo ya Kamandi ya Jeshi la Wanamaji, kuna Fungu maalum la fedha zilizotengwa kununuliwa mafuta ya meli yaani *Marine Fuel* kwa maana hiyo hata mkiangalia bajeti yetu mtaona Fungu hilo limewekwa kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba mafuta ya kutosha yanapatikana kwa ajili ya doria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo hoja nyingine ya msingi iliyotolewa nayo ni migogoro ya mipaka kati ya Kambi za Jeshi na wananchi. Sasa napenda nitoe ufafanuzi

kwamba migogoro hii tunaweza tukaigawa katika maeneo manne. Eneo la kwanza, ni maeneo ambayo bado hayajalipiwa fidia. Ni kweli Jeshi liliyahitaji maeneo hayo kwa ajili ya ulinzi wa nchi yetu lakini mpaka sasa bado wamiliki wake hawajalipwa fidia. Eneo la pili, ni maeneo ambayo Jeshi lipo lakini hayajapimwa. Kwa hiyo, maeneo haya Jeshi lilishapewa lakini ilikosekana fedha za kuyapima ndiyo maana sasa hivi yanaleta migogoro.

Eneo la tatu, ni maeneo ya Jeshi yaliyopimwa lakini yamevamiwa. Yako maeneo mengi ya Jeshi ambayo yana hatimiliki, yana *beacons* katika mipaka yake na bado kuna baadhi ya wananchi wanayavamia. Eneo la nne, ni maeneo yaliyotolewa na vijiji kwa Jeshi kwa wakati huo, siku za nyuma lakini sasa wanayataka tena wao wenyewe. Wanavijiji wanapotoa maeneo kwa ajili ya Jeshi na wakati huo ardhi ilikuwa haina thamani kama sasa baada ya kuona thamani ya ardhi imepanda, walewale waliowakabidhi Jeshi maeneo haya wamekuwa wanadai warudishiwe. Jambo ambalo kwa kweli linaleta utata kwa sababu ni kwamba maeneo hayo kuna suala zima la ulinzi. Kwa hiyo, si rahisi kuweza kuyatoa tu na kuyarudisha kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa ufupi nieleze maeneo ambayo yametajwa katika hotuba ya Kambi ya Upinzani. Kujua maeneo yaliyopimwa na kulipa fidia kwa wananchi. Ulipaji fidia kwa maeneo yaliyopimwa unaendelea kidogo kidogo kulingana na uwezo wa kifedha. Mtaona kwenye bajeti yetu ya mwaka huu, kuna Fungu la fedha kwa ajili ya ulipaji wa fidia katika maeneo yale ambayo yanahitaji fidia upande wa Wizara lakini vilevile kutakuwa na Fungu dogo la upande wa Bajeti ya Ngome.

Mheshimiwa Naibu Spika, unatakiwa ufafanuzi kuhusu maeneo ya Jeshi yaliyozungukwa na makazi. Oldonyo – Sambu WJTZ hakuna mgogoro, Kunduchi Transit Camp, Kyabakali na Biharamulo upimaji na kurekebisha mipaka utafanyika. Hapa tunakusudia kwamba kuna baadhi ya maeneo ya Jeshi ambapo tayari wananchi wameshakuwa wengi katika maeneo yale badala ya kuwaondoa au badala ya kuacha mgogoro huu kuendelea, tumeamua kwa makusudi turekebishe mipaka ili Jeshi libaki eneo lake lakini yale ambayo yameshachukuliwa na wananchi waweze kuendelea kuishi hapo. Maeneo mengine ni Tunduru – Songea, hapa hakuna mgogoro, Kasanga TPDF *Detach,* kesi ya eneo hili ipo Mahakamani, Umoja Camp JWTZ, upimaji utafanyika mwaka huu wa fedha unaokuja. Nyandoto – Tarime, upimaji pia utafayika hapo, Bulombolwa JKT, Mlale JKT, Mgambwa JKT na Cheetah JKT, maeneo haya yatafanyiwa upimaji upya na Buhemba JKT eneo hili halitumiwi na JKT tena, kambi inayotumika sasa ni Rwamkoma JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwasihi Waheshimiwa Wabunge wenzangu waelewe kwamba ipo haja ya maeneo ya Jeshi kulindwa. Maeneo mengi ya Jeshi yako katika maeneo maalum kiulinzi, *strategic point* kwa hiyo si vyema kusema kwamba kwa sababu kuna mahitaji ya ardhi ya wananchi basi Jeshi liondoke tu, huo ulinzi utapatikana vipi? Tukirudi nyuma ni kwamba siku nyingi za nyuma ilikuwa inaonekana wazi kwamba Jeshi na wananchi wanaozunguka Makambi ya Jeshi walikuwa wanaishi kwa amani sana na sababu kubwa kwa wananchi kukaribia Makambi ya Jeshi ni huduma

zinazotolewa na Jeshi. Jeshi wakiwa na Hospitali zao huduma wanatoa kwa raia walioko jirani. Jeshi wakiwa na shule zao, huduma zinatolewa kwa raia walioko jirani.

Kwa hiyo, hakukuwa na migogo siku za nyuma. Siku hizi migogoro imeanza kuibuka kwa sababu ya thamani ya ardhi. Lakini vilevile niwasihi wanasiasa, katika hili tuwe makini sana tunapolizungumza kwa sababu mwanasiasa huwezi ukawa ndiyo chanzo cha migogoro baina ya Jeshi na raia. Ni vyema tukaelewana kwamba Jeshi ni muhimu wawe na maeneo lakini vilevile tutazingatia kwamba kuna umuhimu vilevile wa kuwapa raia wetu maeneo kwa ajili ya shughuli zao za kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni ununuzi wa Meli Vita kubwa kwa ajili ya kuimarisha Kikosi cha Meli Vita kwa ajili ya kulinda bahari kuu. Kama nilivyosema, mkakati upo, ni mategemeo yetu kwamba meli hizi zitapatikana ili kuweza kutimiza azma hiyo ya kulinda maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niingie sasa katika hoja nyingine ambayo inazungumzia suala la Wanajeshi waliooana, mwanamume peke yake ndiye anayelipwa ile posho ya nyumba. Ufafanuzi wake ni kwamba, Jeshi linatakiwa kumpa nyumba Mwanajeshi kama nyumba haipo basi Mwanajeshi hupewa *allowance* ambayo inaitwa *Ngome Allowance*. Kama Wanajeshi wawili wameoana basi watapewa nyumba moja na si kila mmojawao kupewa nyumba yake. Hivyo kama nyumba haipo basi mmojawao atapewa *Ngome Allowance* ili apange nyumba. Wao ndiyo huchagua nani alipwe bila kujali jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba kwa makusudi analipwa yule mwanaume tu si sahihi, wanaamua wenyewe nani alipwe kati ya wao wawili kwa sababu ni jukumu la Jeshi kwa wale wanaostahili sio kuwapa fedha bali ni kuwapa nyumba lakini inapokosekana nyumba basi hutakiwa wao wenyewe waamue ni nani apewe fedha zile na inapotokea kwamba fedha zile imeamuliwa apewe mwanamume au mwanamke anapewa bila kujali jinsia na utaratibu huo hauko Jeshini tu, utaratibu huu ndio unaotumika hata kwa watumishi wa umma wenye stahili ya kupata nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilitolewa na Mheshimiwa Issa Kassim Issa anasema ipelekwe pampu ya maji pale Nyuki Brigade. Kwanza nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Issa, amekuwa mstari wa mbele sana kupigania maslahi ya Wanajeshi. Ameshafika ofisini kwangu mara kadhaa kwa masuala ya Wanajeshi tu. Nichukue fursa hii kumpongeza na nataka nimuahidi hapa leo kwamba pampu anayoitaka itapatikana na itapelekwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni suala la posho ya chakula itolewe kwa Wanajeshi wote. Hoja hii imetolewa vilevile na Mheshimiwa Issa Kassim Issa, akitaka posho hii itolewe kwa Majeshi yote si kwa JWTZ na JKT peke yake. Ufafanuzi ni kwamba posho ya chakula kwa JWTZ hutolewa kulingana na kanuni zinazoongoza uendeshaji wa Jeshi yaani *Defence Force Regulations* hivyo si vyema

kulinganisha na vyombo vingine. Kila chombo huendeshwa kwa Sheria na Kanuni zilizokiunda. Huo ndiyo ufafanuzi kuhusu posho hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niendelee kwenye hoja nyingine inayotaka Serikali ihakikishe kwamba Wanajeshi wote wanajengewa nyumba za kuishi kwenye makambi yao badala ya Wanajeshi hao kupanga uraiani. Wizara ina mkakati wa kuhakikisha kuwa Wanajeshi wote wanajengewa nyumba za kuishi makambini katika mfumo wa *containment,* utaratibu huu utatekelezwa hatua kwa hatua kulingana na uwezo wa Serikali.

Aidha, Serikali ilikamilisha Mkataba na *NSSF* katika kujenga nyumba za Askari Dar es Salaam na Arusha na ujenzi wa nyumba hizo umeshakamilika. Lakini vilevile kama tulivyosema awali katika bajeti ya Wizara ya Ulinzi pamoja na ile ya Ngome na JKT kumekuwa kuna fedha za ukarabati na ujenzi mdogo mdogo mpya ili kuondoa kwa kadri uwezo unavyoruhusu matatizo haya yanayowakabili Askari wetu.

Ni kweli hali ya makazi si nzuri ndiyo maana mwaka juzi Ngome walepewa shilingi bilioni tano, mwaka huu tunaozungumza wamepewa shilingi bilioni 20 na mwakani kama mnavyoona katika vitabu vyetu ni karibu shilingi bilioni 18 kwa ajili ya kufanya ukarabati na kujenga majengo mapya ya gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine ilitolewa na Mheshimiwa George Lubeleje, inataka Serikali iboreshe maslahi ya Wanajeshi. Serikali imekuwa inaboresha maslahi ya Wanajeshi kila mwaka kulingana na uwezo uliopo kifedha. Maeneo yaliyoboreshwa ni mishahara, posho ya chakula, posho zinazoambatana na mishahara kama vile *Ngome Allowance, Instructors Allowance* na *Rental Allowance.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilitolewa na Mheshimiwa Diana Chilolo inasema vijana wanaomaliza mafunzo ya JKT wanaporejeshwa majumbani bila kuajiriwa na wanajua kutumia silaha ni hatari kwa jamii. Kwanza, ni vizuri tukaelewa makusudi au malengo ya kuanzishwa JKT. Kwanza, ni kuunganisha baadhi ya vijana wachache na kujenga utaifa, moyo wa kizalendo miongoni mwao.

Aidha, kuondoa tofauti za kidini, kimila na kielimu. Kufundishwa namna ya kujitegemea kwa maana ya kuzalisha mali, ujasiliamali na ufundi stadi ili waweze kujitegemea na kuandaa Jeshi la Akiba. Kwa hiyo, kwa wale wanaoingia kwa kujitolea kwanza niseme tu vyombo vyetu vyote vya ulinzi na usalama sasa vinaajiri kutoka JKT.

Kwa hiyo, walio wengi wanapata ajira pale lakini bila shaka vyombo hivi haviwezi kuwachukua wote ndiyo maana mashirika mengine kama TANAPA, Makampuni ya Ulinzi yameanza kuchukua vijana kutoka JKT, lakini wanapewa mafunzo pale ili waweze kujiajiri wao wenyewe na hatimaye waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niingie katika hoja ya Mheshimiwa Mwananzila inayosema kwamba Serikali iwalipe Askari posho zao kwa wakati ili waweze kufanya kazi kwa uaminifu. Wizara imekuwa ikilipa mishahara pamoja na posho

zinazoambatana kwa wakati kama ambavyo Serikali inavyoelekeza. Suala hili la kulipwa kwa wakati si tatizo tena kwa sababu fedha zinatoka kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine Serikali itazame uwezekano wa kuwalipa wastaafu pensheni zao kwa kila mwezi badala ya kila baada ya miezi sita. Naomba niseme kwamba utaratibu wa pensheni za wasataafu hupangwa na Wizara ya Fedha na Uchumi. Wizara itawasiliana na Hazina kuona kama kuna uwezekano wa kupitia upya utaratibu huo. Lakini niseme tu siku za nyuma ambazo si siku nyingi zilizopita, tulianza utaratibu wa kuwalipa miezi miwili miwili, ni wao wenyewe waliolalamika wakataka urejeshwe utaratibu wa miezi sita sita. Kwa hiyo, hili ni vema lifanyiwe kazi kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, nadhani sitakuwa na muda wa kuyajibu yote yaliyopo hapa, niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba yale yote ambayo sikuyafikia, tutayajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kujibu hoja ya Mheshimiwa Kijiko inayosema Wizara ijipange katika kulipa madeni, hili nimeshalijibu. Anataka Wizara ipatiwe fedha za kutosha kwa ajili ya Bajeti ya Jeshi, sote tunaomba iwe hivyo.

Waheshimiwa Wabunge ninyi nyote mmezungumza hapa kwa kulisemea vema Jeshi letu la Ulinzi kwamba wanafanya kazi kwa uaminifu, ni vyema wakaangaliwa maslahi yao na sisi sote lengo letu ni hilo lakini mara nyingine changamoto tunayoipata ni ufinyu wa Bajeti. Serikali imekuwa ikiendelea mwaka hadi mwaka kuongeza bajeti hiyo na ni matumaini yetu kwamba hatimaye masuala yote haya yataweza kufanyiwa kazi ili kuwapa mazingira bora ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho ni kuwa, maafisa wa ngazi za juu wastaafu watumiwe katika Jeshi letu. Hili ni wazo zuri ambalo limetolewa na Mwenyekiti wa Kamati. Nataka kusema kwamba hili tutalifanyia kazi na hivi sasa kuna baadhi ya maafisa wastaafu tayari wanatumika katika Jeshi letu. Wapo wakufunzi na wapo wale ambao wamepelekwa nje ya nchi kwa ajili ya kufundisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sitaweza kumalizia zilizobaki, lakini niseme tu kwamba nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa hoja zao nzuri, tutazizingatia na zile ambazo hazijapata majibu, tutaleta kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumeona tu-*break* kuwasikiliza watu wanatuhutubia tu, tuingie kwenye Kamati ya Matumizi halafu turuhusu Wizara nyingine, maana mngeweza kulala usingizi halafu msiwasikie Mawaziri. *(Kicheko)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 38 – NGOME**

Kif. 1001 – *Defence Forces Headquarters' Command*…........................................Sh. 229,758,534,700/=
Kif. 1007 – *Land Forces Command*……………..Sh. 82, 080,788,100/=
Kif. 1008 – *Air Defence Command*……………..Sh. 27,366,164,600/=
Kif. 1009 – *Navy Command* ……………………..Sh. 19,008,620,600/=

**MWENYEKITI:** Nilifikiri mnataka kuchukua mshahara wa Mkuu wa Majeshi hapa, kumbe bahati yetu! *(Kicheko)*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 39 – JESHI LA KUJENGA TAIFA**

Kif. 1001 – *The National Service Force*..……….Sh. 88,469,947,000/=

**FUNGU 57 - WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**

Kif. 1001 – *Administration and General*………..Sh. 12,671,076,000/=

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nilipokuwa nachangia kwa maandishi, nilizungumzia kuhusiana na suala la janga lililotupata kuhusiana na mabomu ya Mbagala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Serikali itueleze, pamoja na kuwa taarifa ile ya uchunguzi haijatoka, mpaka leo tunaisubiria, hatujaipata. Lakini bado Serikali imetoa maamuzi kwamba wananchi wale ambao wanaishi maeneo ya Mbagala kwenye ile Kambi ya Jeshi waendelee kukaa pale. Kwa hiyo, ningependa kujua kwamba ni mikakati gani imefanywa na Serikali kuhakikisha usalama wa raia wale wanaoendelea kukaa pale pale wakati mpaka sasa hivi bado kuna vipande vya mabomu vinaokotwa kwenye maeneo ya watu! Asante.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Sakaya kama ifuatavyo:- Ni kweli kwamba suala hilo lilikuja, lakini kama nilivyosema sikufika mwisho katika majibu yangu ndiyo maana hakupata jibu.

Lakini ukweli ni kwamba, eneo lile limeendelea kufanyiwa ukaguzi. Tumeendelea kufanya ukaguzi, Jeshi la Wananchi linaendelea na ukaguzi. Sehemu kubwa ya eneo lile lililotokea tukio lile na taarifa kwa umma imetolewa na elimu kwa umma imetolewa kwamba wananchi wanaoishi maeneo ya jirani pale wanapoona kitu

chochote chenye dalili ya silaha silaha, basi wasishike, watoe taarifa kwa wahusika ili waweze kufanya utambuzi.

Kwa maana hiyo, ni kwamba eneo lile sasa halitatumika tena kuhifadhi milipuko, badala yake itakuwa ni Kambi tu itakayotumika kwa huduma. Kwa hiyo, hakutakuwa tena na tatizo hilo, isipokuwa mpaka sasa tunaendelea kufanya ukaguzi ili vipande vyote vilivyobaki vya hatari viweze kuhamishwa kutoka kwenye eneo hilo.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu hiyo namba 10, naomba tu labda maelezo zaidi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Detach* iliyoko Kasanga kwa muda mrefu tulikuwa tunafikiria ipate eneo ambalo ni zuri badala ya kukaa kwenye gofu lile la Bismark kwa sababu lile gofu la Bismark ni eneo la kiutalii na watalii wanatoka Ujerumani wengi tu na sehemu mbalimbali kuja kulitembelea eneo lile, lakini sasa hawawezi wakaingia pale kwa sababu limishakuwa *classified* kama ni eneo la kijeshi. Najua siwezi nikazungumzia suala la eneo ambalo lina mgogoro na liko Mahakamani, lakini: Je, si vizuri labda Jeshi likaweza kutafuta eneo lingine ambalo linaweza likajengwa ili kuweza kuwaondoa wanajeshi katika maeneo yale ambayo ni ya magofu? Kwa kweli haipendezi kwa sababu hata mtu akija, anaangalia majengo ambayo yamebomoka bomoka ndiyo wanajeshi wanakaa mle, wala haileti picha nzuri. Sijui labda pengine Waziri alione hilo ili kuweza kuwaweka wanajeshi wetu katika mazingira mazuri zaidi.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Ludovick Mwananzila kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimfahamishe Mheshimiwa Mwananzila kwamba utaratibu wa *detach* katika Jeshi la Wananchi sio utaratibu wa kudumu. *Detach* huwa zinawekwa tu katika eneo ambalo lina tatizo la muda mfupi, na tatizo likimalizika *Detach* inaondolewa. Jeshi letu liliweka *Detach* katika eneo lile kutokana na sababu za ujambazi kukithiri katika eneo lile na wananchi kuishi kwa shida. Ila kwa kuwa shida zimekwisha, wananchi wamesahau. Mara itakapotokea kwamba Jeshi limeridhika kwamba utulivu upo wa kutosha na hakuna tishio lolote la ujambazi, tutaondoa kikosi kile.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Niko katika *Subvote* 1001 – Mshahara wa Waziri. Katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimeomba kupata sababu ni kwa nini vijana wetu wanaomaliza Kidato cha Sita hawaendi katika Kambi za Kujenga Taifa wakati tunajua kabisa moja la lengo ya Makambi yale lilikuwa ni kuwajengea moyo wa utaifa pamoja na uzalendo vijana wetu hapa nchini? Lakini kuanzia miaka ya 1990, vijana wale ambao walikuwa wanatakiwa kwenda Kambini hawakwenda tena na sababu zile mpaka leo kama zipo ni hizo. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu sasa wa kuwapeleka vijana wetu wanaomaliza Kidato cha Sita katika Kambi za Jeshi ili wawe na ule moyo wa utaifa na uzalendo kwa nchi yao?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo:- Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, Serikali imeshaamua kwamba sasa mafunzo ya *JKT* kwa mujibu wa sheria yatarudishwa. Kwa maana hiyo, Serikali ilichokuwa inafanya ni kufanya maandalizi ya kuwapokea wanafunzi hao, ndiyo maana *JKT* katika miaka mitatu iliyopita ukiangalia bajeti yao, mwaka jana walipata shilingi bilioni 3.5, mwaka huu walipata shilingi bilioni 13.5.

Ukiangalia kwenye vitabu, hii bajeti tunayoipitisha sasa kuna shilingi bilioni 12.6, nia na madhumuni ni kuendeleza Makambi yale yawe tayari kwa ajili ya kuchukua vijana hao. Lakini tukumbuke vile vile kwamba sasa hivi wanaomaliza hicho Kidato cha Sita unachozungumzia wako karibu 55,000. Kwa hiyo, maandalizi lazima yafanyike vizuri ili tunapoanza, basi tuanze vizuri. Jambo hilo linafanyiwa kazi. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Sina tatizo na mshahara wa Mheshimiwa Waziri, isipokuwa katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa na ombi mahsusi la kumwagiza yule Mkuu wa Kambi ya Kizumbi kuhudhuria kikao cha kuzungumzia matatizo ya migogoro ya ardhi kule Kata ya Kizumbi, Kijiji cha Mwamashere, tatizo ambalo limekuwa ni kero ya muda mrefu. Sasa ningelipenda Mheshimiwa Waziri hapa anihakikishie kuwa ombi langu hilo mahsusi ambalo ni jepesi kiutekelezaji, litafanyiwa kazi ndani ya siku chache nilizoziomba (anazifahamu yeye Mheshimiwa Waziri).

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana.

**MWENYEKITI:** Mkumbushe. Ana makaratasi mengi sana. Ni tarehe ngapi, wapi na nani wengine watakaokuweko huko? Si umesimama, sasa tuambie wote tusikie.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunisaidia. Mimi nilimwomba suala hili tulizungumze ndani ya wiki mbili zijazo kuanzia sasa kwa mkutano utakaoitishwa na Mkuu wa Wilaya kule Mwamashere ili kusudi Mkuu huyo wa Kambi aweze kusikia kero za wananchi. Mimi mwenyewe nitakuwepo, kwa sababu nimefanya utafiti wa kutosha na kuridhika kuwa kuna kero za msingi, lakini zinatatulika. Ahsante.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimjibu Mheshimiwa Dr. Mlingwa kama ifuatavyo:- Ni kweli kwamba ameleta ombi hilo. Kimsingi tumekubali kwamba wakati tunakwenda pale, tutashirikisha jamii ya pale ili kuzungumza na kupata muafaka juu ya suala hili. Wasiwasi wangu tu ni muda anaozungumza kwamba wiki mbili pengine tutakuwa hata hatujaondoka hapa Dodoma.

Lakini, nilisema vile vile kutokana na kwamba migogoro hii iko sehemu nyingi sana nchini, tumeunda *Task Force* kutoka Makao Makuu pale ili ipite na itushauri

ipasavyo. Namwomba Mheshimiwa Dr. Mlingwa avute subira, *Task Force* hii itakwenda eneo hilo, itazungumza na hao wananchi na hatimaye italeta ripoti na tutaifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Siyo utaratibu kwa mtu ambaye amepewa kazi pale aje azungumze na ninyi. Wenye *political responsibility* ni hawa hawa Mawaziri hawa. Kwa hiyo, umemwalika Waziri aje na amesema atakuja muda ukiruhusu.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo nilipata wivu wakati anaahidi Mheshimiwa Waziri kumpelekea Mheshimiwa Issa pampu ya maji kwenye Kambi yake. Katika mchango wangu na mimi nilisema kwamba Serikali iliniahidi kwamba itachimba kisima katika Kambi ya Jeshi la Wananchi Mwanyanya na kisima hicho hakigharimu pesa nyingi sana. Sasa Waziri atanihakikishia vipi kwamba wanajeshi hao wanapata kisima hicho ili wasipate kuchangannyikana na wananchi?

**MWENYEKITI:** Wewe utachangia shilingi ngapi? Mheshimiwa Waziri, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Masolwa kwamba hana sababu ya kuwa na wivu kwa sababu eneo lake pia tutachukua hatua za kuhakikisha kisima kinajengwa. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka mshahara wa Waziri hasa katika hali hii ngumu ya maisha kama atashindwa kujibu swali langu. Mimi kwa muda mrefu sana tangu hata enzi za Sarungi na wengine nimekuwa nikiomba *JKT* yenye mchepuo wa uvuvi katika Visiwa vya Ukerewe. Ukiangalia hapa kuna michepuo ya *industries* na mambo mengine, lakini: Je, uvuvi na hasa ukizingatia Kilimo Kwanza, kwa nini kusiwe na mchepuo? Nilitegemea Waziri kwa sababu anatoka Visiwani hatakuwa na kigugumizi cha kuweka Kambi kwenye visiwa ili waweze kutumia yale maji na kuleta tekinolojia za kisasa za kuvua kuliko kumwachia Magufuli anakimbizana na wavuvi kushika zana haramu? Nataka ufafanuzi makini na mzito kuliko ule wa kusema bajeti ina ufinyu. Ufinyu tu inapokuja, Ukerewe!

**MWENYEKITI:** Hiyo mpya! Haya Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu hoja ya mama yangu Mheshimiwa Getrude Mongella kwamba tunapolenga katika kuhakikisha vijana wetu wanajitegemea wanapotoka *JKT*, inatia faraja sana tunapopokea mawazo mapya kuhusu namna ya kuiweka mitaala yetu. Kwa hiyo, nimhakikishie tu mama yangu kwamba hoja yake ya kuona namna ya kuweka mtaala tumeipokea, naye mwenyewe kwa kuwa ni msomi atatushangaa sana tukitangaza hapa kwamba tumekubali kabla hatujakaa na watalaam. *(Kicheko)*

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nishukuru kwa sababu Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo letu amezungumzia kuhusu matatizo yetu ya Kizumbi. Nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba tatizo hili ni sugu na namwomba aanze mapema maana hata uchaguzi wetu unaweza ukaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo langu mimi, katika maandishi nilikuwa nimemwambia Mheshimiwa Waziri kwamba Wanajeshi wetu Wastaafu, Shinyanga tuna sehemu kubwa sana ya Wanajeshi na wengi wamestaafu, lakini, mishahara yao wanapewa isivyo. Hivyo, wanaomba na barua nilishamwandikia Waziri wa Fedha na Waziri wa Ulinzi namwambia, wanaomba mishahara hiyo wapewe tarehe 30 Desemba au tarehe 30 Juni ili wahudumie watoto wao wanaokwenda shule, wanaadhirika kiasi cha kutosha. Ahsante.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimemwelewa vizuri Mheshimiwa Masunga, anazungumzia malipo ya pensheni kwa wastaafu. Nilisema wakati najibu hoja hapa kwamba utaratibu uliopo sasa ni kulipa mara mbili kwa mwaka, kila miezi sita. Wanalipwa nadhani Januari, halafu wanalipwa tena Julai. Kwa lengo la kuwa wanalipwa kabla *(pre-payment)* ile ya Julai ndiyo ina-*cover* mpaka Desemba. Sasa, kuna wakati hapa waliomba wao wenyewe kwamba mnatupa kipindi kirefu sana, mnaonaje kama mngebadilisha huu utaratibu? Kweli tulizungumza na Hazina, ikajaribiwa mwezi mmoja tu, wakapewa miezi miwili, malalamiko tuliyoyapata yalikuwa ni makubwa kuliko yale ya miezi sita. Sasa, sina uhakika kinachotakiwa hasa ni nini. Lakini kama ni tarehe tu anazozizungumzia Mheshimiwa Masunga, basi namhakikishia kwamba suala hili tutalifikisha Wizara ya Fedha ili waweze kupata kwa utaratibu huo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami pia nilikuwa napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba, kuna askari wengi hasa wale ambao wamekuwa wakichukua taaluma mbalimbali kama vile ualimu, inakuwa ni vigumu anapochukua taaluma hii kupandishwa cheo, anakaa kwa muda mrefu na wakati mwingine mpaka anastaafu. Sijui kuna utaratibu gani au Wizara iweke utaratibu wa kuweza kuwapandisha vyeo hawa wenye taaluma hasa ya ualimu, na je, wanaweza wakasaidia katika shule za jirani zinazowazunguka kufundisha? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme tu kwamba tumekuwa tukipandisha vyeo watu kama nilivyoeleza awali kutokana na sifa zao mbalimbali, kwanza taaluma za kijeshi, lakini pia vilevile taaluma za kawaida na pia muda wa kukaa kazini. Katika kuhakikisha kwamba vyeo vinatoka kwa haki na kwa wakati, Makao Makuu ya Jeshi imeboresha sana utaratibu wake mwaka huu, vyeo vya kijeshi vimetoka vingi kuliko mwaka wowote katika historia ya nchi yetu. Kwa hiyo, tutaendelea kuliboresha hili na kuhakikisha askari wanapata haki zao.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance an Accounts* ................................ *Sh.* 251,139,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning*..................................... *Sh.* 424,339,000/=
Kif. 1004 - *Internal Audit*................................................*Sh.* 112,942,000/=
Kif. 1005 - *Procurement Management Unit*..............*Sh.* 74,529,000/=
Kif. 1006 - *Legal Services Unit*........................................*Sh.* 49,900,000/=
Kif. 1007 - *Information,*
*Education and Communication* ...........*Sh.*117,034,000/=
Kif. 1008 - *Military Tender Board Unit*............................*Sh.* 97,560,000/=
Kif. 1009 - *Independent Telecommunication*
*network*....................................................... *Sh.* 69,517,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**MHE. SUSAN J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-vote* 2001 Kifungu kidogo cha 220200 - *Utility Supplies and Services.* Nilikuwa ninaomba kupata ufafanuzi, ni kwa nini kifungu hiki mwaka huu hakijatengewa fedha hata kidogo wakati tukijua kuwa wanahitaji maji na mambo mengine? Kwa sababu ninaelewa kwamba *Utililities and Supplies* ni masuala yanayohusu maji, umeme na kadhalika *unless* wamepeleka katika kifungu kingine.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sio sahihi hivyo anavyosema kwamba malipo haya yapo katika kasma nyingine. Haya ni malipo ya *Utilities* kama yanavyoonekana hapa. Kwa hiyo, siyo kila Idara inalipia *utilities* zake kwa mfano katika Wizara hii itakuwa ni idara moja tu ambayo inalipia umeme, maji, na kadhalika.

Kif. 2001 - *Industries Construction and*
*Agriculture*..................................................Sh. 508,917,000/=

Kif. 2002 -*Military Research and*
*Development*.........................…………… Sh. 212,680,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## MIPAGO YA MAENDELEO

## FUNGU 38 – NGOME

Kif. 1001 - *Defence Headquarters*
*Command*.............……………………….. Sh. 18,454,334,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 39 - JESHI LA KUJENGA TAIFA**

Kif.1001 - *The National Service Force* …………Sh. 12,649,883,000/=

**MWENYEKITI:** *Infact* Waziri ulipojibu pale ilikuwa ya maendeleo *re-current expenditure* hukuzitaja ile shilingi bilioni kumi na mbili kwa *JKT*.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha nilizozitaja ni kwa ajili ya maendeleo kwa maana ya ujenzi. Kwa hiyo, fedha hizi zinatumika kwa ajili ya kuyatayarisha hayo makambi ya *JKT* kwa ajili ya *intake* hiyo. Fedha za uendeshaji zitaombwa wakati huo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 57 - JESHI LA KUJENGA TAIFA**

Kif. 1001 - *Administration and General*.....................……………… Sh.0

Kif. 1003 - *Policy and Planning*............………………………………. Sh.0

Kif.1009 - *Independency Telecommunication Network*……..........Sh.2,000,000,000/=

Kif. 2001 - *Industries Construction and Agriculture* ……........................………Sh. 12,915,763,000/=

Kif. 2002 - *Military Research and Development* ……................………..Sh. 114,200,000,000/=

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*

*(Makadirio ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 yalipitishwa na Bunge)*

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011**
**Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla ya yote napenda kuchukua fursa hii kusema kwamba ninaunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi asubuhi ya leo.

Ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, lakini kabla sijafanya hivyo, naomba uniruhusu nikupongeze wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri katika shughuli zetu za leo. Mbali na hayo, kwa kweli umekuwa ni kiongozi ambaye umeonyesha mfano wa kuigwa hapa katika shughuli zetu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue nafasi hii pia nitoe shukrani zangu kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge ambaye kwa kweli na yeye ameliongoza Bunge letu vizuri kwa njia ya viwango na ningeomba unifikishie salamu zangu kwake. Lakini pia ningeomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wenyeviti wa Bunge letu na Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango mbalimbali ambayo wamekuwa wakiitoa katika miaka yote hii kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii niishukuru familia yangu kwa kunipa moyo katika majukumu yangu ya kuwatumikia wananchi. Pia nawashukuru sana waajiri wangu wa Jimbo la Bukoba Mjini kwa kunipa nafasi hii ya kuwawakilisha, ya kuwasemea katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichukue nafasi hii niwashukuru viongozi wa Chama na Serikali wa Mkoa wa Kagera hasa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Mohamed Babu, Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Bukoba Mjini, Waheshimiwa Madiwani ambao tunafanya kazi vizuri, viongozi wa Chama cha Mapinduzi pale Bukoba Mjini wote kwa ushirikiano ambao wamenipa katika kipindi hiki ambacho nimekuwa Mbunge, kipindi hiki cha miaka mitano.

Lakini pia naomba nimshukuru Waziri wangu, Mheshimiwa Lawrence Masha. Kwa kweli mimi naweza kusema tena kwa furaha kabisa kwamba imani aliyonipa wakati nikifanya kazi na tunaendelea kufanya kazi na tunaendelea kufanya kazi kwa kweli sina

lalamiko lolote kuhusu Mheshimiwa Waziri. Kwa kweli amenipa imani ya kutosha katika kufanya kazi katika Wizara hii na ningependa niweke katika *record* kuwa ninamshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ningependa niwashukuru wafanyakazi wenzangu katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ushirikino mkubwa ambao wamenipa. Mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, napenda nichuke nafasi hii nitoe shukrani za kipekee kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda ambaye kwa kweli maelekezo yake mengi kwa kweli nimekuwa nikiyapokea, lakini kubwa ni kuwa nilipopata nafasi ya kusafiri naye katika ziara za ndani ya nchi kwa kweli nilijifunza mengi sana kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Baada ya kusema hayo, naomba nichukue fursa hii kujibu baadhi ya hoja ambazo zimejitokeza katika mjadala wa Wizara hii, lakini hasa ningependa nijikite kwanza katika hotuba ambayo imetolewa na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naitizama hii siyo kama hoja ambayo ameitoa Mheshimiwa Ibrahimu Mohamed Sanya ambaye ni rafiki yangu. Angekuwa ameitoa yeye kama yeye nafikiri tungezungumza vingine, lakini kwa kuwa ametoa msimamo wa Kambi yake, sina budi na mimi nijibu, nitoe msimamo wa Serikali. Kwanza Mheshimiwa Sanya alipokuwa akitoa hotuba yake amezungumzia Polisi hasa kusema kwamba Polisi wamekuwa hawana msimamo, msimamo wao ni kwenda upande wa Chama Tawala na akachukua nukuu moja ambayo ameitoa katika kitu ambacho amekiita Taasisi ya Umoja wa Mataifa *(United Nations International Police Task Force)* na ame-*quote* pale, lakini pia akauliza: Je, Jeshi letu la Polisi linakwenda na nukuu hii?

Naomba niseme na tuweke *record* vizuri tu. Hakuna kitu kama hicho kinachoitwa Taasisi ya Umoja wa Mataifa, yaani *United Nations International Police Task Force* ya Polisi. Haipo. Hiki ni kikosi kazi ambacho kiliwekwa na Umoja wa Mataifa mwaka 1992 mahsusi kushughulikia suala la *Bosnia – Herzegovina* na hii ilitokea kwa sababu ya nchi ya *Yugoslavia* ilivyovunjika, yakatokea matatizo makubwa pale. Kwa hiyo, baada ya hiyo nchi kusambaratika Umoja wa Mataifa uli-*establish,* uliweka hii kama *task force* na ukitazama *task force* kwa Kiswahili maana yake ni kikosi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama Taasisi, hakuna kitu kama hicho. Hii iliwekwa na sasa nukuu aliyoifanya na inaleta picha kama vile nukuu ambayo Umoja wa Mataifa umetoa kama mwongozo wa askari wote duniani ambayo siyo sahihi. Hii *task force* ilikuwa inajaribu kutizama nchi ambayo ilikuwa *established* kama nchi mpya baada ya nchi ya Yugoslavia kuvunjika.

Kwa hiyo, ilikuwa kama wataweka *police force* iwe ni *police* ya aina gani na ndiyo ilikuwa *spirit* ya hiyo nukuu. Kwa hiyo, mimi nasema na kuwaambia ndugu zangu wa Upinzani kuwa, kwa kweli tusijaribu kupotosha mambo na hii mimi nimeichukulia kwa uzito zaidi kwasababu imechukuliwa iwe kama mfano wa kuonyesha kwamba askari wetu ama Jeshi letu la Polisi haliendani na nukuu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule ambako kulikuwa hakuna Jeshi la Polisi na nchi haikuwepo walikuwa ndiyo wanaanza. Baada ya kusema hayo na kusema kuwa hiki kilikuwepo, hotuba hii ambayo ameitoa Mheshimiwa Sanya ambaye ni rafiki yangu, lakini kwa kuwa ameitoa kama Msemaji wa Kambi ya Upinzani sina budi niijibu vilivyo, kilichonisikitisha haina hata hoja moja iliyozungumzia kuhusu kazi kubwa ambayo Jeshi la Polisi katika nchi yetu inafanya katika kulinda amani na katika kuleta mshikamano katika nchi yetu.

Tunao askari wetu wengi wamepoteza maisha, tunao askari wetu wengi ambao wamejitolea katika njia mbalimbali za kuhakikisha kwamba Taifa letu linakaa katika hali ambayo tumekuwa nayo, sasa niseme tu kuwa kwa kweli hilo kidogo mimi nimelichukua na kuona kwamba siyo kitu ambacho kimekwenda sawa, lakini pia niseme kwamba sisi sote ni Watanzania na nchi yetu moja. Hii *speech* ukiisoma kwa umakini sana unaona kabisa kuwa inajaribu ku-*insight* na ku-*excite* Jeshi letu la Polisi liende kinyume na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli inazungumzia matatizo yao, lakini ni katika njia ya ku-*agitate* kuwafanya wafanye mambo ambayo ni tofauti kwa kweli. Kwa hiyo, mimi niseme kuwa katika lugha ambazo tunazitumia ningeshauri tuwe makini sana kwasababu tunaweza kudhani kuwa tunatetea, lakini tukaanza kuanzisha kitu ambacho kinaweza kuleta madhara kuliko tunavyotarajia au tunavyodhani. Katika hoja ambazo wamezitoa Kambi ya Upinzani leo asubuhi wamezungumza juu ya ongezeko la makosa ya jinai na hii ni kama kuashiria kwamba hali inakuwa mbaya, lakini hizi taarifa na hesabu ambazo zimetolewa hapa zimetokana na Jeshi la Polisi lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii kwa kweli tukubalia au tusikubali watu wanavyozidi kuongezeka, shughuli zikazidi kuongezeka. Ina maana kwamba, inaendana na matatizo ambayo yanakuwepo katika jamii. Tanzania siyo kisiwa, hii inatokea kila mahali nchini isipokuwa ni kwamba tutaimarisha zaidi *intelligence* ili kuweza kupata taarifa kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa nchi salama, upelelezi utaendelea na kuhakikisha kuwa mambo yanakwenda vizuri, lakini kubwa zaidi kuweza kupata vitendea kazi ili askari wetu waweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Kambi ya Upinzani wamezungumza juu ya mabadiliko binafsi ndani ya Jeshi la Polisi katika kutekeleza Sheria Na.5 ya mwaka 1992 kwa maana ya kusema kwamba Jeshi la Polisi tuseme kwamba limekuwa likijihusisha na mambo ya siasa kinyume cha taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi ninasema kuwa baada ya kusikiliza hotuba ambayo imetolewa na Kambi ya Upinzani na hoja zao ni kuwa kinachonisikitisha hapa wakati anazungumzia suala hili, anasema : "*lakini inasemekana…*" Sasa ina maana hapa tunazungumzia kitu ambacho hatuna uhakika nacho. Kama inasemekana, inasemekana na nani?

Maana katika Bunge hili inakuwa bora na inapendeza zaidi kama tukisema mambo ambayo tuna uhakika nayo, lakini kubwa tuwe na ushahidi nayo wa kusema kwamba kweli katika Jeshi la Polisi wapo Polisi ambao wanajihusisha na vitendo vya kisiasa.

Lakini hii ya kusema kuwa inasemekana, mimi ninasema siyo sahihi na siyo kuwatendea haki. Jeshi lote la Polisi ni imara, wanafanya kazi nzuri, na ninadhani tusitumie lugha ambayo inaweza ikawavunja moyo.

Mheshimwia Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imetolewa na Kambi ya Upinzani inazungumzia utekelezaji wa ahadi ya kuwaingiza askari kwenye Bima ya Afya, Serikali ya Awamu ya Nne imekwishaamua na utaratibu wote umeandaliwa kuanzia mwezi Julai, 2010 askari watakuwa katika mfumo wa Bima ya Afya.

Katika kujibu suala hili ambalo linaendana na suala la Bima ya Afya, Kambi ya Upinzani wamesema kwamba Serikali ilikuwa imeahidi kuwapa shilingi 200,000 kila mwaka kwa kila askari na hizo zingekuwa katika mshahara wake. Lakini Serikali ilipokaa ikatafakari zaidi ilionekana kwamba hii stahili ambayo tungewapa ya shilingi 200,000 kwa mwaka isingeweza kutosheleza katika matibabu yao hawa askari, kwa hiyo, badala ya kuwapa zile pesa imeonekana tu waweke katika Bima ya Afya wawe kama watu wengine na hiki ni kitu kipya hakijawahi kuwepo. Hapa nadhani Serikali imefanya jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho Kambi ya Upinzani wamekizungumzia ambacho ni makato ya fedha ya shilingi 5,000 kutoka kwenye mishahara ya askari bila ridhaa yao. Hii mimi niseme kwamba si kweli na siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali moja la msingi niliwahi kujibu hapa Bungeni nilieleza kwamba mfuko huu ambao tumekuwa tukiuzungumzia wa shilingi 5,000, mfuko wa kufa na kuzikana ulikuwepo tangu miaka ya 1980, na ni mfuko wa hiyari wala si mfuko wa lazima. Huu ni mfuko ambao tumesema wale ambao wanaona kwamba wanaweza wakapata manufaa zaidi kutokana na mfuko huu wameweza kujianzishia mfuko huu na hicho ni kitu ambacho walikianzisha wao wenyewe. Sasa inapokuja picha ya kuonyesha kwamba hiki ni kitu ambacho wanalazimishwa hii siyo kweli, ni kitu cha hiyari, wale ambayo wanahiyari wanafanya na wasiokuwa na hiyari hawalazimishwi hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo Kambi ya Upinzani wamezungumzia ni uhamisho wa askari bila kuzingatia kazi zao za msingi na haki zao za msingi hasa katika mambo ya malipo na kadhalika. Hili ni jambo ambalo tumekuwa tunalizungumzia, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi amekuwa akilizungumzia na hata jana lilikuwepo swali hapa nimejibu pia, tukisema kwamba ni kweli haki zao za msingi ambazo zinaendana na malipo zimechelewa, lakini yamekuwa ni madeni ambayo tumeahidi tutayalipa baada ya kuyahakiki hayo madeni na hizi ndiyo haki zao za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu malipo ya wazabuni ambayo Kambi ya Upinzani wameyazungumzia, ni kweli suala hilo tunalo bado tunafanya uhakiki na madeni hayo na yatalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia wamezungumzia juu ya udhamini wa askari wakati wa kupata mikopo kutoka benki na hasa mikopo ya *SACCOS*. Hapa tunasema kwamba ni hiyari askari kujiunga katika *SACCOS*, hakuna ulazima lakini kikubwa ni kuona kwamba tunawasaidia kuona kwamba hawaendi mahali ambapo gharama za kupata mkopo zinakuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ambazo zimewekwa ni nyingi lakini kuna hoja moja kubwa ambayo Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa ambaye hapa naona hayupo, Dr. Slaa amezungumzia juu ya mateso na uonevu ambayo wananchi wa Karatu wamekuwa wanapata kutokana na tajiri mmoja anayeitwa Samwel Kastuli, akasema kwamba huyu anashirikiana na vyombo vya dola katika kuwanyanyasa wananchi. *(Makofi)*

Mimi naomba niseme kwamba hii siyo sahihi wala siyo kweli. Vyombo vya dola haviwezi vikashirikiana na mtu kwa kuwavunjia haki Watanzania na kuwanyanyasa Watanzania. Kitu kilichofanyika na nilizungumza na Dr. Slaa nilimwambia aniletee malalamiko kuhusu huyu mfanyabiashara na kweli tumeyapata, pia akanipa majina ya watu ambao wameweka malalamiko yao dhidi ya huyu mfanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumwambia kwamba yanafanyiwa kazi, haitakuwa sahihi kusema hapa kwamba tutafanya nini, kwa sababu huyu anayemtaja ambaye ni mtuhumiwa kwa njia moja au nyingine, maana yake anasema ana kesi kule hatuwezi tukasema tunafanya nini. Vyombo vinavyohusika vitafanya kazi yake na awe na uhakika na amani kwamba haki itatendeka. Na ningependa kuchukua nafasi hii kuwahakikishia wale ambao tumepata majina yao wanaomlalamikia mfanyabiashara huyu wapo watano na malalamiko yao yatafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na suala lingine ambalo amelizungumzia Dr. Slaa na hili linahusu kifo kilichomhusu Ndugu Boya Gusulu huko Karatu, jambo hili limefanyiwa utafiti na kesi imefunguliwa na mtuhumiwa anamashtaka kuhusu suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omari Kwaangw' alizungumzia juu ya mauaji ambayo yalitokea Babati na akazungumzia kwamba askari polisi alihusika katika mauaji haya, hili ni jambo ambalo tumelifuatilia na imegundulika kwamba kuna tuhuma inamhusu askari mmoja na huyo askari amekimbia na tupo katika msako wa kumtafuta na kumpata. Ninachosema ni kwamba hakuna kitu ambacho tunaficha, msako unaendelea na kesi ipo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Omari Kwaangw' kwamba asiwe na wasiwasi na wapiga kura wake awaeze kuwahakikishia kwamba hayo yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema masuala ya sera na yale makubwa namwachia Waziri atakuja kuyajibu, lakini kubwa naomba nitoe shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu naona hadhara hii ndiyo ya mara ya mwisho tunakwenda katika uchaguzi, naomba Mungu atujalie turudi, lakini katika kipindi

ambacho nimejaliwa kuwa Naibu Waziri wote kwa ujumla tumefanya kazi nzuri sana, naomba nitoe shukrani zangu nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo kubwa nataka niliseme kama yupo Mbunge hata mmoja ambaye anaona kwamba Kagasheki kwa njia moja au nyingine alimkwaza basi sitosita kusema kwamba nawaombeni msamaha na ninawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, sasa namwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri, kinachoshangaza Mawaziri hawa wote wamenyoa nywele zote, sasa wanasema akili ni nywele kila moja ana zake wenyewe hawana! *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena nachukua fursa hii kukushukuru sana wewe binafsi, kwa kuongoza mjadala huu kuhusu hoja zilizopo mbele yetu. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wetu wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao katika masuala mbalimbali kuhusu Wizara yangu. Napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja ya Wizara yangu kuanzia hotuba ya Waziri wa Fedha, Waziri Mkuu na Waziri wa Katiba na Sheria hapo jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais Dr. Ali Mohamed Shein na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Dr. Aman Abeid Karume kwa imani kubwa waliyoonesha kwangu kwa kunipatia jukumu la kutumikia wananchi katika Serikali ya Awamu ya Nne katika nafasi na Wizara mbalimbali. Namshukuru pia Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda kwa miongozo yake mbalimbali anayonipatia katika utendaji wangu wa kazi wa kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, naomba nitumie fursa hii kumshukuru tena mke wangu Stella, watoto wangu Chela, Amani na Junior, kwa upendo na uvumilivu wao kwangu ulioniwezesha kutimiza majukumu yangu Kitaifa.

Kwa dhati kabisa nawashukuru wananchi wa Jimbo la Nyamagana kwa kuniamini na kunichagua kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni katika kipindi cha miaka mitano inayoishia mwaka huu. Nawashukuru pia wanachama wa CCM wa Jimbo la Nyamagana kwa kuendelea kuniamini, nawashukuru sana kwa ushirikiano wao na ni imani yangu kwamba hawatafanya makosa, wataendelea kuniunga mkono na kunirejesha Bungeni kwa kipindi kingine cha miaka mitano. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Madiwani wa Jimbo la Nyamagana, uongozi wa Chama ngazi ya Mkoa na Wilaya zinazoongozwa na Ndugu Clement Mabina

na Ndugu Zebedayo Athumani kwa ushirikiano wanaonipatia katika kuwaletea wananchi wa Nyamagana maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru sana Naibu Waziri wangu na Kaka yangu Mheshimiwa Balozi Hamis Suedi Kagasheki kwa msaada mkubwa sana anaonipatia katika kuongoza Wizara hii, tumefanya kazi kwa amani, upendo mkubwa, uelewano, ushirikiano na kwa kuheshimiana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 61, miongoni mwao 47 wamechangia kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge 14 wamechangia kwa kuzungumza. Naomba nikiri kutokana na ufinyu wa muda sitaweza kujibu hoja zote kwa maana ya kujibu hoja kwa hoja, badala yake nitatoa maelezo ya jumla katika maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia. Hata hivyo nikipata fusa nitaanza kujibu hoja moja moja baada ya nyingine. Lakini ilivyo ada tutahakikisha kwamba kitabu maalumu kitawasilishwa hapa ambacho kitajibu hoja zote ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kuwatambua wachangiaji kwa kuanzia na waliochangia kwa maandishi kama ifuatavyo, Mheshimiwa Mkiwa Kimwaga, Mheshimiwa Mwandini Abbas Jecha, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Maulidah Anna Komu, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Janet Mbene, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa *Eng.* Mohammed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Mohammed Sinani, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa *Eng.* Stella Manyanya, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Magalle Shibuda, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Joyce Masunga na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Ibrahim Muhammad Sanya, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Mercy

Emmanuel, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Mohamed Sinani na Mheshimiwa Balozi Khamis Suedi Kagasheki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kujibu hoja moja moja kama nilivyoeleza, kuna hoja angalau mbili, tatu ambazo ni za kiujumla ambazo ningependa kuziongelea. Hoja ya kwanza ambayo imeongelewa na Wabunge wengi ni tatizo ambalo limeanza kujitokeza hapa nchini la wananchi kuchukua sheria mkononi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2007 na 2010, jumla ya vituo vya polisi nane vimevamiwa na wananchi na kuharibiwa, vituo hivyo ni Mbarika, Katoro, Chato, Kongowe, Ilongalo, Kintinku, Matamanga na Hedaru. Matukio haya yanatupatia taabu sana ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika michango ambayo imeletwa hapa na Waheshimiwa Wabunge, Wabunge walio wengi wanaiomba Serikali kutoa fedha za wananchi wa Tanzania kuwajengea vituo vya polisi na kuhakikisha kwamba ulinzi upo karibu, lakini wakati huo huo wananchi wamekuwa wakichukua sheria mkononi, wamekuwa wakivamia vituo vya polisi na wamekuwa wakichukua sheria mikononi pia katika namna nyingine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninavyofahamu haki yoyote inaendana na wajibu, sisi ambao tunatoka Kanda ya Ziwa ambao tuna uzoefu wa kutumia mitumbwi, tunajua kwamba ukiwa unapiga kasia, kasia inatakiwa kupigwa upande mmoja halafu unaenda upande mwingine. Unaenda upande wa haki na wajibu, ukienda upande wa haki tu peke yake bila kuangalia wajibu, huo mtumbwi hautaenda popote, utazunguka pale pale na ndivyo ilivyo katika masuala haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani kwamba wananchi watahitaji kuwa na ulinzi karibu, lakini katika wakati huo huo wanachukua hatua za sheria mkononi na kwenda kuvamia vituo vya polisi. Katika orodha ya vituo ambavyo nimevitaja kulikuwemo na Kituo cha Chato ambacho kama nilivyoeleza katika Bajeti yetu ya mwaka huu, mwaka jana ilibidi tutoe pesa ili kujenga kituo hicho kipya. Lakini mbaya zaidi tukichukulia mfano wa kitendo ambacho kimetokea Hedaru, wananchi wenye hisia kali wameenda kuvamia kituo kwa taarifa walizokuwa wamepata kwamba ndani ya kituo kulikuwa kuna wahalifu ambao walikuwa wamemtoa kafara binti mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tushukuru Mungu kwamba kutokana na jitihada za askari polisi ambao walikuwa humo ndani waliweza kuondoka wao na kuwaondoa wale watuhumiwa, wananchi wangefanikiwa katika dhamira yao, hao watuhumiwa saa hizi wasingekuwepo, hawa askari pia wangekuwa wamekufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini haikupita siku moja yule mtoto aliyekuwa anatafutwa akakutwa yupo hai akiwa na baba yake mzazi, nawaomba wananchi wa Tanzania waliruhusu Jeshi la Polisi lifanye kazi yake. Sisemi kwamba hakuna polisi ambao wanakiuka utaratibu hao wapo ni wachache, lakini walio wengi kama mnavyosema ninyi wenyewe ndani ya Bunge hili wanafanya kazi ngumu katika hali

ngumu, wanastahili pongezi kwa kazi wanayoifanya. Kuchukua sheria mkononi siyo njia muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuwakumbusha Watanzania, ninaposema haki inakuja na wajibu, hawa askari polisi vituo vyao vikiwa vinavamiwa naomba Watanzania wakumbuke kwamba sheria ya Tanzania, tukienda kwenye *Penal Code*, Kifungu cha 18 kinamruhusu kutumia kama sijakosea, kinamruhusu mtu kutumia nguvu kulinda mali yake hata kama hiyo mali ni mali ya Serikali. Hawa ni askari, wananchi wanaenda kuvamia vituo, wanahatarisha maisha ya askari wenye silaha, hawa askari wakirudishia itakuwaje? Ndiyo hapo Wizara yangu tena itaombwa kuunda Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana Waheshimwia Wabunge wakirudi majimboni kwao watusaidie kuwaelimisha wananchi kwamba haki inaenda na wajibu na kwamba siyo polisi wote ambao wanatenda makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuongelea maslahi ya askari. Kwanza naomba kuwashukuru Wabunge wote waliochangia katika hoja za maandishi pamoja na kwa kuzungumza kwa uchungu ambao wameonesha kuhusu hali ya askari hapa nchini. Ni kweli kabisa kwamba hali zao ni duni na tumekuwa tukijitahidi kuboresha hali za askari hawa mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Issa Kassim Issa umetuomba kwamba badala ya kutafuta kutoka kwenye sungura mdogo tujitahidi kutafuta angalau mbuzi mdogo. Lakini napenda kusema tu katika Awamu ya Nne ya uongozi wa Chama cha Mapinduzi, haka kasungura kadogo kamenenepa. Nianze kwa kusema kwamba natambua kabisa kama nilivyosema kwamba hata hapo walipo askari hata sisi viongozi wao tungependa kuwaongezea zaidi. Lakini lazima twende awamu kwa awamu kutokana na fedha ambazo tunatengewa. Tumefanikiwa na naomba tukumbuke yale ambayo tumefanikiwa kufanya kwa sababu isije ikaonekana kwamba hakuna ambacho kimefanyika katika kuboresha maslahi ya askari. *Ration allowance* ya askari polisi imepanda kutoka shilingi 60,000 mpaka 100,000. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri Bima ya Afya sasa hivi imepatikana kwa ajili ya askari wetu. Hii Bima ya Afya si kwa ajili ya askari tu lakini pamoja na mwenza na watoto wanne na hii inaanza tarehe Mosi Julai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za askari zimeanza kujengwa. Mheshimiwa Idd Azzan, umenieleza kuhusu nyumba za askari hapo Kinondoni na umesema kwamba sitaki kutembelea, siyo kweli, siyo kwamba sitaki kutembelea, ukweli ni kwamba nimetembelea nyumba nyingi sana za askari na kila nikipita nashikwa na huzuni. Nimeona ni vyema badala ya kutembelea tu nyumba ambazo nafahamu hali yake heri nitafute mipango ya kuweza kujenga nyumba zingine nyingi zaidi ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwishaanza na mipango ya kujenga nyumba kama ilivyoelezwa katika hotuba yangu ya Bajeti, nisingependa kuanza kuyarudia tena. Lakini

pia sasa hivi Wizara yangu imesaini *Memorandum of Understanding (MOU)* na kampuni moja ya Kichina ambayo inaitwa *Complaint* kwa matumaini kwamba tutafute na nasisitiza kusema kwamba tunatafuta mkopo wa bei nafuu kutoka kwa Serikali ya China, hatujafanikiwa bado. Lakini lengo letu ni kwamba tukifanikiwa na Kampuni hii ya *Complaint* kupata huo mkopo wa bei nafuu kutoka China tutakuwa tuna uwezo wa kujenga nyumba za askari 24,000 ambazo kwa kweli zitatusaidia kumaliza tatizo la nyumba za askari nchi nzima wakiwemo ndugu zetu wa Kinondoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tungependa kufanya zaidi lakini tunafanyakazi kutokana na Bajeti tuliyonayo. Juzi tu kwenye Baraza la Mawaziri tumepandisha umri wa kustaafu kwa ajili ya askari polisi wa vyeo vidogo na nia ni kwamba katika ile *Miscellanies Amendment Act* ambayo italetwa kwenye Bunge hili Waheshimiwa Wabunge mkiridhia tutaipitisha, lengo ni kwamba Makoplo na Makonstebo ambao kwa sasa wanastaafu wakiwa na umri wa miaka 45 wataweza kustaafu wakiwa na miaka 50. Ma-*Sergeant* ambao wanastaafu wakiwa na miaka 50 waweze kustaafu wakiwa na miaka 55. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maduka ya *duty free* tayari imeshakubalika kwamba askari wa jeshi la polisi ambao walikuwa hawana maduka ya *duty free* huko awali nao watapata fursa ya kupata maduka ya *duty free*. Kinachofanyika hivi sasa ni kwamba tuko katika maongezi na wenzetu wa Mamlaka ya Mapato ili kuainisha ni bidhaa gani ambazo zitaweza kuuzwa katika maduka hayo. Naamini kabisa katika mwaka huo wa fedha hayo maduka yatafunguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niendelee kuongelea kidogo. Mheshimiwa Naibu Waziri ameelezea huo mfuko wa hiyari wa kuzikana, ningependa kuongezea kitu kimoja. Serikali ya Awamu ya Nne ni sikivu inaelewa matatizo askari wake wanapata. Ningependa kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba Kanuni za Kudumu za mwaka 1964 *(Standing Orders)* zimebadilishwa na ifikapo tarehe Mosi Julai watumishi wote wa Serikali wakiwemo askari watakuwa na stahili zao za mazishi ambazo ni tofauti na ilivyokuwa ambazo zitawahusisha familia pia. Huko awali zilikuwa haziwahusishi familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la maslahi ya askari Mheshimiwa Haji Juma Sereweji uliulizia suala la Makamishina wa Polisi kupatiwa magari kama ilivyo kwa Majenerali katika Jeshi la Wananchi, hiyo siyo sera yetu sasa hivi. Sisi tunachokifanya ndani ya Jeshi la Polisi ni kwamba Kamishina akiwa anastaafu yeye anapewa gari aliyokuwa anaitumia kwa kipindi cha miezi sita halafu gari inarejeshwa. Lakini tunayo mapendekezo ambayo yanafanywa kazi kuweza kuangalia suala hili. *(Makofi)*

Baada ya kueleza hayo masuala kwa ujumla, ningependa kujibu kutokana na muda nilionao hoja chache moja moja ambazo zimetolewa. Mheshimiwa Magalle Shibuda kaka yangu umetoa hoja nyingi sana. Tulikuwa tunakaa pale tunaangalia tulikuwa tunaona kama ni *phases* ya *Ph.D*, lakini karibu hoja zote ambazo umezitoa zinahusu matatizo ambayo yametokea kwenye Jimbo lako kule Maswa. Lakini kama tulivyokueleza ofisini kwetu siku tatu zilizopita kwamba kuna timu kutoka Makao

Makuu ya Jeshi la Polisi ambayo itakwenda jimboni kwake kwenda kuchunguza yale yote ambayo umetufikishikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Charles Mwera na Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, mliulizia tatizo la ile *issue* ya kudhalilisha akina mama kule Mkoa Mara. Niseme tu kwamba tayari tulikuwa tumeshaunda Tume mbili. Tume ya kwanza iliundwa ikafanyakazi yake ili kuhakiki kila ambacho kilikuwa kimefanyika, tulipeleka watu wengine kule ambao walikuwa nje ya Jeshi la Polisi. Wakiwemo wenzetu wa Usalama wa Taifa na kadhalika. Lakini niliamua baada ya kupata ombi maalum kutoka kwako Mheshimiwa Mwera kwamba kitengo chetu cha malalamiko ndani ya Wizara kitakutana nawe ili mkae wewe utoe ushahidi ulionao na wao wapate fursa ya kuongea na wale mashahidi ambao utawataja ili tutafute ukweli wa suala hili. Naomba uwe na imani na sisi. Pia tunajua kwamba hawa ni mama zetu na tusingependa wadhalilike, kama kuna askari ambao walihusika katika vitendo kama hivi naomba nikuthibitishie kwamba hatua zitachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu Mheshimiwa Anna Abdallah aliulizia kuhusu uraia wa nchi mbili yaani *dual nationality*. Ningependa kusema kwamba kimsingi suala hili limejadiliwa kikamilifu na Serikali zote mbili yaani Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Uamuzi umefikia kwamba suala hili kwa sasa hivi si muafaka. Lakini mchakato ambao unaendelea ni kuangalia uwezekano kama nilivyowahi kueleza ndani ya Bunge hili kuanzisha *permanent resident* (ukazi wa kudumu) hapa nchini kwa sasa hivi rasimu ya Waraka la Baraza la Mawaziri umeshaandaliwa na mchakato unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Issa Kassim Issa ametuomba kwa kutambua kwamba Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Uhamiaji amestaafu kwamba tufanye mchakato haraka na kumshauri Mheshimiwa Rais amteue Kamishina mpya. Mheshimiwa Issa Kassim Issa tumekusikia na hiyo kazi tayari imekwishafanyika. Tuko katika mchakato wa uteuzi. halafu Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir ameulizia Kituo cha Polisi Nchinga ambacho kimejengwa na wananchi lakini hakijaanza kutumika kutokana na ukosefu wa nyumba kwa ajili ya askari na ameomba kwamba wapatiwe vifaa. Mimi ninachomuahidi Mheshimiwa Mudhihir ni kwamba Jeshi la Polisi litafanya tathimini ya gharama na tutajikusanya kutokana na fedha tulizonazo ili hivyo vifaa vipatikane ili ujenzi ufanyike. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Mariam Kasembe alikuwa na hoja ya kwamba nyumba za kuishi askari pale *Kilwa Road* bado ziko tupu, ningependa kumfahamisha kwamba zote katika maghorofa 54 yaani jumla ya familia 216 zimehamiwa na askari na tayari wanaishi.

Halafu Mheshimiwa Bujiku Sakila ameulizia makazi ya ofisi Wilayani Kwimba kwamba haina Kituo Ofisi kutoka Ukoloni na kwamba kituo cha polisi Ngudu ni kibovu hakina hata choo. Niseme tu kwamba tayari mkandarasi ameshapatikana. Huyo mkandarasi ni *Kashele Enterprises* na tunaamini hizo kazi zitakuja kufanyika. Pia ameulizia kuhusu gari bovu alilonalo pale, ningeomba kumfahamisha pamoja na Wabunge wengine kuwa mwaka jana nilivyokuwa nasoma hotuba yangu ya Bajeti

nilieleza kwamba Wilaya zote zitapata magari, kama ulivyoona kwenye jedwali ambalo liko kwenye hotuba yangu ya Bajeti kila Wilaya ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepatiwa gari na haya magari yatapatikana Agosti mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mama Mongella, kwanza naomba nikuthibitishie kwamba Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Ukara, itajengwa. Umeuliza kuhusu maendeleo ya kesi ya Izinga Ukerewe, Mwanza tuseme tu kwamba mpaka sasa hivi watuhumiwa saba wamekamatwa na wamefikishwa Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda niliokuwa nimepewa hayo ndio ambayo nimeweza kuyachangia. Baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa na Kuafikiwa)*

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

Kifungu 3001 – *Fire and Rescue Services* … … … … Sh. 2,881,654,730
Kifungu 3002 – *Fire and Rescue Services Training Inst*...Sh. 636,235,270

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

### Fungu 28 – Jeshi la Polisi

Kifungu 2001 – *Police Mainforce* … … … … … … …Sh. 80,175,852,700

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba maelezo kidogo kuhusu kifungu kidogo 210100 *Basic Salaries – non pensionable*.

**MWENYEKITI:** Rudia tena hatukusikia.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Kifungu 210100 *Basic Salaries*. Ukiangalia katika mishahara yao katika mwaka huu ukilinganisha na mwaka jana zimepungua kwa kiasi cha shilingi bilioni 15. Nilikuwa naomba kupata maelezo ni kwa sababu na huku tukijua kwamba mishahara ya wafanyakazi wengi imepanda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umekipata vizuri hicho kifungu? Maana yake hapa mnajibu *specific* kwa hatujafika Fungu la Wizara.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimemuelewa vizuri hapa tunazungumzia juu ya *military payroll* ni kifungu ambacho kiko *very specific* katika *police*.

**MWENYEKITI:** Una-*clarify* tu lakini hurusiwi kusema mara mbili.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani labda hatujaelewana nilichohoji ni kifungu cha kwanza 210100.

**MWENYEKITI:** Imefanya nini?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Nimeuliza ni kwa nini mishahara uki-*compare* na mwaka jana kuna upungufu wa shilingi bilioni 15 ndio nilitaka kupata ufafanuzi yaani wa mwaka jana ulikuwa shilingi bilioni 20 sasa hivi ukiangalia utakuta ni shilingi bilioni tano tu.

**MWENYEKITI:** *Okay,* umeeleweka ni *Basic Salary Penshionable* Fungu 20 kwa nini mwaka jana kulikuwa na fedha nyingi za mshahara kuliko mwaka huu mmepunguza au mmefanyaje?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ni kweli kabisa kwamba zimepungua lakini siyo imepungua katika kifungu kwa sababu zimesambazwa katika vifungu vingine huku. Kwa mfano ukienda kwenye *sub vote 2013*, Polisi Ilala kulikuwa hakuna kitu mwaka jana lakini sasa hivi kuna shilingi bilioni 1.3 sasa hizi zimeelekea kwenye *sub-vote* ambazo zimekwenda Mikoa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Police Marine* … … … … … … … … … Sh. 1,281,518,000
Kifungu 2003 – *Railway Police Division* … … … … … …. Sh. 474,121,000
Kifungu 2004 – *Police Signals Branch*. … … … … … … Sh. 3,656,281,000
Kifungu 2005 – *Police Zanzibar* … … … … … … … …. Sh. 8,071,226,000
Kifungu 2006 – *Police Airwing* … … … … … … … … …. Sh. 1,473,085,000
Kifungu 2007 – *Tazara Police* … … … … … … … … … … Sh. 755,084,000
Kifungu 2008 – *Field Force Unit* … … … … … … … …. Sh. 37,035,220,000
Kifungu 2009 – *Traffic Police* … … … … … … … … … Sh. 1,948,449,000
Kifungu 2010 – *Police Airport* … … … … … … … … … …. Sh. 662,447,000
Kifungu 2011 – *Police Dog and Horses* … … … … …. Sh. 1,090,834,000
Kifungu 2012- *DSM Special Zone*… … … ..................Sh. 3,125,649,000
Kifungu 2013- *Police Ilala* … … … ...............................Sh. 3,789,350,000
Kifungu 2014- *Police Kinondoni* … … … ...................Sh. 3,772,719,000
Kifungu 2015- *Police Temeke* ... ... ... ... ......................Sh. 2,208,430,000
Kifungu 2016- *Police Arusha*... ... ... ... ......................... Sh.3,269,859,000

Kifungu 2017- *Police Iringa*... ... ... ... ..........................Sh.2, 514,225,000
Kifungu 2018- *Police Kilimanjaro*... ... ... ... ................Sh. 3, 379,415,000
Kifungu 2019- *Police Kigoma*... ... ... ... ... ..................Sh. 2,374,730,000
Kifungu 2020- *Police Kagera* ... ... ... ... ... ..................Sh. 2,777,984,000
Kifungu 2021- *Police Lindi*... ... ... ... ... ..........................Sh.1,810,240,000
Kifungu 2022- *Police Mwanza*... ... ... ... ... ..................Sh. 3,679,064,000
Kifungu 2023- *Police Mara*... ... ... ... ... .......................Sh. 2,286,709,000
Kifungu 2024- *Police Tarime –Rorya*... ... ... ... ... ...........Sh. 1,166,400,000
Kifungu 2025- *Police Mbeya*... ... ... ... ... .......................Sh. 2,899,196,000
Kifungu 2026- *Police Mtwara*... ... ... ... ... .................Sh. 2,025,331,000
Kifungu 2027- *Police Morogoro*... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 3,440,973,000
Kifungu 2028- *Police Manyara*... ... ... ... ... .. ... ... ... ...Sh.1,998,789,000
Kifungu 2029- *Police Singida*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 2,193,183,000
Kifungu 2030- *Police Pwani*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 2,652,336,000
Kifungu 2031- *Police Ruvuma*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 2,044,776,000
Kifungu 2032 - *Police Rukwa*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 2,039,128,000
Kifungu 2033 - *Police Shinyanga*... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 2,771,168,000
Kifungu 2034 - *Police Tabora*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ..Sh.2,199,754,000
Kifungu 2035- *Police Tanga*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 2,795,045,000
Kifungu 2036- *Police Mjini Magharibi* ... ... ... ... ... ... Sh. 1,991,424,000
Kifungu 2037- *Police Kusini Unguja*... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 1,617,467,000
Kifungu 2038- *Police Kaskazini Unguja* ... ... ... ... ... ... Sh. 1,272,321,000
Kifungu 2039- *Police Kusini Pemba*... ... ... ... ... ... ... ... Sh.1,391,653,000
Kifungu 2040- *Police Kaskazini Pemba* … … … … ... Sh. 1,515,885,300
Kifungu 2041- *Police Dodoma*… … … … ... ... ... ... ...Sh. 3,243,775,000
Kifungu 3001- *Police College Moshi*… … … … ... ... ..Sh. 4,019,805,000
Kifungu3002– *Police College*… … … … ... ... ... ... ... .Sh. 1,738,660,000
Kifungu4001 – *Police Vehicles Maintenance Unit* … Sh. 3,020,521,000
Kifungu 5001 – *Police Medical Unit* … … … ... … … Sh. 1,990,122,000
Kifungu 6001 – *Police Building Brigade* … … … … … Sh. 4,753,308,000
Kifungu 7001 – *Criminal Investigation Division* … … Sh. 21,185,874,000
Kifungu 7002 – *Stock Theft Prevention Unit* … … … … Sh. 771,559,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 29- Jeshi la Magereza**

Kifungu 1001 - *Prison Headquarters* … … … … ... ... Sh. 6,333,371,000

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye kifungu kidogo 210100, *Basic Salaries*. Nilikuwa naomba maelezo kutoka kwa Waziri pamoja na kwamba yale ya mwanzo sikuyaelewa vizuri kwamba kifungu hiki mishahara imepungua kwa shilingi milioni 200 na nikiangalia katika *department* zote hakuna sehemu ambayo mishahara ya mwaka jana haikuwepo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba anipe maelezo ni kwa nini mwaka huu mishahara ya hawa watu wa *prisons* imepungua kwa kiasi hicho?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ambayo ameuliza Mheshimiwa Susan Lyimo kwa hapa ni tofauti na ilivyokuwa katika ile *vote* nyingine ya Jeshi la Polisi. Ile ilikuwa wazi kama nilivyoeleza kwamba pesa zimehamia mikoani, hapa kilichotokea ni *re-adjustment* katika *organization* ya Jeshi lenyewe na ndio maana suala hili limetokea. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Parole Department*… … … ... ... ... … Sh. 418, 263,300
Kifungu 2002 - *Prisons Welfare and Rehabilitation*…Sh. 81,239,911,200
Kifungu 2003 – *Resettlement of Offenders* … … … Sh. 1,008,528,800
Kifungu 3001 – *Prison Staff College*… … … ... ... ... ... Sh. 1,248,221,600
Kifungu 3002 – *Prison Driving School* … … … ... ... ... ...Sh. 229,735,700
Kifungu 3003 – *Prison Trade School* … … … ... ... ... ... Sh. 501,362,700
Kifungu3004 – *Prison College Kiwira*… … … ... ... ... ... Sh. 903,785,100
Kifungu 4001 – *Prison Building Brigade* … … … ... ... Sh. 1,172,237,100
Kifungu 4002 – *Prison Industries*… … … ... ... ... ... ... ... Sh. 433,810,700
Kifungu 4003 – *Prison Farms*… … … ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 736,711,800

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 51- Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kifungu 1001 – *Administration and General* … … … Sh. 1,512,439,500

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika mchango wangu pamoja na mambo mbalimbali niliyoelezea ya nyumba za askari, lakini nilizungumzia pia suala la Kinondoni kupandishwa hadhi kuwa Mkoa wa Kipolisi. Majengo na vitu vinavyotumika ni vile vile nilikuwa nataka kufahamu ni lini sasa vituo vya Magomeni na Polisi Mabatini Kijitonyama vitafanyiwa ukarabati na upanuzi ili kukidhi haja lakini pia kuwekewa vifaa kwa ajili kufanyia kazi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa toka Kinondoni imekuwa Mkoa wa Kipolisi majengo bado ni yale yale, lakini hiyo inatokana na ufinyu wa Bajeti tuliyonayo na kwa kweli tungependa kuweza kupanua ofisi na kadhalika. Lakini kimsingi ambacho kimefanyika ni kwamba kwa maana ya *operationalisation* yaani jinsi askari wanavyofanya kazi na kwamba tumewapa Kamanda wa Mkoa na kadhalika; moja kuongeza askari lakini pia kuhakikisha kwamba shughuli zao zinafanywa kwa uharaka zaidi katika *command* ya jeshi la polisi ndio sababu tumefanya hivyo. Pale ambapo tutaweza kupata fedha kushughulikia suala ambalo amelieleza Mheshimiwa Mbunge tutafanya lakini hali ya Kibajeti ndio hiyo. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Vote 51, program 10 sub- vote 1001,* sina haja na mshahara ya Waziri, nilikuwa nataka maelezo tu, kwenye mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua uhai na mwelekeo wa Bodi hii ya *Parole*. Bodi hii ilianzishwa kupunguza msongamano wa wafungwa ndani ya Magereza, lakini naona kama vile haipo. Nilitaka kuelewa tu, hii Bodi ipo na inafanya kazi zake?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumthibitishia Mheshimiwa Zungu kwamba hii Bodi inafanya kazi na ipo na sio tu kwamba ipo kwa ngazi ya Taifa, ipo mpaka kwenye ngazi ya mikoa. Hivi sasa tunavyoongea ninazo *files* karibia 230 ofisini kwangu hapa ambazo zimepitishwa kutoka mikoani mpaka ngazi ya Taifa ambazo zinasubiri sahihi yangu ili kuwaachia wafungwa kwa namna ya *parole*. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nazungumzia makazi ya askari. Sina shida na mshahara wa Waziri. Makazi ya askari pale Shinyanga Mjini, askari Magereza na Polisi ni duni sana, wengi wanaishi kwenye nyumba zilizojengwa wakati wa ukoloni na mimi kabla sijazaliwa. Nilipendekeza Serikali kupitia Wizara hii iweke mipango ya muda mrefu ya kuhakikisha kuwa tatizo la makazi ya askari linatatuliwa. Nampongeza Waziri alivyozungumza kuhusu ule ujenzi wa nyumba zitakazotosheleza askari 24,000 lakini huu ni mpango mdogo tu na ni mmoja, naomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwa nini Serikali isione haja ya kuwa na mpango wa muda mrefu wa kutumia fursa kama vile Shirika la Nyumba kujenga nyumba zitakazopangisha askari, mifuko ya jamii itakayojenga nyumba kwa ajili ya askari au Serikali kuwa na Bajeti kila mwaka ya kushughulikia ujenzi wa nyumba za askari ili kusudi tuondokane na tatizo hili kuliko mipango ilivyo sasa hivi ambavyo ni vipande vipande. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kubishana na kaka yangu Mheshimiwa Dr. Mlingwa kuhusu mipango ya ujenzi wa nyumba za Serikali, mipango ya muda mrefu ipo pamoja na mipango ya muda mfupi na kwa mfano kama sasa hivi hizo nyumba ambazo zinajengwa pale *Kilwa Road*, zile ambazo zimejengwa Zanzibar, zimejengwa kutokana na msaada na ufadhili na pesa ambazo zimetokana na *NSSF* ambazo zimefadhiliwa na Hazina na kama nilivyoeleza lengo kama tukifanyikiwa na huu mradi wa *Complant* ni kujenga nyumba 24,000. Kwa kweli nyumba 24,000 sio nyumba chache kwa kweli zinaweza zikastahili, zinaweza zikasaidia kumaliza tatizo la nyumba za askari nchi nzima. Lakini zaidi ya hapo, mimi mwenyewe nimeshafika pale Shinyanga, Jimboni kwa Mheshimiwa na nimeona kwamba askari wako pale na kwa kweli wamejitolea kujenga nyumba za hadhi nzuri, matofali ya kuchoma na mabati kutokana na nguvu zao wenyewe, mikakati yetu ya sasa hivi ni pale ambapo tutakuwa na uwezo wa kutumia nguvu zetu sisi wenyewe ndani ya Wizara, kutumia vikosi vyetu vya ujenzi tutajenga, pale ambapo tutaweza kupata pesa kutoka *NSSF* tutazitumia na tukifanikiwa kupata huu mradi wa *Complaint* tutaweza kumaliza tatizo la nyumba kwa askari nchi nzima.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi pia wakati nachangia hasa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu nilikuwa nimezungumzia juu ya tatizo kubwa la usafiri, kwamba katika Mkoa wa Singida gari ni moja tu ambalo linategemewa kwenye Mkoa mzima na nikawa nimeomba kwamba waweze kupatiwa gari lakini nikawa nimeshauri kwamba mpango na utaratibu ambao Waziri Mkuu amepiga marufuku ununuzi wa magari kwenye Wizara nyingine na sekta mbalimbali kwamba basi nguvu zile na pesa zinazokuwa-*saved* zielekezwe katika Jeshi la Polisi ili waweze kupatiwa usafiri. Nilikuwa naomba tu maelezo hasa katika Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kiambatanisho D kimeeleza kila kitu. Mheshimiwa Waziri ukipenda kuongeza. Kiambatanisho D kwenye hotuba yake ameeleza kila Wilaya.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kama ulivyosema ukiangalia kiambatanisho D ukurasa wa 67 kwa Singida kama Mkoa wamepewa magari mawili kwa ajili ya *FFU* ukienda ukurasa wa 70 pale Singida, Wilaya ya Singida imepewa gari moja, Iramba imepewa gari moja na Manyoni wamepewa gari moja. Ukienda ukurasa wa 72 *RPC* wa Singida nae amepewa gari moja na pale ambapo magari waliyokuwa nayo kwa mfano *RPC* magari hayo yataendelea kutumia katika Mkoa huo huo. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Katiba ya nchi hii inatambua uwepo wa aina mbili tu za majeshi yaani Jeshi la Wananchi na Jeshi la Polisi na kwa kuwa mara nyingi katika chaguzi mbalimbali tumeshuhudia watu wakipigwa hasa upande wa upinzani na hivi majuzi kule Kilimanjaro eneo la *KCMC* inasemekana kwamba vijana wa Chama cha Mapinduzi ambao walikuwa wametoka kwenye Kambi walifika na kuwapiga wananchi. Sasa nilikuwa naomba maelezo kutoka kwa Waziri ni hatua gani ambayo wamechukua na je, ni halali kwa vyama vya siasa kuwa na majeshi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kumsahihisha Mheshimiwa Susan Lyimo kwamba ukiangalia Katiba yetu ni majeshi ni Jeshi la Wananchi, Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza. Jeshi la Magereza ulikuwa umelisahau. Niseme kwamba hakuna chama ambacho kimeruhusiwa kuwa na majeshi. Napenda kutambua kwamba pale ulipokuwa unaongea umesema kwamba inasemekana kwamba hayo yametokea, lakini kwa taarifa niliyonayo mimi sivyo hivyo unavyosema wewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna watu wamepigana. Kilichotokea kwa taarifa niliyo nayo ni kwamba kuna vijana wa Chama cha Mapinduzi ambao walikuwa wanatoka kwenye Kambi yao katika mechi wanarudi mjini, wakakutana na vijana wa CHADEMA ambao walikuwa katika eneo hapo karibu. Vijana wa CHADEMA walianza kuwazomea wakaanza kuwaambia vitu kama hivi na wakaanza kusema mambo mengi sana. *(Makofi)*

Sasa mimi ninavyofahamu kama nilivyoeleza Mheshimiwa Mwenyekiti, haki na wajibu, hawa ni vijana, kama wangekuwa hawataki kupigwa wasingezomea. Sasa kitu nitakachosema tu ni kwamba kuna vijana wa CCM walioumia na kuna vijana wa CHADEMA walioumia, wote walitoroka baada ya hapo na tuliona kwamba lilikuwa ni jambo la nani, tukaamua kwamba tuliachilie hilo jambo. Lakini kama unafahamu wale vijana waliopigwa kwa pande zote wa CHADEMA watusaidie na sisi tutatafuta wa CCM tuwachukulie hatua za kisheria. *(Makofi)*

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilizungumzia suala la umeme unaotumika pale Maswa kwa askari polisi kwa kutumia *style* ya LUKU ya pamoja kama mabweni ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anajibu sikusikia eneo hilo mahali popote pale na kwa sababu askari walioko Maswa wanahitaji kujua ni nini hatma ya tatizo hili ukizingatia tunaelekea katika kipindi cha uchaguzi. Waziri anasema nini na anawapa matumaini gani askari walioko pale Wilaya ya Maswa?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii tumeipokea leo na nitakachofanya nitamwomba *RPC* muhusika atupatie taarifa kamili kuhusu hili tatizo ili tuangalie ni nini ambalo tunatakiwa kufanya.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru Serikali kwa namna inavyofuatilia hili suala la akina mama wa Kebweye. Wakati nikichangia niliulizia kuhusu Bajeti ya mwaka jana iliyohusu Kituo cha Nyamwaga, Kegonga pamoja na Borega ambapo wanajeshi wa Jeshi la Polisi sasa hivi ni wengi pale, wanapata shida sehemu ya kuishi nilitaka nipate ufafanuzi kuhusu jambo hilo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba tulitamka kwamba tungejenga hivyo vituo na hizo pesa zilikuwa zitoke Hazina kutokana na kuandaa huo Mkoa mpya wa Tarime - Rorya wa kipolisi. Tumeahidiwa na Hazina kwamba hizo pesa zitapatikana na vituo hivyo vitajengwa. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa naulizia moja ya sababu ya askari polisi kupandishwa mshahara ni mpaka apate cheo na askari wengi wamekuwa wakifanya kazi kwa muda wa miaka mingi wako kwenye daraja moja na ukizingatia kwa sasa hivi hali ya maisha ni ngumu na hawawezi kujielimisha kwa kutumia mishahara yao. Mimi ningeiomba Serikali iongeze wigo wa vigezo ili askari hawa ambao hawajapandishwa cheo waweze kuongezwa mishahara yao badala kusubiri kupandishwa ndiyo waongezwe mshahara.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa jeshi liko katika mkakati wa maboresho, mpango mzima wa maboresho sasa

hivi umefikia hatua ambapo unafikishwa kwenye Baraza la Mawaziri wiki ijayo baada ya hapo maelekezo tutakayopewa na Serikali ndiyo hayo tutakayoyafuata.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kuna tatizo katika Ziwa Tanganyika, wavuvi wamekuwa wakivamiwa na kunyang'anywa mali zao. Suala hili lililetwa Bungeni mwaka 2007, Serikali ikaniahidi kwamba italifanyia kazi. Lakini tatizo kubwa ni kwamba wanatakiwa kuchangia mafuta kwa ajili ya boti ya polisi ili waweze kufanya doria. Sasa kwa sababu Serikali itafanyia kazi mpaka sasa hivi hilo suala bado linaendelea, wavuvi wanatakiwa kujinunulia mafuta kwa ajili ya boti zao na bado wanunulie mafuta boti la polisi, hawana *choice* bila hivyo hawapati ulinzi wa doria. Kwa hiyo, wameniomba niliulizie je, Serikali ina mpango gani kwa sababu wamechoka kununua mafuta kwa ajili ya boti la polisi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumjibu Mheshimiwa Mhonga kama ifuatavyo, kwanza hapo kuna matatizo mawili, kuna tatizo la uhalifu ndani ya ziwa lenyewe na kuongeza namna ya kuweza kuwa na doria. Pili kulikuwa kuna suala la mafuta, kwanza nimhakikishie kwamba siyo kwamba jeshi la polisi na Wizara tulikuwa hatuifanyii kazi na nimeeleza kwamba tunafungua *Maritime Police College* pale Mwanza kutokana na uhisani wa Serikali ya Marekani ambapo wamekubali kutupatia boti 12. Hizo boti 12 hazitakaa pale Ziwa Victoria, hizi boti zitasambazwa kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo kuelekea pale Kigoma ili kuweza kutusaidia kuhakikisha kwamba doria inafanyika na sisi ndani ya Jeshi la Polisi tutajitahidi kuangalia namna ya kuweza kuongeza pesa za mafuta ambazo zinapelekwa kwa ajili ya hizi boti ili kuweza kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nakuomba Mheshimiwa Mbunge kutokana na hali halisi ya sasa hivi pale wananchi wanapoombwa kuchangia pamoja na kwamba siyo lazima kwamba wachangie lakini tutawaomba kwamba kutokana na sera yetu ya Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi waendelee kutusaidia na tunawashukuru sana kwa kazi ambayo wameifanya mpaka hivi sasa.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na niko programu hiyo hiyo. Wakati nachangia niliongea kwa uchungu sana kuhusiana na hali mbaya ambavyo Vituo vyote vya Polisi Wilaya ya Urambo inayo pamoja na vituo vingine vyote ikiwepo kile cha Kaliua, Ulyamkulu pamoja na kile cha Usoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vyote hivi havina vitendea kazi kabisa. Nikianza na suala la usafiri hakuna kuanzia Wilayani pale. Nashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri nimeona kwenye kitabu chake Wilaya ya Urambo imepata gari moja, lakini Wilaya ya Urambo ina jiografia kubwa. Kwanza pia tuko mpakani, uhalifu unatokea kila leo, mauaji yanatokea ndani ya wiki hii tunapoongea mauaji sehemu tatu yametokea watu karibu saba wameshapoteza maisha. Askari hawawezi kutembea kwa ajili ya kwenda kuwahi matukio hayo. Kwa hiyo, wahalifu wako wanapeta. Kwa hiyo gari moja halitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri pia afikirie kuhusiana na hilo, pia kituo hiki hakina kompyuta hata moja. Tunatumia *typewriter* moja ya miaka 15 iliyopita na yenyewe pia ni mbovu. Kituo hiki hakina nyumba za watumishi, zipo chache sana na zenyewe ni zile za miaka 47 iliyopita. Nyumba zile zinatia huruma, ukifika juu kwenye mapaa zimewekwa matofali kwa sababu mapaa yanaezuliwa na upepo. Watumishi ni wachache sana katika Wilaya ya Urambo kwa ujumla. Naomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie kwa jicho la huruma Wilaya ya Urambo kwa sababu tunaenda kwenye uchaguzi, Wilaya nzima ina watumishi 93, kumi na mbili kati yao wako masomoni, 81 hawatoshi na hali ya Urambo ni hali ambayo tuko mpakani kwa hiyo hali ni tete. Tunaomba Serikali iangalie kwa jicho la huruma, ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya Bajeti, tunalo tatizo la idadi ya askari hapa nchini. Uwiano kama nilivyoeleza ni askari mmoja kwa wananchi 1,300 na tunafanya kila ambacho tunaweza ili kubadilisha hali hii. Lakini ambacho namuahidi Mheshimiwa Sakaya ni kwamba Wilaya yako itapata mgao wa askari wa ziada mara baada tu wakimaliza mafunzo pale *Police College* tutakuongezea askari. Kama ulivyoeleza mwenyewe unahitaji gari. Tunaelewa, hili ni tatizo la nchi nzima. Lakini kama tulivyoonyesha katika hotuba yetu ya Bajeti kwenye jedwali. Nafikiri hii ni mara ya kwanza tumeweza kutoa magari mengi kiasi hiki mpaka kila Wilaya imepata gari. Nakuomba kwamba uivumilie Serikali yako pale ambapo tutapata magari mengine hayo magari yatafika. Suala ujenzi wa nyumba za askari na hali ya vituo pale ndivyo ilivyo nchi nzima na ndiyo maana tunatafuta namna ya kuweza kuboresha kote hapa nchini. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu hiyo hiyo na mimi wakati nachangia niliandika kuhusu hali ya majengo ya kituo cha Polisi cha Sumbawanga pamoja na vituo vile vya mpakani kwa kweli hali yake hairidhishi hata kidogo. Majengo ni ya zamani sana toka wakati wa ukoloni tena yale yaliyojengwa kwa mawe. Ofisi zilizoongezwa ongezwa pale ukienda kwenye Ofisi ya *OCD* Ofisi ya Upelelezi na *traffic* pale kwa kweli inasikitisha ni majengo ambayo yanaonekana ni chakavu kabisa.

Mheshimiwa Waziri amezungumzia programu ya kujenga nyumba za wafanyakazi na ana mkataba na Wachina ambao wanataka kufanya hiyo kazi. Kwa kweli ni aibu sana hata yeye mwenyewe kama Waziri angekwenda katika Ofisi ya *OCD* hata Ofisi ya Mkoa nayo pia, unakuta ofisi nyingine haina vifaa kabisa, haina viti ina mabenchi ya zamani, hakuna viti vyenye hadhi. Polisi unakuta wakati mwingi wamesimama, wale wateja wanaokwenda pale nao pia wanasimama tu kwa sababu mazingira katika ofisi zile inasikitisha, majengo yanasikitisha au sijui ni kwa sababu ya upembezoni kwamba hakuna watu wanaokwenda kwenda huko Sumbawanga, Rukwa na nini.

**MWENYEKITI:** Sasa umaize bwana, maana yake unazunguka tu.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Ndiyo Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu unipe fursa niweze kuzungumza. Tuko mpakani na Zambia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge nilikuwa nadhani unamalizia, tena unasema nikupe fursa. Si wakati wa kuzungumza sasa, ni kutaka ufafanuzi.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZIMLA:** Haya naomba Mheshimiwa Waziri atuambie programu maalum kwa ajili ya kuboresha majengo ya vituo vya polisi na vifaa vinavyotumika katika Ofisi hizo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu hoja ya Mheshimiwa Mwananzila kama ifuatavyo. Kama ambavyo nilishaeleza kwamba tunatambua kabisa kwamba vituo na ofisi za polisi nchi nzima zinahitaji ukarabati. Katika programu yetu sasa hivi tunachoangalia ni kwamba kuna Wilaya zingine hata Ofisi hawana. Tutajitahidi kujenga katika Wilaya ambazo hazina halafu tutaanza kukarabati zile ambazo zipo. Tutaenda awamu kwa awamu kutokana na bajeti tuliyonayo. Umeniomba kwamba niangalie suala la Ofisi kama vile ninavyoangalia suala la nyumba za kuishi askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ningekuwa na bajeti ambayo inakidhi mahitaji yote ningeangalia yote kwa pamoja. Lakini katika kupanga na kuchgua niliona kwamba ni vema hawa askari wetu ambao wanafanya kazi ngumu tuhakikishe kwamba wao kwanza tuwaweke katika sehemu nzuri manyumbani kwao. Hapo kwa pesa ndogo tuliyonayo tutaendelea kukarabati ofisi na pale ambapo tutapata pesa ya kutosha tutakuwa na mkakati wa kutengeneza ofisi na nyumba zote kwa pamoja.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye programu hiyo hiyo. Sina tatizo na mshahara wa Waziri. Lakini katika mchango wangu nilizungumzia suala la Tume za mara kwa mara kwa matatizo yanayosababishwa na askari pale ambapo wameitwa kufanya kazi. Ningependa kupata maelezo kama Waziri suala hili analionaje, kwangu ni kero.

**MWENYEKITI:** Nadhani umelielewa swali. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa hoja ya Mheshimiwa Lembeli na labda tu niseme hivi inawezekana kwamba pale ambapo tutakuwa tumeleta sheria hapa mbele ya Bunge kuhusu Idara yetu ya Malalamiko ili kuweza kuirasimisha na kuwa na sheria ambayo inaweza ikaonyesha kabisa mipaka yake ni ipi. Naamini kabisa hiyo inaweza kutusaidia kabisa kuondoa huu utaratibu wa kuweka Tume mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lazima tu niseme kwamba hata pale ambapo tutakuwa tuna sheria ambayo inaongoza Idara hii ya Malalamiko bado inaweza ikatokea mara moja moja na naamini itakuwa mara chache sana haja ya kuweza kuweka Tume ili kuweza kushughulikia malalamiko ya wananchi na askari wenyewe.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na muda nalazimika kutumia Kifungu cha 104(i) kwamba iwapo zimesalia dakika 10 kabla ya kufikia muda wa kuahirisha Kikao cha Bunge na Kamati ya Matumizi bado haijamaliza kupitisha mafungu, Mwenyekiti anaweza kuongeza muda usiozidhi dakika 30 bila kuihoji Kamati ili kumaliza shughuli ya kupitisha mafungu yanayobakia. Kwa hiyo, naongeza dakika 30 baada ya muda wa kuahirisha kikao ili tumalize mafungu ya Wizara hii.

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*……………….Sh. 307,062.500
Kifungu 1003 - *Policy and Planning*……………………..Sh. 302,731,600
Kifungu 1004 - *Probation and Community Services Division*…..........................................................Sh.1,195,901,000
Kifungu 1005 - *Information, Education and Communication*...............................................................Sh. 96,378,800
Kifungu 1006 - *Management Information System Unit*…........................................................................Sh. 90,419,300
Kifungu 1007 - *Internal Audit Unit* …………….....…….Sh. 118,574,200
Kifungu 1008 - *Procurement Management Unit*…….Sh. 179,746,600
Kifungu 1009 - *Complaints Division*……………………..Sh. 492,875,100
Kifungu 1010 - *Legal Services Division*………………….Sh. 102,690,200
Kifungu 4001 - *Refugees Unit*…………………………….Sh.680,093,200

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji**

Kifungu 2001 - *Immigration Zanzibar*………………..Sh. 3,411,396,000
Kifungu 2002 - *Immigration Mainland*………………Sh. 23,348,269,000
Kifungu 2003 - *Regional Immigratoin Offices*……..Sh. 5,963,924,000
Kifungu 2004 - *TZ Regional Immigration Training Academy*……..................................................…..Sh. 559,541,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 14 – Jesh la Zimamoto na Uokoaji**

Kifungu 3001 - *Fire and Rescue Services*……………….Sh. 800,000,000
Kifungu 3002 - *Fire and Rescue Services Training Inst*…..Sh. 99,217,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 28 – Jeshi la Polisi**

Kifungu 2001 - *Police Mainforce*…..………………….Sh. 9,713,160.000
Kifungu 2002 – *Police Marine*……………………………Sh. 578,837,000
Kifungu 2004 – *Police Signals Branch*………………….Sh. 1,500,000,000
Kifungu 2005 – *Police Zanzibar*………………………….Sh. 450,000,000
Kifungu 2006 – *Police Airwing*……………………………Sh. 600,000,000
Kifungu 2017 – *Police Iringa*………………………………Sh. 253,000,000
Kifungu 2020 – *Police Kagera*…………………………….Sh. 100,000,000
Kifungu 2022 - *Police Mwanza*………………………..Sh. 1,170,000,000
Kifungu 2023 - *Police Mara*…………………………….Sh. 1,252,400,000
Kifungu 2027 - *Police Morogoro* ……………………….Sh. 300,000,000
Kifungu 2041 - *Police Dodoma*……………………….Sh. 2,500,000,000
Kifungu 3001 - *Police College Moshi* ……………………Sh. 200,000,000
Kifungu 3002 - *Police College*…………………………..Sh. 350,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 29 – Jeshi la Magereza**

Kifungu 1001 – *Prisons Headquarters*………………….Sh. 800,000,000
Kifungu 2002 - *Prisons Welfare and Rehabilitation* ……...............................……………….Sh. 2,000,000,000
Kifungu 4001 – *Prison Building Brigade*……………….Sh. 3,000,000,000
Kifungu 4002 – *Prison Industries*……..…………………..Sh. 813,583,000
Kifungu 4003 – *Prison Farms* …………………………….Sh. 5,000,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 51 – Wizaya ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kifungu 1001 – *Administration and General* ……………Sh. 97,995,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning*……………………Sh. 3,503,366,000
Kifungu 4001 – *Refugees Unit*………..............……………………..Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji**

Kifungu 2002 – *Immigration Mainland*……………..Sh. 26,808,667,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Bunge Zima na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liyakubali kuyapitisha Makadirio haya kwa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja ilitolewa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yamepitishwa rasmi na Bunge hili. Nachukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote kwa kujibu kwa ufasaha hoja mbalimbali na kuifahamu vizuri Wizara yenu na watendaji wenu tunawashukuru sana. Tunawatakia kazi njema, tunategemea ulinzi wetu, tunavitakia vyombo hivi na tunashukuru kwa kazi zote zilizofanywa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge asubuhi nadhani nilitangaza kwamba kesho ile *NGO* ya Bunge ya Idadi ya Watu na *TAPAC* watakuwa na kikao saa 5 .00 asubuhi kule *Dodoma Hotel*. Nadhani waliopewa mwaliko au wanachama wanapaswa kuwa na *t-shirts* zao, nafikiri wamegaiwa. Lakini baada ya kusema hivyo, naomba niwashukuru sana kwa kazi tuliyoifanya wiki yote hii. Tumefanya kazi nyingi, najua tuna matatizo mengi, lakini nadhani inaeleweka. Tuendelee kumaliza hii kazi vizuri. Niwatakie jioni njema na kesho Jumapili njema, tukutane Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.47 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu, Tarehe 28 Juni, 2010 saa tatu asubuhi)*